


KITANZI CHA SHABA

KILICHOMNYONGA MWANA WA MWAZOA

JUZUU YA KWANZA

Mwandishi

Abul-Fadhli Kassim Ibn Mafuta Ibn Kassim



©Haki ya kunakili imehifadhiwa na Mwandishi wa kitabu hiki.

Chapa ya Kwanza 2014

KIMETOLEWA NA KUSAMBAZWA NA:


MARKAZ IBN TAYMIYYAH - PONGWE

P.O.BOX 398 TANGA,

www.markazpongwe.com

PONGWE- TANGA,

TANZANIA.





إِنَّ الْحَمْدَ لِلَّهِ، نَحْمَدُهُ وَنُسْتَعِينُهُ وَنَسْتَغْفِرُهُ، وَنَعُوذُ بِاللَّهِ مِنْ شُرُورِ أَنْفُسِنَا،
وَسَيِّئَاتِ أَعْمَالِنَا، مَنْ يَهْدِهِ اللَّهُ فَلَا مُضِلَّ لَهُ، وَمَنْ يَضِلَّ فَلَا هَادِيَ لَهُ،
وَأَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ
وَرَسُولُهُ.

قال تعالى: ﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنتُمْ
مُسْلِمُونَ﴾ (آل عمران: ١٠٢).

﴿يَا أَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا
وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالًا كَثِيرًا وَنِسَاءً وَاتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي تَسَاءَلُونَ بِهِ وَالْأَرْحَامَ إِنَّ اللَّهَ
كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيبًا﴾ (النساء: ١)

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَقُولُوا قَوْلًا سَدِيدًا * يُصْلِحْ لَكُمْ أَعْمَالَكُمْ
وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَمَنْ يُطِيعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ فَازَ فَوْزًا عَظِيمًا﴾
(الأحزاب: ٧٠-٧١).

أما بعد، فإن أصدق الحديث كتابُ الله، وأحسنَ الهدي هدي محمد ﷺ،
وشرُّ الأمور محدثاتها، وكلُّ مُحدثة بدعة، وكل بدعة ضلالة، وكل ضلالة في
النار.


UTANGULIZI

Sifa njema zote ni za Allah Jalla Jalaaluh aliyeniwafikisha kuifanya kazi hii adhimu ya kupambana na watu wa batili, na kwa hilo ninatarajia malipo mema kutoka kwake -Sub'haanahu wata'ala- katika siku ambayo haitasaidia mali wala watoto.

Kisha Swala na Salaamu zimfikie kipenzi chake **Nabii Muhammad** pamwe na Aali zake watwahaarifu na Maswahaba wake waongofu aliowaridhia na wote walioiandama njia yao kwa wema hadi siku ya malipo.

Kwa kupitia tafiti za kielimu na mijadala ya kidini yenye kuchunga adabu na mipaka ya Sharia za Allah, hupatikana ndani yake faida nyingi kwa umma, hasa wanapokuwa watafiti wa mambo ni watu wenye elimu, weledi wa mambo na uadilifu katika kutoa hukumu. Kinyume chake, hakutakuwa na faida yoyote zaidi ya kukithiri upotoshaji wa haki, na hili ndilo lililopo hapa ulimwenguni, hasa katika zama hizi ambazo zimedhihiri kalamu chafu kwa wingi, na waandishi waongo, mafedhuli, wasio na weledi katika nyanja za dini, wala uwezo wa kutafiti mambo kutoka kwenye vyanzo vyake.

Katika dunia tunayoishi kuna madhehebu mengi, mitazamo tofauti na fikra mbalimbali zinazokinzana, na hii ndiyo hali ya kibinadamu ilivyo, jambo la msingi kwa kila mtu ni kujitahidi kushikamana na haki kutokana na hoja za kielimu zilizomfikia. Utawaona wafuasi wa madhehebu au mitazamo au fikra mbalimbali wakitoa juhudi kubwa ya kujitangaza mbele za watu kuwa wao ndio walioshikimana na haki na wanastahiki kufuatwa, lakini wakati huo huo utawaona hawako tayari kumuona mtu yeyote anawakosoa au kuzijadili hoja walizosimamia, na yeyote atakayewakosoa basi watamtuhumu kuwa ni mchochezi, mjinga, kibaraka, mwenye nia mbaya, na mfano wa tuhuma kama hizo, bali wako tayari kumdhuru kwa njia yoyote ile, ima kwa kumpiga au kwa kumuua, iwe kwa siri au kwa dhahiri. Watu wa aina hii ni watu waliofilisika kwa hoja, na si rahisi kwao kuifikia haki na uongofu, kwa sababu akili zao haziko tayari kukubali kwamba inawezekana kuwa haki iko kwengine na si kule waliko wao, na kwa hali zao hizo ni kama wanatwambia; haki siku zote iko pamoja na wao hata kama hawana hoja na batili iko kwa wengine hata kama wana hoja za msingi.




Lakini jambo la ajabu kwa watu hawa ni kuwaona siku zote wanatoa juhudi za kuwaponda watu wa mrengo mwingine bila ya kujali watu hao wana utukufu wa kiasi gani kwa wafuasi wao.

Hali hii itakudhihirikia kwa kukisoma kitabu **'Shimo Refu'** cha **Mshia Jaafar Mwazoa** ambacho amekiandika kwa lengo la kukijibu kitabu chetu **"UYAHUDI NYUMA YA PAZIA LA AHLUL-BAITI"** (**Itikadi ya Shia Ith'naashariyya juu ya Qur-ani**). Mwandishi huyo chipukizi wa Shia Ithnaashariyya amejifedhehesha yeye na Mashia wenzake kwa kuandika kitabu ambacho hakina maadili ya Kiislamu kwa kukishehenesha matusi na lugha za kinyaa zilizoambatana na makosa mengi ya kielimu na udhaifu wa kujenga hoja.

Inafahamika kwamba, Mashia wameandika vitabu vingi sana kwa lugha ya Kiswahili, wakijitangaza kupitia vitabu hivyo kuwa wao wako katika haki, na wito wao ni kuitaka jamii ya wanaosoma na kuzungumza Kiswahili hasa Ahlu Sunna wabadilike wawe Mashia, na katika uandishi wao huo huwatukana sana Maswahaba na watu wema waliotangulia ambao wanaheshimiwa na Ahlu Sunna wal-Jamaa, lakini wao bila kujali heshima na utukufu wa watu hao waliwatukana na kuwalaani. Na kwa bahati mbaya jamii ya Ahli Sunna ilikaa kimya na kuonesha uvumilivu wa hali ya juu, jambo ambalo Mashia walilitafsiri kuwa ni kushindwa kwa mahasimu zao kujibu hoja.

Lakini kilipotoka kitabu chetu **"UYAHUDI NYUMA YA PAZIA LA AHLUL-BAITI"** (**Itikadi ya Shia Ith'naashariyya juu ya Qur-ani**), Mashia walipata mshtuko mkubwa na kubabaika, ndipo walipomtumia kijana wao Jaafar Mwazoa ili kukijibu kitabu chetu hicho. Ukweli ni kwamba Mashia walifurahi sana na kupata faraja kwa kuona kuwa wamepata mkombozi wakidhani kuwa wamelipa deni kubwa lililowaelemea. Lakini ni ukweli usiopingika kuwa; Shia Ith'naashariyya bado wana deni kubwa la kukijibu kitabu chetu **'Uyahudi nyuma ya pazia la Ahul-Baiti'** kwa kuwa mpaka sasa hakujapatikana majibu ya kielimu ya kukijibu kitabu hicho zaidi ya matusi na ubabaishaji.




Na hilo utalifahamu kwa kukisoma kitabu chetu hiki '**KITANZI CHA SHABA KILICHOMNYONGA MWANA WA MWAZDA**' kwa sababu kitabu hiki kimesafisha kila walipochafua, na kuweka sawa kila walipobabaisha, halikadhalika kimezifichua njama chafu za Mashia, pamoja na fitna za mwanzilishi wa pote hili (**Myahudi Abdullahi Ibnu Sabai**) kwa hoja za kielimu, huku tukiypuuzia mbali matusi yote waliyoyatoa dhidi yetu.

Ndugu msomaji! Hii itakuwa ni juzuu ya kwanza ya kitabu chetu '**KITANZI CHA SHABA KILICHOMNYONGA MWANA WA MWAZDA**' Juzuu hii imekusanya SURA SITA. Sura hizo zimebeba maudhui mbalimbali hali ya kuwa ni majibu ya maudhui alizozileta Mshia Jaafar Ammar Mwazoa kwenye kitabu chake '**SHIMO REFU**'. Juzuu hii tumeihusisha na zile maudhui ambazo hazihusiani kabisa na kadhia ya kupotoshwa Qur-ani tuliyoizungumzia kwenye kitabu chetu '**UYAHUDI NYUMA YA PAZIA LA AHLIL-BAITI**'. Hivyo basi, mpangilio wa kitabu chetu hiki utakuwa ni huu ufuatao;-

SURA YA KWANZA, NENO LISILO BUDI, tumeigawa sura hii kwenye nukta kuu nne; **Nukta ya kwanza**; tumekutajia matusi ya Jaafar Mwazoa aliyomtukana **Allah Jalla Jalaaluh, matusi yake dhidi ya watu wema** na matusi yake dhidi yangu. Tumefanya hivyo kwa lengo la kukuonesha kiwango cha maadili ya bwana huyu tunayejadiliana naye. Na kwa kuchunga heshima zetu na heshima za wasomaji wetu, hatukumjibu lugha zake chafu kwa kuchelea kutumbukia kwenye malumbano ya matusi, jambo ambalo halina faida yoyote kwa wasomaji.

Nukta ya pili; tumekutajia makosa ya Mshia huyu kwa lengo la kukubainishia kiwango cha elimu yake, na namna asivyostahiki kuyazungumzia masuala haya mazito. Pamoja na udhaifu wake huo lakini Mshia huyu alikuwa na ujasiri wa kijinga uliompelekea kunikosoa sehemu ambayo sikukosea, kwa kunitaka nizifanyie kazi kanuni za lugha ya kiarabu katika maandishi ya Kilatini! na wakati huo huo yeye akashindwa kuzifanyia kazi kanuni hizo kwenye Lugha husika ya Kiarabu. Na jambo baya zaidi, ni kuwa makosa yake hayakuishia kwenye uandishi wa lugha ya Kiarabu tu bali alifikia kukosea mpaka kwenye maandiko matakatifu (Aya za Qur-ani na matini za Hadithi).




Nukta ya tatu; nukta hii tumeiweka kwa ajili ya kumjadili **Bwana AbdulRazaq Amir Juma**, mwalimu wa Jaafar Mwazoa ambaye ndiye aliyepewa dhamana ya kukipitia kitabu '**Shimo Refu**'. Tumemjadili juu ya kadhia za **Maulidi, Khitma, na Kuzuru makaburi**, kwa sababu ya yeye ameyafanya masuala haya kuwa ndio kigezo cha kututoa sisi anaotuita Mawahabi katika duara la Ahlu Sunna wal Jamaa! Pamoja na majibu yetu kwenye masuala hayo pia tumemjibu Mshia huyu tuhuma zake nyingine.

Nukta ya nne; kupitia nukta hii tumekubainishia kuhusu **CHOZI LA UONGO JUU YA WITO WA UMOJA**, hii ni nukta ya mwisho katika sura hii, katika nukta hii tumetoa sababu za msingi zenye kuthibitisha uongo wa Mashia wa kutaka umoja na Masuni, na hali ya kuwa wao hawako tayari juu ya hilo. Katika kukuthibitishia hilo tumekutajia vitendo na kauli za Wanazuoni wao zinazoelezea kuwa umoja baina ya Shia na Sunni ni jambo muhali (lisilowezezana). Kisha tukaihitimisha sura hii kwa maelezo mafupi juu ya harakati za kuleta umoja baina ya Shia na Sunni zilizofanywa na baadhi ya Wanazuoni walioishi katikati ya karne ya ishirini. Ukiirejea historia hiyo utabainikiwa na khiyana walioifanya Wanazuoni wa Shia dhidi ya harakati hizo kwa kukiuka makubaliano yaliyowekwa.

SURA YA PILI; AHLU SUNNA WAL-JAMAA, katika sura hii tumeelezea ni nani Ahlu Sunna, baadhi ya majina yao, mwanzo wa kudhihiri jina hili, baadhi ya sifa zao n.k., tumefanya hivyo pamoja na kuzitaja kauli za wanachuoni wenaotegemewa kwa lengo la kuufichua uongo unaofanywa baadhi ya waandishi kwa lengo la kuipotosha maana sahihi ya Ahlu Sunna wal-Jamaa, pia tumekuletea mjadala na Mshia Jaafar Mwazoa juu ya ubabaishaji wake kuhusu kauli ya Ibn Siiriin. Na mwisho wa sura hii tumemaliza kwa kukutajia juhudi zilizofanywa na Ahlu Sunna dhidi ya hadithi za kutunga.

SURA YA TATU; UWAHABI, katika sura hii tumeielezea historia ya **Sheikh Muhammad Bin Abdil Wahabi** kwa ufupi, na hali halisi ya watu wa miji yake, **kiitikadi, kiibada, kielimu, kitabia, na kisiasa**, halikadhalika tumekutajia daawa yake na hatua alizozitumia katika ulinganizi, pia tumekutajia hali za maadui zake pamoja na uzushi wao waliomzushia pamoja na majibu yetu dhidi ya uzushi huo




nukta moja baada ya nyingine, pia tumeitaja historia sahihi ya kisiasa na vita baina ya Sheikh Muhammad na maadui wa daawa yake, kwa lengo la kufuta dhana potofu zinazoenezwa na maadui kwa kufuata fikra chafu za Kafiri wa kizungu **Mr Humphrey** na wasaidizi wake. Na vile vile tumekubainishia ujinga wa Mshia Mwazoa kuhusu uhusiano wa Taliban na Uwahabi.

SURA YA NNE; katika sura hii tumekuelezea maovu yaliyofanywa na **Mashia Ithnaashariyya** katika kipindi cha dola yao, **Dola ya Swafawiyya (Safavid Empire)** iliyosimama baina ya mwaka **1524-1736 A.D.** Malengo na madhumuni ya kukuwekea sura hii; kwanza ni kukufahamisha kiwango cha chuki na uadui walionao Mashia dhidi ya Ahli Sunna wote, bila ya kubagua baina ya Mawahabi au Mashafii n.k.

Pili, ni kuwafahamisha Mashia kuwa hawana haki ya kuwatuhumu wengine kwa uovu wa kubuni na hali ya kuwa historia yao imesheheni mambo mengi maovu tena ya kinyama dhidi ya Waislamu na binadamu kwa ujumla.

SURA YA TANO; MYAHUDI ABDULLAHI IBN SABAI, katika sura hii tumeelezea mwanzo wa kudhihiri kwa Ushia na mwanzilishi wake **Myahudi Abdullahi Ibnu Sabai** kupitia riwaya na kauli kutoka kwa Mashia na Masuni zenye kuthibitisha juu ya kuwepo kwa mtu huyu bila ya kupitia kwa **Twabari** wala **Seif Ibn Umar,** tumefanya hivyo kwa lengo la kuyavunja madai ya uongo yaliyoletwa na **Mshia Murtadha Al-Askariy** na wote wanaomuunga mkono, vile vile tumezetaja athari mbaya alizoziacha Myahudi huyo ndani ya madhehebu ya Shia Ith'naashariyya, kisha tukakuletea majibu dhidi ya ubabaishaji uliofanywa na Mshia Jaafar Mwazoa kuhusu kuwepo kwa Myahudi huyu.

Mwisho tukaihitimisha sura hii kwa kukutajia baadhi ya mifano yenye kukuthibitishia hujuma iliyofanywana Maghulaati ambao ni wanafunzi wa Myahudi wa Abdullahi Ibnu Sabai kwa kutunga hadithi na kuzibambika kwa Maimamu wa Ahlil-Baiti kisha kuzipenyeza kwenye vitabu vya Mashia na wao wakazisadikisha hadithi hizo wakidhani kuwa ni mafunzo ya Ahlil-Baiti kumbe ni bidhaa mbovu zenye asili ya Kiyahudi.



SURA YA SITA; NAMNA MASHIA WALIVYOFELI KATIKA HARAKATI ZAO ZA KUUSAFISHA UZANDIKI WA MAGHULAATI KWENYE MADHEHEBU YAO. Kuna sababu nyingi za msingi zilizopelekea kuiweka sura hii, na miongoni mwa sababu hizo ni hizi zifuatazo;


Kwanza; kukuthibitishia kwamba huu Ushia Ithnaashariyya wa tunaouona ni zao safi la Maghulaati ambao ni wanafunzi wa Myahudi Ibn Sabai, na wala hautokani na mafunzo ya Ahlul-Baiti, na hilo ni kutokana na Maghulaati hao walivyofanikiwa kutunga riwaya nyingi mno tena kwa muda mrefu na kuzinasibisha kwa Maimamu wao.

Pili; kukuonesha kuwa Mashia hawawezi kuwakwepa Maghulaati na uzushi wao kwenye madhehebu yao, kwani kuwakataa Maghulaati ndio kuukataa Ushia wenyewe, na hilo ni baada ya kushindwa wanachuoni wao kuweka misingi madhubuti ya uchambuzi wa habari zao na riwaya zinazonasibishwa na Maimamu wao.

Tatu; ni kukufahamisha namna Wanazuoni wa Shia Ithnaashariyya wasivyokuwa na adabu za Kiislamu pindi wanapotofautiana baina yao wenyewe kwa wenyewe, hasa pale walipofikia kutukanana matusi makubwa, kuzuliana uongo, kukufurishana na kuharamisha baadhi yao kuswali nyuma ya wengine, bali walifikia kuuwana! Tumeyataja haya pia kwa lengo la kumuweka sawa Mshia **Abdul Razaq Amir Juma** na kumwambia yeye na Mashia wenzake hawana haki ya kuwatuhumu hao wanaowaita Mawahabi kwa mambo yanayofanywa na wajinga miongoni mwao, na wakati huo huo wakizifumbia macho aibu kubwa zilizofanywa na Wanazuoni wao wakubwa.

Nne; Kuyavunja madai ya uongo ya Mshia Mwazoa pale alipodai kuwa **Akhbaariyyuuna** si **Mashia Ith'naashariyya**, na jambo lililompelekea kudai hilo ni kuwa wanachuoni wengi wa **Akhbaariyyuuna** na baadhi ya **Usuliyyuuna** wametamka wazi kwenye vitabu vyao kwamba; Qur-ani iliyoko mikononi mwa Waislamu ni batili, imepunguzwa na madhalimu.

Ndugu msomaj! Kwa ufupi huo ndio muundo wa juzuu hii ya kwanza ya kitabu chetu '**KITANZI CHA SHABA KILICHOMNYONGA MWANA WA MWAZOA**'.



Hivyo basi, baada ya juzuu hii jiandae kuipokea juzuu ya pili ambayo imebeba hoja zenye nguvu zenye kuthibitisha kwamba Maulamaa wakubwa wa Shia lth'naashariyya wanaitakidi itikadi ya kikafiri ya kwamba; Qur-ani tuliyonayo waislamu si kamili, kwa kuwa madhalimu walioiandika walizipunguza baadhi ya Aya na kuzibadilisha nyingine. Na hiyo ndiyo maudhui mama ya mzozo uliopo baina yetu na Mashia.


Tunamuomba Allah atuwafikishe kwenye haki

Hakika yeye juu ya kila kitu ni Muweza

Abul-Fadhli Kassim Bin Mafuta Bin Kassim

Al-Khamisi, tarehe 10| Muharram |1435 H sawa na 14| 11| 2013

Pongwe-Tanga



SURA YA KWANZA

NENO LISILO BUDI

1- KUHUSU MATUSI YA JAAFAR MWAZOA;

Kitabu 'SHIMO REFU' cha Jaafar Mwazoa, ni kitabu kilichosheheni lugha chafu za kihuni na matusi ya wazi wazi, kejeli, dharau na utovu wa adabu kwa viumbe hadi kwa Muumba Allah Jalla wa A'laa.


Ukweli ni kwamba matusi ya Jaafar Mwazoa yamemuumbua mwenyewe na kuifahamisha jamii ya watu wenye hekima na busara kuwa yeye ni mtu wa aina gani, na amekulia katika malezi ya sampuli gani, si hivyo tu, bali pia amewaumbua na kuwadhalilisha waliomlea na kumsomesha. Haingii akilini kwa mtu mstaarabu, mwenye akili timamu, aliyekulia katika maadili mema ya kiislamu ashike kalamu ili aandike mambo ya dini na kujadili kadhia za kielimu, kisha akawa anawatukana watu bila ya sababu za msingi, huko ni kuporomoka kimaadili na kuihujumu fani hii ya uandishi wa mambo ya dini.

Katika sehemu hii nitaorodhesha baadhi ya matusi yake kama mfano tu, ili ndugu msomaji ujionee mwenyewe tunajadiliana na mtu wa aina gani?

Matusi yake dhidi ya Allah -Jalla Jalaaluh-;

Jaafar Mwazoa katika ukurasa wa 47 alipokuwa akiwazungumzia hao anaowaita Mawahabi na itikadi zao, amesema:

"Ni lazima sote tuamini kuwa Mungu ana mwili kama sisi, ni lazima tuamini kuwa MUNGU AMEKAA KWENYE KITI NA BOGI LAKE NI KUBWA KULIKO KITI CHAKE IKABIDI LIMWAGIKE HUKU NA HUKU, Mungu wa kiwahabi ameshindwa kuumba kiti kinachomtosa!"



Kisha akakariri tena kauli hiyo ya Kufuru kwenye ukurasa wa 245, kwa kusema:

"Mungu wetu na Masunni ni yule Mungu ambaye hana mfano¹.....Mungu wenu anakaa kwenye kiti (Mungu wa vipi), TENA MUNGU WENU ANA BOGI KUBWA KULIKO KITI CHAKE, hivi Mungu huyu ndiye mnayemuabudu na ndiye atakayewatia peponi? Ama kweli AL-JUNUUNU FUNUUNU."

MAJIBU YETU

Siamini kuwa Bwana huyu alipoyatamka maneno haya alikuwa na akili timamu! Kwa sababu haiwezekani kwa mtu mwenye akili timamu kutamka matusi makubwa kama haya dhidi ya Mola wake aliyemuumba kutoka kwenye tone la Manii! Pamoja na matusi yake hayo yaliyojaa Kufuru ya wazi, pia Jaafar Mwazoa amewasingizia Waislamu kwa jambo ambalo hana ushahidi nalo.

Bogi, ni neno lililo Swahilishwa (limetiwa kwenye Kiswahili) kutoka kwenye lugha ya kiingereza, likiwa na maana ya behewa linalovutwa na garimoshi. Na kwa lugha ya Kiswahili cha mtaani bogi ni MAKALIO MAKUBWA! Na Jaafar ameikusudia hii maana ya pili na kumsifu nayo Allah kwa dhulma na uadui, kwa kusingizia kwamba eti Mawahabi wanasema hivyo, na hali ya kuwa huo ni uongo aliouzuwa yeye mwenyewe, na kwa kupenda kwake kutukana, akamtukana mpaka Mola aliyemuumba.


Pia tunampa Challenge (**chalenji**) Jaafar Mwazoa na Mashia wenzake watuambie ni kitabu gani, cha mwanachuoni gani miongoni mwa hao wanachuoni wa ki-Wahabi - kama unavyowaita- aliyetamka maneno hayo ya Kufuru? Tunaomba uthibitisho wa hilo kwa hoja za kielimu kama nyinyi ni wenye kusema kweli.

2- Matusi yake dhidi ya Swahaba Muawiyah -Radhia Ilaahu an'hu-

Amesema Jaafar Mwazoa katika ukurasa wa 38-39 akimtukana Swahaba Muawiyah radhia Ilaahu an'hu kwa kumlaani:

¹ -Hapo penye uwazi aliiandika Aya ya II katika Surat Shuura isemayo;

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ kwa maandishi yasiyo ya kiarabu, na jambo hili kwetu sisi Ahlu Sunna halifai, kwa sababu hupotosha matamshi ya Qur'ani na kuinyima haki yake.



"Kwa hiyo Usunni huu unaozungumziwa hapa ni Usunni wa MAL'UUNI MUAWIYA BIN ABII SUFIYAAN....."

MAJIBU YETU

Haya ni matusi makubwa kwa Swahaba huyu ambaye Ahlu Sunna wanamuheshimu. Jaafar Mwazoa anamtukana Swahaba huyu kwa kumlaani, na huku akitoa chozi la uongo la kutaka umoja na Masunni, na hali ya kuwa yeye anajua wazi kuwa Masunni wote mpaka hao wasiokuwa Mawahabi pia wanamuheshimu Swahaba huyu, lakini kwa kupenda kwake matusi hakujali hisia za hao anaowaita kwenye umoja! Hivi bado mnataka umoja na hali hamkomi kututukania wabora wetu?

3- Matusi yake dhidi ya Sheikhu-Islaami Ibn Taymiyyah -Rahimahu Ilaahu-;

Amesema Jaafar Mwazoa katika ukurasa wa 31 akimlaani Sheikhu-Islaam Ibn Taymiyya;

"Anasema Ibnu Mafuta kwa nukuu ya Ibnu Taymiya MUNGU AMLAANI....."

MAJIBU YETU

Hatuna shaka kwamba laana hii itamrudia yeye mwenyewe na wale wote waliomfundisha kuwalaani watu wema. Lau kama Mshia Mwazoa ana mapenzi ya kweli na watu wa dini na chuki dhidi ya watu wa batili, basi angezipeleka laana zake kwa wanachuoni wa madhehebu yake wanaoitukana Qur'ani, kama vile **Al-Bahraani, Al-Kaashaaniy, Ni'matullaahi Al-Jazaairiy, Haaj Mirza Nuuri Twabarsiy Al-Mazindarani** na wengineo waliotamka wazi kuwa hii Qur'ani tuliyonayo ina mapungufu.

4- Matusi yake dhidi yangu;

Amesema katika ukurasa wa 76;

"Hiki ndicho kilichonifanya niseme kuwa FEDHULI HUJU hajui anachodai wala anachokisema!!!"

Amesema katika ukurasa wa 103;

"...ni kwa nini MWENDAWAZIMU HUYU hakunukuu kwa kuanzia kiashiria kilichopo katika Aya ya kwanza...."

Amesema katika ukurasa wa 108;

"Hivi ndivyo tunavyoweza kusema kwenye mifano yote iliyobakia ambayo ABU JAHLI KASSIM MAFUTA ameinukuu..."

Amesema katika ukurasa wa 121;

"Tungependa kumwambia Ibnu Mafuta asiwe MPUUZI kwa kiwango hiki kwani upuuzi mwingine unaepukika."

Amesema katika ukurasa wa 140;

"Je huoni kuwa WAHABI HUYU ANA WENDAWAZIMU NA UHAMNAZO ULIOPITA MIPAKA?!!"

Amesema katika ukurasa wa 142;

"Maelezo yote haya, FEDHULI HUYU WA KIWAHABI KWA KUJAWA NA UHAMNAZO...."

Amesema katika ukurasa wa 152;

"Na kwa ukweli kabisa nafika mahala NATILIA SHAKA USALAMA WA AKILI NA UELEWA WAKE."

Amesema katika ukurasa wa 153;

"Lakini sasa napenda niseme wazi tena kwa kinywa kipana kuwa WAHABI HUYU NI HAMNAZO!"

Akasema tena katika ukurasa huo huo;

"...bali tufungamanishe madai yetu na ithibati ya yeye MAFUTA JUU YA UPUNGUANI WAKE."

Pia amesema tena kwenye ukurasa huo huo;

"KAMA HUO SI UPUNGUANI NI NINI?!!"

Amesema katika ukurasa wa 170;

"...IKIWA HUO ALIQUNYA NI UHARO².....!!!"

Amesema katika ukurasa wa 111;

"Hii inaonesha wazi kuwa BWANA HUJU HANA TOFAUTI NA PUNDA, ambaye bila shaka hata umbebeshe vitabu maisha yake yote, hakuna mwenye matarajio kwamba kuna siku eti punda huyo atakuwa mwanachuoni mkubwa! KWANI ULIWAHI KUONA PUNDA AKAWA PROFESA?"

MAJIBU YANGU

Pamoja na matusi yote haya, lakini mimi binafsi nimeona nisimjibu, wala nisiige lugha yake, kwa kuchunga heshima yangu pamoja na heshima za wasomaji, na hayo ndiyo maadili mema ya dini yetu, kama tulivyofunzwa na wazazi wetu na masheikh zetu waliotusomesha, Allah awarehemu wote na atusamehe sisi na wao. Na sikunyamaza kwa kushindwa kutukana. Lakini ninachoweza kumwambia Jaafar Mwazoa ni hii kauli aliyoisema Mshairi mmoja wa Kiarabu alipotukanwa;

شَاتَمَنِي عَبْدُ بَنِي مَسْمَعٍ فَصُنْتُ عَنْهُ النَّفْسَ وَالْعَرَضَا
وَلَمْ أُجِبْهُ لاحتقاري له ومن يعضّ الكلب إن عضًا

Amenitukana mtumwa wa banii Mis'mai *** Nikalinda nafsi (yangu) na heshima.

² -Ewe Mshia Jaafar Mwana wa Mwazoa! Lugha hizi za Uharo na kinyesi zina nafasi gani kwenye vitabu vya kielimu? Huoni haya!!!

Sikumjibu kwa kumdharau yeye*** Ni nani amng'tae mbwa kama atamng'ata!

5- MAKOSA YA JAAFAR MWAZOA

Uandishi katika mambo ya dini ni jambo linalohitaji umakini na uangalifu wa hali ya juu, kutokana na ukubwa na heshima ya mambo yenyewe, mwandishi wa fani na mijadala ya kidini anatakiwa awe na maarifa ya kutosha, uelewa mkubwa juu ya kadhia anazozindika, na uadilifu kwenye nafsi yake, hata na watu anaotofautiana nao kimawazo na misimamo.

Mwandishi asikubali kuvutwa na utashi wa nafsi, chuki binafsi, upenzi na ushabiki wa kimadhehebu, na kama atalikubali lolote kati ya sifa hizi mbaya zimtawale, basi upotoshaji wa haki utachukua mkondo wake.

Lakini pia tukubaliane kuwa, mwanadamu vyovyote atakavyojipinda na kutoa juhudi kubwa, bado kazi yake haitasalimika na makosa, lakini maadamu kosa lake halipotoshi maana, na wala si kiashiria cha ujinga wa mwandishi, waungwana wenye kutambua mambo, husahihisha kosa ikibidi kufanya hivyo, na kumfumbia macho mkosaji, hawambezi, wala hawamtukani, bali husema: *hiyo ni kazi ya mwanadamu...*


Mtu mwenye kusukumwa na chuki binafsi, au ushabiki wa kimadhehebu hupatiliza kila kitu, hadi kufikia kulifanya jambo ambalo si kosa kuwa ni kosa. Na hilo ndilo lililomkumba Jaafar Mwazoa. Bwana huyu kwa kuwa amekiandika kitabu chake '**Shimo Refu**' huku akiwa amezingirwa na chuki binafsi, hali hiyo imempelekea kumtoa katika uadilifu, sifa ambayo ni muhimu sana kwa kila mwandishi kusifika nayo.

Na huu ufuatao ni ushahidi miongoni mwa ushahidi mwingi uliomo kwenye kitabu chake 'Shimo Refu' unaothibitisha hilo, lakini kwa kuhofia kurefusha nitakudokeza kidogo tu.

Amesema Jaafar Mwazoa katika ukurasa wa 125 alipokuwa akinikosoa kwa kuwa nimeandika kwa Kiswahili Muhammad Ibnu Ali;

Abuu Ja'far Muhammad bin (na sio Ibnu kama alivyoandika Kassim, kwani kanuni za ki-imlaai haziruhusu neno hilo kuandikwa Ibnu iwapo liko kati ya Ma'arifa mbili....

MAJIBU YETU



Kabla ya kumjibu Jaafar Mwazoa ni vyema nikaanza kwa kumuusia kwa kumwambia maneno haya ya Abul-Ataaiyah;

لَا تَنَّهُ عَنِ خُلُقِي وَتَأْتِي مِثْلَهُ****عَارٌّ عَلَيْكَ إِذَا فَعَلْتَ عَظِيمٌ.

Usiikataze tabia kisha nawe ukaifanya mfano wake *** Itakuwa ni aibu kubwa kwako ukiifanya!

Ni kweli Mimi nimeandika; **Muhammad Ibnu Ali** kwa lugha ya Kiswahili kwa maandishi ya Kilatini, maandishi ambayo agh'labu hayachungi kanuni za lugha ya Kiarabu, kama vile kanuni za Khattwi, Imlaai, wala Nahwu na Swarfa, kwa hiyo sikuona ulazima wa kuzifanyia kazi kanuni za kiarabu kwenye maandishi ya Kiswahili. Ama kwenye maandishi ya kiarabu, nimezichunga kanuni hizo, na ndio maana hakupata mahali pa kunikosoa.

Lakini jambo la ajabu, tena ajabu kubwa! Ni pale Jaafar Mwazoa aliponikosoa mimi kwa jambo ambalo si kosa, kisha na yeye katika sehemu hiyo hiyo akakosea zaidi, kwa kuliandika neno hilo hilo kimakosa –kwa mujibu wa kanuni zake- zaidi ya mara hamsini ndani ya kijitabu chake chenye kurasa 254!

Ukweli ni kwamba, Samaahatu Sheikh Jaafar Mwazoa alikuwa akisukuma maneno ya kiarabu bila kuchunga kanuni za Nahwu, Swarfa, wala Imlaai, ili mradi dau lifike Pwani, lakini wakati huo huo ananishupalia mimi nichunge kanuni za Imlaai kwenye maandishi ya Kiswahili, na huku yeye akishindwa kutwabiq (kufuata) kanuni hizo katika lugha husika.

Na ushahidi wa hilo ni pale alipoliandika neno BIN (kwa Kasra katika الباء (Al-Baau) na usahihi alitakiwa alitie Saakina. Halikadhalika ameweka Sukuun katika Nuun kila alipoliandika neno hilo, utadhani neno hilo ni **Mabniyyun a'las-Sukuuni**, na hali ya kuwa neno hili linakuwa Marfuu kwa dhamma (**BNU**), na ni Manssubu kwa Fat'ha (**BNA**) na ni Majruuru kwa Kasra (**BNI**), yeye kila mahali ameandika **bin, bin, bin.....!!!** Hivyo basi, kwa mujibu wa kanuni yake hiyo ya kuchunga kanuni za lugha ya kiarabu kwenye maneno ya Kiswahili, atakuwa ametenda makosa mawili kwa mpigo! Hilo ni Mosi ambalo linahusu uandishi wa Kiswahili.

Pili, ama kwenye uandishi wake wa herufi za kiarabu, ameshindwa kuuzuia udhaifu wake juu ya lugha hii adhim. Kwa hakika amejifedhehesha mno na amemfedhehesha mwalimu wake aliyekipitia kitabu hicho, kwa sababu kuna makosa mengi mno, tena mpaka kwenye uandishi wa Aya za Qur'ani na Hadithi za Bwana Mtume swalla llaahu alayhi waalihi wasallam, mpaka huwa najiuliza; Hivi huyu **AbdulRazak Amir Juma aliyepewa dhamana ya kukipitia kitabu hiki cha mwanafunzi wake hakuyaona makosa haya?** Au yeye na mwanafunzi wake hawachekani katika hili? Kwa hakika sipati picha lau kama Bwana Mwazoa angekiandika kitabu chake kwa lugha ya kiarabu, sijui ingekuwaje! Ikiwa hizi ibara alizozinukuu tu kwa mtindo wa **(copy & paste)** hali ni hii, je angeandika kwa Inshaa yake mwenyewe tena kwa lugha ya kiarabu hali ingekuwaje!!!

Kwa hakika kitabu '**Shimo Refu**' cha Mshia Jaafar Mwazoa kimetudhihirishia kiwango chake cha elimu na upeo wa maarifa yake, kwa sababu kitabu chake kimejaa makosa mengi mno kwa kiwango kisichovumilika, na kukufanya usiamini kuwa mwandishi wake aliwahi kukaa japo wiki moja kwenye vikao vya elimu. Na haya yafuatayo ni baadhi ya makosa yake³;

i. Makosa yake katika Qur'ani;

Mwandishi huyu amekosea mpaka kwenye Aya za Qur'ani, jambo ambalo ni nadra kupatikana kwa wanafunzi wa madrasa za dini kwa kiwango cha awali! Na haya yafuatayo ni baadhi ya makosa yake:-

Aya ya kwanza aliyoikosea ni Aya ya 120 ya Surat Al-Baqarah, Mshia huyu bila ya kujali heshima ya Kitabu Kitukufu cha Allah, ameiandika Aya hii katika ukurasa wa 46, hivi;

وَلَنْ تَرْضَىٰ عَنْكَ الْيَهُودُ وَلَا النَّصَارَىٰ حَتَّىٰ تَتَّبِعَ مِلَّتَهُمْ

Hizo sehemu tulizozipigia mstari chini ndizo sehemu alizozikosea, na hiyo ni kwenye Aya moja tu, tena kipande cha Aya na si Aya kamili!

³ -Katika sehemu hii nitayataja makosa yake machache kama mfano tu, na wala sitampatiliza kwa kila kosa alilolifanya, kwa sababu makosa yake ni mengi mno na lau kama nitampatiliza, basi kitabu kitarefuka.

Kosa lake kwanza, liko katika sehemu ya kwanza tuliyoipigia mstari chini, pale alipoandika **Yaa (Yee)** mahali pa Alifu Maqsuur. Likawa neno linasomeka; TARDHII, badala ya TAR'DHAAA!!!

Kosa lake la pili, liko katika sehemu ya pili tuliyoipigia mstari, pale alipoambatanisha **Daali** yenye Dhumma na **Waawu**, na hali ya kuwa Waawu hiyo ni herufi ya A'tfi (kiunganishi), na inajitegemea. Likawa neno hilo linasomeka; YAHUUUU LAN-NASWAARII... kwa kuvuta Daali badala ya kusomeka YAHUUUU WALAN-NASWAARAA!!

Kosa lake la tatu, ni kuiandika **Yaa (Yee)** mahali pa Alifu Maqsuur katika Neno NASWAARAA, na kutokana na uandishi wake litakuwa neno hili linasomeka NASWAARII!

Kosa lake la nne, ni kwenye mstari wa nne, alipoandika **Yaa (Yee)** mahali pa Alifu, na kwa sababu hiyo likawa neno hilo linasomeka HATTII badala ya HATTAA!

Na sahihi alitakiwa aiandike Aya hiyo hivi:

{وَلَنْ تَرْضَىٰ عَنْكَ الْيَهُودُ وَلَا النَّصَارَىٰ حَتَّىٰ تَتَّبِعَ مِلَّتَهُمْ}

Makosa yote hayo ni kwenye kipande cha robo Aya tu!

Kosa lake la tano, liko katika ukurasa wa 95 pale alipoandika Aya ya 61 ya Surat Aali Imraan hivi; فَقُلْ تَعَالَوْا نَدْعُوا kwa kuirufaisha Fi'lun Mudhaari'i (ندعو) ambayo ni Majzuum, na alama yake ya Jazmu ni kuondoshwa herufi ya mwisho ambayo ni Waau.

Kisha Mshia huyo hakutosheka na kuiandika **"Waau"** peke yake, bali akaongezea mbele yake **"Alifu"**! Na usahihi alitakiwa aiandike Aya hii hivi; (فَقُلْ تَعَالَوْا نَدْعُ), lakini yeye kwa ufundi mwingi akaiweka **"Waawu"** na akaongeza juu yake ziada ya **"Alifu"**, anadhania kuwa herufi hizo zinawekwa kama mapambo!

Kosa lake la saba, liko katika ukurasa wa 67, alipoiandika Aya ya 1 katika Surat Nuuh hivi: {إِنَّا أَرْسَلْنَا نُوحًا إِلَىٰ قَوْمِهِ} na sahihi alitakiwa aiandike hivi: {إِنَّا أَرْسَلْنَا نُوحًا إِلَىٰ قَوْمِهِ}

Kwa kuandika Hamzatul-Wasli badala ya Hamzatul-Qatw'i.

Kosa lake la nane, liko katika ukurasa wa 69, alipoiandika Aya ya 5 ya Suurat Shua'raa hivi:

{وَمَا يَأْتِيهِمْ مِنْ ذِكْرٍ مِنَ الرَّحْمَنِ مُحَدَّثٍ إِلَّا كَانُوا عَنْهُ مُعْرِضِينَ}

Kwa kuandika Hamzatul-Wasli katika neno "illaa" badala ya Hamzatul-Qatw'i.

Kosa kama hilo amelifanya alipoiandika Aya ya 2 ya Suratul-Anbiyaa. Amelirudia kosa hilo hilo katika ukurasa wa 70, alipoiandika Aya ya 2 ya Surat Yusuf. Amelirudia kosa hilo hilo katika ukurasa wa 91, alipoiandika Aya ya 7 ya Surat Aali Imraan. Amelirudia tena kosa hilo hilo katika ukurasa huo huo alipoiandika Aya ya 79 ya Surat Al-Waaqia' Akalikariri tena kosa hilo hilo katika ukurasa huo huo alipoiandika Aya ya 33 ya Surat Al-Ahzaabi na Aya hiyo hiyo katika ukurasa wa 94.

Na katika ukurasa wa 95 akafanya virozo zaidi, akazikusanya Alifu mbili zikawa zimefuatana kama vigongo vya **Fyata (Manati/Panda)**, pale alipoiandika Aya ya 23 ya Surat As-Shuura hivi!

{قُلْ لَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا إِلَّا الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَىٰ}

Na sahihi alitakiwa aiandike Aya hii hivi:

{قُلْ لَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا إِلَّا الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَىٰ}

Kwa kweli makosa yake ya aina hii katika uandishi wake wa Aya za Qur'ani ni mengi mno mpaka nimechoka kuyahesabu!

ii- Makosa yake katika uandishi wa Riwaya;

Kosa lake la tisa, liko katika ukurasa wa 54, pale alipoiandika riwaya iliyomo kwenye **Ad-Durru Al-Manthuuru** kutoka kwa Abu Bakri Ibn Muhammad Ibn Amri Ibn Hazmi, kwamba amesema Twalha; "لَإِنْ حَدَّثَ بِهِ حَدَّثٌ لَنَتَزَوَّجَنَّ نِسَانَهُ". Kosa lake hapa,

ni kuiandika "In Shartiyya" kwa kuitia Fataha, ikawa yasomeka; 'La-an' badala ya kusomeka; 'La-in'.

Na kosa lake la kumi, ni kulitia Jarri kwa Kasra neno Nisaa likawa lasomeka hivi; "Nisaa-ih" badala ya kusomeka "Nisaa-ahu" kwa kuwa ni Mansuubu kwa Fataha, kwa sababu ni Maf'uulun-Bihi (mtendewa).

Na Sahihi alitakiwa aandike hivi; لَيْسَ حَدَّثَ بِهِ حَدَّثٌ لَنْتَرْوَجَنَّ نِسَاءَهُ...!

iii- Makosa yake mengine;

Kosa lake la kumi na moja; liko katika ukurasa wa 113, pale aliporufaisha Khabari ya Kaana badala ya kuinasibisha! Yeye ameandika hivi;

علي بن أبي حمزة كان واقفي المذهب، ضعيف، كذاب، متهم!!!

Kwa mujibu wa kanuni za lugha ya kiarabu, hivyo alivyoandika Mshia Mwazoa, maneno hayo tuliyoyapigia mstari yatakuwa yanasomeka hivi; **Dhaifun Kadhaabun, Muttahamun**, na kusoma hivyo ni makosa makubwa sana. Na sahihi alitakiwa aandike hivi; **Dhaifan, Kadhaaban, Muttahaman**, na si **Dhaifun, Kadhaabun, Mutahamun**, kwa sababu hizo zote ni Khabari za Kaana.

Kuandika Hamzatul-Wasli mahali pa Hamzatul-Qaiw'i;

Makosa ya aina hii ni mengi mno kwa kiwango cha kutia aibu! Jaafar Mwazoa katika uandishi wake hakutofautisha katika kuandika Hamzatul-Wasli (i) na Hamzatul-Qatw'i (i), yeye aliamua kusukuma tu, na hapa nitaitaja mifano michache, na hilo litakuwa ni;

Kosa lake la kumi na mbili, liko pale alipoliandika jina la kitabu chake 'Shimo Refu' kwa kiarabu; الهوة السحيقة التي سقط فيها ابن مفاوتا ameliliandika neno tulilolikoleza wino kwa Hamzatul-Qatw'i badala ya kuandika kwa Hamzatul-Wasli kama hivi; ابن. Kosa hili amelikariri kila alipoliandika jina la kitabu chake kwa kiarabu!!!

Kosa lake la kumi na tatu, liko katika ukurasa wa 15 wa kitabu chake, alipokuwa akimnukuu Dr. Twaha Husein kuhusu Ibn Sabai, akaandika hivi; لا نجد لابن سبأ ذكرا
Hapa kosa lake ameweka Hamzatul-Qatw'i mahali pa Hamzatul-Wasli alitakiwa aandike; لابن na si لابن.

Kosa lake la kumi na nne, liko katika ukurasa wa 19 katika kitabu chake, na hapa ndio amefanya vioja vikubwa kwa kukusanya Nasbu na Jarru kwenye neno moja, akaandika; من أعدائه (Min A'daa-aihi)! Na sahihi alitakiwa aandike; من أعدائه. (Min A'daaihi). Mwisho ninamwambia tena Samaahatu Sheikh Jaafar Mwazoa;

لا تَنهَ عَن خُلُقِي وَتَأْتِي مِثْلَهُ****عَارٌّ عَلَيْكَ إِذَا فَعَلْتَ عَظِيمٌ.

Usiikataze tabia kisha nawe ukaifanya mfano wake* Itakuwa ni aibu kubwa kwako ukiifanya!**

Sasa yeye si kwamba ameifanya tabia hiyo hiyo tu, bali amefanya makosa zaidi ya hayo tena kwa mara nyingi!!!

6- MJADALA JUU YA MANENO YA MSHIA ABDULRAZQA A. JUMA

Bwana AbdulRazaq Amir Juma ambaye ni mwalimu wa Jaafar Mwazoa, ndiye aliyepewa dhamana ya kukipitia kitabu '**Shimo Refu**' cha mwanafunzi wake huyo, lakini ameshindwa kutekeleza dhamana aliyopewa kama ulivyojionea mwenyewe katika sehemu zilizotangulia hapo nyuma.

Kitabu kimejaa makosa mengi katika maandishi ya lugha ya kiarabu, makosa ya kimaadili, pamoja na kupoteza muelekeo kwa kuikwepa mada husika.

Yote hayo Bwana AbdulRazaq hakuyaona, alichokiona yeye kwenye kitabu hicho ni kuvuliwa Mawahabi kwenye Usunni! Bila ya kufahamu kwamba wao hawana uwezo wa kuwatoa hao waitwao Mawahabi kwenye Usunni hata shibri moja.

Shia na wengineo katika watu wa bidaa wameona njia rahisi ya kuihujumu itikadi ya Ahlu Sunna, na kuvihujumu vitabu vyao, na maulamaa wao, ni kuwapachika jina la

Uwahabi ili hujuma yao hiyo ifanyike kwa urahsi, lakini *walillaahil-hamdu* mbinu hiyo imefeli.

Kwa mfano; utaona wanapotaka kuzishambulia hadithi za Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam zilizomo kwenye vitabu vinavyoheshimika kwa Ahlu Sunna kama vile Sahihi Bukhari, au Sahihi Muslim, utaona wanasema; Mawahabi kwenye kitabu chao hiki.....!

Wanapotaka kuwashambulia baadhi ya Maswahaba, kama vile Swahaba mtukufu Muawiya Ibn Abi Sufiyan radhia Ilaahu an'huma, utaona wanasema; huyu ni kiongozi wa Mawahabi.....! Wanawashambulia wanachuoni wakubwa katika madhehebu za Ahli Sunna kwa kupitia jina la Uwahabi, utaona wanawatukana wanachuoni kama; **Al-Bukhaariy, Muslimu, Abdullahi Ibn Ahmad Ibn Hanbali, Ibn Khuzayma, Abu Ya'laa, Ad-Daarimiy, Ibn Battwa, Ibnu Taymiyya, Ibnul-Qayyim, Ad-Dhahbiy, Ibn Kathiiri** na wengineo, kwa madai ya kwamba na hawa nao ni Mawahabi.

Ndugu msomaji! Utangulizi uliotolewa na AbdulRazaq katika kitabu cha mwanafunzi wake umeonesha miqdari na upeo wake wa kielimu.

Kwa kuwa mtangulizi huyo hakutofautiana na mwanafunzi wake, bali maneno yake yamefanana na maneno ya mwanafunzi wake katika Jazba na kukosa busara, sambamba na hilo ameshindwa kuyanyofoa makosa mengi yaliyomo kwenye kitabu hicho, na badala yake na yeye ameongezea kukitoa heshima kitabu hicho, kwa kutumia lugha za chuki, uongo na utovu wa adabu. Na miongoni mwa maneno ya jazba aliyoyatoa AbdulRazaq, ni pale aliposema katika ukurasa wa (vi);

"Kundi hili la kiwahabi lililoasisiwa kwa misingi ya kisiasa mwanzoni mwa karne ya kumi na nane lau kama wangeachwa waishi peke yao katika dunia hii basi wangeuwana wao kwa wao kutokana na tafauti za kimtazamo."

MAJIBU YETU

Tafadhali Bwana AbdulRazaq, soma kwanza habari za wanachuoni wenu wa Shia Imaamiyya, Ith'naashariyya, baina ya Akh'bariyyiina na Usuuliyiina katika kitabu hiki, uone mizozo iliyojiri kati ya wanachuoni wenu. Kwa hakika wanachuoni wenu wameonesha ujahili wa hali ya juu, hadi kufikia hatua kutukanana, kukufurishana na kuuana. Kisha baada ya hapo ndio uwazungumzie hao unaowaita Mawahabi na wengineo wasio kuhusu. Akaendelea kusema tena katika ukurasa wa (vii):

"Mawahabi hawajatosheka na kukufurisha na kupora misikiti ya Ahlu Sunna wal-Jamaa tu, bali sasa wanataka kuwapokonya Masunni jina lao! Ati wao sasa ndio Masunni! Halafu na Masunni watakuwa nani? Kwani Mawahabi siku hizi **mnasoma maulidi, kuzuru makaburi**, na kufanya khitma?"

MAJIBU YETU

Kutokana na maneno haya yalivyokosa muelekeo wa kielimu, sitapoteza muda kuyafafanua na kuyajibu, bali nitayachagua yaliyo na afuweni kati ya hayo ili nisikupotezee muda wako ndugu msomaji.

Kwa muktadha wa kauli ya Mshia AbdulRazaq ni kuwa ili mtu awe Sunni ni lazima asome **Maulidi, Khitma na Kuzuru makaburi**. Suala la kuzuru makaburi hilo halina tatizo, kwa sababu ni jambo limethibiti kupitia mafundisho sahihi ya Bwana Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam, isipokuwa tunachokipinga sisi ni baadhi ya mambo ya shirki na uzushi yaliyoingizwa katika hizo ziara za makaburi. Kwa hiyo hatupingi ziara za makaburi bali tunahimiza kama alivyohimiza Mtume wetu swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam.

Ama suala la Khit'ma (**kusoma Qur'ani kisha kuzipeleka thawabu za kisomo hicho kwa maiti**), suala hili wametofautiana wanachuoni wa Ahlu Sunna juu ya kuwa thawabu zake zinamfikia maiti au laa. Imamu Maaliki na Imamu Shaafiy na wengineo katika wanachuoni wa Ahli Sunna wao wanaona kuwa thawabu hizo hazimfikii maiti. Kwa ushahidi zaidi soma kauli hii ya Imamu An-Nawawiy aliyefariki

mwaka 676 Hijiriyya, alipokuwa akiisherehesha hadithi isemayo; atakapokufa mwanadamu yamekatika matendo yake akasema;

"وأما قراءة القرآن وجعل ثوابها للميت والصلاة عنه ونحوهما فمذهب الشافعي والجمهور أنها لا تلحق الميت."

"Ama kusoma Qur-ani na kuzipeleka thawabu zake kwa maiti na kumswalia na mfano wa hayo, katika madhehebu ya Shaafiy na Jumhuuri (wengi katika wanachuoni) thawabu zake hazimfikii maiti.⁴" Naye Imamu Al-Hattwabiy, mmoja kati ya wanachuoni katika madhehebu ya Maalik anasema;

"والمشهور من مذهب إمامنا الشافعي وشيخه مالك والأكثرين كما قاله النووي في فتاويه وفي شرح مسلم أنه لا يصل ثواب القراءة للميت." انتهى . مواهب الجليل (٦٢٧/٢).

"Na kauli mashuhuri katika madhehebu ya Imamu wetu Shaafiy na Sheikh wake, Imamu Maalik, na wengi ni kama alivyosema An-Nawawiy katika fat'wa zake katika Sherhe ya (sahih) Muslim, ni kuwa thawabu za kisomo hazimfikii maiti.⁵" Je, Bwana AbdulRazaq na hawa nao ni Mawahabi kwa sababu hawasomi Khitma?

Ama suala la kutosoma maulidi, hilo si jambo la kututoa sisi katika duara la Ahlu Sunna wal-Jamaa, kwa sababu hizi zifuatazo;

Kwanza; ni kutokana na jambo lenyewe lilivyo mbele ya hao wenye kusoma maulidi, wao wenyewe wanasema; maulidi ni ADA tu, na si katika IBADA kabisa, amesema **Sheikh Muhammad Ibn Abi Bakar⁶** katika kitabu chake **As-Swaai'qatul-Muhriqah**, ukurasa wa 22, akimnukuu **Sayyid Muhammad Ibn Alawiy Al-Maalikiy**;

"إِنَّا نَقُولُ وَقَدْ قُلْنَا مِنْ قَبْلُ؛ إِنَّ الاجْتِمَاعَ لِأَجْلِ الْمَوْلِدِ النَّبَوِيِّ الشَّرِيفِ مَا هُوَ إِلَّا أَمْرٌ عَادِيٌّ، وَلَيْسَ مِنَ الْعِبَادَةِ فِي شَيْءٍ، وَهَذَا مَا نَعْتَقِدُهُ وَنَدِينُ اللهُ تَعَالَى بِهِ..."

"Kwa hakika sisi tunasema, na tumeshasema kabla ya hapo; kukusanyika kwa ajili ya maulidi ya Mtume mtukufu, halikuwa ila ni jambo la kiada (kawaida) tu, na wala

⁴-Tazama Al-Minhaaj Sharhu Muslim Ibn Al-Hajjaaj, juzuu 6 ukurasa wa 94.

⁵-Mawaahibul-Jaliil, juzuu 2 ukurasa wa 627.

⁶-Sheikh Muhammad Ibn Abi Bakar, ni mmoja miongoni mwa wanafunzi wakubwa wa Sheikh Muhammad Ibn Ayyuub, na hivi sasa ndiye Mudiir wa **Ma'ahad Shamsil-Ma'arifi**, iliyopo jijini Tanga-Tanzania.

si katika dini kabisa, na hivi ndivyo tunavyoitakidi na kumuabudu Allah Ta'ala kwayo."

Sasa Bwana AbdulRazaq! Hivi kweli kwa akili yako, mtu anaweza kutolewa katika msimamo wa dini kwa kuacha au kupinga jambo ambalo halihusiani na dini kwa Ndewe wala Sikio?

Pili, ni kauli za wanachuoni wa Ahlu Sunna zenye kukemea na kutahadharisha juu ya baadhi ya vitendo vinavyofanywa kwenye maulidi na hao wanaoyasoma. Amenukuu Imamu Al-Qurtubiy katika tafsiri yake kutoka kwa Imamu Abu Bakar At-Twurtuushiy, aliulizwa kuhusu watu wanaokusanyika sehemu moja, wakawa wanasoma Qur'ani, kisha mwimbaji anaimba mashairi (Kaswida), pia wanapiga Dufu na Nai, kisha wanacheza, je itafaa kuhudhuria katika hafla zao au laa?

فأجاب: مذهب الصوفية؛ أن هذه بطالة وضلالة، وما الإسلام إلا كتاب الله وسنة رسول الله صلى الله عليه وآله وسلم، وأما الرقص والتواجد، فأول من أخذ به أصحاب السامري، لما اتخذ لهم عجلا جسدا له خوار، فأتوا يرقصون حوله ويتواجدون وهو- أي الرقص- دين الكفار وعباد العجل، وإنما كان مجلس النبي صلى الله عليه وآله وسلم مع أصحابه كأنما على رؤوسهم الطير والوقار، فينبغي للسلطان ونوابه أن يمنعوا من الحضور في المساجد وغيرها ولا يحل لأحد يؤمن بالله وباللوم الآخر أن يحضر معهم ويعينهم على باطلهم. هذا مذهب الإمام الشافعي ومالك وأبي حنيفة وأحمد وغيرهم وأئمة المسلمين) أه.

"Akajibu; katika madhehebu ya Masufi, hii ni batili na ni upotofu, haukua uislamu isipokuwa ni kitabu cha Allah na Sunna za Mtume wake swalla Ilaahu alayhi wasallam. Ama kucheza na kupandisha midadi, wa mwanzo waliozusha ni wafuasi wa Saamiriy, walipotengeneza ndama mwenye kuunguruma, wakaanza kucheza kando kando yake, na huko (kucheza) ni dini ya Makafiri, wenye kuabudu ndama...inatakiwa kwa mtawala na manaibu wake kuwazuia watu hao kuhudhuria misikitini na sehemu nyinginezo (kwa ajili ya kufanya mambo hayo), na si halali kwa yeyote anayemwamini Allah na siku ya mwisho kuhudhuria pamoja nao, na wala asiwasaidie juu ya batili yao (hiyo). Haya ndiyo madhehebu ya Imamy Shaafiy,

Maalik, Abu Hanifa, Ahmad na wengineo katika wanachuoni wa kiislamu.⁷ Kisha akasema Imam Ibn Hajar Al-Haithamiy:

"فتأمله واحفظه فإنه الحق وغيره باطل الذي غايته القطيعة والائتمام"

"Yazingatie (maneno haya) na uyahifadhi, kwani hiyo ndiyo haki, na yasiyokuwa hayo ni batili ambayo mwisho wake ni kukatana na kupata madhambi.⁸"

Bila shaka kwa maelezo hayo tuliyoyatoa umefahamu kuwa, si Shia wala Sufi aliye na uwezo wa kututoa kwenye duara la Ahli Sunna wal-Jamaa, kwa sababu hatusomi Maulidi, Khitma na kuyapinga baadhi ya mambo yaliyozushwa katika dini. Kisha akasema tena Bwana AbdulRazaq katika ukurasa huo huo;

"Isitoshe Mawahabi vilevile wamepora historia ya Sunni na Shia katika nchi hii na kuifanya kuwa ni historia yao, siku hizi wanajifaharisha na historia ya harakati za Mufti wa zamani Sheikh Hasan bin Ameir, Sheikh Hasan alikuwa ni wahabi?"

MAJIBU YETU

Majibu dhidi ya maneno yake hayo, hayahitaji lazima uwe Sheikh au Profesa, bali akili ya kawaida tu inatosheleza kuujuu udhaifu wake na kugundua kuwa Mshia huyu anazungumza kwa msukumo wa chuki na uadui.

Kwanza, ni Wahabi gani huyo aliyedai kuwa Sheikh Hassan bin Ameir naye alikuwa ni katika Mawahabi?

Pili, Bila shaka Sheikh Hassan bin Ameir ana mema na mazuri aliyoyafanya, ambayo yanawafanya watu kumtaja kwa sifa nzuri, na hivyo si vibaya kama anastahiki, na ikawa hakupatikani ndani yake upotoshaji wa haki kwa kufanya hivyo.

⁷ - Tazama tafsiri ya Al-Qurtubiy juzuu ya II ukurasa wa 212-213, iliyochapishwa na Dar Al-Kitabil-Arabi, Beirut-Lebanon.

⁸-Tazama kitabu chake 'Kaffu Ar-Rua'l' ukurasa wa 76, iliyochapishwa na Dar Al-Kutubi Al-Ilmiyyah, Beirut-Lebanon.

Na hakuna mtu yeyote mwenye akili timamu atakayesema kuwa ukimsifu mtu kwa mema aliyoyafanya, basi tayari umeshadai kuwa yuko katika madhehebu yenu? Kwa hiyo, alichotakiwa kukifanya Bwana AbdulRazaq ni kututajia huyo Wahabi aliyefanya hivyo, pamoja na kuyadhihirisha madai yake kielimu. Ama kurusha maneno hewani na kuwatuhumu watu bila ya hatia, si katika mwenendo wa watu waadilifu.

Kisha Mshia huyo akaendelea na maswali yake ya aina hiyo, na akamalizia kwa lugha za uongo na utovu wa adabu, akasema katika ukurasa wa (viii):

"Ndugu msomaji, katika kitabu hiki utagundua kuwa kijana huyo kama ilivyo ada ya vijana wa kiwahaabi alivamia kwa pupa mambo asiyoyajua na ambayo walimu wake hawakujaribu kuyafanya kwa sababu wanajua matokeo ya kuyavamia mambo hayo. Walimu wake wanamtambua kijana huyo kama kijana mdogo anayetaka ukubwa kabla ya elimu na umri kufika! Alaa kulli haali, hayo ni yao wenyewe. Ustadh Ja'afar Mwazoa amejandaa kwa safari ndefu ya kumwelimisha kijana huyu yale yote yaliyo nje ya upeo wa akili yake finyu na utovu wa adabu kwa viongozi wa kidini."

MAJIBU YETU

Kwanza, ninasema; Al-hamdulillaahi, ninamshukuru Allah kuwa sikukurupuka katika uandishi wa kitabu changu '**Uyahudi nyuma ya pazia la Ahlul-Baiti**', bali ni mkusanyiko wa tafiti za kielimu zilizoiweka wazi madhehebu ya Shia na kuiweka katika uhalisia wake, na hiyo ndiyo sababu iliyowafanya Shia, vijana na wazee wao wababaike na hatimae kuandika vitabu ambavyo havina kima katika ulimwengu wa wasomi. Na hili litakubainikia ukisoma kitabu chetu hiki kwa umakini, Insha-Allah. Ama kauli ya Mshia AbdulRazaq aliposema; "*Walimu wake wanamtambua kijana huyo kama kijana mdogo anayetaka ukubwa kabla ya elimu na umri kufika...*" Bila shaka haya ni maneno ya uongo yenye utovu wa adabu. Labda nikuulize Bwana AbdulRazaq; ni Waalimu wangu wapi hao waliosema maneno hayo? Kwa sababu mimi nimesoma **Madrasat Shamsiyya**-Tanga kwa miaka takriban kumi, kuanzia

katika Far'u (Tawi) la Madrasat Shamsiyya Pongwe kwa Ustadh wangu **Imamu Ibn Kassim** hadi makao makuu kwa **Sheikh Muhammad Ibn Ayyuub** –Allah amrehemu na amsamehe makosa yake-.

Na walionisomesha hapo, wengi wao bado wako hai, kama vile; **Sheikh Muhammad Ibn Abi Bakar**, ustadh **Yusuf Ibn Abdillahi** (Subkiy) **Ustadh Seif Ibn Hasan**, **Ustadh Suruuru Ibn Raashid Az-Zak'waniy** na wengineo –Allah awalipe kila la kheri na atuongoze sisi na wao kwenye njia ya haki-, kisha nikajiunga na **masomo ya Thanawi katika chuo cha Kisauni Islamic Institute**, Mombasa-Kenya.

Baada ya hapo nilijiunga na **Daarul-Hadiithi Dammaaj**-nchini Yemen, kwa **Sheikh Muqbil Ibn Haadi Al-Waadi'y** –Rahimahullaahu wa rafa'a darajatahu fil-Iliyyiina-, kisha nilichaguliwa kujiunga na **Islamic University of Madina**, faculty of Hadith (Prophet's Tradition) & Islamic Studies, katika mji mtakatifu wa Mtume swalla llaahu alayhi waalihi wasallam (Madina) KSA.

Ni mwalimu wangu gani aliyenisomesha katika sehemu hizo nilizokutajia aliyenituhumu kwa tabia ya kutaka ukubwa, na kwa munasaba upi? Hebu nitajie japokuwa mmoja tu, ukiwa wewe ni katika wenye kusema ukweli!

Ama aliposema kuwa mimi ninadai ukubwa kabla ya elimu na umri kufika, hiyo ni kauli ambayo aghlabu inatoka kwa watu wenye maradhi ya husda na chuki. Au kwenu nyinyi Mashia mtu yeyote akisimama kuwajibu na kubainisha ubaya wa fikra zenu na itikadi zenu chafu, tayari mtu huyo amedai ukubwa? Kwani wewe Bwana AbdulRazaq ulitaka nifikishe miaka mingapi ndio nianze kubainisha upotevu wa Mashia?

Ama kuhusu matusi yake aliposema; "Ustadh Ja'afar Mwazoa amejiandaa kwa safari ndefu ya kumwelimisha kijana huyu yale yote yaliyo nje ya upeo wa akili yake finyu na utovu wa adabu kwa viongozi wa kidini."

Kuhusu safari ndefu ya mwanafunzi wako Jaafar Mwazoa, mimi ninasema; ni kweli wewe na mwanafunzi wako bado mna safari ndefu ya kuufikia ukweli na kuisibu haki. Na hilo si rahisi kwenu kutokana na njia mlioichagua, mmeichagua njia ya

Maghulaati na Wazandiki mkaifanya kuwa ndiyo dini, huku mkizidanganya nafsi zenu kuwa mmekamatana na njia ya Ahlul-Baiti, hivyo basi ni muhali kufika.

Ama suala la mimi kuelimishwa na Mwazoa au yeye kuelimishwa na mimi, hilo si jambo la ajabu katika ulimwengu huu, hasa kama uwezekano wa kufanya hivyo upo, lakini kwa mtu mwenye akili timamu na heshima, hapati la kujifunza kutoka kwenye kitabu chake zaidi ya matusi na matao (majivuno).

Ama kuhusu matusi uliyonitukana kwa kuniambia kuwa; upeo wa akili yangu ni finyu, na nina utovu wa adabu kwa viongozi wa kidini⁹, hapa sina la kukujibu zaidi ya kukwambia kama nilivyomwambia mwanafunzi wako;

شَاتَمَنِي عَبْدُ بَنِي مِسْمَعٍ فَصُنْتُ عَنْهُ النَّفْسَ وَالْعَرِضَا
وَلَمْ أُجِبْهُ لاحتقاري له ومن يعص الكلب إن عصًا

Amenitukana mtumwa wa banii Mis'mai *** Nikajikinga naye nafsi na heshima.
Mimi sikumjibu kwa kumdharau *** Kwani ni nani amng'atae mbwa akimng'ata!

7- CHOZI LA UONGO JUU YA WITO WA UMOJA

Miongoni mwa nyavu za Shia walizozitega ili kuwanasa wajinga na wachache miongoni mwa wenye tamaa katika Ahlu Sunna, ni kauli mbiu ya UMOJA wa Kiislamu. Na ukweli ni kwamba Shia hawataki umoja, bali wanachokitaka ni kuitumia mbinu hii kuwaingiza Ahlu Sunna kwenye kufu za Ushia.

Chozi hilo la uongo linabainika kwa sababu hizi zifuatazo:-

Sababu ya kwanza; ni tofauti zetu juu ya mapokeo ya dini na tafsiri ya mapokeo hayo. Sisi Ahlu Sunna wal-Jamaa tumeipokea dini yetu kupitia kwa Maswahaba watukufu wa Mtume Muhammad swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam, na tunaitakidi kuwa wao ni watu wema, tena waadilifu.

Ambapo Shia, wao hawaoni hivyo, bali wanawatukana Maswahaba hao na kuwakufurisha, kwa kudai kuwa Maswahaba wote waliritadi na kurudi kwenye ukafiri baada ya kifo cha Mtukufu Mtume swalla Ilaahu alayhi wasallam.

⁹-Hapa anawakusudia masheikh wao wawili, ambao ni watukanaji wa kubwa, wanaowatukana Maswahaba wa Mtume swalla Ilaahu alayhi wasallam, nao ni Mzee Omari Mayunga na Mzee Abdillahi Nassir! Kwa Shia ukimsema Mayunga au Abdillahi Nassir kwa kumwita mwongo, utakuwa mtovu wa adabu, lakini ukisema Abu Hureira Mwongo, Abu Bakar na Umar ni madhalimu, Aisha ni hiyo ni alama ya kuwa unawapenda Ahlul-Baiti!!!

Na wao Shia hawakubaliani na mapokezi ya Maswahaba ila yale yaliyopokewa kutoka kwa Ali tu na, na Maimamu wanaotokana na kizazi chake.

Na katika kuendeleza kampeni zao hizo, Shia wanaandika vitabu kwa lugha mbalimbali ikiwemo lugha ya Kiswahili, na kuvichapisha, kisha kuvigawa bure, au kwa thamani ndogo, na hali ya kuwa vitabu hivyo vimejaa matusi na kashfa za wazi dhidi ya Maswahaba hao, ambao Ahlu Sunnat wal-Jamaa wanaamini kuwa ni watu bora, na ni kiunganishi muhimu baina yao na Mtume Muhammad swalla llaahu alayhi waalihi wasallam.

Na mfano wa vitabu hivyo ni; vitabu vya Mayunga, kama Tafsiri yake aliyoiita **Tafsiri yenye kubainisha**, chapa ya kwanza na ya pili, **Taarekh ya Kiislamu**, **Meza ya uchunguzi** na **Zao la Saqiifa**, na vitabu vya Mshia **Tijani Samawi**, na vitabu vya Mshia **Abdillahi Nassir** na vinginevyo, ukivisoma vitabu hivi hupati tabu kuona matusi yao dhidi ya wema hao waliotangulia.

Sababu ya pili; ni kauli za wanachuoni wa Shia lthnaashariyya zenye kuihujumu Qur'ani, kwa kudai kwamba Qur'ani hii tuliyonayo si kamili, kwa sababu walioikusanya ni Maswahaba na wao ni watu madhalimu! Pamoja na wanachuoni hao kutoa kauli hizo za kikafiri, bado watu hao wanatajwa kwa heshima na taadhima kubwa kwa Mashia, na vitabu vyao bado vinachapishwa.

Sababu ya tatu; ni wao kuzikumbatia riwaya chafu za uongo na simulizi za kikafiri zilizojaa Ghuluu (kuvuka mipaka ya dini) na kuzijaza kwenye vitabu vyao vya kutegemewa, asili ya riwaya hizo ni uongo uliotungwa na **Maghulaati na Wazandiki**, ambao ni wafuasi wa Myahudi Abdullahi Ibn Sabai.

Kutokana na utofauti uliopo baina ya misingi ya dini yetu na ile misingi ya dini ya Ushia na muundo wake, ni vigumu au ni muhali kuleta umoja baina yao na waislamu wa Ahlu Sunnat wal-Jamaa bila kukaa na kuzijadili tofauti hizo, kisha wao wakubali kuachana na uzandiki huo, au kila watu wabaki na muelekeo wao, badala ya kumwaga chozi la uongo la kuleta umoja.

Ushahidi kutoka kwa wanachuoni wa Shia juu ya kutowezekana kuleta umoja;-

Nimeyatamka maneno hayo si kwa lengo la kuleta uchochezi, au kupinga umoja wa umma, laa haasha, bali ni kutokana na uhalisia wa mambo ulivyo, na hilo linashuhudiwa na wanachuoni wakubwa wa madhehebu ya Shia lthnaashariyya. Na miongoni mwa wanachuoni wao wenye kutoa ushuhuda huo ni Mshia Ni'matullaahi Al-Jazaairiy aliposema:

"إننا لا نجتمع معهم على إله ولا على نبي ولا على إمام وذلك أنهم يقولون أن ربهم هو الذي كان محمد نبيه وخليفته بعده أبوبكر- ونحن لا نقول بهذا الرب، ولا بذلك النبي، بل نقول؛ إن الرب الذي خليفة نبيه أبو بكر ليس ربنا، ولا ذلك النبي نبينا" اهـ..

"Sisi Shia hatuwezi kuungana pamoja nao (Ahlu Sunna) juu ya Mungu, wala Nabii, wala Imamu, ni kwa sababu wao wanasema kuwa; Mungu wao ni Yule ambaye Mtume wake ni Muhammad na Khalifa baada yake ni Abu Bakar. Sisi (Shia Ith'naashiria) tunasema; hatumuamini Mungu huyo wala Mtume huyo.

Bali tunasema Mungu ambaye Abu Bakar ni Khalifa wa Mtume wake, huyo si Mungu wetu, wala huyo Mtume pia si Mtume wetu.¹⁰"

Swali, ikiwa sisi hatuwezi kuwa kitu kimoja na nyinyi juu ya Allah aliyetuumba, ambaye ndiye Mola wetu mwenye kuabudiwa kwa haki, kwa kuwa Mola wetu sisi si Mola wenu nyinyi, wala Nabii wetu si Nabii wenu nyinyi, sasa twaungana kwenye lipi?

Na mwanachuoni mwingine wa Shia anayeiunga mkono nadharia hii, ni Mshia Murtadha Al-Askariy, alipokuwa akielezea tofauti za kimapokeo baina ya madhehebu za Kiislamu, na athari zake, zikiwemo kugawanyika umma kwenye makundi na madhehebu mengi, akasema;

"Basi je! **Ni vipi itawezekana kuwaunganisha waislamu ikiwa wamo ndani ya hali kama hii ya kutofautiana?** Si hivyo tu, bali miongoni mwao yako mambo wanayohitilafiana, ambayo baadhi yake tumeyataja kama mfano hapo kabla.

Kamwe maafikiano hayawezi kupatikana baina ya waislamu kwa hali kama hii, ambayo ni ya wao kubakia kuwa ni wenye kufuata jitihada za waliopita hapo kabla.

Inawapasa waislamu wakubali kila kundi liuweke wazi mtazamo wake kuhusu Uislamu na tafsiri ya Qur'ani, pia litoe maoni yake juu ya ijthadi

¹⁰- Tazama Al-An'waarun-Nu,maanuyyah cha Ni'matullahi Al-Jazairi juzuu ya 2 ukurasa wa 278.

mbali mbali zilizofanywa na wanachuoni hao waliopita hapo zamani, ambazo chanzo cha kuhitilafiana kinatokana na ijthadi hizo."¹¹ Mwisho wa kunukuu.

Muhtasari wa hoja hii;

- Mshia Murtadha Al-Askariy anaona kwamba ni jambo lisilowezezana kuleta umoja baina ya madhehebu za Kiislamu, na wakati huo huo waislamu bado wamo kwenye tofauti zao.
- Na moja kati ya sababu kubwa anazoziona kuwa ni tatizo kwa waislamu ni kulazimiana kwao na jitihada zilizofanywa na waliowatangulia (Maswahaba na wanachuoni waliokuja baada yao).
- Ufumbuzi, ni lazima wenye kutofautiana wakae pamoja, kisha waziweke bayana tofauti zao, kisha waachane na jitihada za hao waliotangulia.

Ndugu msomaji! Bila shaka, juhudi hizo hazijafanyika, na wala hakuna mpango wa kuziendea. Na kama tulivyoona kwenye maneno ya Mshia Murtadha kuwa umoja huo umefungwa kwa masharti hayo aliyoyataja mbayo hayajatekelezwa bado! Swali, je pale Mashia wanapotuita kwenye umoja, ni umoja uliojengwa kwenye misingi gani?

Ushahidi wa matusi ya Shia dhidi ya Maswahaba;-

Ndugu msomaji! Kama utakumbuka vizuri tumeleeza kwamba sababu ya kwanza iliyopelekea kushindikana kuleta umoja baina ya Shia na Sunni ni tofauti za kimapokeo.

Sunni wanaipokea dini yao kutoka kwa Mtume swalla Ilaahu ayhi wasallam kupitia kwa Maswahaba, kwa hiyo Masunni wanaamini kwamba Maswahaba ni watu bora, waliowaadilifu. Ama kwa upande wa Shia wao wanaona tofauti, bali wao wanaitakidi kwamba Maswahaba wote ni Makafiri isipokuwa wachache. Na katika sehemu hii tutazitaja kauli chache za baadhi ya Wanachuoni wao kwa lengo la kukuthibitishia.

Kauli ya kwanza; amesema Mshia Ni'matullaahi Al-Jazaairiy;

فإن أغلب الصحابة كانوا على النفاق، لكن كانت نار نفاقهم كامنة في زمنه، ولذا قال عليه السلام: "ارتدّ الناس كلهم بعد النبي صلى الله عليه وآله وسلم إلا أربعة: سلمان، وأبو ذر، والمقداد، وعمار. وهذا مما لا إشكال فيه. اهـ.

"Maswahaba wengi walikuwa kwenye unafiki, lakini moto wa unafiki wao ulijificha katika zama zake (Mtume) na kwa sababu hii amesema (Abu Ja'far) a.s; **watu wote waliritadi (walikufuru) baada ya Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam**

¹¹-Tazama Ma'alimu I-Madrasatani, sehemu ya kwanza ukurasa wa 3-4, kilichotarjumiwa na Msabaha Shabani Mapinda, kimetolewa na kuchapishwa na Al-Itrah Foundation Dsm.

isipokuwa watu wanne tu; **Salmaan, Abu Dharri, Miq'dad na Ammar**, na hili ni miongoni mwa mambo yasiyokuwa na utata ndani yake¹²."

Kauli ya pili; amesema Mshia Al-Majlisiy katika kitabu chake '**Bihaarul-An'waari**' akielezea juu ya ukafiri wa Abu Bakar na Umar, na kuwalaani:

«أقول: الأخبار الدالة على كفر أبي بكر وعمر وأضربهما وثواب لعنهم والبراءة منهم، وما يتضمن بدعهم أكثر من أن يذكر في هذا المجلد أو في مجلدات شتى، وفيما أوردنا كفاية لمن أراد الله هدايته إلى الصراط المستقيم»

"Habari zinazofahamisha juu ya ukafiri wa Umar na Abu Bakari na mfano wao, na thawabu zinazopatikana katika kuwalaani na kuwafanyia uadui, na habari zilizokusanya bidaa zao ni nyingi sana (kiasi ambacho hatuwezi) kuzitaja kwenye Mjalladi (**Volume**) huu, wala katika Mijalladi mingine mbalimbali, lakini tuliyoyataja yanatosha kwa yule anayetaka kuongoka njia iliyonyooka.¹³"

Kauli ya tatu; Mwanachuoni wa aitwaye Al-Ayaashi amesimulia riwaya kutoka kwa Abu Jaafar, akijibu swali aliloulizwa, ni kina nani Maadui wa Allah? Akasema:

"الأوثان الأربعة ... قال: قلت من هم؟! قال: أبو الفيصل ورمع ونعثل ومعاوية ومن دان بدينهم، فمن عادى هؤلاء فقد عادى أعداء الله."

"Ni masanamu wanne, akasema muulizaji ni kina nani hao (Masanamu wanne)? Akasema Abu Jaafar; ni Abu Faisal, (Abu Bakar), Rumau (Umar), Na'thal (Uthman) na Muawiyah, na wanaofuata dini yao. Atakayewafanyia uadui watu hawa, atakuwa amewafanyia uadui maadui wa Allah.¹⁴" Kisha akasema Al-Majlisiy katika Biharul-An'waari akiifafanua riwaya hii;

"وأبو الفيصل أبوبكر لأن الفيصل والبكر متقاربان في المعنى ورمع مقلوب عمر ونعثل عثمان."

"Abu Faisal ni Abu Bakar, kwa sababu neno Faisal na Bakri yanakaribiana kimaana (katika lugha ya kiarabu) na Rumau, limegeuzwa kutoka kwenye Umaru, na Na'thal ni Uthman."

¹² - Tazama kitabu chake kichafu alichokiita 'Al-An'waarun-Nu'maaniyyah' juzuu ya 1 ukurasa wa 81.

¹³ - Tazama Bihaarul-An'waari juzuu ya 30, ukurasa wa 399.

¹⁴ Tazama tafsiri yake juzuu ya 2 ukurasa wa 122.

Kauli ya nne; mwenye kitabu kiitwacho; **Nafahaatu Al-Laahuti fiy la'ani Al-Jibti wat-Twaaghuuti**, ambaye ni Mshia **Ali Ibn Hilaali Al-Karkiy (Al-Muhaqiqu At-Thaanii)** aliyefariki mwaka 948 Hijiriyya, yeye baada ya kuzitaja riwaya za kuwalaani Abu Bakar, Umar na Uthman na kuwakufurisha akasema;

"وهذا النحو في كتب أصحابنا مما لو تحرى المتصدي لحصره جمع منه مجلدات ولم يأت على آخره، وقد أورد الأمين الضابط الثقة محمد بن يعقوب الكليني في كتابه الكافي من ذلك شيئاً كثيراً، وفيه أحاديث باللعن الصريح، والحث عليه من الأئمة".

"Na mfano wa (kauli) hizi katika vitabu vya wenzetu (Shia), lau kama mtu atapupia kuzikusanya, basi atakusanya Mijalladi na hataweza kufikia mwisho wake, na amezitaja muaminifu, mwenye kudhibiti, Thiqa Al-Kulayniy katika kitabu chake Al-Kaafi sehemu kubwa katika riwaya hizo, na ndani yake kuna hadithi za kuwalaani waziwazi (kina Abu Bakar, Umar na Uthman) na mahimizo ya Maimamu juu ya kufanya hivyo."

Kauli ya tano; amesema tena Al-Majlisiiy;

"وعقيدتنا في التبرئ: أننا نتبرأ من الأصنام الأربعة: أبي بكر وعمر وعثمان ومعاوية، ومن النساء الأربع: عائشة وحفصة وهند وأم الحكم، ومن جميع أتباعهم وأشياعهم، وأنهم شر خلق الله على وجه الأرض، وأنه لا يتم الإيمان بالله ورسوله والأئمة إلا بعد التبرئ من أعدائهم"

"Itikadi yetu katika kufanya uadui; sisi (Shia) tunawafanyia uadui Masanamu wanne; Abu Bakar, Umar, Uthman na Muawiyah, na kwa upande wa wanawake ni wanne; Aisha, Hafsa, Hindu na Ummul-Hakam¹⁵, na wafuasi wao wote, na (tunaitakidi) kwamba wao ndio waovu zaidi miongoni mwa viumbe vya Allah vilivyoko juu ya ardhi, na haitimii imani ya kumuamini Allah, Mitume wake na Maimamu isipokuwa baada ya kuwafanyia uadui (hawa) maadui wao."

Kauli ya sita; Amesema tena Ni'matullaahi Al-Jazaairiy;

«... إنه قد وردت في روايات الخاصة أن الشيطان يغل بسبعين غلاً من حديد جهنم ويُساق إلى المحشر فينظر ويرى رجلاً أمامه تقوده ملائكة العذاب وفي عنقه مائة وعشرون غلاً من أغلال جهنم فيدنو الشيطان إليه ويقول: ما فعل الشقي حتى زاد علي في العذاب وأنا أغويت الخلق وأوردتهم موارد الهلاك، فيقول عمر للشيطان: ما فعلتُ شيئاً سوى أنني غصبت خلافة علي بن أبي طالب. والظاهر أنه استقل سبب شقاوته ومزید عذابه ولم يعلم أن كل ما وقع في الدنيا إلى يوم القيامة من الكفر والتناق واستيلاء أهل الجور والظلم إنما هو من فعلته هذه...»

¹⁵ -Ummu-Hakam Bint Abi Sufyan, aliyekuwa mke wa I'yaadh Ibn Ghanmi, kisha akamtaliki kisha akaolewa na Abdullahi Ibn Uth'man At-Thaqafiy.

"Zimekuja katika riwaya za Khaasa (Shia) kwamba shetani atafungwa minyororo sabini ya chuma cha Jahannam, kisha ataburutwa kupelekwa kwenye uwanja wa hesabu, atatazama (mbele) atamuona mtu mbele yake anakokotwa na Malaika wa adhabu, na hali ya kuwa shingoni mwake ana minyororo mia na ishirini katika minyororo ya Jahannam, shetani atamkaribia na atasema; amefanya nini muovu huyu mpaka akanizidi katika adhabu na hali mimi nimewapoteza viumbe wote na nimewaingiza katika sehemu za maangamivu! Umar atasema kumwambia shetani; sikufanya kitu chochote zaidi ya kuupora Ukhalifa wa Ali Ibn Abi Twalib. Dhahiri ni kuwa ataiona ndogo sababu ya uovu wake na kuzidi kwa adhabu yake, lakini hajui kuwa kila lililotokea duniani mpaka siku ya Kiama, miongoni mwa ukafiri, unafiki, kutawala watu waovu, madhalimu ni kutokana na kitendo chake hiki...¹⁶"

Uchambuzi mfupi juu ya kauli hizi:-

Kwa mujibu wa kauli hizi za Maulamaa wa Shia lth'naashariyya ni kwamba Maswahaba wote wa Mtume Muhammad swalla llaahu alyhi waalihi wasallam ni Makafiri na Wanafiki. Ama kwa upande wa Ahli Sunna, wao wanaamini na kuitakidi kwamba Maswahaba wote ni waadilifu na wao ndio walioipokea dini kutoka kwa Mtume swalla llaahu alayhi waalihi wasallam, na Uislamu huu walionao Masunni tangu hapo zamani hadi leo ni mafunzo yaliyopokewa kutoka kwa hao Maswahaba ambao kwa Shia ni Makafiri wenye kustahiki laana!!!

Je inawezekana vipi kwa Shia kutafuta umoja na watu ambao wanawaitakidi kuwa dini yao wameichukua kutoka kwa watu Makafiri? Kama wao wako tayari kwa hilo – na huo ni uongo- basi wajue wazi kwamba sisi Ahlu Sunna hatuko tayari kuungana na watu wanaowakufurisha, na kuwalaani watu bora kwetu.

Bali sisi tunaamini kwamba misimamo yao hii ni miongoni mwa athari mbaya alizozipandikiza Myahudi Ibn Sabai na wanafunzi wake waovu. Na kwa sababu hiyo umoja baina yetu na wao ni muhali mpaka waachane na misimamo hiyo na mingineo ya kikafiri na warudi kwenye Uislamu sahihi.

¹⁶ -Tazama Al-An'waaru An-Nu'maaniyyah juzuu 1 ukurasa wa 18-28.

Jaafar Mwazoa alivyouchangua wito wa umoja;-

Miongoni mwa ushahidi wa wazi wa kuonesha kwamba Mashia hawako tayari kuwa katika umoja na Masunni, bali wanawataka Masunni wawe kama Mashia katika kuwachukia, kuwatukana na kuwalaani Maswahaba, ni kitendo cha utovu wa adabu kilichofanywa na mwandishi wa kitabu '**Shimo refu**', Jaafar Mwazoa, kijana huyu amekosa haya, akatamka wazi wazi kwa kinywa kichafu; "**Usunni huu unaozungumziwa hapa ni Usunni wa Mal'uun Muawiya Bin Abi Sufiyaan,..**"

MAJIBU YETU

Ninasema; sisi tunajua kuwa Mashia ni mahodari sana wa kutukana na kuwalaani Maswahaba wa Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam, kwa kuwa dini yao imejengwa juu ya misingi hiyo, lakini Bwana Mwazoa umeshindwa kuzizuia hisia japo kwa kufanya Taqiyya wakati wa kulingania huo umoja?

Hivi Mwazoa hujui kwamba hao Ahlu Sunna unaowalingania kwenye huo umoja hewa wanamuheshimu Muawiya na Maswahaba wengine radhia Ilaahu an'hum, na kuwazingatia kuwa ni watu bora baada ya Mitume wa Allah? Sasa kuwatukana hao ni kujenga huo umoja mnaoulingania au ni kuubomoa?

Hivi kama ni wewe Jaafar Mwazoa, kweli utakubali mtu akwambie; mimi ninataka urafiki na wewe na ninakupenda sana, lakini ninamchukia sana baba yako!!!

Kwa sababu baba yako ni MAL'UUNI! Kisha haachi kumtaja baba yako kwa ubaya kila anapopata fursa ya kufanya hivyo. Kama wewe ni mtu mwenye akili timamu, utaukubali urafiki wa aina hiyo? Au babako ni bora zaidi kuliko Maswahaba?

Ukweli ni kwamba, juhudi zenu zote mlizozitoa kwenye kitabu chenu '**Shimo Refu**' za kuwaita watu kwenye huo umoja wa uongo, zimeporomoshwa na ibara yako hii moja tu uliposema; "MAL'UUNI MUAWIYA.." kwa sababu mmeshindwa kuificha agenda yenu ya siri.

Hivi mnadhani kuwa mnaweza kuwadanganya waislamu kwa kuwaambia Muawiyah radhia Ilaahu an'hu ni Swahaba wa ki-Wahabi? Ni dharau ya kiasi gani hiyo kwao, au mnadhani kuwa wao ni watu Mabahau kiasi cha kuwabadilishia Almasi kwa Kokoto!

Katika kitabu chetu **Uyahudi nyuma ya pazia la Ahlul-Baiti** tumeelezea namna baadhi ya Masunni walivyotoa juhudi zao kwa Ikhlasu kwa ajili ya kuleta umoja baina ya Ahlu Sunna na Shia, lakini Mashia hawakuwa tayari, bali katika kipindi hicho Shia waliendelea kuandika na kuchapisha vitabu vyenye kuwatukana na kuwakufurisha Maswahaba! Na jambo hilo likawa kikwazo juu ya kupatikana umoja huo, na hiyo ndiyo sababu iliyotupelekea kusema hilo ni; CHOZI LA UONGO JUU YA WITO WA UMOJA.

Harakati za kuleta umoja baina ya Shia na Sunni:-

Katika kitabu chetu **Uyahudi nyuma ya Pazia la Ahlul-Baiti** nilizungumzia juu ya harakati za kuleta ukaribu na umoja baina ya Ahlu Sunna na Shia lth'naashariyya, nikasema hivi;

Mnamo mwaka 1364 Hijiria, sawa na mwaka 1947 AD, walikusanyika baadhi ya wanachuoni wa kiislamu katika mji wa Cairo nchini Misri, kwa lengo la kuunda chombo kimoja kitakachozikurubisha madhehebu mbili kubwa; Ahlu Sunna na Shia lth'naashiria.

Miongoni mwa wanachuoni hao kwa upande wa Ahlu Sunna ni;

1. Sheikh Mah'moud Shiltuuti aliyekuwa Mufti wa Azhar kwa wakati huo.
2. Sheikh Abdul-Majid Saliim.
3. Sheikh Mustafa Abdul-Rzaaq.

Na kwa upande wa Shia lth'naashiria ni;

1. Sheikh Muhammad Taqiy Al-Qummi.
2. Sheikh Abdul-Husein Sharafud-Din Al-Musawiy.
3. Sheikh Muhammad Hasan Buroujurdij.

Jambo hili lilipokelewa na Maulamaa wengi wa Ahlu Sunna kwa moyo mkunjufu kwa kuudhania dhana njema upande wa pili, lakini kumbe mambo si kama walivyodhania.

Dr. Mustafa As-Sibaa'i'y ni miongoni mwa wanachuoni wa upande Ahlu Sunna waliokuwa wakiliendea mbio suala hili la umoja na kuleta ukaribu baina ya pande hizi mbili, yeye binafsi anatumaelezea haya yafuatayo;

"Mnamo mwaka 1953, nilimtembelea Abdul-Husein Sharafud-Din nyumbani kwake katika mji mwa Sour uliopo Jabal Aamil (Lebanon), walikuwepo hapo baadhi ya Maulamaa wa Shia, tukazungumzia umuhimu wa kuunganisha neno letu na kutangaza upendo baina ya makundi mawili ya Shia na Ahlu Sunna, na miongoni mwa sababu kubwa zitakazo pelekea hilo, ni kutembeleana Maulamaa wa pande mbili, na kutoa vitabu ambavyo vinalingania kwenye ukaribu.

Abdul-Husein alikuwa amehamasika sana na fikra hiyo, na yakatimia maafikiano ya mkutano utakaowakusanya Masunni na Mashia ili kutimiza lengo hili.

Nikatoka kwake nikiwa nina furaha sana, kwa sababu nimelifikia lengo. Kisha nikaelekea Beirut na nikawatembelea wakuu mbali mbali wa Shia; wanasiasa, wafanyabiashara na malenga kwa ajili ya kutimiza lengo hili hili, lakini hali ndiyo iliyonizuia kuitimiza fikra hii.

Haukupita muda mrefu, nikashtukizwa na kitabu alichokitoa Abdul-Husein kuhusu Abu Hureira, kilichojaa matusi (dhidi ya Abu Hureira)!!..Kisha akasema; "Kwa kweli nimeshangazwa na msimamo wa Abdul-Husein na maneno yake!

Na huo ni msimamo ambao hauoneshi kuwa Maulamaa wa Shia ni wa kweli katika kuleta ukaribu, wamejenga vituo kwa ajili ya wito huu, wameanzisha magazeti na wamewaajiri baadhi ya Maulamaa wa Azhar kwa ajili ya kuitimiza lengo, lakini hatuioni athari hiyo ya ukaribu kwa Maulamaa wa Shia waliopo Iraq, Iran na miji mingine. Jamaa hawa bado wanaendelea na msimamo wao uliopo katika vitabu vyao, kwa kuwatukana Maswahaba na kuleta taswira ya uongo dhidi ya hali waliyokuwa nayo Maswahaba katika kutofautiana, **utadhani kwamba makusudio ya ukaribu huo, ni kuwaingiza Ahlu Sunna katika Ushia, na si kuzifanya madhehebu hizi mbili kuwa karibu.**"¹⁷ Mwisho wa kunukuu.

Ndugu msomaji! Kabla ya Dr. Mustafa As-Sibai kutoa juhudi hizo, alisimama Sheikh Muhibbud-Din Al-Khatibu kuipinga fikra hii, lakini kwa wakati ule alionekana kuwa ni mtu asiyeutakia mema uislamu kwa kuipinga umoja huo. Sheikh Muhibbud-Din aliona mbali, baada ya kuvidurusu vitabu vya kishia na kuzijua itikadi zao, aligundua kwamba haiwezekani Shia na Ahlu Sunna kuwa pamoja.

¹⁷-Tazama kitabu "**As-Sunnatu wa makaanatuha fit-Tash'ri'il-Islami**" ukurasa wa 10-12 chapa ya Al-Maktabul-Islaami ya mwaka 1985, na ukurasa wa 23-26 chapa ya Dar Al-Warrak ya mwaka 2003.

Sheikh Muhibbud-Din Al-Khatibu aliipinga fikra hiyo kwa kuandika kitabu maarufu kwa jina la "Al-Khutuutu Al-A'ridha". Alibainisha katika kitabu hicho namna ilivyokuwa muhali kuziunganisha madhehebu hizi mbili; Shia na Ahlu Sunna, na miongoni mwa sababu alizozitoa; ni imani ya Shia juu ya kupotoshwa Qur'ani na kuamini kwamba kuna Qur'ani nyingine iliyokamilika zaidi ya hii tuliyonayo. Je, Sheikh Muhibbud-Din aliwazulia uongo Shia au ni hakika? Kitabu hiki kimethibitisha ukweli wa jambo hilo kwa hoja za kielimu.

Na mwisho ninathubutu kusema; mtu yeyote anayelingania umoja baina ya Shia na Ahlu Sunna, atakuwa ima haujui Ushia, au ni kibaraka anayetumikia njama za siri kwa lengo la kuuhujumu Uislamu."

Haya ndiyo niliyoyasema katika kitabu chetu Uyahudi nyuma ya pazia la Ahlul-Baiti, lakini maneno haya hayakupata majibu yoyote, zaidi ya kukithirisha kumwaga chozi hilo la uongo juu ya kuleta umoja, lakini wakati huo huo wa kumwaga chozi la uongo, uhalisia unawafichua kwamba wao hawako katika ukweli, kwa sababu vitabu hivyo hivyo walivyoviandika kwa lengo la kujidai kulingania umoja vimejaa matusi dhidi ya Maswahaba wa Mtume swalla llaahu alayhi waalihi wasallam!

SURA YA PILI

AHLU SUNNA WAL-JAMAA

Ni nani Ahlu Sunna wal-Jamaa?

Neno Ahlu Sunna linatumika kwa maana mbili kuu:

Maana ya kwanza, ambayo ni maana pana, nayo ni:- *Ahlu Sunna ni Muislamu yeyote ambaye si Shia wala Ibadhi, anayeukubali na kuukiri Ukhalifa wa makhalifa wanne waongofu kwa kumtanguliza Abu Bakar Siddiq, kisha Umar Ibnul-Khattwabi, kisha Uthmani Ibn Affaan, kisha Ali Ibn Abi Twalib -radhia Ilaahu an'hum*.¹⁸

Pia imesemwa kuwa:- Ahlu Sunna ni makundi matatu; **Salafiyyah, Ash'ariyyah na Maaturidiyyah**¹⁹. Na kwa mujibu wa taarifu (definition) hii wanaingia **Salafiyyuun, Ash'ariyyah na Maaturidiyyah** ambao wengi wao ni wafuasi wa madhehebu kuu nne, kama vile; wafuasi wa madhehebu ya **Abu Hanifa, Maalik, Shaafiy na Ahmad Ibn Hanbali** -rahimahumu Ilaahu-.

Maana ya pili:-Maana ya pili ya matumizi ya neno Ahlu Sunna, ambayo ndiyo maana sahihi, ni ile taarifu iliyotolewa na baadhi ya wanachuoni kwamba:-

"Ahlu Sunna wal-Jamaa ni Muislamu yeyote anayeshikamana na kitabu cha Allah na Sunna sahihi za Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam, na akafuata njia ya wema waliotangulia, njia ya Maswahaba, Taabi'ina na njia ya Maulamaa waongofu waliokuja baada yao, kama vile; Abu Hanifa, Maalik, Shaafi, Ahmad Ibn Hanbal, Abdullahi Ibn Mubaarak, Awzaai'y, Bukhari, Muslim, Abu Daud, Tirmidhiy na wengineo katika wanachuoni wa Fiq'hi na Hadithi.

¹⁸ -Tazama maelezo ya Ibn Taymiyyah katika kitabu chake '**Minhaajus-Sunna**' juz 1 uk 121 Pia tazama kitabu '**Lawaamiu An-waaril-Bahiyyah**' cha Imamu As-Safaariniy, juzuu ya 1 ukurasa wa 73.



Na akajiepusha na mambo ya uzushi katika dini, vile vile akaamini Qadari, na Majina ya Allah na Sifa zake kama walivyoamini Salaf Swaalih, bila ya kufanya Ta'wiil, wala Ta'twiil (kuzipinga), wala Tamthiili (kufananisha), wala Tak'yiif (kuzipa namna), wala Tahriif (kupotosha)²⁰.

Na kwa mujibu wa Taarifu hii wametoka Maturiidiyyah na Ash'ariyyah pamoja na makundi mengine ya bid'a, kwa sababu makundi yote hayo yamekhalifu njia ya Salaf katika masuala ya itikadi, hasa kuhusu Sifa za Allah, na wakafuata njia ya Khalaf. Na hii ndio sababu iliyompelekea mwanachuoni mkubwa wa Kisufi **Sheikh Ahmad Siddiq Al-Ghumariy** (Sheikh wake **Sayyid Hasan Ali As-Sagaaf**) kuwatoa Ash'ariyya kwenye duara la Ahli Sunna na kuwahesabu kuwa ni katika Ahlul-Bida'a, pale aliposema;

"والآية صريحة في أن الأشعرية مبتدعة، زائغون، ومن زعم أنهم أهل السنة والجماعة فهو كافر، مكذب بخبر الله تعالى..."

"Aya inaweka wazi kwamba Ash'ariyya ni Wazushi na ni wapotevu. Na atakayedai kwamba Ash'ariyya ni katika Ahlu Sunna wal-Jamaa, basi huyo ni kafiri! Anayemkadhibisha Allah katika habari zake....²¹"

Bwana huyu ambaye ni mmoja kati ya Wanazuoni wakubwa wa ki-Sufi, pamoja na kwamba yeye si katika hao Mawahabi, bali ni miongoni mwa wapinzani wakubwa wa hao waitwao Mawahabi, lakini yeye kwa mtazamo wake anawaona kuwa Ash'ariyya, ni wazushi na si katika Ahlu Sunna, pamoja na kuwa amepatia katika hilo, lakini sisi hatukabaliani na msimamo wake wa kuwakufurisha watu bila ya hatia.

²⁰-Tazama maelezo kama haya katika vitabu vifuatavyo; i. 'Sharhu Aqidati Twahaawiyyah' cha Ibn Abil-Izzi Al-Hanafiy, ukurasa wa 36. ii. Maj'muu Fatawa ya sheikhul-Islami Ibn Taymiyyah 3/375 iii. Al-Khutab wal-l'tibaar" cha Al-Maq'riziy, juzuu ya 2 ukurasa wa 358-359, chapa ya Maktaba Thaqaaafatid-Diniyyah, Cairo. iv. Al-Intisaaru li Ahlis-Sunnati wal-hadiith, majibu dhidi ya Hassan Ibn farhan Al-Maalikiy, cha Sheikh Abdul-Muhsin Al-Abbad, uk 164.

²¹-Tazama kitabu chake Al-Iqliid ukurasa wa 15.

Amesema tena Al-Ghumaariy:

"والذي كان عليه النبي صلى الله عليه وآله وسلم، وأصحابه: هو العمل بكتاب الله تعالى وسنة رسوله صلى الله عليه وآله وسلم، واعتقاد كل ما جاء فيهما: كما جاء بدون تشبيهه المجسمة ولا تأويل المعطلة المشبهة من المعتزلة والأشعرية، وغيرهما من الفرق الضالة المبتدعة." الأجوبة الصارفة لإشكال حديث الطائفة ص ٧٤ بواسطة ذم الأشاعرة ص ٤١.

"Msimamo aliokuwa nao Mtume swalla llaahu alayhi waalihi wasallam na Maswahaba zake ni; kukifanyia kazi Kitabu cha Allah na Sunna za Mtume wake. Na kuitakidi kila kilichokuja katika (Kitabu na Sunna) kama kilivyokuja humo, bila ya kufananisha kwa Mujassima wala Ta'wiil za wenye kupinga, wenye kufananisha miongoni mwa Mu'tazila, Ash'ariyya na wengineo miongoni mwa watu wa makundi yaliyopotea." Mwisho wa kunukuu.

Mitazamo mingine:-

Pamona na kukutajia mitazamo hiyo miwili juu ya maana ya Ahli Sunna, lakini nataka ufahamu kwamba wapo baadhi ya wanachuoni wa madhehebu ya Ash'ariyyah wamedai kwamba; makusudio ya Ahlu Sunna wal-Jamaa ni wafuasi wa **Abul-Hasan Al-Ash'ariy na Abu Mansuur Al-Maaturiidiy peke yao**²² madai ambayo si sahihi kabisa.

Pia wapo baadhi ya wanachuoni waliowagawa Ahlu Sunnat wal-Jamaa kwa kuzingatia namna ya kuamiliana kwao na maandiko ya Sifa za Allah, wamewagawa kwenye makundi mawili;

1) **Salaf** na 2) **Khalaf**, miongoni mwa wanachuoni hao ni Imamu **Twaahir Ibn Swaleh Al-Jazaairiy**, mwenye kitabu **Al-Jawaahiru Al-Kalaamiyya fiy Idhaahi Al-Aqiidati Al-Islaamiyya**, kitabu maarufu ambacho husomeshwa kwenye vyuo na Madrasa za humu mwetu, Afrika ya Mashariki²³.

²²-Tazama It'haafu Saadatil-Muttaqiin cha Az-Zabidiy, juzuu 2 ukurasa wa 6.

²³-Soma kitabu Al-Jawaahiru Al-Kalaamiyya, kuanzia ukurasa wa 8-11, juu ya sifa za Allah Sub'haanahu wa Ta'alaa.

Baadhi ya majina ya Ahlu Sunna wal-Jamaa:-

1. Ahlul-Hadithi;

Ahlu Sunna wal-Jamaa, wanajulikana kwa jina la **Ahlu-Hadithi** au **As'haabul-Hadithi**. Na sababu ya kuitwa hivyo ni kutokana na kujishughulisha kwao na Hadithi za Mtume swalla llaahu alayhi waalihi wasallam kwa upokezi na kuzifanyia kazi. Ahlu Sunna walitambulika sana kwa jina hili la **Ahlul-Hadithi** katika karne za mwanzo za uislamu²⁴ Na kwa mujibu wa kauli ya Imamu An-Nawawiy katika Al-Minhaaju Sharhe ya Muslim Ibn Hajjaaj, Ahlu Sunna ndio hao hao Ahlul-Hadithi.²⁵

2. Salafiyyuun;

Jina la pili walilotambulika nalo Ahlu Sunna wal-Jamaa, walitambulika kama **Madrasatun Salafiyyatun**, au wafuasi wa madhehebu ya Salaf Swaalih. Na Salaf Swaalih maana yake ni; Wema waliotangulia, miongoni mwao ni; Maswahaba, Taabiina (wanafunzi wa Maswahaba) na walioufuata mwenendo wao kwa wema katika zile karne tatu bora.²⁶

²⁴-Tazama kitabu '**Sharafu As'haabil-Hadiithi**' cha Imamu Al-Khatiibu Al-Bagh'daadiy, ukurasa wa 44, chapa ya Dar Al-Furqaan, 2008, Cairo.

²⁵-Tazama '**Al-Minhaaj Sher'he ya Sahihi Muslimu Ibn Hajjaaj**' ya Imamu Nawawiy juzuu ya 13 ukurasa wa 68-69. Pia tazama **Fat'hul-Bari** ya Al-Hafidh Ibn Hajar juzuu ya 13 ukurasa wa 306.

²⁶-Tazama Kitabu "**IL-Jaamul-Awaami**", kitabu hiki ni katika vitabu vya mwisho katika utunzi wa Imamu Al-Ghazaali, alikiandika kitabu hiki mnamo mwezi wa mfungo tisa mwaka 505 Hijiriyah, kabla ya kufariki kwake kwa muda mfupi, kwa sababu yeye alifariki mnamo siku ya jumatatu, tarehe 14 mwezi wa mfungo tisa mwaka 505 Hijiriyah. Ukweli ni kwamba katika kitabu hiki Imamu Al-Ghazaali amekwenda tofauti na msimamo wake wa ki-Ash'ariyyah na madhehebu ya Khalaf katika kuzifanyia Ta'wiil sifa za Allah, na ameitetea madhehebu ya Salaf kwa kuzithibitisha sifa hizo za Allah kwa dhahiri yake mpaka baadhi ya chapa za asili zimeandikwa juu ya kitabu chake; "**Risaalatun fi Madh'habi Ahlis-Salafi**" (Risala katika madhehebu ya Salaf). Katika waliokithibitisha kitabu hiki kuwa ni cha Imamu Al-Ghazaali ni Imamu Taajud-Din As-Subkiy katika kitabu chake '**Twabaqaatus-Shaafiyyah Al-Kubra**', juzuu ya 6 ukurasa wa 225, pia kimethibitishwa na: **Twaash Kubra Zaadah, Ibn Qadhi Shuhba, Az-Zabidiy** na **Husein Al-Waasitwi** katika kitabu '**At-Twabaqaatul-Aliyyah**'.

Kitabu hiki cha Imamu Ghazaali kimechapishwa Istanbul mwaka 1278 H. halikadhalika kimechapishwa Cairo mwaka 1303 H na mwaka 1309. Na kwengineko.

Mwanzo wa kudhiri jina la Ahlu Sunna wal-Jamaa;-

Inafahamika kwa kila mwenye kuifuatilia historia ya Uislamu kwamba katika zama za Mtume swalla llaahu alayhi waalihi wasallam na zama za Makhaliifa wawili, Waislamu wote walikuwa katika msimamo mmoja kiimani –ukiwatoa Wanafiki-, hakukuwa na makundi yenye imani tofauti, kwa hiyo wote liliwatosha jina la uislamu.

Hali hiyo iliendelea hivyo hadi katikati ya Ukhalifa wa Khalifa wa tatu (Uth'man Ibn Affan radhia llaahu an'hu), na baada ya kuwasili Myahudi Abdullahi Ibnu Sabai, ndipo zilipoanza kujitokeza baadhi ya fikra, na kudhiri makundi tofauti yenye sura za kisiasa, na jambo hilo lilipelekea kuuwawa Khalifa wa tatu Uth'man Ibn Affan radhia llaahu an'hu.

Watu waovu wakiwemo wafuasi wa Ibn Sabai walijificha ndani ya safu za waislamu kwa lengo la kuleta farka, na kuzorotesha harakati za kuueneza Uislamu, na kwa kiasi fulani walifanikiwa na waliwapata baadhi ya waislamu wageni, hasa wale wasio na ufahamu wa kutosha katika dini. Kundi hili liliunga mkono mauaji hayo ya dhulma dhidi ya mtawala huyo na kuona kuwa ni haki yake kuuwawa.

Kundi la pili; ni kundi la Maswahaba, na wengi katika Taabiina, wao hawakukubaliana na mauaji hayo ya kidhalimu.

Kundi kubwa la Maswahaba na Taabiina waliokuwepo **Makka, Madina, Basra, Kufa** na sehemu nyingine isipokuwa watu wa Sham, waliona kabla ya kuchukua hatua yoyote lazima kwanza apatikane kiongozi, kisha Sheria ichukue mkondo wake dhidi ya wauwaji, na hiyo ndiyo ilikuwa rai sahihi.

Na wote kwa umoja wao wakamteua Ali Ibn Abi Twalib radhia llaahu an'hu kuwa Khalifa na wakampa Bai'a (Kiapo cha utifu).

Ama watu wa Sham, wakiongozwa na Swahaba Mtukufu **Muawiya Ibn Abi Suf'yan** radhia llaahu an'huma, wao hawakukubaliana na rai hiyo, bali walishurutisha lazima kwanza washughulikiwe watu waliomuua Uthmani, kisha mambo mengine yaendeleo. Kwa hiyo, wao hawakukubaliana na uteuzi wa Ali na wala hawakuwa tayari kumpa Bai'a.



Baada ya hapo, kulizuka mambo mengi sana, lakini jambo kubwa ambalo halitasahaulika katika historia ya waislamu ni mapigano makubwa yaliyogharimu roho za waislamu wengi sana! Nayo ni mapigano ya "**Siffin**"²⁷ yaliyotokea mwezi wa mfungo tano, mwaka 37 Hijiriyya.

Makundi ya pande hizi mbili, upande wa Ali na upande wa Muawiya, wote walikuwa na itikadi moja tu, walikuwa katika Sunna za Mtume swalla Ilaahu alayhi wasallam na walilazimiana na Jamaa ya Waislamu, na hayakuwa makundi mawili yenye itikadi tofauti, bali tofauti zao zilikuwa ni juu ya wakati gani sahihi wa kuwakamata na kuwasimamishia KISASI watu waliomuua Uthman radhia Ilaahu anhu, je kitangulizwe kisasi kwanza kama wanavyotaka watu wa Sham au ni uteuzi wa Kiongozi kwanza kama walivyotaka Waislamu wote? Na hilo linathibitishwa na Ali Ibn Abi Twalib radhia Ilaahu an'hu pale aliposema;

"بدء أمرنا أنا التقينا والقوم من أهل الشام، والظاهر أن ربنا واحد ونبينا واحد، ودعوتنا في الإسلام واحدة، ولا نستزيدهم في الإيمان بالله والتصديق برسوله، ولا يستزيدوننا، الأمر واحد إلا ما اختلفنا فيه من دم عثمان ونحن منه براء."

"Na mwanzo wa jambo letu, ni kwamba sisi tulikutana na jamaa miongoni mwa watu wa Sham, **na dhahiri ni kwamba Mola wetu ni mmoja, na Nabii wetu ni mmoja, na Daawa yetu katika uislamu ni moja, hatuwazidi wao katika kumuamini Allah, wala katika kumsadikisha Mtume wake, na wala wao hawatuzidi sisi, sote jambo (letu) ni moja tu**, isipokuwa kwa yale tuliyotofautiana kuhusu damu ya Uthmani, na hali ya kuwa sisi tuko mbali na hilo (hatuhusiki)."²⁸

Ndugu msomaji! Hiyo ndiyo hali halisi, hakukuwa na Ushia huu uliopo jana na leo, Waislamu wote walikuwa kwenye msimamo mmoja, walikuwa kwenye mafunzo ya Mtume (Sunna) ama jamaa (Umoja) kwa wakati huu ulitoweka mpaka ilipofanyika Sulhu na watu wakawa chini ya kiongozi mmoja.

²⁷-**Siffiin** ni eneo ambalo liko ndani ya nchi ya Syria ya sasa.

²⁸-Tazama kitabu cha Shia '**Nahjul-Balaagha**' juzuu ya 3, ukurasa wa 648.

Kwa mujibu wa kauli hii ya Ali Ibn Abi Twalib radhia llaahu an'hu inabatilika ile dhana potofu inayoenezwa na baadhi ya wasiofahamu au wenye malengo machafu kwamba vita hivi vilikuwa ni baina ya Masunni wakiongozwa na Muawiya dhidi ya Shia waliongozwa na Ali.

Baada ya kwisha vita vya Siffin kwa kufanyika Sulhu baina ya makindi mawili ya Waislamu yaliyopigana, likadhihiri kundi la **Khawaariji**, kundi hili lilijitenga kutoka kwenye jeshi la Ali radhia llaahu an'hu, likamuasi na kujitoka kwenye Utiifu wake. Na tofauti baina ya kundi hili la Mawakhariji na Waislamu wengine ni tofauti za kiitikadi na si tofauti za kisiasa, na ndio maana Makhawariji walifikia kumkufurisha (kumtoa kwenye Uislamu) na kumuua kila aliyemuunga mkono Ali Ibn Abi Twalib au Muawiya. Na ikawa hiyo ndiyo sababu ya kuzuka vita vya **Nahrwaan** baina ya jeshi la Ali radhia llaahu llaahu an'hu na kundi hilo ovu la Khawaarij.

Kwa ujumla ni kwamba hali ya Waislamu ikawa katika matatizo na misukosuko, fitna zilikithiri, na kila muda ulivyosonga mbele ikawa hali ya mizozo inachukua sura nyingine tofauti na ilivyokuwa kabla ya hapo.

Kwa upande wa jeshi la Ali Ibn Abi Twalib radhia llaahu an'hu lilikuwepo kundi la wauwaji wa Uthmani walioongozwa na Myahudi Ibn Sabai, Myahudi huyu alitumia mizozo hii kama ndiyo kivuli cha kupenyeza itikadi zake za ki-Yahudi, na miongoni mwa itikadi alizozipenyeza ni:-

- 1) **Itikadi ya kuwa Ali ni Mungu** anayestahiki kuabudiwa, lakini madai yake haya hayakufaulu, na hilo ni kutokana na hatua kali alizozichukua Ali dhidi yake na wafuasi wake.²⁹
- 2) **Itikadi ya Ghuluu kwa kumpa Ali na kizazi chake sifa alizostahiki kusifiwa kwazo Allah peke yake.** Wafuasi wake (Sabaiyya) walitunga riwaya nyingi za kumkweza na kumtukuza Ali na kizazi chake nyuma ya pazia la mapenzi kwa Ahlul-Baiti.

²⁹-Tazama katika kitabu '**Al-An'waarun-Nu'maniyyah**', juzuu ya 2 ukurasa wa 234. Pia tazama kitabu cha Kishia; Mikesha ya Peshawar ukurasa wa 28 cha Sultan Waizin Muhammad Al-Musawiy As-Shirazy.

- 3) **Itikadi ya Uwasii wa Ali, na kwamba yeye ni Wasii wa Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam**, na ni Khalifa baada yake. Katika hili pia alifanikiwa, na wafuasi wake walitunga riwaya nyingi mno.
- 4) **Itikadi ya Al-Baraa, Kuwakashifu na kuwatukana Maswahaba**, hasa Abu Bakar, Umar na Uthmani, kwa madai ya kwamba wamemdhulumu Ali haki yake ya Ukhalifa. Na kupitia fikra hizi zilitungwa hadithi nyingi zisizo na mfano.

Baada ya kujitokeza makundi yenye mitazamo na itikadi tofauti na mafunzo aliyoyafunza Bwana Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam, na kinyume na mwenendo wa Jamaa ya Waislamu, wale waliobakia kwenye Sunna na mafunzo ya Mtume waalitwa **Ahlu Sunna** (watu wa Sunna), kwa sababu ya kushikamana na Sunna, na kwa kuwa hawakujingiza kwenye makundi hayo ya uzushi (BID'A).

Na walisifiwa kwa sifa ya **Al-Jamaa** (Jamaa/Umoja), kwa sababu hawakumuasi kiongozi na wala hawakuingia katika makundi maovu, bali walishikamana na umoja wa waislamu kama alivyoamrisha Mtume swalla Ilaahua alayhi waalihi wasallam. Na ama zile tofauti zilizotokea baina yao na kufikia kupigana, hazikuwa za kiitikadi.

Na makundi mengine yalijulikana kama makundi ya **Ahlul-Furqat wal-Bid'a** (watu wa farka na uzushi). Na kudhihiri kwa makundi hayo ya bid'a na fikra za kizushi uongo ulikithiri, **ndipo jina la Ahlu Sunnat wal-Jamaa lilipodhihiri, kama nembo ya waislamu safi waliosimama kwenye mafunzo ya Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam na Makhaliifa wake waongofu radhia Ilaahu anhum.** Amesema Muhammad Ibn Siiriin, ambaye ni mmoja kati ya wanafunzi wakubwa wa Maswahaba, aliyefariki mwaka 110 Hijiriyah:

لَمْ يَكُونُوا يَسْأَلُونَ عَنِ الْإِسْنَادِ فَلَمَّا وَقَعَتِ الْفِتْنَةُ قَالُوا سَمُّوا لَنَا رِجَالَكُمْ فَيُنْظَرُ إِلَى أَهْلِ السُّنَّةِ فَيُؤْخَذُ حَدِيثُهُمْ
وَيُنْظَرُ إِلَى أَهْلِ الْبِدْعِ فَلَا يُؤْخَذُ حَدِيثُهُمْ.

"Watu walikuwa hawaulizii kuhusu sanad (Mtiririko wa wapokezi), lakini ilipotokea fitna wakawa wanasema; tutajieni wapokezi wenu, kisha hutazamwa Ahlu Sunna na kuchukuliwa hadithi zao, na hutazamwa watu wa bid'a na zinarudishwa hadithi zao.³⁰"

Kwa hiyo, neno Ahlu Sunna lilitumika kwa wakati huo kama nembo ya watu waliobakia kwenye mafunzo ya Bwana Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam. Na makusudio ya fitna, ni fitna ya kuuwawa Khalifa Uthmani radhia Ilaahu an'hu mnamo mwaka wa 40 Hijiriyah.

BAADHI YA SIFA ZA AHLI SUNNA WAL-JAMAA

Marejeo yao:-

- i- **Katika Itikadi;** Marejeo ya Ahlu Sunna wal-Jamaa katika mambo ya itikadi, ni **Kitabu cha Allah na Sunna sahihi na kuzitafsiri kama zilizotafsiriwa na Salaf Swalih bila ya Ta'wiil, wala Tahriif (Kupotosha), wala Tamthiil (Kufananisha), na wala hawatumii Qiyasi wala akili katika kumjadili Allah na dhati yake.** Kwa sababu wanaamini kwamba akili haina uwezo wa kuyajadili mambo ya ghaibu.
- ii- **Katika Fiq'hi na Sheria;** Marejeo ya Ahlu Sunna wal-Jamaa katika sheria za dini, ni **Kitabu cha Allah, Sunna sahihi** za Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam, **Ijmai** (Maafikiano ya Maulamaa wa umma) na **Qiyasi** (Kipimo) kilichosahihi.
- iii- Na hawatofautishi baina ya **Hadithi Aahaad na Mutawatiri**, bali hadithi yoyote iliyothibiti kwa njia sahihi zinazokubalika kutoka kwa Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam wanaamini na kuifanyiakazi.

³⁰ - Tazama utangulizi wa Sahihi Muslim, juzuu ya 1 ukurasa wa 11, hadithi nambari 27.

Itikadi yao juu ya Majina na Sifa za Allah;-

Ahlu Sunna wal-Jamaa wanaitakidi kwamba Allah ana Majina mazuri na Sifa zilizotukuka, wanaamini Majina yake na Sifa zake bila ya kumfananishi Allah na yeyote kwa sababu hana mfano, na wala hawapingi chochote katika Majina hayo na Sifa hizo, wala hawafanyi Ta'wiil. Na hawamthibitishii Jina wala Sifa ila vile alivyojisifu mwenyewe katika Kitabu chake au kupitia ulimi wa Mtume wake swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam.

Msimamo wao kuhusu Imani;-

Msimamo wa Ahlu Sunna wanaitakidi kuhusu imani;- imani ni itikadi ya moyoni, kutamka kwa ulimi na vitendo, na imani inazidi kwa utiifu na inapungua kwa kufanya maasia. Msimamo huu ni kinyume na msimamo wa makundi ya upotevu kama vile Murjia wao wanaitakidi kwamba matendo hayaingii katika jina la imani, kwa hiyo maasia yoyote atakayoyafanya mja hayataathiri katika imani yake.

Pia msimamo huu ni kinyume na msimamo wa kundi potovu la Khawaarij, wao wanaitakidi kwamba imani haizidi wala haipungui na kitendo chochote cha maasia atakachokifanya mja kitamsababishia kuingia motoni milele na hatatoka tena.

Msimamo wao kuhusu kuonekana Allah;-

Ahlu Sunna wal-Jamaa wote wanaamini kwamba waumini watamuona Allah huko Akhera kwa macho yao, katika uwanja wa hesabu na katika Pepo.

Imani yao Kuhusu Qur-ani;-

Ahlu Sunna wal-Jamaa wote wanaamini kwamba Qur-ani ni maneno ya Allah, na maneno yake ni Sifa yake na si kiumbe, na mtu yeyote atakayesema Qur-ani imeumbwa huyo kwa Ahli Sunna ni Kafiri.

Imani yao kuhusu Qadar:-

Ahlu Sunna wal-Jamaa wanaamini Qadar (makadirio ya Allah kwa viumbe wake) na haitimii imani ya Qadar isipokuwa kwa kuamini ngazi hizi nne;

- i- Kuamini kutangulia elimu ya Allah juu ya kila kitu, Allah alikijua kila kitu kabla ya kukimba, namna kitakavyokuwa, wakati wake na hatima yake.
- ii- Kuamini kwamba Allah amekiandika kila alichokijua katika Lauhil-Mahfuudhi.
- iii- Kuamini utashi wa Allah juu ya kila kitu, anachokita kitakuwa na asichokitaka hakiwi.
- iv- Kuamini uumbaji wa Allah, na kwamba kila kisichokuwa yeye na Sifa zake basi hicho ni kiumbe cha Allah Jalla Jalaaluh.

Msimamo wao kuhusu Maswahaba:-

Msimamo wa Ahlu Sunna wal-Jamaa kuhusu Maswahaba, wao wanaitakidi kuwa Maswahaba wote ni waadilifu, lakini hawakukingwa kufanya makosa. Na wanaitakidi kuwa Swahaba mbora baada ya Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam ni **Abu Bakar As-Siddiq**, kisha **Umar Ibn Al-Khatwabi**, kisha **Uthmani Ibn Affan** kisha **Ali Ibn Abi Twalib** radhia Ilaahu an'hum.

Hizi ni baadhi ya Sifa muhimu za Ahli Sunna wal-Jamaa, na yeyote mwenye imani iliyokinyume na hizi tulizozielezea hapa, basi huyo si katika Ahli Sunna wal-Jamaa hata kama atajinasibu na kulidai hilo. Kwa hiyo, si kila anayejinasibu na moja kati ya madhehebu nne anakuwa Sunni hata kama atakwenda kinyume na misingi mikuu ya Ahli Sunna, hapana sivyo hivyo.



MJADALA NA MSHIA MWAZOA KUHUSU KAULI YA IBNU SIIRIIN

Baada ya kukupa maelezo kwa muhtasari kuhusu Ahli Sunna wal-Jamaa, kuanzia Taarifu ya neno Ahli Sunna, majina yao, mwanzo wa kudhihiri jina hilo, pamoja na kukutajia baadhi ya sifa na alama zao, katika sehemu hii nitakufungulia mjadala mfupi dhidi ya maneno ya Mshia Jaafar Mwazoa.

Na kwanza nitaanza na upinzani wake aliouleta juu ya kauli ya Ibnu Siiriin inayothibitisha uwepo wa istilahi ya Ahlu Sunna tangu karne ya mwanzo, na si baada ya kuja Abul-Hasan Al-Ash'ariy, kama anavyodai yeye na Mshia mwenzie Bwana Abdillahi Nassir. Amesema Mshia Jaafar Mwazoa kwa ujeuri katika ukurasa wa 37:

"Majibu haya ya Ibnu Mafuta ni ya kipuuzi mno, na yanadhihirisha utupu wake juu ya ujuzi wa historia ya Kiislamu na misukusuko yake. Ndugu mwislamu!! Ahlu Sunna wanaotajwa hapa kwenye naswi ya Ibnu Siiriin ni wale ambao mkabala wao ni Ahlul Bid'a kama maelezo yalivyotaja jambo hilo wazi wazi pale yaliposema: **فَيُنْظَرُ إِلَى أَهْلِ السُّنَّةِ فَيُؤَخَذُ حَدِيثَهُمْ** Wanaangaliwa Ahlu Sunna na kuchukuliwa hadithi yao **وَيُنْظَرُ إِلَى أَهْلِ الْبِدْعِ فَلَا يُؤَخَذُ حَدِيثَهُمْ** Wanaangaliwa Ahlul Bida'i na haichukuliwi hadithi yao.

Kisha akaendelea kusema:

Istilahi mbili hizi za Ahlu Sunna na Ahlul Bid'a ndizo zinazoweza kufichua ukweli wa uhalisia wa kihistoria anaoutaja Mafuta hapa. Sasa je? Ni lini istilahi hizi zilitumika katika mizani ya elimu ya Hadithi? Na je? Ni lini istilahi mbili hizi zilipotea na kutoweka kiasi cha kutoonekana leo katika ulimwengu wa uchambuzi wa hadithi katika Uislamu?"

MAJIBU YETU

Majibu yetu dhidi ya uongo na ufedhuli huu wa Mshia Mwazoa yatakuwa kwenye nukta kuu tatu:

Nukta ya kwanza, ni kuhusu matusi yake alipotukana kwa kusema;

'Majibu haya ya Ibnu Mafuta ni ya kipuuzi mno, na yanadhihirisha utupu wake juu ya ujuzi wa historia ya Kiislamu....

Ninasema;- Hoja na matusi ni vitu viwili tofauti, si kila mtu ana uwezo wa kusimamisha hoja kwa kile anachokitakidi, lakini kila mtu anaweza kutukana, kwa sababu matusi hayaihitajii uwe mwana taaluma. Hivyo basi, pamoja na kwamba naweza kumjibu maneno yake kwa lugha za matusi kama alivyofanya yeye lakini kwa kuchunga heshima yangu na heshima za wasomaji nitajizuia, kufanya hivyo.

Nukta ya pili, ni kuhusu kauli yake aliposema;

"Ahlu Sunna wanaotajwa hapa kwenye naswi ya Ibnu Siiriin ni wale ambao mkabala wao ni Ahlul Bid'a..."

Ninasema; ni kweli hayo ndiyo makusudio ya neno Ahlu Sunna ki-istilahi, ikisemwa Ahlu Sunna wanakusudiwa mkabala wao ni **Ahlul-Bidaa, ambao ni Shia, Ibadhi, Mu'tazila, Qadariyya, Masufi** na wengineo.

Istilahi hiyo ilitumika hivyo hapo zamani na hadi leo bado inatumika hivyo hivyo, na Insha-Allaah itaendelea kutumika hivyo mpaka kitakaposimama Qiyama. Na haitatokea hata siku moja isemwe Ahlu Sunna, halafu makusudio yake yawe ni Shia au Khawaariji, kwa sababu hawa wote ni watu wa bidaa.

Nukta ya tatu, ni kuhusu kauli yake aliposema;

Ni lini istilahi hizi zilitumika katika mizani ya elimu ya Hadithi? Na je? Ni lini istilahi mbili hizi zilipotea na kutoweka kiasi cha kutoonekana leo katika ulimwengu wa uchambuzi wa hadithi katika Uislamu?"

Ninasema; tangu zilipoanza kutumika istilahi hizi karne ya mwanzo, ziliendelea hivyo hivyo bila ya kubadilika, na zitaendelea kutumika hivyo hivyo. Ama madai ya kwamba istilahi hizi zilitumika kisha zikatoweka katika ulimwengu wa uchambuzi wa hadithi, hayo si madai ya kweli, na Mwazoa hana ushahidi wowote wa kielimu unaounga mkono madai yake haya batili. Na ukweli ni kwamba, bado

matumizi ya istilahi hizo yangalipo, na kuna ushahidi mwingi kwenye vitabu vya elimu ya **Jarhu Wa Ta'diil** na elimu za **Rijaali** wenye kuthibitisha hilo.

Kwa hiyo, ninakariri tena kwa kusema; istilahi ya maneno haya; '**Ahlu Sunna**', na '**Ahlul-Bidaa**' iko vile vile kama yalivyotumika hapo awali, na hayajabadilika kama vile ambavyo hazikubadilika istilahi za maneno; **Hanafiyya, Maalikiyya, Shaafiyya, Hanaabila, Zaidiyyah, Ibaadhiyya, Ithnaashariyya na mengineyo**, bali kilichojitokeza ni kuiboresha na kuitanua zaidi istilahi hiyo na matumizi yake kwa kuviingiza vinavyostahiki kuingia au kuvitoe visivyostahiki kuwemo.

Ama juhudi zinazofanywa na baadhi ya wapotoshaji kwa kutaka kuviingiza visivyokuwemo kwa maslahi yao na kutaka kuupotosha ukweli, kama alivyodai Mshia **Tijani Samawi**, kwenye kitabu chake alichokiita; الشيعة هم أهل السنة SHIA NDIO AHLU SUNNA!!!!³¹ Ahli Sunna wamezigundua juhudi hizo chafu na kuweka misingi ya kuibatilisha. Kisha akasema Mshia Jaafar Mwazoa katika ukurasa wa 37;

"Kwanza kabisa namshauri mwanangwa wa Mafuta arejee mlango wa mabaahithul Alfaadhi katika soma la Usuulul fiq'hi, apate kujua -maana hajui- kuwa neno moja laweza kutumika kwa maana tofauti kulingana na zama (maraahili) za kihistoria zilizopitia. Mfano neno Sayyaarah (سَيَّارَة), neno hili limetumika kwenye Qur'an Surat Yusuf aya ya 19 Mola Mtukufu asema:.....وَجَاءَتْ سَيَّارَةٌ..... Ukaja msafara.

Kisha Jaafar Mwazoa akahoji katika ukurasa wa 37-38 kwa kusema;

"Swali ni, je neno Sayyaarah ambalo hufasiriwa kwa maana ya msafara, leo lina maana hiyo hiyo? Au maana yake imebadilika? Bila shaka maana yake imebadilika, leo Sayyarah ina maana ya gari. Au Ibn Mafuta wataka utufasirie hiyo aya hapo juu "likaja gari....." kulikua na gari wakati huo? Na ukisema hivyo utakua wasema maneno ya ajabu kabisa!

³¹-Maajabu ya dunia haya!!! Haya tangu lini Mashia wakawa ni Ahlu Sunna?

MAJIBU YETU

Kwanza, ninapenda kumfahamisha Mshia Mwazoa kwamba suala la mabadiliko katika istilahi za kimaneno kutoka kwenye matumizi ya zamani kwenda kwenye matumizi mapya kulingana na hali za watu na taaluma zao, ni katika masuala ya mwanzo katika fani ya Usuulul-Fiqhi, kwa hiyo kudhania kwamba hilo ni jambo kubwa sana lisilojulikana na watu wengine ni ulimbukeni!

Pili, anatakiwa Mshia Mwazoa afahamu kwamba si kila neno linabadilika matumizi yake kwa sababu ya kurefuka zama na marahili za kihistoria. Hivyo basi, tunamwambia; kuna maneno hayabadiliki hata kama zitapita karne mia mbili. Kwa mfano; maneno kama **Ahlu Sunna wal-Jamaa, Shia Ith'naashariyya, Zaidiyya, Ismailiyya, Ibaadhiyya Hanafiyya, Maalikiyya, Shaafiyya, Hanaabila**, n.k. maana ya maneno haya kiistilahi yataendelea kubakia hivyo hivyo na haitatokea hata siku moja mtu aseme; **Shia Ithnashariyya** halafu ikawa anawakusudia **Maibadhi** au **Shia Zaudiyya**, ila tukubaliane kwamba kuna uwezekano wa kutanuka kwa matumizi ya maneno haya ya kiistilahi, kwa sababu ya kutanuka uwanja wake. Kwa mfano; tangu hapo zamani inaposemwa; Shia Ith'naashariyya, humaanisha kila mwenye kuamini Uimamu wa Maimamu kumi na mbili, na kuitakidi kuwa Maimamu hao ni Maasumun. Na kwa maana hiyo, neno hili liwanaingia Mashia wote wenye imani hiyo bila ya kuwabagua **Usuuliyyuuna** wala **Akhbaariyyuuna**, pamoja na kwamba katika zama za Maimamu wa Shia hadi karne ya kumi moja hijiriyya, hakukuwa na watu waitwao **Usuuliyyuuna** wala **Akhbaariyyuuna**, kwa hiyo kutokea kwa mirengo hii miwili kisha ikahusishwa na Shia Ith'naashariyya haimaanishi kwamba maana ya neno Shia Ithnaashariyya limebadilika kutoka katika istilahi yake ya zamani na kuja kwenye istilahi mpya. Na hivyo hivyo kutokea mirengo ya ki-Fiq'hi ndani ya madhehebu ya Ahli Sunna, kukazalikana madhehebu kuu nne; **Hanafiyya, Maalikiyya, Shaafiyya** na **Hanaabila**, hakupelekea kubadilika istilahi ya neno **Ahli Sunna wal Jamaa**, na jambo hili halimtatizi mtu yeyote mwenye akili timamu na utambuzi wa istilahi za kielimu, kwa kuwa kilichotokea hapo ni kutanuka kwa istilahi hiyo na si kubadilika uhalisia wake. Na kwa maelezo haya tuliyoyatoa inabatilika kauli chafu ya Mshia Jaafar Mwazoa pale aliposema katika ukurasa wa 38;



"Nukta ninayotaka kukutanabahisha ewe Allamah mwanangwa wa Mafuta ni kwamba kufanana kwa matamko si lazima kuandamane na kufanana kwa maana pia. Neno moja laweza likatumika kwa maana fulani leo baada ya miaka mia moja likatumika kwa maana nyingine tofauti, **hivyo kujaribu kulibebesha neno maana ambayo haikutumika katika wakati wake ni upeo wa ukaragosi**, na hilo ndilo shimo refu alilotumbukia mwanangwa wa Mafuta katika mas-alah hayo."

MAJIBU YETU


Kwa kuwa Mshia Mwazoa hakuleta hoja yoyote ya kielimu zaidi ya matusi tu, tutamuachia mwenyewe matusi yake. Kisha akasema katika ukurasa wa 38;

"Iwapo Usunni wa kweli hasa ni huu anaoutaka Mafuta kwa maelezo haya basi hilo ni tusi zito mno kwa Masunni kuliko kuwa ni sifa au jibu murua dhidi ya Sheikh Abdillahi Naasir. Hiyo ni kwa sababu tamshi "**Ahlu Sunna**" linaloongelewa hapo na Ibnu Siiriin lilimaanisha **watu wenye mwenendo wa kumlaani Abu Turaab Ali Bin Abii Talibi (a.s.)**. Na tamshi "**Ahlul Bida'a**" lilikusudiwa **wale wote waliodai Ubora wa Ali (a.s.)** mbele ya Maswahaba wengine hususan Uthman Bin Affan."

MAJIBU YETU

Kama umeyasoma maelezo yetu juu ya mwanzo wa kudhihiri jina la Ahli Sunna utabainikiwa na madai haya ya uongo ya mwandishi huyu wa Shia ya kwamba Ahlu Sunna waliokusudiwa na Imamu Ibn Siiriin ni watu waliokuwa wakimlaani Ali Ibn Abi Twalib radhia Ilaahu anhu. Na halikadhalika ubatili madai haya unadhihirika kwa sababu hizi zifuatazo;

1. Hakuna riwaya sahihi zilizopokewa kutoka kwa wapokezi wenye kutegemewa zinazoonesha kuwa Ahlu Sunna wal-Jamaa walikuwa wakimtukana na kumlaani Ali Ibn Abi Twalib radhia Ilaahu an'hu.
2. Ahlu Sunna tangu karne ya mwanzo, msimamo wao ni kuwaheshimu Maswahaba wote wa Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam na



kuwataja kwa wema, na kuwaombea radhi kwa Allah Subhaanahu wa Ta'ala, na ndio maana hutaona katika kitabu chochote cha Sunni kikitaja vibaya Ali, wala Fatima, wala watoto wao, seuze huko kuwalaani.

3. Ama kipindi cha mizozo ya kisiasa baina ya watu wa Iraq na watu wa Sham, kulitokea baina ya watu wa pande hizi mbili kutukanana. Lakini viongozi wote pamoja na wengi katika wafuasi wao walikuwa katika msimamo mmoja wa dini na itikadi. Lakini ni jambo lisilopingika kwamba kwenye kundi la watu wa Iraq, ambao wengi wao walikuwa katika jeshi la Ali Ibn Abi Twalib radhia Ilaahu anhu, walijificha **Sabaiyya** na wao walikuwa wakivuka mipaka juu ya Ali hadi kumpa sifa ya Uungu, na kazi yao ilikuwa ni kuchochea fitna.

Ali aliwaadhibu wengi wao kwa kuwachoma moto, na watu hawa (**Sabaiyya**) ndio waliohukumiwa kuwa ni watu wa bida'a, kwa upande wa kundi la Ali.

Na wala si kweli kuwa kila aliyekuwa katika jeshi la Ali radhia Ilaahu an'hu aliitwa mtu wa bida'a kama anavyodai Mshia Jaafar Mwazoa. Na kwa upande wa Sham, ambao wengi wao walikuwa katika jeshi la Muawiya radhia Ilaahu an'hu, walijificha ndani ya jeshi hili watu waovu katika **Nawaasib**, wao walikuwa na chuki dhidi ya Ali na Ahlul-Baiti kwa ujumla, na walikuwa wakimlaani Ali, na kazi yao kubwa ilikuwa ni kuchochea fitna baina ya pande mbili zenye kuhasimiana, na hawa (**Nawaasib**) pia walihukumiwa kuwa ni watu wa bida'a kwa upande wa Muawiyah.

Kwa hiyo, si katika uadilifu kuwahukumu watu wote kwa vitendo vinavyofanywa na waovu wachache miongoni mwao.

4. Ama kuhusu wale wenye kudai ubora wa Ali, hawa hawakupewa hukumu ya Ahlul-Bidaa moja kwa moja, kwa sababu katika hao kuna waliokuwa wakimwona Ali kuwa ni bora kuliko Uthman, hawakuthubutu kumtukana yeyote katika Maswahaba, si Abu Bakar, wala Umar wala Uthman, hawa walihesabika ni katika Ahlu Sunna, na mfano wa hao ni Imamu Abdul-Razaq As-Swan'aniy, Imamu An-Nasaaiy n.k. katika wanachuoni wa hadithi kwa Ahlu Sunna, na kama atanasibishwa na Ushia ni kwa hili la kumfadhilisha Ali juu ya Uthman radhia Ilaahu an'huma.

5. Ama wale waliomfadhilisha Ali pamoja na kuwatukana Maswahaba wengine, hawa walihukumiwa kuwa ni watu wa bid'aa, kwa sababu ya huku kuwatukana Maswahaba, na si kwa sababu ya kumwona Ali kuwa ni bora.

TUHUMA ZA MWAZOA DHIDI YA MISINGI YA HADITHI YA AHLU SUNNA

Baada ya Mshia huyu kufeli katika jaribio lake la kuyapotosha maneno ya Imamu Muhammad Ibn Siiriin, akafuatishia udanganyifu na ubabaishaji dhidi ya misingi thabiti ya Ahlu Sunna katika masuala ya elimu ya hadithi na wapokezi wake. +Akasema Mwazoa katika ukurasa wa 39;


"Maelezo haya hayaoneshi mizani yoyote ya vipimo vya kuikubali hadithi au kuikataa, bali lengo kuu lilikuwa kuwainua watu fulani na kuwatweza wengine kwa kuangalia nani kasema nini kuhusiana na kifo cha Uthman na msimamo wa mpokezi huyo wa hadithi juu ya hilo. Na jambo hilo kweli likaathiri sana ulimwengu wa hadithi kiasi cha kutiliwa mashaka wapokezi wengi wa hadithi na kukataliwa hadithi zao kwa kuwa tu wanampenda Ali (a.s.) jambo li+nalowafanya wajumuishwe katika kundi la "Ahlul Bida'a"

Pia amesema katika ukurasa wa 40;

"Nususi hizo hapo juu na nyingi nyinginezo ambazo hatukuzitaja zaonesha hali ilivyokuwa wakati huo, kwamba yeyote anayetambulika kuwa karibu na Ali (as) hilo lilitosha kumtia ila, kama alikuwa mkweli ataitwa mwongo na kama alikuwa mwenye kutegemewa atakuwa hafai tena kutegemewa. Ikawa kusimama na Ali (as) ni alama ya kuwa wewe ni mtu wa bid'ah na ukisimama na maadui wa Ali wewe ni mtu wa Sunnah!!"

MAJIBU YETU

Maneno haya ya Mshia Jaafar Mwazoa hayana ukweli hata kidogo, bali hizi ni fikra za kumezeshwa ambazo hazina chembe ya utafiti wa kielimu, na lau kama angekuwa ni mkweli kwenye madai yake angetoa ushahidi wa kielimu. Hilo ni mosi.



Pili, lau kama angekuwa na ufahamu wa kawaida tu juu ya ubovu wa misingi ya madhehebu yao ya Shia katika elimu ya hadithi na wapokezi wake, basi asingethubutu kuzungumza chochote dhidi ya Ahli Sunna.

Ukweli ni kwamba, Wanachuoni wa Ahlu Sunnat wal-Jamaa tangu karne za mwanzo wameweka misingi madhubuti ya hadithi, na kanuni imara kwa wapokezi wa habari, kwa lengo la kupambana na harakati za waongo miongoni mwa Wazandiki, na wengineo wenye lengo baya la kuipotosha dini aliyokuja nayo Mtume swalla llaahu alayhi waalihi wasallam. Na kwa kuwa suala hili ni suala la dini, wanachuoni wa hadithi wa Ahlu Sunna walichunga sana sifa ya uadilifu katika kuwahukumu watu, na kuweka pembeni utashi wa nafsi zao na ushabiki wa kimadhehebu, mpaka ilifikia baadhi ya waliwajeruhi na kuwasema vibaya baba zao, kaka zao na wengineo katika jamaa na marafiki. Na kwa kuchunga uadilifu na amana katika dini, kuna watu ambao kauli zao dhidi ya watu wa miji fulani, au madhehebu fulani hazikubaliwi, kwa sababu ya kuwa na chuki binafsi dhidi ya watu wa miji hiyo, au madhehebu hayo. Na mfano wa karibu tunaoweza kumpa Mshia Mwazoa na wengineo mfano wake wenye malengo mabaya ya kuipotosha ukweli bila ya elimu, ni hii kauli aliyoitoa Imam Al-Hafidh Ibn Hajar Al-Asqalaaniy, aliposema kuhusu Abu Is'haaq Al-Juuzajaaniy;

"وَمَّا يَنْبَغِي أَنْ يُتَوَقَّفَ فِي قَبُولِ قَوْلِهِ فِي الْجَرِّ مَنْ كَانَ بَيْنَهُ وَبَيْنَ مَنْ جَرَّحَهُ عِدَاوَةٌ سَبَّهَا
الْاِخْتِلَافُ فِي الْأَعْتَادِ، فَإِنَّ الْحَادِقَ إِذَا تَأَمَّلَ ثَلَبَ أَبِي إِسْحَاقَ الْجَوْرَجَانِيَّ لِأَهْلِ الْكُوفَةِ رَأَى
الْعَجَبَ وَذَلِكَ لِشِدَّةِ انْجِرَافِهِ فِي النَّصَبِ وَشُهْرَةِ أَهْلِهَا فِي التَّشْيِيعِ، فَتَدْرَاهُ لَا يُتَوَقَّفُ فِي جَرِّ
مَنْ ذَكَرَهُ مِنْهُمْ بِلِسَانِ ذَلِيقٍ وَعِبَارَةٍ طَلْقَةٍ، حَتَّى أَحَدًا يَلِينُ مِثْلَ الْأَعْمَشِ، وَأَبِي نُعَيْمٍ وَعَبِيدِ
اللَّهِ بْنِ مُوسَى، وَأَسَاطِينِ الْحَدِيثِ وَأَرْكَانِ الرِّوَايَةِ، فَهَذَا إِذَا عَارَضَهُ مِثْلُهُ أَوْ أَكْبَرُ مِنْهُ
فَوَثَّقَ رَجُلًا ضَعْفَهُ قُبُلَ التَّوَثُّيقِ، وَيَلْتَجِئُ بِهِ عَبْدُ الرَّحْمَنِ بْنُ يُوسُفَ بْنِ خِرَاشٍ الْحَافِظُ
الْمُحَدِّثُ، فَإِنَّهُ مِنْ غُلَاةِ الشَّيْعَةِ، بَلْ نُسِبَ إِلَى الرَّفْضِ فَيُتَأَنَّى فِي جَرِّهِ لِأَهْلِ الشَّامِ
لِلْعِدَاوَةِ الْبَيْنَةِ فِي الْأَعْتَادِ، وَيَلْتَجِئُ بِذَلِكَ مَا يَكُونُ سَبَبَهُ الْمُنَافَسَةُ فِي الْمَرَاتِبِ، فَكَثِيرًا مَا
يَفْعُ بَيْنَ الْعَصْرِيِّينَ الْاِخْتِلَافُ وَالتَّبَايُنُ...."

"Na katika yanayotakiwa; ni ku-Tawaqaf (kusubiri) katika kuikubali kauli ya Kumjeruhi mtu ambaye kuna uadui kati yake na huyo anayemjeruhi, uadui ambao sababu yake ni tofauti za kiitikadi. Hakika mtu mwerevu anapozingatia Jarhe ya Abu Is'haaq Al-Juuzajaniy kwa watu wa Kuufa, ataona maajabu, na hilo ni kutokana na kupotoka kwake kulikotokana na Nasbi (uadui dhidi ya Ahlul-Baiti), na kutangaa

watu wa Kuufa katika Ushia. Utamuona (Abu Is'haaq Al-Juuzjaaniy) hajichungi katika kumjeruhi mtu anayemtaja katika wao (watu wa Kuufa) tena kwa lugha ya ukali na ibara isiyo na mipaka, mpaka alifikia kumdhoofisha mtu kama Al-A'mash, Abu Nuaim, na Ubaidillahi Ibn Musa na vigogo katika hadithi na nguzo (wanaotegemewa) katika riwaya. Basi huyu (Al-Juuzjaniy) akipingana na mtu mfano wake, au aliye zaidi yake (mtu huyo) akampa Wathaqa mtu ambaye yeye (Al-Juuzjaniy) amemdhoofisha, itakubaliwa Wathaaqa (ya mtu huyo, na haitachukuliwa kauli ya Juuzjaniy). Na ataunganishwa pamoja na (Al-Juuzjaaniy katika hukumu hiyo) Abdur-Rahman Ibn Yusuf Ibn Khiraash, mwanachuoni wa hadithi, mwenye hifdhhi nzuri, kwa sababu yeye ni katika Ghulaati wa Shia, bali pia amenasibishwa na Uraafidha (kuwatukana Abu Bakar na Umar), mtu huyu itachukuliwa Jarhu yake kwa watu wa Sham kwa tahadhari, kwa sababu ya uadui wake wa wazi katika itikadi.

Pia itaunganishwa na hukumu hii, Jarhu ambayo sababu yake inatokana na ushindani wa kugombea vyeo, na mara nyingi hutokea tofauti na migongano kwa watu wanaoishi katika zama moja.³² Mwisho wa kunukuu.

Ndugu msomaji! Huo ni mfano mmoja kati ya mifano mingi inayotonesha uadilifu na umadhubuti wa Ahli Sunna katika misingi ya upembuzi wa habari, na uchunguzi wao juu ya wapokezi wa hadithi. Shia hawana misingi kama hii wala inayokaribiana na misingi hii. Na kwa maelezo haya mafupi, utabainikiwa na maneno ya uongo yaliyotamkwa na Mshia Jaafar Mwazoa pale aliposema:

"yeyote anayetambulika kuwa karibu na Ali (as) hilo lilitosha kumtia ila, kama alikuwa mkweli ataitwa mwongo na kama alikuwa mwenye kutegemewa atakuwa hafai tena kutegemewa...."

³²-Tazama kitabu Lisanul-Mizaani, cha Al-Haafidh Ibn Hajar Al-Asqalaaniy, juzuu ya I ukurasa wa 22-23, chapa ya Dar Ehia Al-Tourath Al-Arabi, chapa ya pili ya mwaka 2001, iliyochapishwa Beirut-Lebanon.

Ndugu msomaji! Insha-Allaah katika sehemu hii ifuatayo nitakutajia sababu zilizowafanya Ahlu Sunna wazikatae baadhi ya riwaya za wapokezi wa Shia.

wapa nafasi wazandiki kuiharibu dini yao na hilo litakudhihirikia kwa kusoma vitabu vikubwa vya Shia hadithi na kupitia vitabu vyao vya Jarhe wa Ta'diil.

waliojificha nyuma ya pazia la Ahlil-Baiti kwa lengo la kuuvuruga Uislamu, na wanachuoni wao walishindwa kuzizuia hadithabla ya kulijibu swali hili, ni vyema tukakufunulia japo kwa ufupi historia na hali halisi ilivyokuwa hapo nyuma na juhudi zilizofanywa na Maulamaa wa Ahlu Sunna katika harakati zao za kupambana dhidi ya Wazandiki. **Riwaya za kutunga ni bidhaa mbovu za Wazandiki, Wazushi na Maghulaati (wafuasi wa Ibnu Sabai)** ambao walifikia kutunga hadithi na kumzulia uongo Bwana Mtume swalla llaahu alayhi waalihi wasallam, na Maimamu kwa lengo la kuivuruga dini ya Allah kwa kuingiza batili na kujali maslahi yao binafsi.

Kuna sababu nyingi zilizopelekea kutokea wimbi hili, hasa hasa katika kipindi cha nusu ya pili katika karne ya kwanza, zama za Mukhtaar At-Thaqafiy,³³ yeye alitoa juhudi kubwa katika kuwalinda Wazandiki na Maghulaati na kuwapa nguvu. Miongoni mwa sababu zilizopelekea kutokea kwa wimbi hilo la riwaya za kutunga, ni hizi zifuatazo:-

- i. Mizozo ya kisiasa.
- ii. Kujipendekeza kwa watawala.
- iii. Tofauti za Madhehebu katika masuala ya Fiqhi na Itikadi.
- iv. Taassubi za ki-Miji, Lugha na Ukabila.
- v. Uzandiki.³⁴
- vi. Walinganizi wenye kutumia visa na simulizi za kusionua.
- vii. Waombaji.

³³-Mukhtaar Ibn Abi Ubayd Ibn Mas'oud At-Thaqafiy, amezaliwa mwaka 1 H na kufariki mwaka 67 H. Alikuwa mtawala wa Kufa baada ya kufanya mapinduzi dhidi ya Utawala wa Banii Umayya na aliwauwa kwa kuwalipizia kisasi baadhi ya walioshiriki kumuua Husein Ibn Ali radhia llaahu an'huma.

³⁴-**Uzandiki**:- ni hali ya mtu kujidhihirisha kuwa yeye ni Muislamu, na huku akiwa ameficha ukafiri kwa nia ya kuuvunja Uislamu. Na Mzandiki ni mtu mwenye tabia hiyo.



Hukumu ya kutunga hadithi:-

Kwa mujibu wa misingi ya Ahlu Sunna wal-Jamaa kutunga Hadithi na kumzulia uongo Bwana Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam ni jambo baya la haramu. Kuna ushahidi mwingi katika Qur-ani na Sunna juu ya uharamu wa kitendo hicho. Miongoni mwa ushahidi huo ni kauli yake Allah aliposema:-

{ إِنَّمَا يَفْتَرِي الْكَذِبَ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِآيَاتِ اللَّهِ وَأُولَئِكَ هُمُ الْكَاذِبُونَ } (النحل: ١٠٥)

[Kwa hakika hapana vingine, wanaozua uongo ni wale ambao hawaziamini Aya za Allah. Na hao ndio waongo.] Surat An-Nahli Aya 105. Na kauli yake Allah aliposema:

{ إِنَّ الَّذِينَ يَفْتَرُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ لَا يُفْلِحُونَ } [النحل: ١١٦]

[Kwa hakika wale ambao wanamzulia Allah uongo hawatafaulu..] Surat An-Nahli Aya ya 116. Amesema Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam:

{ مَنْ كَذَبَ عَلَيَّ مُتَعَمِّدًا فَلْيَتَّبِعُوا مَقْعَدَهُ مِنَ النَّارِ }

[Atakayenzulia mimi uongo, na ajichagulie makazi yake motoni.] Hadithi imepokewa na Imamu Al-Bukhari na Muslim kutoka kwa zaidi ya Maswahaba sabini.

Hukumu ya mtungaji wa hadithi:-

Ama kuhusu hukumu ya mwenye kutunga Hadithi na kumzulia uongo Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam wametofautiana wanachuoni wa Ahlu Sunna kwenye rai tatu;

Rai ya kwanza: Mwenye kumzulia uongo Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam kwa makusudi ni sawa na mwenye kumzulia uongo Allah. Kwa hiyo, mwenye kufanya hivyo atakuwa amekufuru na damu yake ni halali. Ni mamoja uongo huo umehalalisha haramu na kuharamisha halali au laa. Na hii ni rai ya Imamu Abu Muhammad Al-Juweiniy baba yake Imamu Al-Haramain, Ibn Al-Arabi katika wanachuoni wa ki-Malik na Abul-Fadhli Al-Hamadani katika wanachuoni wa ki-Hanbali.

Rai ya pili: ni kinyume na rai ya kwanza, hatakuufuru hata kama uongo huo umehalalisha haramu na kuharamisha halali. Na hii ni rai ya Abul-Maali Al-Juweiniy.

Rai ya tatu: Mwenye kutunga Hadithi ya uongo hatakuafuru maadamu riwaya hiyo haijahalalisha haramu au haijaharamisha halali. Na kama riwaya hiyo itahalalisha haramu au kuharamisha halali basi atakufuru mtunzi wa riwaya hiyo. Na hii ndiyo rai ya Jumhuuri (wanachuoni wengi) katika Ahlu Sunna. Na Hadithi zake hazitakubaliwa tena hata kama atatubia, na toba yake hiyo itakuwa ni baina yake na Mola wake.

Hukumu ya mwenye kupokea hadithi za kutunga;-

Kwa kuwa wapokezi wa Hadithi za kutunga wanatofautiana katika upeo wao wa kimaarifa, na uwezo wa kudhibiti na kupambanua habari, halikadhalika wanatofautiana katika malengo na msukumo wa kufanya hivyo, wanachuoni wa Hadithi wamezitofautisha hukumu zao.

Na hilo ni kutok

ana na kuwa, wapo miongoni mwao waliozipokea Hadithi na riwaya za kutunga wakiwa ni:-

- i. Wajinga, ambao hawajui kuwa Hadithi hiyo kuwa ni ya kutunga. Huyu atakuwa amepewa udhuru kwa sababu ya ujinga wake.
- ii. Mjuzi, anaipokea na kuitaja Hadithi ya kutunga kwa lengo la kubainisha uongo wake.
 - a) Ima kwa kusema wazi wazi kwamba Hadithi hii ni Maudhuu (ya kutunga).
 - b) Au kwa kuitaja Hadithi hiyo kwenye vitabu maalumu vilivyotungwa kwa ajili ya kubainisha Hadithi dhaifu na za kutunga.
 - c) Au kwa kuitaja hadithi hiyo na Sanad yake. Jambo hili wamelifanya sana wanachouni wa Hadithi na hata wanachuoni wengine. Njia hii ya pili iliwafaa watu wa karne za mwanzo. Ama kwa wakati wa sasa haitafaa kufanya hivyo kwa sababu ya kukithiri ujinga hasa katika elimu hii na istilahi zake.
- iii. Mjuzi, anaipokea Hadithi ya kutunga bila ya kubainisha uongo wake. Bila shaka, kitendo hiki ni haramu.

Huu ndio ufafanuzi wetu kwa ufupi juu ya ubabaishaji alioufanya Mwazoa kwenye kauli ya Ibn Siiriin. Na ukweli ni kwamba masuala haya yanahitaji wasaa na ufafanuzi wa kutosha katika sehemu zake, na Allah akitupa uhai, uzima na salama tutayafafanua masuala haya kwenye kitabu chetu, **'Nadharia ya uadilifu wa Maswahaba'** Inasha-Allaah.

والله الموفق والهادي إلى سواء السبيل!!!

SURA YA TATU

UWAHABI

1- UWAHABI NI NINI?

Uwahabi ni jina la kubandika (**lakabu**) linalotumiwa na mahasimu wa Ahli Sunna kwa lengo la kuwakebehi na kuwabeza. Na mara nyingi jina hili hutumiwa na watu wa bidaa kama **Shia, Ibadhi, Masufi** na wengineo.

- Ni kina nani Mawahabi?

Baada ya kujua maana ya Uwahabi, ni vyema ukafahamu pia ni kina nani Mawahabi/Wahabiyya kwa mtazamo wa hao wenye kubeza. Anasema **Khalifa Khamis Mohammed mtunzi wa kitabu 'Upotevu wa Madhehebu ya Uwahabi'**³⁵ ambaye ni Sufi mwenye mrengo wa Kishia;

"Mawahabi au kama wanavyojiita "Answaru Sunna" ni kikundi cha watu ambao wao wenyewe wanajiita Waislamu, lakini kwa hakika ni genge lililojiandaa na kusimama imara kabisa kuupiga vita Uislamu kwa hali na mali na kuvunja hadhi na heshima ya Mtume Muhammad (S.W.A.) ikiwa ni pamoja na kuwatukana, kuwakashifu Maimamu, na kuzipondaponda jitihada zao sahihi."³⁶

Pia amesema tena;-

"Neno Uwahabi limetokana na jina la Abdul- Wahabi ambalo ni jina la baba wa Sheikh Muhammad Abdul-Wahhabi. Wale wanaofuata itikadi yake potovu ndio wanaoitwa Wahabiyya"³⁷

³⁵-Kitabu hiki tumekijibu kwenye kitabu chetu tulichokiita '**Ukweli kuhusu historia ya Sheikh Muhammad bin Abdil-Wahabi na daawa yake**', tafadhali usikikose.

³⁶ -Tazama **Kitabu 'Upotevu wa Madhehebu ya Uwahabi'** chapa ya 10, ukurasa wa ii.

³⁷ -Tazama kitabu hicho hicho katika ukurasa wa I.

- **Uchambuzi wetu juu ya maelezo haya ya uongo:-**

Mtu yeyote mwenye maarifa ya kawaida hapati tabu ya kugundua uongo na ujinga uliomo kwenye maelezo haya ya Khalifa Khamisi na mfano wake. Kwa sababu mtu yeyote mwadilifu anafahamu jinsi Serikali ya Saudi Arabia -ambayo wanachuoni wake wote ni hao mnaowaita Mawahabi- inavyotoa juhudi na gharama kubwa za kuutumikia Uislamu na Waislamu, kwa mfano:-

Ukiitizama misikiti miwili mitakatifu (**Haram ya Makka na Madina**), Mashaai'ri za **Mina, Muzdalifa, na Arafah** na huduma wanazozitoa kwa Mahujaji wanaokwenda kuhiji katika nyumba takatifu utadhihirikiwa na ukweli huu ninaokuelezea.

Wachilia mbali mashirika yao binafsi na ya kiserikali yenye lengo la kuusaidia na kuuendeleza Uislamu na Waislamu duniani, na taasisi zake za kielimu, kama vyuo vikuu vya Kiislamu vilivyopo Makka, Madina na Riyadh na kwengineko, ambavyo vimesaidia kwa kiasi kikubwa kuueneza Uislamu Ulaya, Afrika, Amerika ya Kusini na Kaskazini na Mashariki ya mbali, bali na katika nchi za Kiarabu, yote hayo ni ushahidi wa kutosha juu ya kuuthamini kwao Uislamu na Waislamu. Kwa hiyo hata kama mtu ana chuki binafsi lakini mbele ya haki anatakiwa ajikaze katika kuusema ukweli na kuutetea na huo ndio uungwana.

Ama kuhusu maelezo ya Khalifa Khamisi kuwa Mawahabi wanavunja hadhi na heshima ya Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam, haya ni maelezo yaliyojaa chuki, uongo na ujinga, na ndiyo maana mwandishi wake ameshindwa kuyathibitisha madai yake hayo kwa hoja za kielimu. Ukweli ni kwamba hao wanaoitwa Mawahabi ndio watetezi wakubwa wa mafunzo ya Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam kwa kauli zao na vitendo vyao, na ushahidi juu hilo ni mwingi haudhibitiki.

Ama madai ya Khalifa Khamisi kuwa Mawahabi wanawatukana na kuwakashifu Maimamu na kuzipondaponda jitihada zao, nayo pia ni madai ya uongo ya mtu aliyefilisika, na kama ni mkweli basi na atulettee ushahidi wa kielimu juu ya madai yake hayo.

Lakini jambo la ajabu na la kushangaza kwa Bwana huyu, ni kumuona anavyotoa juhudi kubwa katika kuwatuhumu Ahli Sunna kwa tuhuma za uongo, na wakati huo huo anayafumbia macho matusi ya wazi wazi dhidi ya Maswahaba wa Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam yanayotolewa na marafiki zake wa karibu, Mashia Ith'naashariyya, bali anaonesha ushirikiano wake na wao kwa ukaribu mno!!! Na hali ya kuwa Mashia wanawatukana watukufu hao na kuwalaani wazi wazi, kupitia sauti zao, vipeperushi vyao na vitabu vyao!! Hivi kweli hao Maimamu anaodai kuwa Mawahabi wanawatukana, na Maswahaba wa Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam ni wapi waliobora zaidi na wanaostahiki kutetewa kama kweli Khalifa Khamisi ana ghera na dini ya Allah?

2- HISTORIA FUPI YA SHEIKH MUHAMMAD BIN ABDIL WAHABI

Ndugu msomaji! Tuhuma za uzushi na uongo zimekuwa nyingi mno dhidi ya Sheikh Muhammad Bin Abdil Wahabi na wafuasi wake, kwa hivyo nimelazimika kukuletea historia fupi ya Sheikh huyu na daawa yake ili ubainikiwe na ukweli Insha-Allah.

i- Jina lake na Mwaka wa kuzaliwa kwake na kufa kwake;

Jina lake ni; **Sheikh Muhammad Bin Abdil-Wahabi, Bin Sulaiman, Bin Ali, Bin Muhammad Bin Ahmad Bin Rashid, At-Tamimiy.**

Amezaliwa mnamo mwaka 1115 Hijiriyya sawa na mwaka 1703 AD, katika mji wa Uyaina, Riyadh - Saudi Arabia. Na kufariki mwaka 1206 Hijiriyya.

ii- Kusoma kwake na Masheikh wake;

Sheikh Muhammad -Allah amrehemu- alisoma Qur-ani na kuihifadhi yote kabla ya kufikia umri wa miaka kumi, alikuwa ni mtu mwenye maarifa mazuri na hifidhi kali. Alisoma elimu za fiq'hi kwa baba yake, ambaye alikuwa ni Qadhi wa mji wa Uyainah, kama alivyokuwa babu yake Sheikh Suleiman ni Qadhi katika mji huo, kwa hiyo alikulia katika nyumba yenye wasomi wa dini.

Sheikh Muhammad alisafiri kwa ajili ya kutafuta elimu katika miji mbalimbali kama vile; **Makka, Madina, Basra, n.k.**

Ama Masheikh waliomsomesha ni wengi sana, miongoni mwao ni hawa wafuatao; **Sheikh Abdullahi Bin Ibrahim Bin Seif, Sheikh Muhaddith, Muhammad Hayat Sindiy, Sheikh Al-Musnid; Abdullahi Bin Saalim Al-Basriy, Sheikh Abdul-Latif Al-Afaaliqiy Al-Ahsaaiy.**

iii- Madhehebu yake katika Itikadi na Fig'hi:-

Tukimtazama Sheikh Muhammad bin Abdil-Wahabi kwa upande wa madhehebu yake kupitia vitabu vyake na vitabu vya wanafunzi wake, na hata kwa kuzitazama kauli za wanachuoni walioishi katika zama zake ambao hawakuwa na chuki binafsi dhidi yake, utafahamu kwamba Sheikh Muhammad Ibn Abdil Wahabi –rahimahu llaahu- alikuwa ni mfuasi wa madhehebu ya **Salaf Swalih**, ambayo ndiyo madhehebu ya Maimamu wakubwa wa Ahli Sunna wal-Jamaa kama vile; **Abu Hanifa, Malik, Shaafiy, Ahmad Ibn Hambali na wanafunzi wao.**

Ama katika masuala ya **Sheria na Fiqhi**, Sheikh Muhammad bin Abdil Wahabi alikuwa ni mfuasi wa madhehebu ya **Imamu Ahmad Ibn Hanbali**, ambaye ni mmoja kati ya Maimamu wa nne wa madhehebu ya Ahlu Sunna wal-Jamaa.

Kwa hiyo, hakuleta dhehebu jipya wala hakudai hilo, bali alikuwa akiwafuata Maimamu wa Ahli Sunna wal-Jamaa kwa hoja na dalili pamoja na kuwaheshimu, na vitabu vyake na vya wanafunzi wake ni ushahidi tosha juu ya hilo.

Hivyo basi, badala ya kunukuu historia ya mtu mwema kama huyu kutoka kwa **Mkristo Mr. Humphrey**, kama wanavyofanya maadui zake (Mashia na Masufi) ni vyema tukachukua maelezo ya wanachuoni wetu wa Kiislamu walioifuatilia historia yake kwa uadilifu na umakini, baada ya kutembelea mazingira ya Sheikh Muhammad Ibn Abdil-Wahabi na kuisoma itikadi yake pamoja na itikadi ya wafuasi wake.

Na miongoni mwa wanachuoni hao ni mwanachuoni mkubwa wa Yemen, **Imamu Muhammad bin Ali As-Shaukaniy** anatuelezea kuhusu Sheikh Muhammad bin Abdil-Wahabi kwa kusema hivi:-

«وكان حنبليًا، ثم طلب الحديث بالمدينة المشرفة فعاد إلى نجد وصار يعمل باجتهادات جماعة من متأخري الحنابلة كابن تيمية وابن القيم وأضرابهما. وهما من أشد الناس على معتقدي الأموات، وقد رأيت كتابًا من صاحب نجد - وهو عبد العزيز بن سعود - الذي هو الآن صاحب تلك الجهات أجاب به على بعض أهل العلم، وقد كاتبه وسأله بيان ما يعتقده فرأيت جوابه مشتملاً على اعتقاد حسن موافق للكتاب والسنة فالله أعلم بحقيقة الحال».

"Alikuwa ni mfuasi wa Hanbali, kisha akatafuta elimu ya hadithi katika mji mtukufu wa Madina, kisha akarudi Najdi akawa anazifanyia kazi jitihada za kundi la wanachuoni wa ki-Hanbali waliokuja nyuma, kama Ibn Taimiyya, Ibnul-Qayyim na mfano wao. Na wao ni katika watu walio na msimamo mkali dhidi ya wenye kuitakidi (itikadi mbaya³⁸) **kwa wafu**. Niliwahi kukiona kitabu kutoka kwa mtawala wa Najdi - naye ni **Abdul Aziz bin Suudi**- ambaye ndiye aliyekuwa mtawala katika sehemu hizo akiwajibu baadhi ya wanachuoni, walimuandikia wakimuulizia ubainifu wa kile anachokiitakidi, nikaiona jawabu yake imebeba itikadi nzuri inayoafikiana na Kitabu (Qur'ani) na Sunna. Na Allah ndiye anayejua zaidi hakika ya hali"³⁹

Naye **Imamu Muhammad bin Hasan Al-Hajawiy**, ambaye ni miongoni mwa Maulamaa wa Maghribi (Morroco), yeye ana haya ya kusema kuhusu Sheikh Muhammad bin Abdil Wahabi;

«وعقيدته السنة الخالصة على مذهب السلف المتمسكين بمحض القرآن والسنة، لا يخوض التأويل والفلسفة، ولا يدخلهما في عقيدته. وفي الفروع مذهبه حنبلي غير جامد على تقليد الإمام أحمد ولا من دونه، بل إذا وجد دليلاً أخذ به وترك أقوال المذهب، فهو مستقل الفكر في العقيدة والفروع معاً». (الفكر السامي: ٣٧٢/٢).

³⁸-Miongoni mwa itikadi mbaya kwa wafu, ni kuitakidi kwamba wanaouwezo wa kuleta kheri au kuondoa shari na kwa sababu hiyo baadhi ya watu wanakwenda kwenye Makaburi ya watu wanaowaitakidi kuwa ni wema na Kuswali na Kusujudu, au Kufanya Twawafu, au Kuchinja wanyama, Kuweka nadhiri na Kuomba Dua mbalimbali n.k.

³⁹ -Tazama Al-Badru At-Twaali', juzuu ya 1 ukurasa wa 357.

"Itikadi yake ni ya Sunna iliyosafi, **iliyo kwenye madhehebu ya Salaf, wenye kushikamana na Qur'ani na Sunna tu**, wala haingii kwenye Ta'wiil wala Falsafa, wala haviingizi viwili hivyo kwenye itikadi yake. **Ama katika matawi; madhehebu yake ni mfuasi wa Hanbali**, si mwenye kuganda juu ya kumfuata Imamu Ahmad kiupofu pasi na wengine, bali akipata dalili anaichukua na anaachana na kauli za madhehebu, yeye ni mtu mwenye fikra huru katika itikadi na matawi kwa pamoja"⁴⁰ Ama kuhusu wafuasi wa Sheikh Muhammad Bin Abdil-Wahabi, ambao ni wakazi wa miji ya Dir-iyah, **Imamu As-Sayyid Shukriy Al-Aluusi** -Allah amrehemu-, yeye ana haya ya kutwambia;

"والحاصل على مذهبهم في أصول الدين مذهب أهل السنة والجماعة، وأن طريقهم طريقة السلف التي هي الطريق الأسلم، بل الأحكم..... وأنهم في الفروع على مذهب الإمام أحمد بن حنبل -نصر الله وجهه- ولا ينكرون على من قلد أحدا من الأئمة الأربعة..."

"Kwa ujumla, madhehebu yao katika misingi ya dini ni madhehebu ya Ahlu Sunna wal-Jamaa, **na njia yao ni njia ya Salaf**, ambayo ndiyo njia ya salama zaidi, bali ndiyo iliyo na ufanisi zaidi....Na wao katika matawi (ya dini) **wako katika madhehebu ya Imamu Ahmad Ibn Hanbali** -Allah autie nuru uso wake-, na wala hawampingi yeyote anayemfuata mmoja kati ya Maimamu wanne....."⁴¹ Kisha akasema;

"غير أنهم في بعض المسائل إذا صح لهم نص جلي من كتاب أو سنة غير منسوخ ولا مخصص ولا معارض بأقوى منه وقال به أحد الأئمة الأربعة أخذوا به وتركوا المذهب، كإرث الجدة والإخوة فإنهم يقدمون الجد بالإرث وإن خالف مذهب الحنابلة..."

"Isipokuwa wao katika baadhi ya masuala kama litakaposihi kwao andiko la wazi katika Kitabu (Qur'ani) au Sunna na likawa halikufutwa, wala halikuhusishwa, wala halikupingana na dalili iliyo na nguvu zaidi kuliko hiyo, na ikawa ameisema mmoja kati ya Maimamu wanne, wanaichukua kauli hiyo na wanaachana na madhehebu.

⁴⁰ -Tazama Kitabu 'Al-Fikru As-Saamiy', juzuu ya 2 ukurasa wa 372.

⁴¹-Tazama kitabu Taarekh Najdi cha Sayyid Mahmoud Shukriy Al-Alousiy, ukurasa wa 51, kilichochapishwa na Maktabatu-Thaqaafati Diiniyya - Qairo.

Kwa mfano, ni (suala la) Kurithi babu pamoja na ndugu, wao wanamtanguliza babu katika kurithi, hata kama hilo linatofautiana na madhehebu ya Hanbali..."⁴²

Ndugu msomaji! Hiyo ndiyo hali halisi ya itikadi ya Sheikh Muhammad bin Abdil Wahabi na wafuasi wake, kama lilivyoshuhudiwa jambo hilo na wanachuoni hao wa Kiislamu, halikadhalika vitabu vyake na vitabu vya wanafunzi wake vinajielezea wazi juu ya msimamo wake kiitikadi na ki-Fiqhi.

Baada ya kuifahamu itikadi ya Sheikh Muhammad na wafuasi wake, hebu sasa tuitazame hali ya jamii yake, ilikuwaje?

3- HALI YA KIJAMII KATIKA MIJI YAKE;-

i- Hali zao katika itikadi na imani;

Watu wa Najdi katika zama za Sheikh Muhammad Ibn Abdil Wahabi hawakutofautiana sana na watu wa miji mingine ya Kiislamu, itikadi potofu na imani za kishirikina zilienea kwa kasi, watu walizama kwenye matambiko na kuabudu makaburi na mizimu, watu wengi walibobea kwenye bidaa, na dhulma, wanyonge walidhulumiwa, na mwenye nguvu ndiye mwenye haki. Na sababu kubwa ya mambo hayo ni kuenea kwa ujinga katika miji ya waislamu. Anasema Imamu As-Shaukaniy -Allah amrehemu-;


"وكانت تلك البلاد قد غلبت عليها أمور الجاهلية وصار الإسلام فيها غريباً...."

"Ilikuwa miji hiyo imezidiwa na mambo ya Jaahiliyya, na Uislamu ulikuwa mgeni..."⁴³

Hali ya miji hii ya Najdi kwa wakati huo haikutofautiani sana na hali ya miji yetu katika Pwani ya Afrika ya Mashariki, utawaona watu wengi wanaojinasibisha na Uislamu wanafanya mambo ambayo misingi yake ni kinyume kabisa na Uislamu. Kwa mfano; suala la kuiomba mizimu, si tu kwamba ni ujahili wa zama, bali ni Shiriki yaani ni kinyume na kuamini kwamba afaaye kuombwa ni Allah peke yake, na kwamba kufanya hivyo ni kinyume na Tauhiid.

⁴² -Tazama 'Tarekh Najdi' ukurasa wa 51-52.

⁴³ Tazama Al-Badru At-Twaali', juzuu ya 1 ukurasa wa 182.



Katika miji yetu wapo waislamu ambao hufanya **Matambiko** na kuomba kwa **Kinyamkera, Korero, Mikole, Mwanambago, Kabogo, Kifudu, Mwakakogwa** n.k. hayo yote ni katika mambo ya Ushirikina yaliyo kinyume na Tauhiid (Kumuabudu na kumuomba Allah peke yake).⁴⁴

Na huko Najdi alikotokea Sheikh Muhammad Ibn Abdil Wahabi, jamaa zake walikuwa wakifanya matambiko kama hayo kwenye **Mapango, Mitende**, na kwenye kaburi la **Zaid Ibnul Khattwabi**⁴⁵ radhia Ilaahu anhu, wanakwenda kuomba **mali, watoto, kuponya maradhi yao**, na kila shida inayowakabili.

Katika mji wa **Al-Fidaa** kulikuwa na mtende dume uliojulikana kwa jina la **Al-Fihaali**, wanaume kwa wanawake walikwenda kwa ajili ya kuomba watoto, na kutabaruku. Wanawake waliochelewa kuolewa walikwenda kuomba waume wa kuwaowa, na huku wakisema;

"يا فحل الفحول ، أريد زوجًا قبل أن يحول الحول"

"Ewe dume wa madume! Ninataka mume kabla ya kwisha mwaka huu."

Na huko sehemu za Dir-iyah, watu wa huko walikuwa wakiabudu Pango kubwa walilokuwa wakiitakidi kwamba asili yake ni mwanamke aitwaye **Binti Amir**, wanadai kuwa mwanamke huyo alipiga ukelele wa kuomba msaada kwa Allah amnusuru dhidi ya dhulma ya watu waovu, ndipo Allah alipomfungulia Pango hilo naye akaingia.

Watu wa eneo hilo walilifanya Pango hilo kuwa ni mzimu, walikwenda kuomba hapo, walipeleka vyakula, walichinja wanyama na kuweka nadhiri. Na kwa masikitiko makubwa wanachuoni wao walizinyamazia kimya shirki hizo mpaka zikazoeleka na kuwa ni jambo la kawaida.

Sheikh Muhammad Ibn Abdil Wahabi baada ya kurudi kutoka masomoni alianza kazi ya Daawa (ulinganizi) na kuwakataza watu na Shirki hizo kama ilivyokuwa Daawa ya Mtume swalla Ilaahu alayhi wasallam.

⁴⁴ -Tazama maneno mfano wa haya kwenye kitabu 'Upotofu wa Madhehebu ya Uwahabi' ukurasa wa 80.

⁴⁵ -Ndugu wa Khalifa wa pili Umar Bin Al-Khattaab radhia Ilaahu an'hu

Ndugu zake, jamaa zake wakaribu, watawala na wanachuoni waovu, wote walimpinga na kulichafua jina lake, lakini Sheikh hakukata tamaa, aliendelea na kazi hiyo adhimu, mwisho walipanga njama za kumuua, Sheikh akalazimika kuhama mji aliozaliwa (Al-Uyaina) na kwenda **Dir'iyya**, mji uliokuwa chini ya utawala wa **Mfalme Muhammad bin Suudi** -Allah amrehemu- yeye alimpokea kwa heshima na taadhima na kumkirimu.

ii- Hali zao katika ibada na elimu ya dini;-

Hali ya kiibada na elimu ya dini ilikuwa ni dhaifu mno katika miji ya kiislamu, kiasi ambacho watu walikuwa hawasimamishi Swala wala hawatekelezi chochote katika mambo ya Uislamu, kwa ufupi watu walikuwa ni Waislamu wa majina tu. Sheikh alifanya daawa kwa njia ya kuwasomesha watu na kuandika vitabu, na kuwapelekea risala (barua) zilizobeba nasaha kwenda kwa watawala wa miji mbalimbali na wanachuoni wao, akiwataka warudi kwenye mafunzo sahihi ya Uislamu. Daawa hii ilileta matunda mazuri na kuurudisha uhai wa Uislamu katika miji. Na ushahidi wa hilo ni haya maneno ya Imamu Shaukaniy -Allah amrehemu-;

"ومن دخل تحت حوزته أقام الصلاة والزكاة والصيام وسائر شعائر الإسلام، ودخل في طاعته من عرب الشام الساكنين ما بين الحجاز وصعدة غالهم إما رغبة وإما رهبة، وصاروا مقيمين لفرائض الدين بعد أن كانوا لا يعرفون من الإسلام شيئاً ولا يقومون بشيء من واجباته إلا مجرد التكلم بلفظ الشهادتين على ما في لفظهم به من عوج وبالجملة فكانوا جاهلية جهلاء كما تواترت بذلك الأخبار إلينا."

"Na aliyeingia kwenye himaya yake anasimamisha Swala, anatoa Zaka, anafunga na hutekeleza zilizobaki katika nembo za Uislamu. Waliingia katika utawala wake Waarabu wa Sham wanaoishi baina ya Hijaaz (Makka na Madina) na Sa'dah (Yemen) na wengi wao waliingia ima kwa mapenzi au kwa kuogopa, **na wakawa wanasimamisha Faradhi za dini baada ya kuwa hawajui kitu chochote katika Uislamu na wala hawatekelezi yaliyowajibu isipokuwa kutamka Shahada mbili tu** pamoja na upogo (kupinda) uliopo kwenye matamshi yao. Kwa ujumla watu walikuwa katika ujinga uliopindukia kama zilivyotufikia habari kwa wingi."⁴⁶

⁴⁶ Tazama Al-Badru At-Twaali'u juzuu ya I ukurasa wa 356.

Hiyo ndiyo hali halisi ilivyokuwa wakati wa kudhihiri daawa ya Sheikh Muhammad bin Abdil Wahabi.

4- DAAWA YA SHEIKH MUHAMMAD BIN ABDIL WAHABI KWA WATU WAKE

Pamoja na upinzani mkubwa uliomkabili Sheikh Muhammad na Propaganda iliyokuwa ikifanywa na mahasimu zake kwa lengo la kumchafua, pamoja na hayo Daawa yake ilikubalika kwa watu wa miji mbalimbali na hatimae kujiunga nae na kumnusuru. Na kwa ufupi, Daawa yake ilikuwa katika hatua kama nne;-

i- Hatua ya kwanza;-

Kufundisha elimu

Sheikh Muhammad Bin Abdil Wahabi –Allaah amrehemu- alitoa juhudi kubwa ya kusomesha elimu ya dini. Na kwa juhudi yake hiyo, Allah alimuafikisha kutoa wanafunzi wengi mno, na miongoni mwao ni watoto wake; Husein, Abdullahi, Ali na Ibrahim, hawa walikuwa ni wanachuoni wakubwa katika wakati wao.

ii- Hatua ya pili;-

Kuandika vitabu

Sheikh pia alijishughulisha sana na uandishi wa vitabu, na vitabu vyake viliwalenga sana watu wa kawaida na wanafunzi wenye kuanza sasa kutafuta elimu, na kwa sababu hiyo vikawa vitabu vyake ni vidogo, vyenye lugha nyepesi. Na miongoni mwa vitabu hivyo ni;-

- 1- Kitabu At-Tawheed
- 2- Kashfu Subhaati
- 3- Thalaathatul-Usuuli au Usuulu Thalaathah
- 4- Qawaaidul-Arba'a
- 5- Usuulu As-Sittah
- 6- Nawaaqidhul-Islaami
- 7- Masaailul-Jaahiliyya
- 8- Mukhtasaru Siirati Ar-Rasuuli swalla Ilaahu alayhi wasallam
- 9- Kitabul-Kabaairi

10- Ar-Raddu Alaa Ar-Raafidha

11- Fadhaailul-Qur'ani

12- Tafsiru Ayaatil-Qur'anil-Kariim

13- Al-Hadiithi (Mijelledi minne) Na vinginevyo ambavyo vinafika takribani vitabu arobaini.

iii- Hatua ya tatu;-

Kuandika barua

Sheikh Muhammad Bin Abdil Wahabi aliwaandikia barua wakuu mbali mbali wa miji kwa lengo la kuwafikishia Daawa.

Na ushahidi wa hilo, ni mwaka 1204 H/1789 A.D. ulipozuka mzozo wa kuvunjwa majengo ya makaburi na kukatazwa watu kuwaomba watu wema waliokufa, Sheikh Muhammad Bin Abdul Wahabi alimpelekea barua Shariif Ghalib, aliyekuwa mtawala wa Makka kwa lengo la kumnasihi na kumbainishia hali halisi na kiini cha mzozo, na hii ifuatayo ni matini ya barua hiyo;

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

من محمد بن عبد الوهاب إلى العلماء الأعلام في بلد الله الحرام، نصر الله بهم دين سيد الأنام عليه أفضل الصلاة والسلام، وتابعي الأئمة الأعلام.

سلام عليكم ورحمة الله وبركاته؛ وبعد: جرى علينا من الفتنة ما بلغكم، وبلغ غيركم، وسببه: هدم بناء في أرضنا على قبور الصالحين، ومع هذا نهيناهم عن دعوة الصالحين، وأمرناهم بإخلاص الدعاء لله. فلما أظهرنا هذه المسألة، مع ما ذكرنا من هدم البناء على القبور، كبر على العامة، وعاضدهم بعض من يدعي العلم، لأسباب ما تخفى على مثلكم، أعظمها اتباع الهوى، مع أسباب آخر.

فأشاعوا عنا: أنا نسب الصالحين، وأنا على غير جادة العلماء، ورفعوا الأمر إلى المشرق والمغرب، وذكروا عنا أشياء يستحي العاقل من ذكرها؛ وأنا أخبركم بما نحن عليه، بسبب أن مثلكم ما يروج عليه الكذب، ليتبين لكم الأمر، وتعلموا الحقيقة. فنحن - والله الحمد - متبعون لا مبتدعون، على مذهب الإمام أحمد بن حنبل... ثم اعلّموا وفقكم الله: إن كانت المسألة إجماعاً، فلا نزاع، وإن كانت مسائل اجتهاد، فمعلومكم أنه لا إنكار في من يسلك الاجتهاد؛ فمن عمل بمذهبه في محل ولايته، لا ينكر عليه. وأنا أشهد الله وملائكته، وأشهدكم أني على دين الله ورسوله، وإني متبع لأهل العلم، غير مخالف لهم؛ والسلام.

"Kutoka kwa Muhammad bin Abdil-Wahabi kwenda kwa Maulamaa watukufu wa mji mtukufu wa Allah -kwa kupitia wao Allah ainusuru dini ya Bwana wa watu, zishuke juu yake swala na salaam, na wafuasi wa Maimamu watukufu.

Assalaam alaykum warahmatullaahi wabarakatuh; ama baada ya yaliyotangulia, zimepita baina yetu fitna kwa kiasi kilichowafikia na kuwafikia wengineo, na sababu yake ni kuyavunja majengo yaliyoko katika nchi yetu kwenye makaburi ya watu wema, pamoja na haya tuliwakataza watu kuwaomba watu wema na tuliwaamrisha kumtakasia Allah kwa maombi.

Tulipoyadhihirisha masuala haya na yale tuliyoyataja ya kuvunja majengo yaliyopo juu ya makaburi, jambo hilo lilikuwa kubwa kwa watu wajinga, wakisaidiwa na baadhi ya wanaodai elimu, kwa sababu ambazo hazijifichi kwa watu mfano wenu, sababu kubwa zaidi ni kufuata matamania pamoja na sababu nyinginezo.

Wakatupakazia kwamba sisi tunawatukana watu wema, na kwamba mimi siko katika njia ya Maulamaa, na wakalinyanyua jambo hili hadi mashariki na magharibi, wakatutaja sisi kwa mambo ambayo mwenye akili huona aibu kuyataja.

Mimi nitakuelezea msimamo tulionao, kwa sababu watu mfano wenu ni katika wasiodanganywa, ili ubainikiwe na jambo hili na ujue uhakika wake.

Sisi -wali llaahil hamdu- ni wenye kufuata, na wala si wenye kuzusha, tuko kwenye madhehebu ya Imamu Ahmad Ibn Hanbali....Kisha juweni -Allah awape Tawfiiq- kama masuala (haya ya kuvunja makaburi yanafaa) kwa makubaliano ya wanachuoni wote basi hakuna mzozo, na kama ni masuala ni ya jitihada basi mnajua kuwa haifai kumpinga mtu anayeifanyia kazi jitihada yake, (kwa sababu) mtu hapingwi kwa kufuata madhehebu yake kwenye mahali pa utawala wake.

Na mimi ninamshuhudiza Allah na Malaika wake na ninakushuhudizeni nyinyi pia kwamba mimi niko kwenye dini ya Allah na Mtume wake na ninawafuata wanachuoni na si mwenye kutofautiana nao. Wasallaam.⁴⁷ Mwisho wa kunukuu.

⁴⁷-Tazama Ad-Duraru As-Saniyya, juzuu ya ukurasa wa 57-58, na Muallafaat Sheikh Muhammad bin Abdil-Wahabi, ukurasa wa 40.

iv- Hatua ya nne;-

Kupeleka wajumbe kwa wakuu wa miji

Sheikh Muhammad alitumia njia tofauti za daawa kama alivyofanya Bwana Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam, na miongoni mwa njia hizo ni kuwatumia wajumbe ambao wengi wao ni katika wanafunzi wake kwenda katika miji mbalimbali ili kuwabainishia watu kile wanachokiitakidi, na kwa lengo la kufuta udanganyifu uliokuwa ukienezwa na mahasimu zake. Na utaratibu huu uliendelezwa na wanafunzi wake hata baada ya kifo chake.

Na ushahidi wa hilo ni mwaka 1211 Hijiriyya Mfalme **Abdul-Aziz bin Muhammad bin Suudi** mmoja kati ya wafalme walionufaika na Daawa ya Sheikh Muhammad Bin Abdil Wahabi alituma jopo la Maulamaa kutoka Najdi wakiongozwa na **Sheikh Hamad Bin Nasri bin Muammar** kwenda Makka kwa Shariif Ghaalib kwa ajili ya mjadala wa kielimu⁴⁸.

Na katika mwaka 1215 Hijiriyya Mfalme huyo aliwaandikia Maulamaa na watawala wa miji akiwabainishia msimamo wa Daawa yao na ukweli wa kile wanachokilingania, kwa mfano aliwapelekea watu wa Yemen baadhi ya vitabu vyake, anasema Imamu Shaukaniy -Allah amrehemu-;

"وفي سنة ١٢١٥ وصل من صاحب نجد المذكور مجلدان لطيفان أرسل بهما إلى حضرة مولانا الإمام حفظه الله أحدهما يشتمل على رسائل لمحمد بن عبد الوهاب كلها في الإرشاد إلى إخلاص التوحيد والتنفير من الشرك الذي يفعله المعتقدون في القبور. وهي رسائل جيدة مشحونة بأدلة الكتاب والسنة، والمجلد الآخر يتضمن الرد على جماعة من المقصرين من فقهاء صنعاء وصعدة ذكروه في مسائل متعلقة بأصول الدين وجماعة من الصحابة، فأجاب عليهم جوابات محررة مقررة محققة تدل على أن المجيب من العلماء المحققين العارفين بالكتاب والسنة.

⁴⁸-Tazama Rawdhatul-Afkaari wal-Afhaami, cha Husein bin Ghannaam, ukurasa wa 197-198.

"Mnamo mwaka 1215 Hijiriyya ilifika kutoka kwa mtawala wa Najdi (vitabu vilivyo kuwa katika) Mijalladi miwili iliyomizuri, aliipeleka kwa Maulaana Imamu -Allah amuhifadhi-, mjalladi wa kwanza umekusanya vitabu vya Muhammad bin Abdil Wahabi vyote viko katika kuelekeza kwenye Ikhlas na Tauhiid, na kuwakimbiza watu kwenye Shirki ambayo walikuwa wakiifanya wenye kuitakidi (itikadi mbaya) katika makaburi. Navyo ni vitabu vilivyosheheni hoja za Qur'ani na Sunna, na Mjalladi mwingine umekusanya majibu dhidi ya jamaa waliozembea miongoni mwa wanachuoni wa San'a na Sa'dah waliofanya nae Mudhaakara kwenye masuala yanayofungamana na misingi ya dini na kuhusu jamaa katika Maswahaba, akawajibu kwa majibu yaliyohaririwa, yaliyothibitishwa, yaliyohakikiwa vizuri, yanayofahamisha kwamba aliyejibu ni miongoni mwa Maulamaa wenye kuhakiki mambo na ni katika watambuzi wa Kitabu (Qur'ani) na Sunna."⁴⁹

5- MAADUI ZAKE NA UZUSHI WAO

Sheikh Muhammad bin Abdil Wahabi-Allah amrehemu- ni katika watu waliopata upinzani mkubwa sana kutoka kwa baadhi ya wanachuoni waliotofautiana nae katika misimamo. Na kwa masikitiko makubwa wapinzani wake wengi walitumia mbinu za uongo na uzushi zaidi kuliko hoja za kielimu, na baadhi yao walikuwa ni watu waliosifika kwa elimu. Na huu ufuatao ni miongoni mwa uongo wao;-

i- Kumzulia kuwa alidai Utume;-

Wamedai maadui wa Sheikh Muhammad bin Abdil Wahabi kwa lengo la kumchafua na kuichafua Daawa yake, kwamba Sheikh Muhammad alikuwa akidai Utume! Na mtu wa kwanza kuleta madai hayo alikuwa ni Sheikh **Muhammad Ibn Abdir-Rahman Ibn A'faaliq**, aliposema;

والله لقد ادعا النبوة بلسان حاله لا بلسان مقاله، بل زاد على دعوى النبوة، وأقمتموه
مقام الرسول، وأخذتم بأوامره ونواهيه

"Wallaahi alidai Utume kwa ulimi wa hali yake na si kwa maneno yake, bali alizidi juu ya madai Utume, na mkamuweka mahali pa Mtume na mkazichukua amri zake na makatazo yake."⁵⁰

⁴⁹ -Tazama Al-Badru At-Twaali'u juzuu ya 1 ukurasa wa 356.

⁵⁰ - Tazama Daawa Al-Munaawi-ina uk wa 97.

Kisha ukaendelezwa uongo huo na **Bwana Ahmad Ali Al-Qibbaniy** katika kitabu chake **Faslul-Khitabi** ukurasa wa 167 kwa kuhoji;

"أتري أن كل هؤلاء العلماء الذين هم ورثة الأنبياء ضلّوا وأضلّوا من نحو ستمائة سنة إلى أن بعث الله متنبّي العيّنة داعياً إلى دين الإسلام"

"Hivi unaona kwamba hawa Maulamaa wote ambao ndio warithi wa Mitume wamepotea na wamepoteza watu kwa kiasi cha miaka mia sita mpaka Allah alipomleta mwenye kudai Utume kutoka Uyainah kuwa ndiye mlinganizi wa Uislamu"?

Naye **Sharifu Alawi Al-Haddaadi** anauendeleza uongo huo dhidi Sheikh Muhammad kwa kusema katika kitabu chake **Misbaahul-Anaami** ukurasa wa 4:-

"وكان يضمّر دعوى النبوة، وتظهر عليه قرائنها بلسان الحال، لا بلسان المقال، لثلاث تنفر عنه الناس، ويشهد بذلك ما ذكره العلماء من أن عبد الوهاب كان في أول أمره مولعاً بمطالعة أخبار من ادعى النبوة كاذباً كمشيملمة الكذاب وسجاح والأسود العنسي وطلحة الأسدي وأصراهم."

"Na alikuwa anaficha (moyoni mwake) madai ya Unabii, na zinadhihiri juu yake dalili zake kwa ulimi wa hali, na si kwa ulimi wa maneno, ili watu wasimkimbie, na linashuhudiwa hilo na yale waliyoyataja Maulamaa kwamba Abdul Wahabi alikuwa mwanzoni mwa jambo lake akipenda kusoma habari za wenye kudai Utume kama Musailima Al-Kadhaab, Sajaah, Al-As'wad Al-Ansiy, Tulaiha Al-Asadiy na mfano wao."

Lakini Maulamaa wa Ahli Sunna kwa wakati huo hawakukaa kimya walimjibu kwa majibu mazuri kabisa, miongoni mwao ni **Sheikh Suleiman Ibn Suhmaan** katika kitabu chake alichokiita '**Al-Asinnatul-Hidaadi fiy Raddi Alaa Alawi Al-Haddaadi**, pale aliposema;

"والجواب أن يقال لهذا الملحد المفتري: هذا من أبطل الباطل وأمحل المحال وبطلانه من وجوه: الوجه الأول: أنه زعم أنه يضمّر دعوى النبوة، وهذا أمر قلبي لا يطلع عليه إلا الله، فكيف ساغ له أن يدعي علم ما في القلوب مما لا يطلع عليه إلا علام الغيوب."

"Na jawabu ni kumwambia huyu Mulhid mwenye kuzua; (kauli yako) hii ni ya batili mno, na ni katika mambo ya muhali kabisa, na ubatili wake uko kwa njia nyingi;

Njia ya kwanza; ni pale alipodai kuwa (Sheikh Muhammad) anaficha (moyoni mwake) madai ya Utume. Sasa likiwa hili ni jambo la moyoni, hakuna anayeweza kulijua isipokuwa Allah, basi vipi imefaa kwake kudai ujuzi wa mambo yaliyomo moyoni (mwa mtu) miongoni mwa yale ambayo hawezi kuyajua isipokuwa (Allah) mjuzi wa mambo ya ghaibu"?

Na miongoni mwa wanachuoni walioueneza uongo huo ni hawa wafuatao;-

- **Ahmad Zain Dahlaani** katika kitabu chake '**Ad-Duraru As-Saniyya fiy Raddi Alaal-Wahaabiyya**' katika ukurasa wa 47.
- **Mshia Al-Aamilyi** katika Kitabu chake '**Kashful-Irtiyaabi an Atbaai**' Ibn **Abdil Wahabi**', ukurasa wa 3.
- **Jamiil Sidqiy Az-Zahaawiy** katika kitabu chake '**Al-Fajru As-Saadiq**', kwenye ukurasa wa 17.
- **Na Ahmad Mukhtaar Pasha Al-Muayyad**, katika ukurasa wa 5 wa kitabu chake '**Jalaaul-Awhaami**'.

Msimamo wa Sheikh Muhammad dhidi ya tuhuma hii:-

Sheikh Muhammad Ibn Abdil Wahabi –Allah amrehemu- alikuwa kinyume na itikadi hii ya kikafiri ambayo wamemzushia mahasimu wake, watu wa bidaa miongoni mwa Mashia na Masufi. Sheikh Muhammad Ibn Abdil-Wahabi –Allah amrehemu- alikuwa akisema waziwazi:-

"وأؤمن بأن نبينا محمداً صلى الله عليه وسلم خاتم النبيين والمرسلين ولا يصح إيمان عبد حتى يؤمن برسالته ويشهد بنبوته".

"Na ninaamini kwamba Nabii wetu Muhammad Swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam ndiye mwisho wa Manabii na Mitume, na wala haitasihi imani ya mja mpaka aamini Utume wake na ashuhudie (akiri) Unabii wake"⁵¹

Pia amesema Sheikh Muhammad:

"وأول الرسل نوح عليه السلام وآخرهم محمد صلى الله عليه وسلم"

"Na wa mwanzo katika Mitume Mursal ni Nuuh, na wa mwisho wao ni Muhammad swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam."

Ndugu msomaji! Hivi kweli inaingia akilini kuwa Sheikh Muhammad Bin Abdil Wahabi atangaze waziwazi kwenye vitabu vyake kwamba Nabii wa Mwisho ni Mtume wetu Muhammad swalla Ilaahu alayhi wasallam, kisha wakati huo huo awe anadai kwamba na yeye ni Nabii?

⁵¹-Tazama Majmuu Muallafaati Sheikh, juzuu ya 5 ukurasa wa 10.

ii- Kumzulia kwamba anamdharau Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam;-

Miongoni mwa tuhuma zao za uongo dhidi ya Sheikh Muhammad Bin Abdil Wahabi, ni madai ya kuwa anamdharau Bwana Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam. Amesema **Sharifu Alawiy Al-Haddaadi** katika kitabu chake **Misbaahul-Anaami**;-

"كان ينتقص النبي ﷺ - كثيراً بعبارات مختلفة، منها قوله: إنه طارش بمعنى أن غاية أمره أنه كالطارش الذي يرسل إلى أناس في أمر فيبلغهم ثم ينصرف، وكان بعضهم يقول عصايا خير من محمد، لأنها ينتفع بها بقتل الحيّة ونحوها، ومحمد قد مات، ولم يبق فيه نفع أصلاً، وإنما هو الطارش ومضى.... ومن ذلك أنه كان يكره الصلاة على النبي ﷺ - ويتأذى من سماعها وينهى عن الجهر بها على المنابر، ويؤذي من يفعله...."

"Alikuwa anamdharau Mtume swalla Ilaahu alayhi wasallam mara nyingi kwa ibara tofauti, miongoni mwake ni kauli yake, kwamba yeye ni **Tarishi**⁵², kwa maana ya kwamba mwisho wa jambo lake ni kuwa yeye (Mtume) ni kama Tarishi tu, ambaye anatumwa kwa watu kwa jambo, anawafikishia kisha anaondoka. Na walikuwa baadhi yao wanasema; fimbo yangu ni bora kuliko Muhammad, hupatikana manufaa kwa fimbo kwa kuulia nyoka na mfano wake, lakini Muhammad ameshakufa, hakuna tena kwake manufaa, na yeye ni kama Tarishi na ameshaondoka....na miongoni mwa hayo ni kwamba anachukia kuswaliwa Mtume swalla Ilaahu alayhi wasallam, na anaudhika kusikia, na anakataza kuidhihirisha juu ya mimbari na anawaudhi wenye kufanya hivyo...."

Msimamo wa Sheikh Muhammad dhidi ya tuhuma hii;-

Sheikh Muhammad Ibn Abdil Wahabi -Allah amrehemu- alikuwa kinyume na tuhuma hii waliyomzushia maadui zake. Hebu isome kauli yake hii iliyojaa heshima kwa Bwana Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam;-

"فرسول الله محمد ﷺ - هو سيد الشفعاء، وصاحب المقام المحمود، وأدم فمن دونه تحت لوائه."

"Mtume wa Allah, Muhammad swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam ndiye Sayyid (Bwana) wa waombezi, na ndiye mwenye mahali penye kuhimidiwa, na Adam na waliochini yake wako chini ya bendera yake."

Amesema tena Sheikh Muhammad Ibn Abdil Wahabi katika '**Majmuu Muallafaat Sheikh'** juzuu ya 4 ukurasa wa 349;

"لابد من الأدب مع رسول الله ﷺ - وتعظيم حرمةه."

"Hakuna budi kumfanyia adabu Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam na kuiadhimisha heshima yake"

⁵² -Tarishi; ni mtu wa cheo cha chini anayetumwa kupelaka ujumbe kama barua n.k.

iii- Tuhuma nyinginezo dhidi ya Sheikh Muhammad

Kwa hakika, ni kwamba Sheikh Muhammad alizushiwa uongo mwingi sana na maadui zake, jambo hilo lilimpelekea **Imamu Mahmuud Shukriy Al-Aluusi** katika kitabu chake Taarekh Najdi kuzitaja tuhuma hizo na kuzijibu. Na miongoni mwa tuhuma hizo ni hizi zifuatazo;-

Anachoma vitabu vya elimu

Anatafsiri Qur-ani kwa kufuata rai yake

Anatumia hadithi zinazoafikiana na msimamo wake

Anapinga Shafaa (uombezi) wa Mtume swalla Ilaahu alayhi wasallam

Anaharamisha kumfanyia ziara Bwana Mtume swalla Ilaahu alayhi wasallam

Anaharamisha kumswalia Mtume swalla Ilaahu alayhi wasallam

Anawakufurisha waislamu, na mtu yeyote anayekuja kwake anamsilimisha upya pamoja na kumlazimisha akubali kwamba yeye na wazazi wake walikuwa ni washirikina!!! Na mfano wa hayo miongoni mwa uzushi ulioenezwa na Mashia na Masufi. Imamu Al-Aluusi alijibu tuhuma hizo kwa kusema maneno haya yafuatayo;

"فكل ذلك زور عليهم وبهتان وكذب محض من خصومهم أهل البدع والضلال. بل أقوالهم وأفعالهم وكتبتهم على خلاف ذلك كله. فمن روى عنهم شيئاً من ذلك أو نسبته إليهم فقد كذب عليهم وافتري، ومن شاهد حالهم وحضر مجالسهم وتحقق ما عندهم علم قطعاً أن جميع ذلك وضعه عليهم وافتراه أعداء الدين وإخوان الشياطين...."

"Yote hayo (yanayosemwa) ni kuwazulia wao, na ni uongo wa wazi kutoka kwa mahasimu zao, watu wa bidaa na upotevu, bali kauli zao, vitendo vyao na vitabu vyao viko kinyume na yote hayo. Atakayepokea kuhusu wao jambo lolote lililokinyume na hivyo, au atakayewanasibishia basi huyo amesema uongo na amewazulia, atakayeshuhudia hali zao, na kuhudhuria vikao vyao, na akahakikisha

waliyonayo atafahamu moja kwa moja kwamba yote (yanayosemwa kuhusu wao) yamezuliwa na maadui wa dini na ndugu wa Shetani....."⁵³ Kisha akasema;

"وغالب من أشاع ذلك هم أهل البدع والأهواء الذين اتخذوا دينهم لهواً ولعباً وكذبوا بأقوالهم وأفعالهم على الدين المبين...."

"Na aghlabu wenye kueneza ubaya huo ni watu wa bidaa na kufuata matamanio, ambao wameifanya dini yao kuwa ni pumbao na mchezo, wakazua uongo kwa kauli zao na vitendo vyao dhidi ya dini iliyowazi....."⁵⁴

6- HALI YA KISIASA;-

Wakati ulipodhihiri ulinganizi wa Sheikh Muhammad bin Abdil Wahabi sehemu kubwa ya miji ya Kiislamu ilikuwa chini ya Dola ya Wauthman (**Ottoman Empire**). Pamoja na kuwepo kwa Dola ya Ottoman lakini bado kulikuwa na vijidola vidogo vidogo vilivyojitawala vyenye, na hilo ni kutokana na kudhoofika kwa utawala wa Ottoman hadi kufikia kutozijali tawala ndogo ambazo hazina maslahi kwao, ima kisiasa, au kiuchumi na hata kijamii, kwa ufupi ni kwamba Dola ya Ottoman kwa kipindi chake cha mwisho ilishindwa kuyatawala maeneo yake jambo ambalo lilipelekea kuzuka vijidola vidogo vidogo.

Katika sehemu za Najdi, Hijaaz, Ahsaai, Najran na kwengineko kulikuwa na watawala mbalimbali wanaojitegemea ambao walikuwa wakijiendeshea mambo yao wenyewe bila ya kuushirikisha utawala wa Ottoman.

Watawala wa **Dir-iyya (Wasaudi)** baada ya kuikubali Daawa ya Sheikh Muhammad bin Abdil Wahabi waliingia katika mizozo na majirani zao na hasa watu wa Hijaaz (Makka, Madina na vitongoji vyake), kwa sababu za kugombania mipaka na tofauti ya misimamo ya dini.

⁵³ -Tazama Taarekh Najdi ya Imamu Al-Alousiy, ukurasa wa 53.

⁵⁴ Tazama kitabu Taarekh Najdi cha Sayyid Mahmoud Shukriy Al-Alousiy, ukurasa wa 56, kilichochapishwa na Maktabatu-Thaqaafati Diiniyya – Qairo.

Wanahistoria hawa; **Dr, Nurud-Din Haatimi, DR. Shakir Mustafa, Dr, Jamal Zakariyya na Muhammad Abdul-Fatah** wanasema katika kitabu chao "**Historia ya bara Arab**" katika ukurasa wa 14 kuhusu hali za nchi mbili hizi;

"Nchi mbili hizi zilipakana, Familiya ya Saud ilitawala sehemu ya Najdi na Bani Hashim walitawala Hijaaz. Kulikuwepo na uadui mkubwa baina yao uliotokana na tofauti za kisiasa na kugombania mipaka na uadui huo ulipata nguvu zaidi kwa sababu ya tofauti za kidini..."

Na miongoni mwa ushahidi wa uadui huo ni;-

i- Kuzuiwa watu wa Dir-iyya kufanya Hija;-

Miongoni mwa matukio ya uadui yaliyofanywa na maadui wa Sheikh Muhammad ni kuwazuia waislamu wa miji yote iliyokubali Daawa ya Sheikh kwenda Makka kuhiji. Na hilo ni kutokana na kuwa watawala wa Hijaaz (Makka na Madina) ndio maadui wakubwa wa Sheikh Muhammad na Daawa yake, kwa hiyo mnamo mwaka 1183 H/1769 A.D. ilitolewa amri rasmi ya kuwazuia waislamu wa miji yote iliyokubaliana na Sheikh Muhammad bin Abdil Wahabi kwenda Makka kwa ajili ya kutekeleza faradhi ya Hija.

Lakini katika mwaka huo huo kuna msafara wa watu wa Hijaaz uliopotea njia na kuangukia kwenye mikono ya watu wa Dir-iyya (Wasaudi), watu wa Dir-iyya hawakuwalipizia ubaya wao, bali waliwakirimu na kuwafanyia ihsani ya hali ya juu na kufikishwa kwao salama, kinyume na walivyotarajia. Kutokana na fadhila hizo walifikisha salamu kwao, na hiyo ikawa ndiyo sababu ya kuruhusiwa watu wa Dir-iyya kwenda Makka kuhiji.

Na kutokana na tukio hilo, mnamo mwaka 1185 H/ 1771 A.D. **Sharif Ahmad bin Said** mtawala wa Hijaaz aliwataka viongozi wa Dir-iyya wapeleke mwanachuoni wao Makka ili wajadiliane na wanachuoni wa huko kwa lengo la kubainisha msimamo wao wa dini. Alipelekwa **Sheikh Abdul Aziz bin Abdillahi Al-Huswayni** akiwa na barua kutoka kwa Sheikh Muhammad bin Abdil Wahabi.

Majadiliano hayo yalileta natija nzuri, kwa sababu viongozi wa Hijaaz walibainikiwa na tuhuma nyingi za uongo alizokuwa akizuliwa Sheikh Muhammad bin Abdil Wahabi yeye na wafuasi wake, na kuanzia hapo kulianza maelewano mazuri baina ya nchi mbili hizi⁵⁵.

Lakini maelewano haya hayakudumu kwa muda mrefu, yalikoma baada ya **Sharif Ahmad bin Said** kuondolewa madarakani, na nafasi yake ikashikwa na mtoto wa ndugu yake **Sharifu Suruuru bin Musaid**, Bwana huyu aliyavunja maelewano hayo na kuwazuia watu wa Dir-iyya kwenda kuhiji Makka.

Katika kipindi cha utawala wa Sharifu Suruuru Wasaudi walipeleka barua ya maombi ili kuruhusiwa kufanya ibada ya Hija, walikubaliwa kwa sharti la kulipa kodi, Wasaudi walilikataa sharti hilo kwa hiyo hawakufanya Hija mwaka huo.

Na baada ya miaka miwili, mnamo mwaka 1197 H/1782 A.D. Mahujaji wa Dir-iyya waliruhusiwa kuingia Makka na sababu ya kuruhusiwa ni baada ya utawala wa Dir-iyya (Wasaudi) kumpelekea zawadi zenye thamani kubwa Sharifu Suruuru.

Mnamo mwaka 1202 H/1787 A.D. alifariki Sharifu Suruuru bin Musaid, na nafasi yake ilishikwa ndugu yake ambaye ni **Sharifu Ghalib bin Musaid**, Bwana huyu alivumilia kwa muda wa miaka miwili tu, na baada ya hapo alirudisha sera zile zile za ugomvi, akatoa hukumu ya kuzuiwa watu wa Dir-iyya kwenda Hija.

Alichukua maamuzi hayo baada ya kuona kuwa hali ya amani inachangia kuenea kwa Daawa ya Sheikh Muhammad bin Abdil Wahabi, kwa hiyo akaona bora kutokuelewana kuliko suluhu inayowatia hasara ya kupoteza wafuasi.

ii- Mwanzo wa vita na sababu zake:-

Mnamo mwaka 1205 H/ 1790 A.D. Sharifu Ghalib alipeleka jeshi la watu takriban 10,000 chini ya uongozi wa ndugu yake **Sharifu Abdul-Aziz bin Musaid** ili kuwashambulia watu wa Dir-iyya, walipofika katika mji wa **As-Sarri** makabila ya **Shamri na Mutwairi** waliungana na jeshi hilo dhidi ya watu wa Dir-iyya.

⁵⁵-Tazama Kitabu Un'waanul-Majdi juzuu ya I ukurasa wa 58-59.

Kisha wakaizingira **Qasru Bassaam** kwa muda wa miezi minne lakini hawakufanikiwa kupata walilolikusudia ndipo waliporudi zao Hijaaz.


Naye Mfalme wa Dir-iyya **Abdul-Aziz bin Muhammad bin Suudi** akatuma kikosi cha jeshi kilichoongozwa na mwanawe **Suudi bin Abdil-Aziz** ili kuzuia hujuma hiyo, watu wa Hijaaz walizidiwa nguvu, na hatimae waliomba msaada kwa mkuu wao Sharifu Ghalibu ambaye alikuja na jeshi katika mwezi mtukufu wa Ramadhani mwaka 1205 H/ Mei 1791 A.D. lakini kwa kuwa msimu wa Hija ulikaribia Sharifu Ghalib alilazimika kurudi Makka. Ndipo mfalme Abdul-Aziz alipoitumia fursa hiyo kwa ajili ya kuwatia adabu watu wa makabila ya **Shamri na Mutwairi** walioshirikiana na watu wa Hijaaz kuwapiga vita watu Dir-iyya.

Mnamo mwaka 1210 H/1795 Sharifu Ghalibu aliandaa tena jeshi kubwa lililoongozwa na **Sharif Fuhaid** kwa ajili ya kuwashambulia watu wa kabila la **Qahtwani** kwa sababu wao wenyewe waliamua kujiunga na utawala wa Wasaudi, kiongozi wa Qahtwani alikuwa Bwana **Haadi bin Qur'mulah**.

Mfalme Abdul-Aziz bin Muhammad alipopata taarifa hizo, kwa haraka alipeleka msaada wa kijeshi kwa watu wa Qahtwani, aliwatuma watu wa makabila ya **Utaibah, Mutwairi, Sahuul, Subai', A'jmani**, na makabila ya sehemu za **Dowsari** ili kuwapa nguvu watu wa Qahtwani. Sharifu Ghalibu na jeshi lake walishindwa vibaya sana na hatimae walikimbia kurudi kwao Hijaaz.

Sharifu Ghalib hakukoma kufanya uchokozi, mnamo mwaka 1212 H/ 1798 A.D. aliandaa jeshi kubwa kwa ajili ya kuyashambulia makabila yaliyomuasi na kujiunga na utawala wa Dir-iyya, hasa watu wa miji ya **Ran-yah, Bisha, na Turba**. Jeshi lake lilipiga kambi katika mji wa **Kharma**.

Mwanzoni mwa vita jeshi la Sharifu Ghalib lilipata ushindi, lakini baada ya mtawala wa Dir-iyya kupeleka msaada wa kijeshi, mapigano yalikuwa makali na hatimae jeshi la Sharifu Ghalibu lilishindwa vibaya na kutimua mbio, huku wakiacha vitu vyao vikitekwa nyara. **Imamu Muhammad bin Ali As-Shaukaaniy** amelizungumzia tukio hili kwa ufasaha zaidi katika kitabu chake **Al-Badru At-Twaali'** alipokuwa akielezea historia ya **Sharrif Ghaalib Ibn Musaa'id** na chokocho zake;



"وأخر ما وقع منه ذلك سنة ١٢١٢ فإنه جمع جيشا كثيرا وغزا نجدا ، وأوقع ببعض البلاد الراجعة إلى سلطان نجد المذكور، فلم يشعر إلا وقد دهمه جيش لا طاقة له به، أرسله صاحب نجد فهزمه واستولى على غالب جيشه قتلا وأسرا، بل جاءت الأخبار بأنه لم يسلم من جيش صاحب الترجمة إلا طائفة يسيرة ، وقتل جماعة من أشرف مكة في المعركة ، وتمت الهزيمة إلى مكة ، ولو ترك ذلك واشتغل بغيره لكان أولى له فإن من حارب من لا يقوى لحربه جر إليه البلوى فإن صاحب نجد تبلغ عنه قوة عظيمة لا يقوم لمثلها صاحب الترجمة."

"Mara ya mwisho kutokea hilo, ulikuwa mwaka 1212 Hijiriyah, (Sharraf Ghaalib) alikusanya jeshi kubwa na kuishambulia Najdi, na aliitaka baadhi ya miji iliyokuwa chini ya mtawala wa Najdi, hakutambua, ghafla akavamiwa na jeshi ambalo hakuwa na uwezo wa kulikabili, jeshi lililotumwa na mtawala wa Najdi. (Mtawala wa Najdi) akamshinda (Sharifu Ghaalib) na akaidhibiti sehemu kubwa ya jeshi lake, kwa kuliuwa na kuliteka. Bali zimekuja habari kwamba hawakusalimika katika wanajeshi wa (Sharraf Ghaalib) isipokuwa watu wachache tu, na waliuwawa katika vita hivyo watu wengi katika Masharifu wa Makka, na ulikamilika ushindi mpaka Makka. Na lau (Sharraf Ghaalib) angeliacha hilo (la kupigana na watu wa Najdi) na akajishughulisha na mambo mengine ingelikuwa ni bora zaidi kwake, kwa sababu anayepigana na mtu asiyemuweza humletea balaa, kwa sababu mtawala wa Najdi alifikia kuwa na nguvu kubwa ambayo hawezi kuikabili mwenye tarjama hii (Sharraf Ghaalib)...."⁵⁶

iii- Sulhu na kuvunjika kwake;-

Baada ya Sharifu Ghalib kushindwa katika mapambano yote hayo alilazimika kufanya suluhu, walifikiana katika sulhu hiyo kuacha vita kwa miaka sita, na waliruhusiwa watu wa miji ya Najdi kwenda Makka kuhiji. Lakini ilipofika mwaka 1217 H/1802 A.D. suluhu ilivunjika, na sababu ya kuvunjika kwake ni kutokana na baadhi ya makabila yaliyokuwa chini ya utawala wa Hijaaz kujiunga na utawala wa Dir-iyah. Sharifu Ghalib alituma ujumbe kwa serikali ya Dir-iyah kwa ajili ya mazungumzo, ujumbe huo uliongozwa na Waziri wake ambaye pia ni mkwewe **Bwana Uthman bin Abdir-Rahman Al-Mudhaifiy**.

⁵⁶-Tazama Al-Badru At-Twaali' juzuu ya 1 ukurasa wa 356.

Inasemekana kwamba Bwana huyu alipokutana na watu wa Dir-iyya aliathirika sana kutokana na tabia zao za ukarimu, upole na namna walivyokuwa madhubuti katika msimamo wao wa dini, hali hiyo ilimpelekea kujitoa kwenye serikali ya mkwewe na kujiunga na serikali ya Wasaudi, kisha akajitenga katika mji wa '**Al-Ubailaa**' uliopo baina ya Twaif na Hijaaz. Jambo hili lilizua mpasuko mkubwa kwenye utawala wa Sharifu Ghalib, na makabila mengi yaliyochoshwa na sera za Sharifu Ghalib walimuunga mkono Bwana Al-Mudhaifiy.

Sharifu Ghalib akapeleka jeshi kumshambulia mkwewe (Al-Mudhaifiy), lakini makabila yote yaliyoasi katika sehemu hizo yaliungana kumpiga Sharifu na mwaka huo wa 1217 H/ 1802 A.D. walifanikiwa kuiteka Twaif na kumfukuza mtawala (Gavana) wa Sharifu Ghalib. Serikali ya Dir-iyya ikamteua rasmi Bwana Al-Mudhaifiy kuwa ndiye Amiri wa mji wa Twaif na miji mingine iliyo karibu.

Baada ya kutekwa Twaif, Amiri Suudi aliamua kukomesha vita na watu wa Hijaaz kwa kupeleka jeshi kubwa kutoka Dir-iyya pamoja na watu wa Twaif kwa Bwana Al-Mudhaifiy. Tukio hilo lilitokea kabla ya msimu wa Hija ya mwaka ya 1217 H/1803 A.D. Sharifu Ghalib aliomba msaada kwa Dola ya Wauthman (Ottoman Empire) lakini hakupata majibu ya kufurahisha. Inasemekana pia alijaribu kuwashawishi Mahujaji ili wamsaidie kupigana na Wasaudi, lakini pia hilo halikufanikiwa.

Imamu Suudi alisubiri mpaka ulipokwisha msimu wa Hija, na Mahujaji waliporudi kwenye miji yao. Sharifu Ghalib alipoona hali ni tete aliamua kukimbilia Jeddah na kwenye kiti chake alimkalisha ndugu yake **Sharifu Abdul-Muin bin Musaid**. Bwana huyu hakutaka makuu, yeye aliamua kujisalimisha na kuomba amani kwa Wasaudi kwa sharti la kulindiwa heshima yake, Wasaudi walimkubalia maombi yake hayo. Katika mwezi wa Muharram, mwaka 1218 H/ 1803 A.D. Wasaudi waliingia rasmi katika mji wa Makka bila ya vita wala kumwaga damu. Na ikatumika mimbari tukufu ya msikiti mtukufu wa Makka kuusoma mkataba wa amani wa kuacha vita kabisa baina ya nchi mbili hizo.

Baada ya hapo Maulamaa wa Dir-iyya na wanafunzi wa Sheikh Muhammad bin Abdil Wahabi walianza darsa zao katika msikiti mtukufu wa Makka. Na mwaka huo huo ndio mwaka aliouwawa Mfalme Abdul-Aziz bin Muhammad bin Suudi na mtu mmoja



mwenye asili ya ki-Kurdi, na sehemu yake ikashikwa na mwanawe Suudi bin Abdil-Aziz.

Kidokezo:-

Uharibifu uliofanywa na maadui wa Sheikh Muhammad Bin Abdil Wahabi:-

Ndugu msomaji! Baada ya historia hiyo fupi, hebu tukitupie jicho kitabu '**Taarekh Najdi**' cha **Imamu Sayyid Mahmuud Shukriy Al-Aluusiyy** alipokuwa akiuelezea unyama wa kutisha uliofanywa na Mamluki wa Kituruki waliotokea Misri chini ya uongozi wa Ali Pasha, Mamluki hao waliuangamiza mji wa Dir-iyya, na mingineyo miongoni mwa miji ya Najdi, miji ambayo wakazi wake wengi ni wafuasi wa Sheikh Muhammad Ibn Abdil Wahabi! Anasema Imamu huyo;

"وبعد أن فرغ العسكر من هدم المدينة وتدميرها رحلوا عنها إلى الموضع المعروف (بالأموي) وهو غدير قرب بلد (ضرمي) كان سعود أمير نجد -رحمه الله تعالى- يجعل فيه خيله أيام الربيع، وبقي العسكر المصري يعيشون في أرض نجد ويخربون البلاد والقرى إلى أن أعادوا إلى بلادهم."

"Baada ya askari (wa Misri) kumaliza kuuvunja mji (wa Dir'iyya) na kuubomoa, wakaondoka kuelekea sehemu inayojulikana kwa jina la (Amawiy) nacho ni kijito kilichopo karibu na mji wa Dharma, mahali ambapo Suudi mfalme wa Najdi -Allah amrehemu- alikuwa akiwafunga Farasi wake siku za Kipupwe. Askari wa Misri walibakia hapo wakieneza uchafu katika nchi ya Najdi, wakivunja miji na vijiji mpaka waliporejea katika miji yao."⁵⁷

Swali:-

Je, baada ya dhulma hii na uonevu wa kiwango hiki bado mlitaka watu wa Najdi wanyamaze na wasijibu mashambulizi? Je, hivyo ndivyo Uislamu ulivyotufundisha? Kuweni waadilifu na wala msiipeleke historia kwa mujibu wa matamano yenu. Kwa hiyo, walichokifanya watu wa Najdi dhidi ya watu wa Hijaaz na washirika wao ni kujitetea na kulipiza kisasi.

Na dini yetu ya Kiislamu imetufundisha kuwa mtu anapofanyiwa dhulma na uonevu na anao uwezo wa kujitetea basi ni ruhusa kujitetea hata kama anayekufanyia dhuluma hiyo ni Mwislamu mwenzako.

⁵⁷ Tazama Taarekh Najdi, cha Imamu Al-Aluusiyy, ukurasa wa 31, chapa ya kwanza iliyochapishwa na Maktabatu At-Thaqaafa Ad-Diniyya, mwaka 2005, Qairo-Misri.



Kwa hiyo, watu wa Najdi walifanyiwa dhulma, walipigwa, waliuwawa, waliporwa mali zao, na nyumba zao zikatiwa moto, bali hata mimea mashambani ilikatwa, ndipo na wao walipoamua kulipiza kisasi, wakawachapa mahasimu zao mpaka wakashika adabu, wakaiteka miji yao, kwa sababu malipo ya uovu ni uovu mfano wake, kama tunavyofunzwa na Qur-ani.

Lakini uovu huo ulifika mwisho pale watu wa Najdi walipojikaza wakapigana kiume na Allah akawapa nusra, wakafanikiwa kuikomboa miji mtakatifu kutoka mikononi mwa wazushi, na hadi leo -walillaahil hamdu- miji hiyo iko kwenye himaya ya Ahli Sunna, na hali hii inawaumiza sana Mashia na mamluki wao.

Hali ya maadui wa Sheikh kidini:-

Wanahistoria wengi hata wale wapinzani wa Daawa ya Sheikh Muhammad bin Abdil Wahabi wanathibitisha kwamba askari wengi waliotoka kwenda kuivamia miji ya Ahli Sunna na kuuwa watu wake hawakuwa ni watu wa kufuata mafunzo ya Uislamu, bali wengine hawakuwa waislamu kabisa! Anasema mwanachuoni wa historia, **Sheikh Abdur-Rahmani bin Hasan Al-Jabraty Al-Azhariy**, aliyefariki mwaka 1240 Hijiriyya, alipokuwa akizungumzia matukio ya mwaka 1227 Hijiriyya katika kitabu chake '**Ajaibul-Aathaari fii Tarajumi wal-Akhbaari**', akiwanukuu baadhi ya viongozi wa jeshi la Muhammad Ali Pasha, anasema baada ya kushindwa vita:

"ولقد قال لي بعض أكابرهم من الذين يدعون الصلاح والتورع: أين لنا بالنصر وأكثر عساكرنا على غير الملة، وفهم من لا يتدين بدين، ولا ينتحل مذهباً، وصحبتنا صناديق المسكرات، ولا يسمع في عرضينا أذان، ولا تقام فيه فريضة، ولا يخطر في بالهم ولا خاطرهم شعائر الدين، والقوم -يعني: الوهابية- إذا دخل الوقت، أذن المؤذنون وينتظمون صفوفًا خلف إمام واحد بخشوع وخضوع، وإذا حان وقت الصلاة والحرب قائم أذن المؤذنون وصلوا صلاة الخوف، فتتقدم طائفة الحرب، وتتأخر الأخرى للصلاة، وعساكرنا يتعجبون من ذلك؛ لأنهم لم يسمعوا به فضلاً عن رؤيته، وينادون في معسكرهم: هلموا إلى حرب المشركين المحلقين الذقون، والمستبحين الزنا واللواط، الشاربين الخمر، التاركين للصلاة، الأكلين الربا، والقاتلين الأنفس، المستحلين المحرمات، وكشفوا عن كثير من قتلى العسكر، فوجدوهم غير مختونين) اهـ

"Waliniambia mimi baadhi ya wakuu wao ambao walikuwa wakijidai kuwa ni wema na kujichunga na mabaya; tungeshinda vipi, na hali ya kuwa askari wetu wengi walikuwa si waislamu, na kuna ambao hawafuati dini, wala hawana madhehebu, na tulisuhubiana na masanduku ya pombe, wala haisikiki katika kambi zetu adhana, wala hakutekelezwi faradhi yoyote, wala haziwapitikii katika akili zao alama za dini.

Na hali ya kuwa hawa jamaa (Mawahabi) unapoingia wakati (wa Swala) wanaadhini wenye kuadhini, wanapanga safu nyuma ya Imamu mmoja kwa unyenyekevu, na ukiingia wakati wa Swala na hali ya kuwa vita vinaendelea, wanaadhini wenye kuadhini kisha wanaswali Swala ya hofu, linasogea kundi moja la wapiganaji, na lirudi nyuma kundi jingine kwa ajili ya swala, na huku askari wetu wakiwashangaa kwa hilo, kwa sababu wao hawajawahi kusikia jambo hilo wachilia mbali kuliona. Kisha wanaitana kutoka kwenye kambi yao; njooni tuwapige washirikina, wenye kunyoa videvu, wenye kuhalalisha Zinaa, Liwatwi, wenye kunywa pombe, wenye kuacha swala, wala riba, wauwaji wa nafsi, wenye kuhalalisha mambo ya haramu, na waliwapekua wengi katika askari waliouwawa wakawakuta hawajatahiriwa⁵⁸

Ndugu msomaji! Hizo ndizo hali za mahasimu wa Sheikh Muhammad bin Abdil Wahabi na wafuasi wake, hata jeshi lao halikuwa jeshi la Kiislamu lililotoka kwa lengo la kuunusuru Uislamu na kulinda heshima ya dini, bali ulikuwa ni mchanganyiko wa wahuni, walevi, makafiri na watu wenye chuki dhidi ya Uislamu na Waislamu.

Ndugu msomaji! Kwa muhtasari huu tutakuwa tumemjibu Mshia Jaafar Mwazoa kuhusu tuhuma zake alizosiita matukio ya kikatili anayodai yamefanywa na Mawahabi, tuhuma ambazo ameziandika katika kitabu chake Shimo Refu ukurasa wa 44-45.

Na kwa muhtasari huu ndugu yangu msomaji utakuwa umefahamu kuwa Sheikh Muhammad bin Abdil Wahabi na Mfalme Abdul-Aziz Muhammad bin Suudi wao ndio waliokuwa wakipigwa vita na walichokifanya wao ni kujihami dhidi ya mashambulizi ya maadui zao, na kwa kitendo chao hicho hawastahiki kulaumiwa, kwa sababu amesema Allah Jalla wa A'laa katika Surat Shuuraa, Aya ya 39-42:

{وَالَّذِينَ إِذَا أَصَابَهُمُ الْبَغْيُ هُمْ يَنْتَصِرُونَ * وَجَزَاءُ سَيِّئَةٍ سَيِّئَةٌ مِثْلُهَا فَمَنْ عَفَا وَأَصْلَحَ فَأَجْرُهُ عَلَى اللَّهِ إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الظَّالِمِينَ * وَكَانَ انتَصَرَ بَعْدَ ظَلْمِهِ فَأُولَئِكَ مَا عَلَيْهِمْ مِنْ سَبِيلٍ * إِيمًا السَّبِيلُ عَلَى الَّذِينَ يَظْلِمُونَ النَّاسَ وَيَبْغُونَ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ أُولَئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ*} [الشورى: ٣٩-٤٢]

[39. Na ambao wanapofanyiwa jeuri hujitetea ***40, Na malipo ya uovu ni uovu mfano wake, lakini mwenye kusamehe, na akasuluhisha, basi huyo malipo yake yapo kwa Allah. Hakika yeye hawapendi wenye kudhulumu ***41, Na wanaojitetea baada ya kudhulumuwa, hao hapana njia ya kuwalaumu ***42, Bali lawama ipo kwa wale wanaowadhulumu watu, na wanafanya jeuri katika ardhi bila ya haki, hao watapata adhabu iliyochungu].

⁵⁸ 'Ajaabul-Aathaari fii Tarajumi wal-Akhbaari', juzuu ya 4 ukurasa wa 140.

Ndugu msomaji! Kwa hiyo maelezo yanayotolewa na waandishi waongo wa Shia na Masufi kama Jaafar Mwazoa na Khalifa Khamis dhidi ya Ahli Sunna wanaowaita Mawahabi ni muendelezo ule ule wa sera za kuchafuana na kupandikiza chuki na kuuficha ukweli.

Lakini walillaahil-hamdu wanachuoni wa Kiislamu wametuhifadhia historia kwa uaminifu wa hali ya juu, na yeyote anayekusudia kuupotosha ukweli historia sahihi itamsuta.

UONGO WA MSHIA MWAZOA KUHUSU UHUSIANO WA TALIBAN NA MAWAHABI

Ndugu msomaji! Hebu turudi tena kwa Mshia Jaafar Mwazoa ili ujionee uongo wake na ujinga wake kwenye maelezo aliyoyatoa kuhusu uhusiano wa Taliban na Mawahabi. Amesema Mshia huyo katika kitabu chake Shimo Refu, ukurasa wa 45:

"Je, kulikuwa na tatizo gani nchini Afghnistani kwa serikali iliyoungwa na Ahlu Sunnat wal-Jamaa chini ya uongozi wa Rabbaani?! **Hivi kwa nini Mawahabi waliifanyia fujo na kusababisha mauwaji makubwa na kuipindua Serikali hiyo, kisha kusimika serikali yao ya kiwahabi chini ya Mwendawazimu Mullah Umar**, na hatimaye baada ya muda serikali hiyo ikawa uchumi wake mkubwa unategemea kuuza "cocaine", bangi na madawa mengine ya kulevyu. Na kubwa zaidi ni kuichukua nchi hiyo na kuiweka chini ya mikono ya nchi za Magharibi mpaka leo!!!

MAJIBU YETU

Kama Jaafar Mwazoa mambo ya kielimu yamemshinda basi hata hizi siasa za kidunia pia hazijui? Maana unaweza kuwadanganya baadhi ya watu katika mambo ya dini kwa sababu hawakusoma, lakini katika Nyanja za kisiasa watu wengi wana utambuzi na maarifa kwa kiasi cha kutokudanganywa kirahisi.

Tukianza na kadhia ya Af'ghanistan, dunia nzima inafahamu kuwa Af'ghanistan chini ya serikali ya **Burhanud-Diin Ar-Rabbaani** ilipinduliwa na kundi la wanamgambo wa Taliban. Baada ya kupita kipindi kirefu Marekani wakishirikiana na Mashia wa **Mazari Sharif (Northern Alliance)**, waliipindua serikali ya Taliban iliyokuwa ikiongozwa na **Mullah Muhammad Umar** na kuisimika serikali yao chini ya **Rais Mshia Haamid Karzay**.

Swali, la msingi la kujiuliza je, Taliban ni Mawahabi? Nadhani hili ndilo jambo ambalo watu wengi hawalifahamu, akiwemo Mshia Jaafar Mwazoa, labda kwa kuona wanamgambo wa Taliban wana ndevu nyingi, na huwenda kwa akili yake akadhania kwamba kila mwenye ndevu ni Wahabi!

Ukweli kuhusu Taliban:-

Ukweli ni kwamba, Taliban ni wapinzani wa mnaowaita Mawahabi, na hilo ni kutokana na tofauti za kiitikadi zilizopo baina yao, kwa sababu Wataliban ki-itikadi ni wafuasi wa **Abu Mansour Al-Maaturidiy**, na katika madhehebu ya fiqhi wao ni wafuasi wa Imamu Abu Hanifa, na Twariqa yao ni Diobandiyya⁵⁹.

Kwa hiyo, **Mullah Muhammad Umar** na viongozi wenzake wa Taliban ki-itikadi ni Maaturidiyya na ki-fiqhi ni Hanafiyya na Twariqa yao ni Diobandiyya, ambayo ni Twariqa ya ki-Sufi iliyoasisiwa katika mji wa Diobandi huko India...⁶⁰

Na hilo limetiliwa nguvu kwa ushahidi wa Watalibani wenyewe, wameeleza katika kitabu chao **Taarekh Dar Al-Uloomi bi-Diobandi**, juz 1 uk 428; "Darul-Uloomi ni ya kiislamu ki-dini, Ahlu Sunna kundi, Hanafi kimadhehebu, **Sufi kimuelekeo**, Maaturidiyya, Ash'ariyya kifalsafa, Jishtiyya kitabia..."

⁵⁹ - Kwa faida zaidi, tazama; <http://www.islamonline.net/politics/2001/09/article25.Shtml>.

⁶⁰ - Tazama [www. Aljazeera.net/news asia/2001/9/916-23-10htm](http://www.Aljazeera.net/news/asia/2001/9/916-23-10htm).

Anasema mmoja kati ya wanachuoni wa Diobandi naye ni **Sayyid Husein Ahmad Al-Madaniy** katika kitabu chake **As-Shihaabu At-Thaaqib**; "Ama wakubwa wetu wanatofautiana na Mawahabi katika mambo yote haya, kwa hiyo kuwanasibisha wakubwa wetu na Uwahabi ni kuwazulia na ni tuhuma ya wazi." Kisha akazitaja tofauti zinazowatofautisha wao na Mawahabi, miongoni mwa hizo ni:

- Mawahabi hawakubaliani na vitendo vya Kisufi kama Muraaqaba, Dhikri...
- Mawahabi hawaelekei kaburi la Mtume wakati wa maombi...
- Mawahabi wanaona kusoma Dalailu Al-Khairaat, Burdah na Hamziyya kuwa ni bid'a na upotevu..
- Mawahabi wanaitakidi kutumia Tumbaku, na Sigara kuwa ni katika madhambi makubwa
- Mawahabi wanapinga Maulidi ya Mtume...

Kwa hiyo, maneno ya Mshia Jaafar Mwazoa aliposema;

"Hivi kwa nini Mawahabi waliifanyia fujo na kusababisha mauwaji makubwa na kuipindua Serikali hiyo, kisha kusimika serikali yao ya kiwahabi chini ya Mwendawazimu Mullah Umar..."

Maneno haya ni miongoni mwa ufedhuli wake ambao haukujengwa juu ya misingi ya kiutafiti, bali ujinga na chuki ndizo zilizomuongoza na kumpelekea kutamka hayo, kwani tangu lini Masufi na watu wa Twariqa wakawa ni Mawahabi? Au kwa sababu ya ndevu? Mbona hata beberu anazo!!!

SURA YA NNE

DOLA YA SWAFAWIYYAH

(SAFAVID EMPIRE 1502-1785 A.D.)

Ndugu msomaji! Kutokana na Mshia Jaafar Mwazoa kutaja katika kitabu chake **Shimo Refu**, katika ukurasa wa 44-45 matukio aliyoyaita kuwa ni ya kikatili yaliyofanywa na Mawahabi⁶¹ bila ushahidi wowote, tumeona itakuwa ni fursa ya dhahabu kwako kukudokezea baadhi ya matukio ya kikatili tena ya kishenzi yaliyofanywa na Mashia Ithnaashariyya wakati wa Dola yao ya Swafawiyya (Safavid Empire) dhidi ya Waislamu wa madhehebu ya Ahli Sunna wal-Jamaa.

Dola ya Swafawiyya ndiyo Dola kubwa pekee ya ki-Shia Ith'naashariyya, na kabla ya hapo Shia Ithnaashariyya hawajawahi kuwa na Dola kubwa kama hii, wala hawana historia ya kueneza Uislamu katika miji ya Makafiri.

Ilikuwepo **Dola ya Faatwimiyya (Fatimid Islamic Caliphate)** iliyosimama mnamo mwaka 358-567 Hijiriyya sawa na 969-1172 A.D. lakini Dola hii ilikuwa ni ya Mashia Ismailiyya (Ismailism).

Pia ilikuwepo **Dola ya Bani Buwaihi/Buwaihiyyuuna (The Buying dynasty)** wenye asili ya Daylami, Kaskazini mwa Iran, mnamo mwaka 930-1048 A.D. na Dola hii ilifanya vituko vingi dhidi ya Uislamu na Waislamu, na inasemekena kuwa Dola hii ilielemea zaidi kwenye mrenge wa **Shia Zaidiyya**.

Katika sehemu hii tutakutajia historia fupi ya Dola ya ki-Shia Ith'naashariyya (Dola ya Swafawiyya) na matukio yao ya kikatili waliyoyafanya dhidi ya Waislamu, na Insha-Allah tutakutajia matukio hayo kwa ushahidi wa marejeo ya vitabu vya historia vyenye kutegemewa, na wala hatutafanya kama alivyofanya Mwazoa kuleta matukio hewa, ambayo hayana ushahidi wowote.

⁶¹ - Walillaahil-Hamdu suala la Uwahabi tumelizungumzia kwa kirefu katika sura iliyopita na tumezibu tuhuma zake zote kwa hoja za kielimu.

Historia ya muasisi wake kwa ufupi:-

Muasisi wa Dola hii ni **Abul Muzaffar Shah Ismail Al-Haadi Ibn Haydar Ibn Al-Juneid As-Safavi** aliyezaliwa Ardabil (kaskazini magharibi mwa Iran) Rajab 25, 892 Hijiriyya, sawa na July 17, 1487, amefariki Tabriz Rajab 18, 930 Hijiriyya, sawa na Mei 23, 1524 A.D, na kuzikwa huko Ardabil.

1- WATAWALA WA DOLA YA SWAFAWIYYA NA VIPINDI VYA UTAWALA WAO

- 1- **Shah Ismail Al-Haadi As-Safavi**, (الشاه إسماعيل الهادي الصفوي) aliyetawala kwa miaka 22, kuanzia mwaka 1502-1524 A.D. Bwana huyu aliwaamrisha wafuasi wake (Kizilbas) wamsujudie na wao wakafanya hivyo.
- 2- **Shah Tahmasp** (الشاه طهماسب الأول) alitawala baada ya kifo cha baba yake kwa miaka 52, kuanzia mwaka 1524- 1576 A.D, akiwa na umri wa miaka 11 tu.
- 3- **Shah Ismail ii**, (الشاه إسماعيل الثاني) alitawala kwa mwaka 1, kuanzia mwaka 1576-1577 A.D. alipinga baadhi ya uzushi wa Kishia, wafuasi wake wakamtuhumu kuwa amekuwa Sunni wakamuua kwa kumuwekea sumu.
- 4- **Shah Mohammed Khodabandeh**, (الشاه محمد خداينده) alitawala kwa miaka 10, kuanzia mwaka 1577-1587 A.D.
- 5- **Shah Abbas (The Great)** (الشاه عباس الكبير), **mwenyewe alijiita mbwa wa kizingiti cha Ali!** (كلب عتية علي) alitawala miaka 42, kuanzia mwaka 996-1038 Hijiriyya, sawa na mwaka 1587-1629 A.D.
- 6- **Shah Safi i**, (الشاه صفي بن صفي ميرزا عباس أو صفي الأول) huyu alikuwa ni mjukuu wa Shah Abbas, alitawala miaka 13, kuanzia mwaka 1629-1642 A.D.
- 7- **Shah Abbas ii**, (الشاه عباس الثاني) alitawala kwa miaka 25, kuanzia mwaka 1642-1667 A.D.
- 8- **Shah Suleiman Safi ii**, (الشاه سليمان صفي الثاني) alitawala kwa miaka 27, kuanzia mwaka 1667-1694 A.D.
- 9- **Shah Sultan Husein**, (الشاه سلطان حسين الصفوي) alitawala kwa miaka 28, kuanzia mwaka 1694-1722 A.D. Bwana huyu alihalalisha pombe katika wakati wake.

- 10- **Shah Tahmasp ii**, (الشاه طهماسب الثاني) alitawala miaka 10, kuanzia mwaka 1722-1732 A.D.
- 11- **Shah Abbas iii**, (الشاه عباس الثالث ميرزا ابن طهماسب) alitawala kwa miaka 4, kuanzia mwaka 1732-1736 A.D.

2- WANACHUONI WA DOLA YA SWAFAWIYYA

Baada ya Mashia lth'naashariyya kupata Dola na kushika hatamu za utawala katika miji ambayo watu wengi ni wafuasi wa madhehebu ya Ahli Sunna, walitumia sera za nguvu katika kueneza itikadi zao za Kishia, na waliwatumia Wanachuoni wao kwa lengo hilo hilo.

Na wanachuoni hao wa Shia walitoa mafunzo mbalimbali ambayo ni kinyume na Uislamu kwa lengo la kuwaridhisha watawala wao waovu, kama vile kufaa kumsujudia kiongozi n.k. Na miongoni mwa Wanachuoni wa Shia wanaotajwa katika kuitumikia Dola hii na malengo yake ni hawa wafuatao:-

- 1- **Ali bin Abdil-Ali Al-Karkiy Al-Aamilyi** maarufu kwa jina la **Muhaqiqi Thani** aliyefariki mwaka 940 Hijiriyya.
- 2- **Zainud-Din Al-Aamilyi** maarufu kwa jina la **As-Shahiid Ath- Thaniy**, aliyeuwawa mwaka 977 Hijiriyya.
- 3- **Al-Muala Muhammad Muhsin Al-Faidhu Al-Kaashaniy**, mtunzi wa vitabu; **Tafsiri As-Swaafiy**, na **Al-Waafiy**, na kitabu hiki ni miongoni mwa vitabu vinane vikubwa vya Shia lth'naashariyya, amefariki mwaka 1091 Hijiriyya.
- 4- **Muhammad Bin Hasan Al-Hurru Al-Aamilyi**, aliyezaliwa mwaka 1033 Hijiriyya sawa na 1623 A.D. aliamia Iran akitokea Jabal Aamil Lebanon mnamo mwaka 1073 Hijiriyya/1662 A.D. na akapewa cheo cha **Sheikhul-Islami na Qadhi wa Maqadhi wote**, alifariki katika mji wa Mash'had mnamo mwaka 1104 Hijiriyya sawa na 1692 A.D. na yeye ndiye mtunzi wa kitabu '**Wasaailu As-Shia ilaa Tahsiili Masaili As-Sharia**' ambacho ni miongoni mwa vitabu muhimu katika madhehebu ya Shia.
- 5- **Mirza Muhammad Baqir Al-Majlisiy**, mwenye kitabu **Biharul-An'waari** na **Mir-atul Uquuli**, amefariki mwaka 1111 Hijiriyya.

6- **Ni'matullahi Al-Jazaairiy**, mtunzi wa kitabu *Al-An'waru An-Nu'maniyya*, amefariki mwaka 1112 Hijiriyya.

ITIKADI POTOFU NA UZUSHI WALIOUDHIHIRISHA

KIPINDI CHA UTAWALA WAO

Baada ya Mashia Ith'naashariyya kupata nguvu za Dola waliamua kulivua vazi la Taqiyya na kudhihirisha yale ambayo hawakuweza kuyadhihirisha kabla ya hapo, na haya yafuatayo ni baadhi ya mambo waliyoyadhihirisha wakati wa Dola yao hiyo:

- ➔ **Tahriiful-Qur'ani**, Maulamaa wa Shia Ith'naashariyya waliidhihirisha itikadi yao chafu ya kwamba; Qur'ani hii tuliyonayo Waislamu mikononi mwetu si kamili! Na ukibahatika kuvisoma vitabu vyao kama; **Tafsiru As-Swaafiy ya Al-Kaashaaniy, Tafsirul-Burhani ya Al-Bahraaniy, Biharul-An'wari na Mir'atul-Uquuli**, vyote vya **Al-Majlisiy, Al-An'waru An-Nu'maniyya** cha **Ni'matullahi Al-Jazairiy** na vinginevyo, ukivisoma vitabu hivyo utaziona riwaya na kauli zenye kuthibitisha ukafiri huo.
- ➔ **Kuwatukana, Kuwalaani na Kuwakufurisha Maswahaba** wa Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam wazi wazi, pamoja na kuwa jambo hili lilikuwepo katika Dola za Shia zilizotangulia, lakini si kwa kiwango kama kilichofikiwa na Dola hii ovu. Wanachuoni wa Dola hii walilifunua pazia la Taqiyya na kuwa wa wazi zaidi katika kuwachukia Maswahaba, na hilo utaligundua kwa kusoma vitabu vyao kama; **Biharul-An'waari** hasa katika juzuu ya 33, na kitabu **Al-An'waaru An-Nu'maniyya** kwa juzuu zake zote nne.
- ➔ **Maombolezo ya Muharram** kwa ajili ya kifo cha Husein, kwa kufanya maandamano na kujipiga kifuani, kichwani n.k.⁶² na jambo hili utaligundua kwa kusoma kitabu '**As-Swilatu baina At-Tasawufi wa At-Tashayyui**', cha Mshia **As-Shaibiy**, ukurasa wa 372.

⁶²-Katika kitabu chetu '**Msimamo wa Ahli Sunna juu ya kifo cha Husein**' tumelibainisha jambo hili kwa hoja za kielimu na kuthibitisha kuwa Shia ndio waliohusika katika mauaji ya Husein radhia Ilaahu an'hu, Allah akifanyie wepesi kutoka kwake.

- ➔ **Kuidhirisha Shahada ya tatu** katika Adhana, na Insha-Allah tutaelezea asili ya Shahada hii kwenye sura ya tano ya kitabu hiki.
- ➔ **Kusujudu juu ya kidongo cha Karbala.** Na hii ni athari iliyobakia hadi leo, ukiingia katika misikiti yao wakati wa Swala utakuthibitikia ukweli wa maneno haya.
- ➔ **Kuyaimarisha Makaburi ya Maimamu** wao kwa kuyajengea nyumba na makuba kwa vito vya thamani.
- ➔ **Kuiteka miji ya Ahli Sunna wal-Jamaa** na kuwalazimisha watu wake wafuate madhehebu ya Shia, kama tutakavyokuelezea katika sura hii Insha-Allah.
- ➔ **Kuwauwa Maulamaa wa Ahli Sunna** na kufukua makaburi yao na kuichoma moto mifupa yao, kama tutakavyokuelezea hapo mbele katika sura hii.

HALI YA UISLAMU KABLA YA DOLA YA SWAFAWIYYA

Kabla ya kudhahiri kwa Dola ya Shia Ith'naashariyya (Dola Swafawiyya) ilikuweco Dola ya Ahli Sunna ya Uthmaniyya (**Ottoman Empire**) iliyoongozwa na watawala wa Kituruki, Dola ambayo ilitawala takriban karne sita na nusu. Dola hii kubwa ya Kiislamu ilisimama kuanzia mnamo mwaka 687 Hijiriyya sawa na mwaka 1289 A.D hadi mwaka 1343 Hijiriyya sawa na mwaka 1924 A.D.

Katika karne ya kumi na nne, kumi na tano, na mwanzoni mwa karne ya kumi sita Milaadiyya (A.D.) Uislamu ulipata nguvu kubwa duniani, na nguvu kubwa hiyo ilitokana na sera za Dola ya **Uthmaniyya (Ottoman Empire)** ya kueneza Uislamu katika nchi za Ulaya, na kwa sababu hiyo ikawa ndiyo Dola kubwa ya Kiislamu yenye nguvu, inayoogopewa na Makafiri. Dola hii ilitawala sehemu kubwa ya Kaskazini mwa **Afrika, Asia, Ulaya Mashariki**, kama vile; **Bulgaria, Austria, Hungaria, Yugoslavia, Romania, Georgia, Armenia** na sehemu kubwa katika nchi za muungano wa **Urusi**.

Watawala wa nchi za Kikristo katika Ulaya Magharibi kama vile; **Italia, Ufaransa, Uingereza, Hispania**, na **Ureno**, walikuwa hawalali kutokana na hofu ya kuingiliwa na Uislamu katika nchi zao. Kwa hiyo, walikuwa wakiitafuta fursa ndogo tu ya kuzizuia harakati za kutanuka kwa Uislamu zinazofanywa na Dola hii au kuiangusha kabisa.

KUSIMAMA KWA DOLA YA SHIA SWAFAWIYYA

NDIYO SABABU YA KUDHOOFIKA KWA NGUVU ZA WAISLAMU

Mnamo mwaka 915 Hijriyya sawa na mwaka 1502 A.D. ilisimama Dola ya Shia Ithnaashariyya (Safavid Empire), ikiongozwa na **Mshia Shah Ismail Ibn Haydar Safavi**. Kusimama kwa Dola hii ya **Kishia Ithnaashariyya** (Dola Swafawiyya) kulikuwa ni balaa kwa Uislamu na Waislamu, kwa sababu ilipelekea kudhoofika kwa nguvu za Dola ya Uthmaaniyya na kupoteza muelekeo wa sera zake za kuunza Uislamu hasa katika nchi za Ulaya ya Mashariki, na kwa hakika jambo hilo lilileta faraja na furaha kubwa kwa Makafiri wa Ulaya na duniani kwa ujumla.

Kuna mambo mengi ya kiuadui yaliyofanywa na Mashia hao yaliyopelekea kudhoofika kwa nguvu za Waislamu na kusimama kwa harakati za Jihad ndani ya Ulaya. Na miongo ni mwa mambo hayo;

Ni pale walipokuwa Waislamu wakipambana na Wakristo kwa ajili kuueneza Uislamu ndani ya Ulaya, na kuihami miji yao isichukuliwe na Makafiri, ndipo Mashia kupitia Dola yao ya Swafawiyya walipoanza mashambulizi yao ya kishenzi dhidi ya Masunni.

Na mfano wa hilo ni pale Mujahiidina wa Ahli Sunna walipokuwa wameizingira nchi ya **Austria** kwa miezi sita, na kukuribia kuingia katika mji mkuu wa nchi hiyo (**Vienna**), ghafla zilifika taarifa za kushitusha kwa mtawala wa Dola ya Uthmaaniyya kwa wakati huyo ambaye alikuwa ni Bwana **Saliim i (Al-Awwal)** kuwa Mashia wanaivamia miji ya Ahli Sunna na kufanya mauaji ya kinyama dhidi ya watu wake.

1- UVAMIZI WA MASHIA KATIKA NCHI YA IRAN

Nchi ya **Iran** kwa zaidi ya karne tisa ilikuwa chini ya Ahli Sunna, na ilitoa Maulamaa wakubwa wa kutegemewa hasa katika madhehebu ya **Shafiy**, mpaka ilipovamiwa na Mashia wa Swafawiyya wakaubadilisha muelekeo wa nchi hiyo kwa dhulma na uadui, wakawauwa Maulamaa wa Ahli Sunna na kuvichoma moto vitabu vyao. Na hii ifuatayo ni baadhi ya miji walivamia katika nchi ya Iran;-


i- Uvamizi wao katika mji wa Tabriz⁶³;

Tabriz ni makao makuu ya Mkoa wa **Azerbaijan** ya **Mashariki nchini Iran**, na ni mji wa nne kwa ukubwa katika nchi hiyo baada ya **Tehran, Mash'had na Isfahan**. Baada ya **Mshia Shah Ismail Safavi** kuuteka mji huu, Mashia waliufanya kuwa ndio mji mkuu wao baada ya **Isfahan**, na kwa wakati huo inakadiriwa kuwa idadi ya wakazi wake ni takriban watu laki mbili (200,000).

Mnamo siku ya Ijumaa, tarehe 1 Muharram, 907 Hijiriyya sawa na tarehe 17 Julay, 1501 A.D. Jeshi la Shia lth'naashariyya likiongozwa na Shah Ismail Safavi waliuvamia mji wa Tabriz, na moja kwa moja walielekea msikiti mkuu wa mji huo, Shah alipanda juu ya mimbari, na kuwalazimisha waliohudhuria msikitini hapo ambao ni Masunni kuwatukana Maswahaba, Abu Bakar, Umar, Uthman na Aisha mke wa Mtume swalla llaahu alayhi wasallam na kuwalaani. Hakuna hata mtu mmoja aliyekubaliana na amri hii, Shah akaliamrisha jeshi lake kumchinja kila aliyekataa kutii amri hiyo, kwa hiyo hakuna hata mtu mmoja katika waliohudhuria aliyepona, wote walikhitari mauti kuliko kuwavunjia heshima Maswahaba watukufu.

Siku ya pili, Shah aliamrisha wakamatwe Maulamaa wote, Maimamu wa misikiti, waadhini, Maqadhi wa mji, na wao pia walilazimishwa kuwatukana Maswahaba na kuwalaani, na atakayekataa achinjwe, kwa siku chache tu alizokaa Tabriz, Shah aliuua zaidi ya watu elfu ishirini (20,000).

⁶³-Kwa faida zaidi kuhusu historia ya uvamizi wao na uchafu walioufanya katika mji huu, soma vitabu vifuatavyo: **Iran Swafawiyya**, cha **Dr, Amir Husein Khunjiy**, ukurasa wa 113-115, na kitabu **Aalim Araai Safawi** ukurasa wa 54.



Wanahistoria wanaoelezea matukio yaliyoikumba **Tabriz** wanasema mnamo mwaka 880 Hijiriyya; Mashia walivunja majengo yote ya kidini, kuanzia **misikiti, madrasa**, na kuzifuta alama zote za kihistoria katika mji huo, halikadhalika waliuvunja msikiti mkuu wa **Tabriz** ambao ulikuwa ukihesabika ni katika kumbukumbu za kifahari za mji huo. Bali walifikia kufukua makaburi na kuitoa mifupa ya Maulamaa wa Ahli Sunna na watu mashuhuri kisha wakaichoma moto na kuyatupa majivu yake barabarani. Pia wanajeshi wa Shia waliwabaka wanawake na kuwanajisi watoto wadogo, na waliwauwa wanawake wenye mimba kwa kuyapasua matumbo yao kisha waliwachoma moto.

ii- Uvamizi wao katika mji wa Mash-had:

Uislamu uliingia katika mji huu wa **Mash'had** uliopo katika nchi ya Iran, katika zama za Khalifa wa tatu **Uthman Ibn Affan** -Allah amridhie-. Na katika mji huu ndipo alipozikwa Imamu wa nane wa Shia Ithnaashariyya, **Imamu Ali bin Musa (Ar-Ridha)** na kaburi lake Mashia wanaliabudu, kwa kuswali, kuomba hapo na kufanya Twawaaf. Mash'had kwa sasa ndio makao makuu ya Mkoa wa **Razan Khorasan**, Asili ya wakazi wa mji huu walikuwa ni Ahli Sunna wal-Jamaa.

Mnamo mwaka 916 Hijiriyya = 1510 A.D Mashia chini ya utawala wa Shah **Abbas Al-Kabiir (The Great)** waliuteka mji huu wa Mash'had kutoka kwa Masunni na kuwauwa watu zaidi ya elfu kumi⁶⁴.

Na baada ya kuuteka mji huu Mashia waliubadilisha mji huu na kuufanya kuwa ni katika miji yao mitakatifu. Shah aliwakataza Mashia kwenda kuhiji Makka bali wakahiji Mash'had kwenye kaburi la Imamu wao Ali Ridha, na yeye mwenyewe Shah Abbas alionesha mfano, alitembea umbali wa kilometa 1200 kutoka mji wa Isfahan hadi Mash'had kwa mguu kwa muda wa siku 28, kwa ajili ya kuhiji kaburi la Imamu Ali Ridha!!!⁶⁵

⁶⁴ -Tazama kitabu **Iran Diraasatun Aamah** cha Dr, Muhammad Wasfiy, ukurasa wa 247.

"إيران دراسة عامة" د. محمد وصفي (ص ٢٤٧).

⁶⁵ Tazama kitabu 'Shah Abbas Al-Kabiir' cha Dr, Badii Muhammad Juma, ukurasa wa 101-102.

iii- Uvamizi wao katika mji wa Shirvan;

Shirvan ni mji uliopo Mkoa wa Khorasan ya Kaskazini nchini Iran, pia mji huu unaitwa **Sharvan, Shirwan, Shervan, Sherwan na Servan** na kwa Kiarabu شيروان. Anaelezea mmoja kati ya jamaa wa ukoo wa Shah Ismail Safavi, mwandishi mashuhuri aitwaye **Ibrahim Sib'ghatu Ilahi Al-Heydariy** juu ya ukatili alioufanya Mshia huyo;

"أَكْثَرَ الْقَتْلِ حَتَّى قَتَلَ مَلِكَ شَرْوَانَ وَأَمْرًا أَنْ يُوَضَعَ فِي قَدَرٍ كَبِيرٍ وَيَطْبَخُ وَأَمْرًا بِأَكْلِهِ فَفَعَلُوا (أي القزلباشية)، وكان لا يتوجه لبلاد في إيران إلا فعل أشياء يندى لها الجبين من قتل ونهب حتى قتل من أعظم علماء العجم "السنة" وحرق كتبهم..... ثم أمر الشاه إسماعيل الجنود بالسجود له. وكان من دمويته أن ينبش قبور العلماء والمشايخ "السنة" ويحرق عظامهم، وكان إذا قتل أميراً من الأمراء أباح زوجته وأمواله لشخص ما."

"Alikithirisha mauaji, mpaka alifikia kumuua mfalme wa **Shirvan**, kisha akaamrisha **awekwe kwenye chungu** kikubwa na **apikwe**, kisha akaamrisha **aliwe, Kizilbas**⁶⁶ wakatekeleza amri hiyo (**wakamla**)!!! Shah hakuingia mji wowote katika nchi ya Iran isipokuwa alifanya mambo (ya kusikitisha) ambayo huchuruzika jasho kwayo paji la uso, kutokana na mauaji (aliyoyafanya) na kupora mali, aliwaua wanachuoni wakubwa wa kiajemi wa Ahli Sunna na kuvichoma moto vitabu vyao.....

Shah Ismail aliwaamrisha askari wake wamsujudie!!! Na kutokana na tabia yake ya kumwaga damu, aliyafukua makaburi ya Maulamaa na Masheikh wa Ahli Sunna na kuichoma moto mifupa yao. Na akimuua kiongozi yeyote anamhalalisha mke wake na mali zake kwa wafuasi wake."⁶⁷

Hivi ndivyo Ushia ulivyoingia katika nchi ya Iran, nchi ambayo asili yake ni Ahlu Sunna tena Mashafii!!! Je, mambo yakifikia hivyo tusemeje? Masunni na Mashia ni ndugu, au ni maadui? Dini yao moja au kila watu na dini yao?

⁶⁶ -**Kizilbas**; ni kabila lenye nguvu nchini Iran, asili yao ni Uturuki, ni muungano wa makabila tisa, walikuwa ni askari watiifu wa Dola ya Safavi.

⁶⁷ Tazama Kitabu '**Unuanul-Majdi**', ukurasa wa 119-120.

2- UVAMIZI WA MASHIA KATIKA NCHI YA AF'GHANISTAN

Uvamizi wao katika mji wa Herat⁶⁸;

Herat ni mji mkubwa uliopo Magharibi mwa nchi ya Afghanistan, na kwa lugha ya Kiarabu unaitwa هَرَات. Mshia Shah Ismail Safavi aliingia katika mji wa Herat msimu wa kipupwe katika mwezi wa Ramadhani mwaka 889 Hijiriyya sawa na mwaka 1510 A.D. Mshia huyu alipeleka jeshi lake huko **Herat**, wakazi wa mji huo walijisalimisha bila ya kuleta upinzani wowote, kwa kuhofia yasijewasibu yaliyowasibu wenzao katika miji mingine.

Wakiwa katika mfungo wa Ramadhani, wakazi wote wa Herat walikusanywa katika Msikiti Mkuu pamoja na wanazuoni wao na viongozi wote wa mji, kisha akalazimishwa **Qadhi mkuu** wa mji huo apande kwenye mimbari **awatangazie watu kuwa yeye amebadilika kutoka kwenye madhehebu ya Sunni kwenda kwenye madhehebu ya Shia Ith'naashariyya, kisha amtukane Abu Bakar, Umar, Uthman na awalaani, pia atoe fat'wa ya kwamba Masunni ni Makafiri!!!** Lakini Qadhi huyo hakukubaliana na amri hiyo. Kizilbas ambao ni askari wa Shah wakalipasua tumbo lake na kuumwaga utumbo wake nje hapo hapo kwenye mimbari.

Baada ya kumuua Qadhi mkuu walimuamrisha **Mufti mkuu** wa mji huo, **Sheikh Al-Hafidh Zainud-Din Ali**, kutekeleza yale waliyomuamrisha Qadhi mkuu, Mufti naye alikataa, bila ya huruma askari hao waovu walilipasua tumbo lake, wakautoa utumbo wake na kuurusha kwa waliohudhuria. Kisha Mashia hao wakauwawa Maulamaa wengi wa Ahli Sunna na viongozi waliobakia na maiti zao wakazichoma moto.

⁶⁸-Tazama maelezo ya habari hizi kwenye vitabu vifuatavyo: **Iran Swafawiyya** cha **Dr, Amir Husein Khunjiy**, ukurasa wa 171-174, chapa ya kwanza ya mwaka 2010 iliyochapishwa na Maktabatu Naafidha. **Kitabu 'Shammul-Awaaridhi fiy dhammi Rawaafidhi'** ukurasa wa 6, cha Mwanachuoni **Mulla Ali bin Sultan Al-Qaariy** aliyefariki mwaka 1014 Hijiriyya, na yeye alikuwa shuhuda wa matukio haya maovu.

Na siku iliyofuata waliwakamata wakuu wengine wa mji huo na kuwafunga jela. Pia walimkamata mjukuu wa **Sheikh Sa'du Din At-Taftazaaniy** ambaye kwa wakati huo ulikuwa umri wake umevuka miaka sabini, walimfunga jela, Bwana huyu alikuwa ni mwanachuoni mkubwa kwa wakati huo na ndiye marejeo ya ulimwengu katika elimu. Shah aliamrisha Sheikh huyu aletwe mbele yake, kisha akamlazimisha atoke kwenye madhehebu ya Ahli Sunna aingie kwenye Ushia, alipokataa, Shah aliamrisha auwawe kwa kukatwa vipande vipande kisha atiwe kwenye moto! Askari wa Shah walitii, na Sheikh alifanyiwa unyama wote huo akiwa katika Swaumu ya Ramadhani -Allah amrehemu yeye na Waislamu wote-.

Kisha askari wa Kishia wakaanza kuuwa raia, wakabomoa misikiti ya Masunni, madrasa zao, na majengo ya kihistoria, mji ukabaki mtupu kabisa, kisha wakafukua makaburi ya wanachuoni na miili yao ikachomwa moto.

3- UVAMIZI WA MASHIA KATIKA NCHI YA IRAQ

Uvamizi wao katika mji wa Baghdad:

Mnamo mwaka 1510 A.D, Mashia waliuvamia mji wa **Baghdad** na kuuteka bila ya upinzani wowote. Mshia Shah Ismail aliwaamrisha wafuasi wake kuuvunja mji, na kuwauwa watu, na kuwaadhibu wengine kwa adhabu kali bila ya hatia yoyote. Pia aliwaamrisha askari wake waovu kuyafukua makaburi ya Maulamaa wa Ahli Sunna na kuitoa miili yao na kuichoma moto! Miongoni mwa makaburi yaliyofanyiwa hujuma hiyo ni kaburi la **Sheikh Abdul-Qadir Jailaniy⁶⁹**, pia waliuliwa watu wa familia yake, na baadhi yao walikimbilia **Sham, Misri na Hijaaz**, halikadhalika walilihujumu kaburi la **Imamu Abu Hanifa**, na habari za kaburi hili tutazitaja hapo mbele Insha-Allah na hapo ndio utafahamu kiwango cha uadui wa Shia lth'naashariyya dhidi ya Ahli Sunna wal-Jamaa.

Anasema **Mshia Badrud-Din Ibn Shad'qami Al-Alawiy** katika kitabu chake '**Tuhfatul-Az'haari**' akielezea mambo aliyoyafanya Mshia Shah Ismail alipoivamia Baghdad;-

⁶⁹-Sheikh mkubwa katika madhehebu ya Hambali, ambaye watu wa Twariqa ya Qaadiriyya wanajinasibisha na yeye na kumtukuza hadi kuvuka mipaka.

"فَتَحَّ بَغْدَادَ وَفَعَلَ بِأَهْلِهَا النَّوَاصِبِ ذَوِي الْعِنَادِ مَا لَمْ يُسْمَعْ بِمِثْلِهِ قَطُّ فِي سَائِرِ الدُّهُورِ بِأَشَدِّ أَنْوَاعِ الْعَذَابِ حَتَّى تَبْشَرَ مَوْتَاهُمْ مِنَ الْمُبُورِ."

"Aliuteka mji wa Baghdad na akawatendea watu wake Nawaasibu (Ahlu Sunna) wenye ukaidi mambo ambayo hayajawahi kusikiwa mfano wake katika zama zote, aliwaadhibu adhabu kali, mpaka alifikia kuwafukua maiti zao kutoka kwenye makaburi"⁷⁰

Ndugu msomaji! Hiki ndio kiwango cha uadui wa Mashia dhidi ya Ahli Sunna wal-Jamaa, hawakutosheka kuwaadhibu waliohai na kuwauwa, bali walifikia kufukua maiti waliomo makaburini na kuwachoma moto!!!

Nadhani Mashia wengi hawaifahamu kabisa historia hii chafu ya wazee wao, ndio maana utawaona vijana wenzangu kama kina Jaafar Mwazoa na mwalimu wake AbdulRazaq Amir Juma wanaropoka ovyo, na lau kama wangekuwa wanaijua historia yao na aibu zilizomo kwenye madhehebu yao wasingethubutu kupanua vinywa vyao vichafu na kuyasema vibaya madhehebu mengine.

KUFUKULIWA KWA KABURI LA IMAMU ABU HANIFA

Miongoni mwa mambo ya kinyama ambayo hayatasahaulika katika historia ya Kiislamu ni kitendo cha Mashia -hawa wanaolilia umoja na Masuni- kulifukua kaburi la **Imamu Abu Hanifa (Nu'mani Ibn Thabit)** –Allah amrehemu- na **kuitoa mifupa yake na kuichoma moto**, kisha wamkazika **Mbwa mweusi mahali pake!!!** Si kwamba unyama huu uko kinyume na maadili ya dini tu, bali uko kinyume kabisa na haki za kibinadamu.

Na jambo ovu zaidi na la kusikitisha ni kuwaona Maulamaa wa **Shia Ith'naashariyya** kama **Ni'matullaahi Al-Jazaairiy** ambaye ni mmoja kati ya Mamluki wa Dola ya Swafawiyya, akilielezea tukio hili kwa kebehi na istihizai! Kwa kudai kwamba uovu huu uliofanywa na watawala wao dhidi ya kaburi la **Imamu Abu Hanifa** eti ni miongoni mwa karama zake! Anasema Mamluki huyo –Allah amlipe anayostahiki-;

⁷⁰-Tazama kitabu '**Audatu As-Swafawiiyina**' cha Abdul Aziz Al-Mahmuud, ukurasa wa 10.

"وأما الكرامات التي ظهرت من قبور أئمتهم الأربعة فهي أكثر من أن تحصى، وأعظمها، الكرامات التي شاهدها الناس من قبر أبي حنيفة؛ وذلك أن السلطان الأعظم شاه عباس الأول لما فتح بغداد أمر بأن يجعل قبر أبي حنيفة كنيفاً . وقد واقف وقفاً شرعياً بغلتيين وأمر بربطهما على رأس السوق ، حتى إن كل من يريد الغائط يركمهما ويمضي إلى قبر أبي حنيفة لقضاء الحاجة . وقد طلب خادم قبره يوماً فقال له : ما تخدم في هذا القبر وأبو حنيفة الآن في أسفل درك الجحيم؟ . فقال : إن في هذا القبر كلباً أسوداً دفننه جدك المرحوم الشاه إسماعيل لما فتح بغداد قبلك فأخرج عظام أبي حنيفة وجعل موضعها كلباً أسوداً فأنا أخدم ذلك الكلب " . ثم قال هذا الرافضي الخبيث؛ "وكان صادقاً في مقالاته لأن المرحوم شاه إسماعيل فعل مثل هذا."

"Ama Karama ambazo zimedhihiri kwenye makaburi ya Maimamu wao wanne (Abu Hanifa, Maliki, Shaafi, na Ahmad) ni nyingi hazidhibitiki. Na karama kubwa zaidi kuliko zote ambayo waliishuhudia watu kwenye kaburi la Abu Hanifa; ni pale **Sultan Mkuu Shah Abbas wa kwanza** alipoiteka Baghdad, aliamrisha kaburi la Abu Hanifa lifanywe kuwa Jaa/Jalala (sehemu ya kutupia takataka), na akaweka Waqfu wa kisheria wa **nyumbu**⁷¹ wawili, na akaamrisha wafungwe sokoni, ili kila anayetaka kukidhi haja anawapanda wanyama hao kwenda kwenye kaburi la Abu Hanifa kwa ajili ya kukidhi haja. Siku moja aliulizwa muhudumu wa kaburi la (Abu Hanifa); wewe unahudumia nini kwenye kaburi hili, na hali ya kuwa Abu Hanifa hivi sasa yuko kwenye tabaka la chini kabisa motoni? Akasema; **kwenye kaburi hili amezikwa Mbwa mweusi**, amezikwa na babu yako marehemu **Shah Ismail** alipoiteka Baghdad kabla yako, aliitoa mifupa ya Abu Hanifa kisha akazika mahali pake mbwa mweusi, kwa hiyo mimi ninamuhudumia mbwa huyo."

Kisha Ni'matullaahi Al-Jazaairiy akamalizia kwa kusema; "**Amesema kweli kwenye maneno yake, kwa sababu Shah Ismail alifanya hivyo.**"⁷²

⁷¹-**Nyumbu** aliyekusudiwa hapa ni mnyama aliyezalikana kutokana na punda na farasi. Inasemekana kuwa nyumbu hao wa kuwapeleka watu kwenye kaburi la Imamu Abu Hanifa lililogeuzwa kuwa choo na jaa, walipewa majina ya Makhaliifa wawili, mmoja alitwa Abu Bakar na mwingine alitwa Umar!!!

⁷²-Tazama **Al-An'waaru An-Nuumaniiyah**, juzuu ya 2 ukurasa wa 324.

Ndugu msomaji! Hawa ndio Shia lth'naashariyya, na hii ndiyo historia yao na hivi ndivyo vituko vyao walivyovifanya dhidi ya Maimamu wa Ahli Sunna, eti leo wao wamekuwa wema, wanamwaga machozi wakililia umoja na Masunni!

Kwa ufupi ni kwamba, Mashia waliendeleza vitendo vyao vya uvamizi kwenye miji mbalimbali ya Ahli Sunna na kufanya mauaji ya kinyama, kama vile; **Khorasan, Diyar-Bakir, Anatolia**, na kuwauwa watu wake, waliendelea hivyo hadi walipofanikiwa kuiteka miji yote iliyopo baina ya **Ghuba ya Uarabuni (Arabian Gulf)** hadi **Caspian sea**, na kuanzia **Mto Furat (Euphrates River)** hadi **Amudarya (Amu River)**.⁷³ Na katika miji yote hiyo, Mashia waliwalazimisha Masunni kufuata itikadi zao chafu kwa nguvu, na kila aliyekataa walimuua, mpaka wanachuoni wa historia wamefikia kutaja idadi ya kutisha kuhusu mauaji hayo. Inasemekana kwamba waliuwawa Masunni zaidi ya milioni moja.

BUNGE LA MASUNNI LAWAJADILI MASHIA

Baada ya Mashia kuiteka miji ya Ahli Sunna na kuwalazimisha Masunni kuingia kwenye Ushia kwa nguvu, na kufanyika kwa mauaji ya kinyama dhidi ya Ahli Sunna na kufukuliwa makaburi ya Maulamaa wao kisha kuchomwa moto miili yao, habari zilifika makao makuu ya Dola ya Uthmaaniyya huko Uturuki, ndipo Bunge la nchi hiyo likakutana mnamo mwaka 920 Hijiriyya/1514 A.D. chini ya usimamizi wa mtawala **Sultan Saliim i (Al-Awwal)** na viongozi wa serikali yake wakiwemo Maulamaa,⁷⁴ Maqadhi, Makamanda wa kivita, na viongozi wa kisiasa, wote walikubaliana kwamba Mashia ni hatari kwa ustawi wa Kiislamu ulimwenguni, kwa hiyo ni lazima itangazwe hali ya hatari, na watu wajiandae kwa ajili ya Jihadi dhidi ya maadui hawa wa Uislamu.

⁷³-Tazama As-Shia fil-Mizaani, juz 24 uk 2 akimnukuu Mustashriq Rolnads katika kitabu chake Aqiidatu Shia, ukurasa wa 77, kilichochapishwa mwaka 1946.

⁷⁴ Na miongoni mwa Maulamaa hao alikuwepo Mwanachuoni mkubwa aliyejulikana kama **Sheikhul-Islami Alaoud-Din Ahmad Aqsaraayi Ar-Ruumiy**, baada ya Mwanachuoni huyo kuelezwa hali halisi ya Mashia na waliyoyafanya dhidi ya Waislamu, Sheikh alitoa fat'wa ya kupigana Jihad dhidi ya waharibifu hao, vibaraka wa Makafiri waliojificha nyuma ya pazia la Ahlil-Baiti kwa lengo la kuubomoa Uislamu.

Na kabla ya kuchukua hatua zozote za kijeshi, mtawala huyo wa Dola ya Uthmaaniyya, **Sultan Saliim i** alimuandikia barua Mshia Shah Ismail ya kumuonya juu ya ubaya wa vitendo vyake, na alimlingania arudi kwenye Uislamu, na barua hiyo ilikuwa na ujumbe huu ufuatao:-

"إن علماءنا ورجال القانون قد حكموا عليك بالقصاص يا إسماعيل بصفتك مرتداً، وأوجبوا على كل مسلم حقيقي أن يدافع عن دينه وأن يحطم الهراطقة في شخصك أنت وأتباعك البلهاء ولكن قبل أن تبدأ الحرب معكم فإننا ندعوكم لحضيرة الدين الصحيح قبل أن نشهر سيوفنا وزيادة على ذلك فإنه يجب عليك أن تتخلى عن الأقاليم التي اغتصبها منا اغتصاباً ونحن حينئذ على استعداد لتأمين سلامتك."

"Kwa hakika Maulamaa wetu na wanasheria wamekuhukumia Kisasi ewe Ismail kwa kukupa wasifu wa mtu Murtaddi (aliyetoka kwenye Uislamu) na wamewajibisha kwa kila Mwislamu wa kweli kuitetea dini yake na kuuvunja **Uzandiki** kwenye utu wako wewe na wafuasi wako wapumbavu, lakini kabla ya kuanza vita na wewe, sisi tunakulingania urudi kwenye hadhira ya dini sahihi kabla ya hatujachomoa panga zetu dhidi yako, na zaidi ya hapo, pia ni wajibu juu yako kuiachia miji yote uliyoipora, na sisi tuko tayari kukupa amani kwa usalama wako."⁷⁵

Masunni waingia kwenye mapambano dhidi ya Shia;-

Pamoja na tahadhari hiyo na kuonywa huko, lakini Mshia Shah Ismail na wafuasi wake hawakujali, walifanya kiburi na kuendeleza ubabe wao dhidi ya Ahli Sunna. Na mnamo tarehe 22/ Muharram/920 Hijiriyya sawa na tarehe 23 August 1514 A.D. Sultan Saliim I alichukua maamuzi ya kuwatetea Ahlu Sunna na miji yao dhidi ya hujuma zilizofanywa na Mashia, na hiyo ndiyo ikawa sababu kubwa ya kutokea mapigano ya **Galdiran** جالديران (**Battle of Caldiran**)⁷⁶, na Mashia walishindwa vibaya sana. Wakafanikiwa kuuteka mji **Tabriz** ambao ndio uliokuwa mji mkuu wa Dola hiyo ovu ya Swafawiyya, na Mshia Shah Ismail alikimbia, na hatimaye mkewe aliangukia kuwa ni jumla ya mateka katika mikono ya Waislamu.

⁷⁵ -Tazama kitabu '**Juhudul-Uthmaniyyiin Li-Inqaadhil-Andalusi**', cha **Dr, Nabiil Abdil-Hayyi Ridh'wani**, ukurasa wa 435. ٤٣٥. ص . نبييل عبد الحي رضوان / د. جهود العثمانيين لإنقاذ الأندلس / د.

⁷⁶ -**Caldiran** ni mji ulipo kwenye Mkoa wa Van Kaskazini Mashariki mwa nchini Uturuki.

Mikataba ya Khiyana;⁷⁷⁻

Baada ya Mashia kushindwa vibaya na kutolewa katika miji ya Waislamu, walianza kutafuta msaada kutoka kwa Wakristo na kuingia nao mikataba ya siri kwa lengo la kuiangusha Dola ya Kiislamu. Miongoni mwa mikataba hiyo ni:-

- ➔ Ushirikiano wa jeshi la baharini baina ya serikali ya **Ureno** na serekali ya Mashia kwa ajili ya kuishambulia **Bahrein na Al-Qatif**, mji uliopo Mashariki mwa **Saudi Arabia (Ash Sharqiyyah)**.
- ➔ Kusaidiana baina yao na Wareno katika kuzima harakati za uasi huko **Balochistan na Makran**, Mkoa uliopo kusini mashariki mwa **Iran**.
- ➔ Kuwepo muungano baina ya serikali ya Mashia na **Ureno** kwa ajili ya kuiangusha Dola ya Kiislamu ya Uthmaaniyya (**Ottoman Empire**).
- ➔ Serikali ya Mashia watakiachia kisiwa cha Hormoz (**Hormoz Island**) kijitawale chini ya usimamizi wa Makafiri wa Kireno na wao hawataingilia kwenye mambo ya ndani ya Hormoz.
- ➔ Halikadhalika Mshia Shah Ismail alipeleka ujumbe فينيسيا **Venice**, nchini **Italia** kwa ajili ya kuomba msaada wa kuishambuli Dola ya Kiislamu ya Uthmaaniyya kwa njia ya baharini na wao wataendeleza mashambulizi yao kwa upande wa nchi kavu. Halikadhalika Shah Ismail alifunga mikataba na serikali ya **Hispania** kwa lengo hilo hilo la kuiangusha Dola ya Uthmaaniyya.

Na miongoni mwa ushahidi wa khiyana za Shia lthnashaariyya dhidi ya Masunni ni ile barua iliyoandikwa na Kamanda wa Kireno **Sir Afonso de Albuquerque** kwenda kwa **Mshia Shah Ismail Safavi** akimwomba ushirikiano wa kuiangusha Dola ya Kiislamu ya Uthmaaniyya (**Ottoman Empire**).⁷⁸ Na barua hiyo ilisema hivi:-

⁷⁷-Soma maelezo ya Khiyana za Mashia Swafawiyya dhidi ya Waislamu kwa urefu zaidi kwenye vitabu vifuatavyo; **Juhuudu Uthmaniyyiina Li-inqaadhil-Andalusi** ukurasa wa 437. **Qira-atun Jadidatun fiy Taarikh Uthmaniyyiina**, ukurasa wa 63. **Ad-Daulatul-Uthmaaniyya Awaamilun-Nuhuudhi wa Asbaabu As-Suqutwi**, ukurasa wa 162-169.

⁷⁸-Tazama **Ad-Daulatu Al-Uthmaaniyya Awaamilu An-Nuhuudhi wa Asbaabi As-Suqutwi**, ukurasa wa 167. Pia tazama kitabu **Qira-atun Jadidat fi Taarekh Uthmaniyyiina**, ukurasa wa 63.

"إنني أقدر لك احترامك للمسيحيين في بلادك، وأعرض عليك الأسطول والجند والأسلحة لاستخدامها ضد قلاع الترك في الهند، وإذا أردت أن تنقض على بلاد العرب أو تهاجم مكة فستجدني بجانبك في البحر الأحمر، أمام جدة أو في عدن أو في البحرين أو القطيف أو البصرة، وسيجدني الشاه بجانبه على امتداد الساحل الفارسي وسأنفذ له كل ما يريد."

"Mimi ninathamini heshima yako kwa Wakristo waishio katika nchi yako, na nitakuletea Manoari, askari na silaha, ili uzitumie dhidi ya kambi za Waturuki (Ottoman Empire) zilizopo India, **na kama utataka kuishambulia miji ya waarabu, au kuishambulia Makka**, utanikuta niko ubavuni kwako kwenye **Red Sea**, mbele ya **Jeddah, Aden, au Bahrein, au Al-Qatiif, au Basra**, na Shah atanikuta niko ubavuni mwake kuanzia pwani ya Uajemi na nitamtekelezea kila anachokitaka."

Njama hizi ziligundulika mapema na makao makuu ya **Istambul** na kuzimwa kwa haraka kabla ya kutokea hujuma yoyote.

HALI YA MAYAHUDI NA WAKRISTO WAKATI WA DOLA YA SWAFAWIYYA

Wakati walipokuwa Waislamu wa Ahli Sunna wakionja moto wa adhabu kutoka kwa watawala wa Dola hiyo ya Mashia kutokana na ukatili na mateso waliyofanyiwa ndani ya miji yao, Mayahudi, Wakristo na Majusi (wenye kuabudu moto) waliishi kwa raha na amani, bila ya bugh'dha yoyote. Anaelezea **Mshia Abbas Iq'baali**:

"ولم يكن الشاه عباس فظاً على غير أهل السنة من دون أتباع سائر المذهب لذا فقد جلب أثناء غزواته لأرمينية والكرج نحو ثلاثين ألف أسرة من مسيحيي هذه الولايات على ما زانداران وأسكنهم بها كما رحل إلى أصفهان خمسين ألف أسرة من أرامنة جلفاء وإيران وبنى لهم مدينة جلفا على شاطئ نهر زاینده رود وأنشأ لهم فيها الكنائس وشجعهم على التجارة مع الهند والبلاد الخارجية بأن أعطاهم الحرية الكاملة."

"Shah Abbas hakuwa na roho mbaya ila kwa Masunni tu, kinyume na watu wa madhehebu nyingine. Katika kipindi cha vita vyake vya **Armenia na Kurj** aliwaleta mateka wa Kikristo zaidi ya elfu thelathini akawapa makazi sehemu za **Mazindarani**, na akazipeleka **Isfahan (Iran)** familia za Kikristo zaidi ya elfu hamsini, na akawajengea mji kwenye ufukwe wa mto **Zayanderud** (زاینده رود)

akawajengea Makanisa na akawahimiza kufanya biashara na India na nchi za nje, akawapa uhuru kamili."⁷⁹

Naye **Mlebanon Shaheen Makarios** katika kitabu chake '**Tarekh Iran**' ukurasa wa 154 anaelezea kwamba Shah Abbas alitoa tamko kwa raia wake akisema kwamba; Wakristo ni rafiki zetu na ni washirika wetu katika nchi yetu, kwa hiyo ni wajibu kwa raia wake kuwaheshimu Wakristo na kuwakirimu popote wanapotaka kuishi! Kisha akasema;

"فتح الشاه موانئ بلاده لتجار الإفرنج و أوصى ألا تؤخذ منهم رسوم على بضائعهم، وألا يتعرض أحد من الحكام أو الأهالي لهم بسوء...."

"Shah akazifungulia bandari za nchi yake kwa ajili ya maslahi ya wafanyabiashara wa kizungu, na akaamrisha wasilipishwe ushuru wowote kwa bidhaa zao, wala wasiguswe kwa ubaya wowote..."⁸⁰


Naye Mshia **Muhammad Jawad Mughniyya** katika kitabu chake **As-Shiatu fil-Miizani juzuu ya II** ukurasa wa 24 chini ya kichwa cha habari "**Daulatun Swafawiyya**" akimuelezea Shah Abbas (The Great) na utawala wake, akasema;

«قال شاهين مكاربوس في «تاريخ إيران»: خطت البلاد في أيامه خطوة واسعة إلى العظمة والتقدم، فكثرت التجارة مع الإفرنج، وتردد التجار والسائحون إلى البلاد، وتوطدت العلاقات الطيبة مع دول أوروبا وسلطان الهند.....».

"Anasema **Shaheen Makarios** katika kitabu '**Tarekh Iran**'; katika wakati wake Miji ilipiga hatua kubwa ya maendeleo, zikakithiri biashara na wazungu, kila mara walifika wafanyabiashara na watalii katika miji (ya Iran) yakaimarika mafungamano mazuri na nchi za Ulaya na ufalme wa India....." Na kabla ya hapo alisema katika ukurasa wa 8;

⁷⁹-Na kwa faida zaidi soma vitabu vifuatavyo; **As-Swafawiyyuuna wa Daulat Uthmaaniyya** cha Abul Hasan Alawiy Al-At'rajjiy, '**Harakaatu Faarisiyya Mudammira**' cha Dr, Ahmad Shebliy '**At-Tashayyu' Al-Alawiy wa Tashayyu' As-Swafawiy'**, cha Dr Ali Shari'ati.

⁸⁰-Tazama '**Tarekh Iran**' ukurasa wa 154 cha **Shaheen Makarios** kilichochapishwa mwaka 1898.



وقال صادق نشأت، ومصطفى حجازي في «صفحات عن إيران»: «وقد نشط الشاه عباس الكبير في إقامة علاقات سياسية مع دول أوروبا مما ساعد على تبادل المعلومات الصحيحة بين إيران وأوروبا، وكان عباس الكبير يبدي روح التسامح الديني نحو غير المسلمين، وكان يهتم بترقية إيران صناعياً.....».

"Wamesema **Sadiq Nash-at na Mustafa Hijaaziy** katika kitabu '**Swafahaat an Iran**';- Shah Abbas Al-Kabiir alichangamkia kuleta mafungamano ya kisiasa na nchi za Ulaya kwa kiasi ambacho ilisaidia kupeana taaluma sahihi baina ya Iran na Ulaya, na Abbas Al-Kabiir alikuwa akidhihirisha roho ya usamehevu wa kidini kwa upande wa wasiokuwa Waislamu, na yeye alikuwa akitilia umuhimu wa kuiendeleza Iran kwa viwanda...."

Ndugu msomaji! Hali ndiyo kama hiyo, wakati misikiti ya Ahli Sunna wal-Jamaa ikibomolewa na wanachuoni wao kuuwawa, Makanisa ya Wakristo, Mahekalu ya Mayahudi na Ma-Temple ya Kimajusi yalishamiri katika miji ya Iran, na wakuu wa Kiyahudi na ki-Kristo na wafuasi wao waliishi kwa raha na amani, na kufanya shughuli zao za kibiashara na harakati za kidini miongoni mwa hizo ni kuwaritadisha Waislamu ndani ya miji yao!!!

Na katika harakati zao hizo za kuwaritadisha Waislamu ndani ya miji yao, inasemekana kuwa **Mshia Shah Abbas (The Great)** alishawishiwa na Maaskofu ili awe Mkristo, na yeye akashawishika kufanya hivyo, lakini hofu juu ya madaraka yake ndiyo yaliyomzuia kuitikia matakwa ya Maskofu hao, lakini pamoja na hofu hiyo, bado alikuwa akidhihiri kwa mwonekano wa ki-Kristo zaidi, kuliko Kiislamu, kwa sababu alionekana akihudhuria kwenye sherehe mbalimbali za ki-Kristo, kama vile: **Krismas, Kipaimara** n.k. na kwenye sherehe hizo za ki-Kristo alikuwa akinywa Mvinyo hadharani hata kama ni katika mwezi mtukufu wa Ramadhani! na marafiki wake wakubwa na washauri wake walikuwa ni Mapadre na Maaskofu!!!

Je lilikuwa lengo la Mashia hao ni kuusimamisha Uislamu na kuwa ukafiri? Bila shaka ndugu msomaji majibu sahihi unayo.

Ndugu msomaji! Ukweli ni kwamba Makafiri walifurahishwa sana na vitendo vilivyofanywa na Mashia vya kuiteka miji ya Masunni na kuwaua raia wake bila ya hatia, kwa sababu jambo hilo liliwashughulisha Masunni wakalazimika kuacha kupigana Jihad na Makafiri wa Ulaya na badala yake waliwashughulikia Mashia. Kwa hiyo Mashia wakawa ndio wakombozi wao, mpaka Mkristo mmoja wa Ulaya **(Ferdinand)** alifikia kusema;

"لولا الصفويون في إيران لكتنا اليوم في فرنسا وبلجيكا وأوروبا نقرأ القرآن كالجزيين."

"Lau kama (si kudhihiri kwa Dola ya) Swafawiyya huko Iran, leo hii tungelikuwa sisi tunaisoma Qur-ani ndani ya **Ufaransa, Ubelgiji na Ulaya** (kwa ujumla) kama wanavyoisoma wa **Al-geria**, (tungekuwa Waislamu)!⁸¹

⁸¹ -Iran Mina Daakhili ukurasa wa 24

SURA YA TANO

USHIA NA MYAHUDI IBNU SABAI

Ndugu msomaji! Katika sura hii tutakuelezea kuhusu ni nani Shia Ithnaashariyya, na lini ilianza madhehebu hii, na ni nani mwanzilishi wake.

USHIA NI NINI NA ULIANZA LINI?

Hili ni swali muhimu, na majibu sahihi ya swali hili ni muhimu zaidi kuliko swali lenyewe, na tutalijibu swali hili kwa majibu ya aina mbili; aina ya kwanza, ni vile wanavyojibu Shia wenyewe, na aina ya pili, ni vile ukweli ulivyo.

Majibu ya Shia:-

Anasema Mshia Jaafar Mwazoa akimnukuu Mwanachuoni wao wa Kishia aitwaye An-Nawbakhtiy:

"Shia: Ni pote la Ali Bin Abii Talib (a.s) walioitwa wafuasi wa Ali (a.s) tangu enzi za uhai wa Bwana Mtume (s.a.w.w.) na hata baada ya kifo chake. Wao ni maarufu kwa kufungamana naye na kuamini uimamu wake⁸²"

Na anasema; Mshia Sayyid Muhammad Al-Musawiy As-Shiraaziy:

"Kwa kweli alikuwa ni Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe ambaye alilitambulisha neno Shi'a kwa maana ya **"Mfuasi wa Ali bin Abu Talib"** na neno hili lilikuwa likitumiwa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)...."⁸³

⁸²-Tazama Shimo Refu, ukurasa wa 21.

⁸³-Tazama Mikesha ya Peshawar, ukurasa wa 17.

Naye Mwanachuoni mkubwa wa Shia Sheikh **Muhammad Husein Aali Kashiful-Ghita** anafafanua zaidi kwa kusema;

"Hakika mtu wa kwanza kuipanda mbegu ya Ushia katika konde la Uislamu si mwingine isipokuwa ni yule yule aliyekuja na sharia ya Kiislamu ambaye ni Mtume Muhammad (s.a.w.w.). Hii ina maana kwamba, mbegu ya Ushia ilipandwa sambamba na mbegu ya Uislamu mahali pamoja na wakati mmoja, na aliendelea kuipalilia, kuihifadhi na kuitilia maji hadi mti wake ukakua na matawi yake yakatoa maua katika zama za uhai wake mwenyewe, kisha (mti huo wa Ushia) ukatoa matunda baada ya kufariki kwake."⁸⁴

Muhtasari wa majibu yao;

- ➔ Mashia wanadai kuwa wao ni wafuasi wa Ali Bin Abi Twalib na kizazi chake.
- ➔ Pia wanadai kuwa Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam ndiye ambaye alilitambulisha neno Shia kwa maana ya wafuasi wa Ali Bin Abi Twalib.
- ➔ Na wanadai kuwa Mtume swalla Ilaahu alayhi wasallam ndiye mtu wa mwanzo aliyeipanda mbegu ya Ushia katika konde (shamba) la Uislamu. Aliipanda mbegu hiyo sambamba na mbegu ya Uislamu, mahali pamoja, wakati mmoja.

MAJIBU YETU

Kwa ufupi, hivi ndivyo Shia Ithanaashariyya wanavyojibu pindi wanapoulizwa Ushia ni nini na ulianza lini. Sisi hatuna shaka kuwa majibu yao hayo ni ya uongo na hayana ukweli wowote kwa sababu hizi zifuatazo:-

- ➔ Kwanza, katika zama za Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam hakukuwa na Pote (kundi) lililoitwa kwa jina la Pote la Ali, bali kulikuwa na kundi lililoitwa Muhaajirina na Answaari, kama inavyotueleza Qur-ani na Sunna.

⁸⁴-Tazama Asili ya Ushia na Misingi yake ukurasa wa 63.

- ➔ Pili, hakuna Aya yoyote ya Qur-ani wala Hadithi sahihi hata moja ya Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam iliyotambulisha kuwa Shia maana yake ni wafuasi wa Ali bin Abi Twalib radhia Ilaahu an'hu, na hadithi zote wanazozitaja Mashia kama maegemeo yao juu ya uzushi huo ni hadithi za kutunga. Na sisi dini yetu haikujengwa juu ya hadithi za uongo na kutunga.
- ➔ Tatu, Mtume swalla Ilaahu alayhi wasallam hakupanda mbegu mbili, mbegu ya Ushia na mbegu ya Uislamu kama wanavyodai Mashia, bali alipanda mbegu moja tu ya Uislamu.

Ukweli ulivyo:

Ukweli ulivyo ni kwamba, **Mashia ni wafuasi wa Myahudi Abdullahi Ibnu Sabai Al-Himyariy.** Na huwezi kuutengenisha Ushia na **Myahudi** huyo, kwani yeye ndiye aliyeipanda mbegu hii mbaya ya Ushia katika zama za Khalifa wa tatu Uthmani Bin Affaan radhia Ilaahu an'hu nyuma ya pazia la Ahlul-Baiti. Kwa hiyo, huwezi kuujua Ushia kama hukumjua Myahudi Abdullahi Ibnu Sabai na fikra zake na wanafunzi wake, pamoja na mbinu walizozitumia katika kueneza fikra na itikadi zao chafu. Na ukifuatilia maudhui hii kwa makini kwenye kitabu chetu hiki utabainikiwa na ukweli wa haya ninayokueleza.

Inafahamika kwamba Mayahudi tangu hapo zamani walikuwa ni wapinzani wakubwa wa Mitume wa Allah, hasa pale Mitume wanapoleta Sheria na muongozo unaopingana na matashi ya nafsi zao. Waliwakadhibisha Mitume hao na wengine waliwaua kwa dhulma na uadui. Amesema Allah katika Qur'ani kuhusu tabia yao hii:-

{أَفَكَلَّمَا جَاءَكُمْ رَسُولٌ بِمَا لَا تَهْوَىٰ أَنفُسُكُمْ اسْتَكْبَرْتُمْ فَفَرِقًا كَدَّبْتُمْ وَفَرِقًا تَفْتَنُونَ}

[البقرة: ٨٧]

[Hivi kila alipowafikia Mtume kwa yale yasiyopendwa na nafsi zenu mnafanya kiburi! Kundi moja mnalikadhibisha na kundi jingine mnaliua]? [Suratul-Baqarah Aya ya 87].

Bali Allah ametuelezea katika Qur-ani kwamba Mayahudi na Manasara hawataacha kutupiga vita dhidi (milele), mpaka wahakikishe wametutoa kwenye dini yetu, amesema Allah Jalla wa A'laa;

{وَلَنْ تَرْضَىٰ عَنْكَ الْيَهُودُ وَلَا النَّصَارَىٰ حَتَّىٰ تَتَّبِعَ مِلَّتَهُمْ} (البقرة: ١٢٠).

[Katu hawatakuwa radhi nawe Mayahudi wala Wakristo mpaka ufuatae mila yao]
[Suratul-Baqarah, Aya ya 120]

Pia Allah anatuelezea Zaidi kuwa maadui wakubwa wa Waislamu ni Mayahudi na washirikina, amesema Allah Sub'haanahu wa Ta'ala;

{لَتَجِدَنَّ أَشَدَّ النَّاسِ عَدَاوَةً لِلَّذِينَ آمَنُوا الْيَهُودَ وَالَّذِينَ أَشْرَكُوا} [المائدة: ٨٢].

[Hakika utawakuta walio na uadui mkali kuliko watu wote dhidi ya walioamini ni Mayahudi na washirikina]. [Suratul-Maidah, Aya ya 82].

Mayahudi walimpiga vita Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam kwa dhahiri, lakini baada ya kushindwa na kukata tamaa katika harakati zao za kuizuia daawa ya Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam, walianza mapambano na vita vya siri, na kuwazuia wengine ambao hawajamkubali Mtume swalla Ilaahu alayhi wasallam miongoni mwa washirikina wasiamini dini ya haki ya Uislamu kwa kuwaambia kuwa dini ya washirikina ni bora kuliko Uislamu! Amesema Allah;

{أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ أَوْتُوا نَصِيبًا مِّنَ الْكِتَابِ يُؤْمِنُونَ بِالْغَيْبِ وَالطَّاعُوتِ وَيَقُولُونَ لِلَّذِينَ كَفَرُوا هَؤُلَاءِ أَهْدَىٰ مِنَ الَّذِينَ آمَنُوا سَبِيلًا} [النساء: ٥١].

[Je, huwaoni wale waliopewa sehemu katika Kitabu, wanaamini Masanamu na Shetani! Wanawaambia waliokufuru; hawa ndio walioshika njia iliyonyooka zaidi kuliko walioamini (Waislamu)] [Surat An-Nisaai Aya ya 51].

Lakini pamoja na uadui wao huo, na njama zao za kichinichini, Allah alimnusu Mtume wake dhidi ya vitimbi vyao, nuru ya Uislamu ikaenea katika miji, na hatimaye Uislamu ukawa juu ya dini zote, na watu wakaingia katika Uislamu makundi kwa makundi.

Hali iliendelea hivyo mpaka katika zama za Makhalifa wawili watukufu wa Bwana Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam; **Abu Bakar Siddiq** na **Umar Al-Farouq** Allah awaridhie, Uislamu ulizidi kupata nguvu na nuru yake ikaenea duniani kote, ikafika mpaka kwenye miji yao, ikavunja ngome zao na himaya zao, na ikazibatilisha mila zao potofu, ikasimama bendera ya Tawhiid na ikaenea mila ya Nabii Ibrahim alayhi salaam, jambo ambalo lilizidisha chuki zao na uadui wao dhidi ya Uislamu.

KUDHIHIRI KWA IBNU SABAI

Katikati ya utawala wa Khalifa wa tatu, **Uthman Ibnu Affaan** –Allah amridhie- aliwasili katika mji wa Madina Myahudi mmoja aitwaye **Abdullahi Ibnu Sabai** au **Ibnu Saudaa**, akitokea sehemu za San'aa nchini Yemen. Myahudi huyu alidai kuwa amesilimu, na alijidhihirisha kuwa anampenda sana **Ali Ibnu Abi Twalib** na watu wa nyumbani kwa Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam kwa ujumla, lakini lengo lake halikuwa zuri, na hilo lilibainika kutokana na vitendo vyake viovu alivyovifanya na athari mbaya aliyoiacha katika umma wa Kiislamu.

Na maelezo ya wazi juu ya mtu huyu tunayapata kupitia mmoja kati ya wanachuoni wa Shia Ithnaashariyya aitwaye **Abu Amri Muhammad Ibnu Umar Ibni Abdil-Aziiz Al-Kashiy** (aliyefariki mwaka 340 Hijiriyya) pale aliposema;

"ذَكَرَ بَعْضُ أَهْلِ الْعِلْمِ أَنَّ عَبْدَ اللَّهِ بْنَ سَبْيَأَ كَانَ يَهُودِيًّا فَأَسْلَمَ وَوَالَى عَلِيًّا عَلَيْهِ السَّلَامُ، وَكَانَ يَقُولُ وَهُوَ عَلَى يَهُودِيَّتِهِ فِي يُوشَعَ بْنِ نُونٍ وَصِيِّ مُوسَى بِالْعُلُوِّ! فَقَالَ فِي إِسْلَامِهِ بَعْدَ وَفَاةِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فِي عَلِيٍّ عَلَيْهِ السَّلَامُ مِثْلَ ذَلِكَ، وَكَانَ أَوَّلَ مَنْ شَهَرَ بِالْقَوْلِ بِفَرَضِ إِمَامَةِ عَلِيٍّ، وَأَظْهَرَ الْبِرَاءَةَ مِنْ أَعْدَائِهِ وَكَاشَفَ مَخَالِفِيهِ وَأَكْفَرَهُمْ، فَمِنْ هَذَا قَالَ مَنْ خَالَفَ الشَّيْعَةَ: أَصْلُ النَّسِيعِ وَالرَّفِضِيِّ مَأْخُودٌ مِنَ الْيَهُودِيَّةِ".

"Wameelezea baadhi ya wanachuoni kwamba; **Abdullahi Ibnu Sabai alikuwa ni Myahudi**, kisha akasilimu na **akadhihirisha kumpenda Ali** (a.s.), alikuwa akisema na hali ya kuwa yuko katika Uyahudi wake maneno ya Ghululu (kuvuka mipaka) kuhusu Yoshua mwana wa Nuni, Wasii wa Musa! Kisha aliposilimu akasema mfano wa maneno hayo baada ya kufariki Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam. **Na yeye ndiye mtu wa kwanza aliyetangaza kauli ya ulazima wa Uimamu wa Ali!!**

Na akadhihirisha **kuwachukia maadui** zake, na **akawakashifu** wapinzani wake na **akawakufurisha**. Na kuanzia hapo, ndipo wakasema wanaowapinga Shia: Asili ya Ushia umechukuliwa kutoka kwenye Uyahudi"⁸⁵

Naye **Mshia An-Nawbakh'tiy** anafafanua zaidi kwa kusema:

"السَّبَيْئَةُ قَالُوا بِإِمَامَةِ عَلِيٍّ وَأَتَمَّهَا فَرَضُ مِنَ اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ، وَهُمْ أَصْحَابُ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ سَبَّأٍ، وَكَانَ مِمَّنْ أَظْهَرَ الطَّغْنَ عَلَى أَبِي بَكْرٍ وَعُمَرَ وَعُثْمَانَ وَالصَّحَابَةَ وَتَبَرَّأَ مِنْهُمْ، وَقَالَ: "إِنَّ عَلِيًّا أَمَرَهُ بِذَلِكَ" فَأَخَذَهُ عَلِيٌّ فَسَأَلَهُ عَنْ قَوْلِهِ هَذَا، فَأَقْرَبَ بِهِ فَأَمَرَ بِقَتْلِهِ فَصَاحَ النَّاسُ إِلَيْهِ: يَا أَمِيرَ الْمُؤْمِنِينَ اتَّقِمْ رَجُلًا يَدْعُو إِلَى حُبِّكُمْ أَهْلَ الْبَيْتِ وَإِلَى وَلَايَتِكَ، وَالْبَرَاءَةَ مِنْ أَعْدَائِكَ؟ فَصَيَّرَهُ إِلَى الْمَدَائِنِ.

وَحَكَى جَمَاعَةٌ مِنْ أَهْلِ الْعِلْمِ مِنْ أَصْحَابِ عَلِيٍّ عَلَيْهِ السَّلَامُ أَنَّ عَبْدَ اللَّهِ بْنَ سَبَّأٍ كَانَ يَهُودِيًّا فَاسْلَمَ، وَوَالَى عَلِيًّا عَلَيْهِ السَّلَامُ، وَكَانَ يَقُولُ وَهُوَ عَلَى يَهُودِيَّتِهِ فِي يُوشَعَ ابْنِ نُونٍ بَعْدَ مُوسَى عَلَيْهِ السَّلَامُ بِهَذِهِ الْمَقَالَةِ، فَقَالَ فِي إِسْلَامِهِ بَعْدَ وَقَاةِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فِي عَلِيٍّ عَلَيْهِ السَّلَامُ بِمِثْلِ ذَلِكَ. وَهُوَ أَوَّلُ مَنْ شَهَرَ الْقَوْلَ بِفَرَضِ إِمَامَةِ عَلِيٍّ عَلَيْهِ السَّلَامُ وَأَظْهَرَ الْبَرَاءَةَ مِنْ أَعْدَائِهِ، وَكَاشَفَ مُخَالَفَتِهِ. فَمِنْ هُنَا قَالَ مَنْ خَالَفَ الشَّيْعَةَ: إِنَّ أَصْلَ الرَّفْضِ مَاخُودٌ مِنَ الْيَهُودِيَّةِ.."

"**SABAIYYAH**, wanaitakidi Uimamu wa Ali, na kwamba huo Uimamu ni faradhi kutoka kwa Allah Azza wa Jalla, na wao ni wafuasi wa **Abdillahi Ibnu Sabai**, alikuwa ni katika **waliodhihirisha Kumtukana Abu Bakar, Umar, Uth'mani na Maswahaba wengine** na akatangaza uadui dhidi yao, na **akasema kwamba "Ali amemuamrisha kufanya hivyo"**. Ali akamkamata kisha akamuuliza kuhusu kauli yake hii, akakiri, Ali akaamrisha auwawe, watu wakapiga kelele; Ewe Amirul-Muuminina! Unataka kumuua mtu ambaye analingania watu kwenye kuwapenda nyinyi Ahlul-Baiti! Na anawaita watu kwenye kukupenda wewe na kuwachukia maadui zako! Ali akamfukuza, akampeleka Madaain. Na limesimulia kundi kubwa miongoni mwa watu wenye elimu katika wafuasi wa Ali (as) kwamba; **Abdillahi Ibnu Sabai** alikuwa ni Myahudi akasilimu na akampenda Ali (as), alikuwa akisema na hali ya kuwa yuko ndani ya Uyahudi wake: Joshua bin Nun (ndiye mrithi wa Musa) baada ya Musa. Na akasema baada ya kusilimu, baada ya kufariki Mtume swalla Ilaahu alayhi wa Aalihi wasallam kuhusu Ali mfano wa hayo (ya Joshua, kwamba Ali naye ni mrithi wa Mtume swalla Ilaahu alayhi wa Aalihi wasallam).

⁸⁵ - Tazama Bihaarul-An'waari, juzuu ya 25 ukurasa wa 478-479.

Na yeye ndiye mtu wa kwanza kuitangaza kauli ya ulazima wa Uimamu wa Ali (as) na akadhihirisha uadui kwa maadui wa Ali, na akawakashifu (akawatukana) wapinzani wake. Na kuanzia hapo wakasema wapinzani wa Shia: **Asili ya Ushia umechukuliwa kutoka kwenye Uyahudi**⁸⁶.” Mwisho wa kunukuu.

Na amesema **Mshia Ni'matullahi-Jazairiy** aliyefariki mwaka 1112 Hijiria:

”قال عبد الله بن سبأ لعلي بن أبي طالب عليه السلام أنت الإله حقاً فنفاه علي عليه السلام إلى المدائن و قيل إنه كان يهودياً فأسلم، وكان في اليهودية يقول في يوشع بن نون وفي موسى مثل ما قال في علي.”

”Amesema **Abdullahi Ibnu Sabai** kumwambia Ali Ibn Abi Twalib (a.s.) wewe ni ndiye Mungu wa kweli, Ali akamfukuza, akampeleka Madaaini, na inasemekana kwamba alikuwa ni Myahudi kisha akasilimu, na katika Uyahudi wake alikuwa akisema kuhusu Yoshua Bin Nuni na Musa mfano wa aliyoyasema kuhusu Ali.”⁸⁷

Uchambuzi wetu mfupi;

Ndugu msomaji! Maelezo haya ya Mashia kina; **Al-Kashiy, An-Nawbakh'tiy, na Al-Jazaairiy**, yanatuthibitishia juu ya kuwepo kwa Myahudi Abdullahi Ibnu Sabai na harakati zake, kuanzia mwanzo wa kudhihiri kwake, misingi ya daawa yake, malengo yake na athari aliyoiacha. Na kwa kupitia maelezo yao haya, tunapata faida nyingi, na kupata hamu ya kudodosa mambo, na kuchunguza baina ya madai ya Myahudi huyo na msimamo wa Ali Ibn Abi Twalib radhia Ilaahu an'hu na hali halisi ya Shia kupitia vitabu vyao na vitendo vyao. Na kutokana na maelezo hayo mafupi, tumefahamu mambo haya yafuatayo:

- ➔ Uhakika wa uwepo wa Myahudi aliyelitwa Abdullahi Ibnu Sabai.
- ➔ Myahudi huyo, alianza harakati zake kwa kudhihirisha mapenzi kwa Ali.
- ➔ Madai yake ya mwanzo aliyoyadhihirisha kwa watu, ni madai ya kuwa Ukhalifa ni haki ya Ali Ibn Abi Twalib radhia Ilaahu an'hu.
- ➔ Ndani ya madai yake ya kumpenda Ali, na kudai haki ya Ukhalifa wake, Myahudi huyo, alifanya Ghuluu (alivuka mipaka) kwa kumpa Ali sifa ya Uungu.
- ➔ Sambamba na madai yote hayo, Ibnu Sabai alianzisha kampeni za kupandikiza chuki dhidi ya Maswahaba kama Abu Bakar, Umar na Uthman na kuwatukana.

⁸⁶-Tazama katika kitabu chake; "Firaqus-Shia" ukurasa wa 19-20, kimechapishwa na Maktabatu Haidariya iliyoko Najaf chapa ya mwaka 1959 AD.

⁸⁷ - Tazama katika kitabu chake Al-An'waarun-Nu'maaniyyah, juzuu ya 2 ukurasa wa 234.

- ➔ Pia maelezo ya Mashia hao yanatufahamisha kuwepo kwa kikundi cha watu waliojulikana kwa jina la **Sabaiyya**, ambao ni wafuasi wa Myahudi Ibnu Sabai. Wafuasi hao walizirithi fikra zake na mbinu zake, na walijidhihirisha katika jamii ya waislamu kuwa wao ni wapenzi wa Ali na Ahlil-Baiti kwa ujumla, na wakayahalalisha matusi yao dhidi ya Maswahaba kwa kumsingizia Ali Ibn Abi Twalib kwamba eti ndiye aliyewatuma kufanya hivyo.
- ➔ Ripoti ya Mashia hao, inatwambia kwamba Ali hakukubaliana na uovu huo, bali alikabiliana nao kwa nguvu zake zote kwa lengo la kuzima harakati zao chafu.

Ndugu msomaji! Kwa maelezo hayo unatakiwa upime mambo kwa umakini, kisha ulinganishe kwa uadilifu baina ya fikra na harakati za Myahudi huyo, na fikra na harakati za Mashia wa leo! Kama vile; nafasi ya suala la Uimamu na Maimamu, Ghuluu kwa Maimamu wao, matusi dhidi ya Maswahaba kwa madai ya kuwapenda Ahlul-Baiti, Je, mtu akisema; Ushia umetokana na Myahudi Ibn Sabai atakuwa amewazulia?

UDANGANYIFU WA MURTADHA KUHUSU KUTOKUWEPPO IBNU SABAI

Hakuna hata mwanachuoni mmoja wa Shia miongoni mwa waliotangulia aliyepinga kuwepo kwa Myahudi Abdullahi Ibnu Sabai, mtu wa kwanza aliyepinga kuwepo kwa Myahudi huyo kwa upande wa Shia ni Muratadha Al-Askariy. Mshia huyu amefanya utafiti uliojaa uongo mwingi, hasa kupitia vitabu vyake viwili; **Abdullahi Ibn Sabai wa Asaatwiiru Ukhraa**⁸⁸, na **Al-Ustuuratu As-Sabaiyya**, Mshia huyu amekana katakata kwenye vitabu hivyo kuwepo kwa Myahudi huyo, kwa kutumia udanganyifu hasa kwa watu wasio na maarifa juu ya elimu ya uchambuzi wa habari na utafiti wa riwaya.

⁸⁸-Kitabu hiki kimefanyiwa tarjama kwa lugha ya Kiswahili na Ramadhani Kanju Shemahimbo, akakiita kwa jina la; **Abdullahi Ibn Saba' na ngano nyinginezo**, kimetolewa na kuchapishwa na Taasisi ya Kishia Alitra Foundation, Dar es Salaam.

Na kwa hakika Murtadha Al-Askariy hakuleta jambo jipya zaidi ya kuwaiga **Wazandiki**⁸⁹ na **Mustash'riquna**⁹⁰ (**Orientalists**) kama vile; **Israel Fred Landre**⁹¹, **G. Levi Della Vida**⁹² na **Caetani**⁹³, Makafiri hawa ndio watu wa mwanzo kupinga uwepo wa Ibn Sabai kwa hoja kwamba riwaya zilizomtaja zimepitia kwa Seif Ibn Umar, naye ni dhaifu!

Kwa masikitiko makubwa kuna waandishi wengi wa Kiislamu wameathirika na utafiti huu batili uliofanywa na Mustashriqiina hawa, na miongoni mwao ni **Mshia Murtadha Al-Askariy, na Twaha Hussein**.

Na kuna kundi kubwa la watu ambao wameathirika na utafiti wa Mshia Murtadha Al-Askariy na Twaha Husein, bila ya kufanya uchunguzi wa kina, hasa wale ambao uwezo wao ni mdogo katika elimu za uchambuzi wa habari, na miongoni mwao ni mwandishi chipukizi wa Shia Samaahatu Sheikh Jaafar Mwazoa.

⁸⁹-**Wazandiki**; ni wingi wa neno **Mzandiki**, naye ni kila Kafiri aliyeficha Ukafiri wake moyoni na kudhihirisha Uislamu, na tofauti baina ya Mzandiki na Mnafiki ni malengo yao ya kudhihirisha Uislamu, kama malengo ni kuuhujumu Uislamu kwa kupotosha mafunzo yake, basi huyo ataitwa Mzandiki, na kama si hivyo basi huyo atabaki kuwa Mnafiki.

⁹⁰-**Mustashriquna**; ni kundi la Makafiri waliotokea nchi za Magharibi kama vile; **Uingereza, Uholanzi, Ufaransa, Ujerumani, Italia**, n.k., ambao walikwenda nchi za Mashariki ya kati na kwengineko katika nchi za Kiislamu kama vile; **Iraq, Syria, Lebanon, Misri** n.k. kwa ajili ya kuusoma Uislamu kwa lengo la kuupotosha, kuna miongoni mwao waliojijhusisha na elimu za **Hadithi, Historia ya Kiislamu, Fiqhi, Lugha ya Kiarabu** na fani nyingine zenye mahusiano na dini ya Kiislamu.

⁹¹- **Israel Fred Landre** ni Mustashriqi wa Kijerumani, alianza kuandika kadhia za Ibn Sabai katika gazeti la Kijerumani liitwalo **Al-Majallatu Al-Aashuriyya**, mnamo mwaka 1909-1910 AD, na yeje ndiye mwandishi wa Kitabu Abdallah B. Saba...!!!

⁹²- **G. Levi Della Vida** ni Mustashriqi aliyezaliwa mnamo mwaka 1886 AD, aliwahi kuwa Muhadhiri katika chuo kikuu cha Roma Italia, alisomesha katika Kitivo cha Lugha ya Kiarabu, na ndiye mwenye kitabu **'Il Califfato di' Ali Secondo Kitab ansab Al-Ashraf di Baladhuri'** (**Ukhalifa wa Ali katika kitabu Ansabul-Asharaf cha Baladhuri**).

⁹³- **Caetani** ni Mustashriq wa Kitaliano, aliyezaliwa Roma mwaka 1869 na kufariki 1926 AD, na huyu ndiye mwenye kitabu **Hauliyaatul-Islaami**, katika juzuu ya 8 ya kitabu hicho anaelezea matukio ya mwaka 33-35 Hijiriyya, na kupinga kuwepo kwa Ibn Sabai.

Nukuu kutoka kwa Mshia Murtadha Al-Askariy:-

Kwa kuchunga uadilifu na kufuata kanuni za kielimu, tutaanza kwa kuzitazama hoja za Mshia Murtadha Al-Askariy pamoja na kuziweka katika mizani ya kielimu ili kuzipima uzito wake. Amesema Mshia huyu chini ya kichwa cha habari kisemacho; **"Asili ya ngano yenyewe"** katika ukurasa wa 20-21;

"Kisa hiki cha Abdullah Ibn Saba' kina zaidi ya karne kumi na mbili sasa. Wana-historia na waandishi, mmoja baada ya mwingine wakakiandika, na kuongeza zaidi na zaidi juu yake.

Akaendelea;

"Wanahistoria wote wanakubali kwamba ngano hii ilisimuliwa kwanza kabisa na Seif. Wana-historia wafuatao walinukuu moja kwa moja kutoka kwa Seif: 1) Tabari. 2). Dhahabi alisimulia kutoka kwa Tabari. 3). Ibn Abi Bakr amenukuu pia kutoka kwa Ibn Athir 15, ambaye amenukuu kutoka kwa Tabari. 4). Ibn Asakir."

Kisha akasema tena;

"Wafuatao wamenukuu katika mzunguko (siyo moja kwa moja toka kwa Seif): 5) Nicholson kutoka kwa Tabari 2. 6). Ensaiiklopedia ya Uislam kutoka kwa Tabari 2. 7). Van Folton kutoka kwa Tabari 2....."

Kisha akasema;

"Drodha hiyo hapo juu inatoa ushahidi kwenye ukweli kwamba ngano ya Abdullah Ibn Saba' imeanzishwa na Seif na kusimuliwa kwa mara ya pili kutoka kwa Tabari. Kwa hiyo, tabia na historia ya Seif ichunguzwe na kuchambuliwa kwa uangalifu mkubwa⁹⁴."

⁹⁴-Tazama kitabu **"Abdullah Ibn Saba' na ngano nyinginezo"** kilichotarjumiwa na Ramadhani Kanju Shemahimbo, ukurasa wa 20-21.

Amesema tena Murtadha Al-Askari:

"Ibn Asakir anaandika kutoka kwenye chanzo kingine. Ndani ya kitabu chake The History of Damascus (historia ya Damascus) wakati akiandika wasifu wa Talha na Abdullah Ibn Saba, ameandika sehemu za ngano ya Sabaian, kupitia kwa Abul Qasim Samarqandi kutoka kwa Abul Hussein Naquur kutoka kwa Abu Tahir Mukhallas toka kwa Abubakar Ibn Seif toka kwa Sari toka kwa Shuaib Ibn Ibrahim kutoka kwa Seif. Kwa hiyo, wa mwanzo ni Sari, mmoja kati ya sanadi ambazo Tabari amenakili toka kwao⁹⁵."

Kisha Mshia Murtadha Al-Askari katika utafiti wake huo kuhusu chanzo cha habari ya Ibn Sabai akahitimisha kwa kusema:

"Kwa muhtasari tunaweza kusema kwamba wanahistoria wote hawa waliotajwa, wamechukua ngano zao na kisa cha Abdullah Ibn Saba kutoka kwa Seif. Wanne wa wanahistoria hawa: Tabari, Ibn Asakir, Ibn Abibakar na Dhahabi wamechukua ngano zao moja kwa moja toka kwa Seif.⁹⁶"

Jaafar Mwazoa amuiga Murtadha Al-Asakariy:-

Kama nilivyosema kuwa Mshia Jaafar Mwazoa ni miongoni mwa walioathirika na utafiti huu wa uongo uliofanywa na Mshia Murtaza Al-Askariy, kauli yake ifuatayo ni uthibitisho wa wazi juu ya kuathirika kwake na uongo huo. Amesema Jaafar Mwazoa kuanzia ukurasa wa 13-14 katika kitabu chake 'Shimo Refu' baada ya kutukana kama kawaida yake;

⁹⁵ - Tazama Abdullah Ibn Saba' ukurasa wa 37.

⁹⁶ - Tazama ukurasa wa 39 wa kitabu hicho.

"Bali tunachokishuhudia ni kuwa kila aliyemzungumzia Abdallah Bin Sabai basi amenukuu habari hiyo kutoka kwa Twabari katika Tarekhe yake. Naye Twabari amelezea habari hiyo kutoka kwa Seif Bin Umar Attamiimiy. Seif ambaye ni mzushi, mwongo, na mwenye kubuni majina ya watu na kudai kuwa watu hao walipata kuishi hapa ulimwenguni.

Muhtasari wa utafiti wa Murtadha na kuiga kwa Mwazoa:

Kwa mujibu wa utafiti huu uliofanywa na mwanachuoni wa Kishia Murtaza Al-Askariy na kuigwa na Mshia mwenzake Mwazoa, ni kwamba;

1. Hajawahi kuwepo mtu aliyekuwa akiitwa Abdillahi Ibn Sabai.
2. Habari zinazothibitisha kuwepo kwa Ibn Sabai zina zaidi ya karne kumi na mbili!
3. Wanahistoria na waandishi wameafikiana kuwa chanzo cha habari za kuwepo kwa mtu huyo ni Seif Ibn Umar.
4. Waandishi na wanahistoria wote wanaotegemewa katika mambo ya habari kama vile Tabari, Ibn Asakir, Dhahabi na wengineo wamenukuu ngano za kuwepo kwa Ibn Sabai kutoka kwa Seif peke yake.
5. Tabia ya Seif ni mzushi, mwongo hakubaliki, hivyo basi, habari za kuwepo kwa Abdillahi Ibn Sabai ni habari za uongo zilizozuliwa na Seif Ibn Umar At-Tamimiy.

Uchambuzi wetu juu ya utafiti wake huu:-

Kama ulivyojionea hapo nyuma madai ya Mashia hao; Mshia Mwazoa na sheikh wake Murtadha kuwa: habari zote zinazomtaja Abdillahi Ibnu Sabai zimebuniwa na Seif Ibn Umar, na wanahistoria wote wamenukuu habari za Ibnu Sabai kutoka kwake, madai ambayo si ya kweli, bali ni uongo mtupu kama tutakavyobainishia kwa uchambuzi wetu huu, lakini kabla ya kuanza uchambuzi nataka kukudokeza kidogo juu ya mgongano uliopo baina ya mwanafunzi huyu ambaye ni Muqallid (anayefuata kiupofu) na baina ya Sheikh wake (Murtadha Al-Askariy). Sheikh wake anasema; Twabari, Ibnu Asakir, Ibnu Abibakar na Dhahabi wameichukua habari hii moja kwa moja toka kwa Seif.

Naye Mshia Mwazoa anasema; kila aliyemzungumzia Abdallah Bin Sabai amenukuu habari hiyo kutoka kwa Twabari katika Tarekhe yake!!!

Je hapa ukweli ni upi? Ni kuwa Wanahistoria waliotajwa na Murtadha Al-Askariy wamenukuu habari hii moja kwa moja kutoka kwa Seif au wamenukuu kupitia kwa Twabari kama anavyodai Mshia Mwazoa?

Swali jingine, je wanahistoria wa Kiislamu ni hawa tu, hakuna wengine waliomtangulia Twabari? Na je, wanahistoria wa Shia pia wamenukuu habari hii kutoka kwa Twabari au wamenukuu moja kwa moja kutoka kwa Seif? Hebu tuzame pamoja katika uchambuzi huu ili ubainikiwe na ukweli.

RIWAYA ZINAZOTHIBITISHA KUWEPPO KWA IBNU SABAI

Kuna riwaya nyingi ambazo zimo katika vitabu vikubwa vya kutegemewa kwa upande wa Shia na Ahlu Sunna zinazothibitisha kuwepo Myahudi Abdullahi Ibnu Sabai na zimemtaja kama mtu mwenye fikra potofu na malengo mabaya, na riwaya nyingi katika hizo hazikupitia kwa Seif wala hazikutajwa kutoka kwake, bali zimepokewa kwa njia nyingine mbalimbali na kuungwa mkono na Maulamaa wakubwa wa Shia lth'naashariyya.

Pamoja na kuwa riwaya zinazomtaja Ibnu Sabai ni nyingi sana katika vitabu vya Shia lth'naashariyya, sisi tutazitaja riwaya chache tu kwa lengo la kuyabatilisha madai haya ya uongo yaliyoletwa na Mshia Mur'tadha, na kuigwa na Mshia chipukizi Jaafar Mwazoa na wengineo wanaopinga kuwepo kwa Myahudi Abdillahi Ibnu Sabai. Na riwaya zote nitakazozitaja hazikunukuliwa kutoka kwa Twabari, na wala hazikupokewa kutoka kwa Seif Ibn Umar At-Tamimiy, na hizi zifuatazo ni baadhi ya riwaya hizo hebu zisome kwa umakini:

RIWAYA ZA SHIA ITH'NAASHARIYYAH

Riwaya kwanza

قال الكشي: عن محمد بن قولويه قال: حدثني سعد بن عبد الله قال: حدثني يعقوب بن يزيد، ومحمد بن عيسى، عن علي بن مهزيار، عن فضالة بن أيوب الأزدي، عن أبان بن عثمان قال: سمعت أبا عبد الله يقول: لعن الله عبد الله بن سبأ، إنه ادعى الربوبية في أمير المؤمنين، وكان والله أمير المؤمنين عبدا طائعا، الويل لمن كذب علينا، وإن قوما يقولون فينا ما لا نقول في أنفسنا، نبأ إلى الله منهم.

Amesema (mwanachuoni wa Kishia) Al-Kashiy: "Kutoka kwa Muhammad Ibn Quulawayhi, amesema; amenisimulia Sa'd Ibnu Abdillahi, amesema; amenisimulia Ya'qub Ibn Yazid na Muhammad Ibn Isa, kutoka kwa Ali Ibn Mih'ziyaar, kutoka kwa Fadhaalah Ibn Ayoub Al-Azdiy, kutoka kwa Abaana Ibn Uth'man, amesema (Abaana Ibn Uth'man): Nimemsikia Abu Abdillahi anasema: **Allah amlaani Abdullahi Ibnu Sabai**, kwa sababu yeye amedai kwamba, Amiril-Muuminina (Ali) ni Mungu. Na (Wa Ilaahi) alikuwa Amiril-Muuminina ni mja mtiifu, basi maangamivu ni kwa wale wanaotuzulia uongo, na kwa hakika kuna jamaa ambao wanatuzulia mambo ambayo hatuyasemi, sisi tunajitakasa kwa Allah na wao⁹⁷"

Riwaya ya pili

قال الكشي: "حدثني محمد بن قولويه القمي، قال: حدثني سعد بن عبد الله بن أبي خلف القمي، قال: حدثني محمد بن عثمان العبدى، عن يونس بن عبد الرحمان، عن عبد الله بن سنان، قال: حدثني أبي عن أبي جعفر محمد الباقر قوله: "إن عبد الله بن سبأ كان يدعي النبوة، ويزعم أن أمير المؤمنين - عليه السلام - هو الله، تعالى عن ذلك علواً كبيراً." اهـ

Amesema Al-Kashiy: "Amenisimulia Muhammad Ibn Quulawayhi Al-Qummiy, amesema; amenisimulia Sa'd Ibn Abdillahi Ibn Abi Khalaf Al-Qummiy, amesema; amenisimulia Muhammad Ibn Uth'man Al-Abdiy, kutoka kwa Yunus Ibn Abdil-Rahman, kutoka kwa Abdillahi Ibn Sinani, amesema; amenisimulia baba yangu kutoka kwa Abu Ja'far Muhammad Al-Baaqir kwamba; **Abdullahi Ibnu Sabai** alikuwa akidai Utume na anadai kuwa Amiril-Muuminina (Ali) Alayhi Salaam ni Mungu -Allah ametakasika na hilo kutakasika kukubwa-⁹⁸"

⁹⁷ -Tazama vitabu vya Kishia vifuatavyo: Ikh'tiyaaru Ma'rifatir-Rijaali cha Al-Kishiy, ukurasa wa 324. Bihaarul-An'waari cha Muhammad Baaqir Al-Maj'lisiy, juzuu ya 25 ukurasa wa 478.

⁹⁸ - Tazama Ikh'tiyaar Ma'rifatir-Rijaal, ukurasa wa 98-99.

Riwaya ya tatu

وروى بإسناده عن محمد بن خالد الطيالسي ، عن ابن أبي نجران ، عن عبد الله (بن سينان) ، قال : قال أبو عبد الله رضي الله عنه : إنا أهل بيت صديقون لا نخلو من كذاب يكذب علينا ويسقط صدقنا بكذبه علينا عند الناس ، كان رسول الله صلى الله عليه وآله وسلم أصدق الناس لهجة وأصدق البرية كلها ، وكان مسليمة يكذب عليه ، وكان أمير المؤمنين عليه السلام أصدق من برأ الله بعد رسول الله صلى الله عليه وآله وسلم ، وكان الذي يكذب عليه ويعمل في تكذيب صدقه ويفترى على الله الكذب عبد الله بن سبأ. "

Na amepokea (Al-Kashiy) kwa Sanad yake, kutoka kwa Muhammad Ibn Khalid At-Twayaalisii, kutoka kwa Ibn Abi Naj'ran, kutoka kwa Abdillahi (Ibn Sinan), amesema; amesema Abu Abdillahi radhia Ilaahu an'hu: Sisi Ahlul-Baiti ni wa kweli, lakini hatuepukani na waongo wanaotuzulia uongo na kuuporomosha ukweli wetu mbele za watu. Alikuwa Mtume wa Allah swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam ni mkweli mno wa watu kwa kauli, na ni mkweli mno kuliko viumbe vyote, na alikuwa Musailimah akimzulia uongo. Na alikuwa Amiril-Muuminina (Ali) alayhi salaam ni mkweli zaidi katika viumbe vya Allah baada ya Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam, na aliyekuwa akimzulia uongo na akifanyakazi katika kuukadhibisha ukweli wake na aliyekuwa akimzulia uongo Allah ni **Abdillahi Ibn Sabai**.⁹⁹"

Riwaya ya nne

وروى بإسناد آخر عن يعقوب بن يزيد ، عن ابن أبي عمير ، وأحمد بن محمد بن عيسى ، عن أبيه ، والحسين بن سعيد ، عن ابن أبي عمير ، عن هشام بن سالم ، عن أبي حمزة الثمالي ، قال : قال علي بن الحسين صلوات الله عليهما: لعن الله من كذب علينا إني ذكرت عبد الله بن سبأ فقامت كل شعرة في جسدي ، لقد ادّعى أمراً عظيماً! ما له لعنه الله ، كان على رضي الله عنه والله عبداً لله صالحاً ، أخوا رسول الله صلى الله عليه وآله وسلم ، ما نال الكرامة من الله إلا بطاعته لله ورسوله ، وما نال رسول الله صلى الله عليه وآله وسلم الكرامة من الله إلا بطاعته لله. "

Na amepokea tena kwa sanadi nyingine, kutoka kwa Ya'qub Ibn Yazid kutoka kwa Ibn Abi Umair na Ahmad Ibn Muhammad Ibn Isa kutoka kwa baba yake na Husein Ibn Said kutoka kwa Ibn Abi Umair kutoka kwa Hisham Ibn Salim kutoka kwa Abu Hamza At-Thumaali, amesema; amesema Ali Ibn Husein (s.a.): Allah amlaani anayetuzulia uongo, hakika mimi nilimtaja **Abdullahi Ibnu Sabai** zikasimama nywele zote kwenye mwili wangu, kwa sababu amedai jambo kubwa sana! Ana nini huyu? Allah amlaani, wallaahi alikuwa Ali radhia Ilaahu an'hu ni mja wa Allah aliyemwema, ndugu wa Mtume swalla Ilaahu alayhi wasallam.

⁹⁹-Tazama Ikh'tiyaar Ma'rifatir-Rijaal ukurasa wa 324, na Bihaarul-An'waar juzuu ya 25 ukurasa wa 478-479.

Na (Ali) hakuupata utukufu kutoka kwa Allah isipokuwa kwa utiifu wake kwa Allah na Mtume wake, na Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi hakuupata utukufu isipokuwa kwa kumtii Allah.¹⁰⁰"

Riwaya ya tano

حدثني محمد بن قولويه ، قال : حدثني سعد بن عبد الله ، قال : حدثنا يعقوب ابن يزيد ومحمد بن عيسى ، عن ابن أبي عمير ، عن هشام بن سالم ، قال : سمعت أبا عبد الله يقول وهو يحدث أصحابه بحديث عبد الله بن سبأ ، وما ادعى من الربوبية في أمير المؤمنين علي بن أبي طالب."

(Amesema Al-Kashiy); amenisimulia Muhammad Ibn Quulawayhi, amesema; amenisimulia Sa'd Ibn Abdillahi, amesema amenisimulia Ya'qub Ibn Yazid na Muhammad Ibn Isa kutoka kwa Ibn Abi Umair kutoka kwa Hisham Ibn Salim, amesema; nimemsikia Abu Abdillahi akisema na hali yakuwa anawasimulia wafuasi wake habari za **Abdillahi Ibn Sabai**, na vile alivyodai Uungu kwa Amirul-Muuminina Ali Ibn Abi Twalib.

Muhtasari wa riwaya hizi:

Ndugu msomaji! Ukizisoma riwaya hizo tano za Shia kwa utulivu na umakini, utabainikiwa na mambo haya matano yafuatayo:

1. Uhakika wa kuwepo kwa Myahudi Abdullahi Ibnu Sabai.
2. Yeye ndiye aliyedai kuwa Ali Ibnu Abi Twalib ni Mungu.
3. Kazi yake kubwa ilikuwa ni kumzulua uongo Ali Ibnu Abi Twalib radhia Ilaahu an'hu.
4. Myahudi huyo amelaaniwa na Imamu wao wa sita; Abu Abdillahi Ja'far As-Saadiq.
5. Ukiwatazama wapokezi wote waliomo kwenye riwaya hizo, kuanzia mwanzo hadi wa mwisho, hutamuona mpokezi aliyetajwa kwa jina la **Seif Ibn Umar At-Tamimiy**.

Baada ya maelezo yote hayo, utabainikiwa kwamba Murtadha Al-Askariy, Jaafar Mwazoa na wenye kuafikiana na wao katika suala hili ni wajinga au ni waongo, waliokusudia kuupotosha umma.

¹⁰⁰-Tazama Ikh'tiyaari Ma'rifatir-Rijaali ukurasa wa 324 hadithi namba 173, na Bihaarul-An'waari, juzuu ya 25 ukurasa wa 478.

RIWAYA YA AHLU SUNNA

Baada ya kuzitaja riwaya tano kutoka kwenye vitabu vya Shia lth'naasharia zinazoufichua uongo wa **Mur'tadha Al-Askariy** na Mashia wenzake pale walipodai kwamba riwaya zote zilizomtaja **Abdullahi Ibn Sabai** zimetungwa na **Seif Ibn Umar At-Tamimiy**, na wakadai kwamba wana-historia wote kama vile; Twabari na wengineo wamenukuu habari hizo kutoka kwa Seif peke yake.

Pamoja na kwamba riwaya hizo zimetosheleza kulifikia lengo na kusimamisha hoja dhidi yao, lakini si vibaya katika sehemu hii nikakutajia japo riwaya moja tu kutoka kwa Ahlu Sunna kati ya riwaya nyingi zilizomo kwenye vitabu vya kutegemewa ambazo hazikupitia kwa Seif wala Twabari, tutazitaja riwaya hiyo kwa sanad yake pamoja na kumtolea ufafanuzi mfupi kila mpokezi aliyekuwemo kwenye riwaya hiyo. Na riwaya yenyewe ni hii ifuatayo kama ilivyonukuliwa na **Al-Imamu Al-Haafidh Abul-Qaasim Ali Ibn Hasan Ibn Hibatillahi Ibn Abdillahi Ibn Husein Ibn Asaakir**, aliyefariki mwaka 571 Hijiria:

أخبرنا أبو محمد بن طاوس وأبو يعلى حمزة بن الحسن بن المفرج ، قالوا: أنا أبو القاسم بن أبي العلاء ، نا أبو محمد بن أبي نصر ، أنا خيثمة بن سليمان ، نا أحمد بن زهير بن حرب ، نا عمرو بن مرزوق، أنا شعبة، عن سلمة بن كهيل عن زيد قال : قال علي بن أبي طالب : مالي ولهذا الحميت الأسود ؟ يعني عبد الله ابن سبأ وكان يقع في أبي بكر وعمر."

"Ametuelezea Abu Muhammad Ibnu Twausi na Abu Ya'laa Hamza Ibnu Hasan Ibni Al-Mufarrij, wamesema: Ametusimulia Abul-Qaasim Ibnu Abil-Alaa'i, ametusimulia Abu Muhammad Ibnu Abi Nasri, ametusimulia Khaithama Ibnu Suleiman, ametusimulia Ahmad Ibnu Zuheir Ibni Harbi, ametusimulia Amru Ibnu Mar'zuuq, ametusimulia Shu'bah kutoka kwa Salamah Ibni Kuheili kutoka kwa Zaid, amesema (Zaid): amesema Ali Ibn Abi Twalib: ana nini huyu msusuavu mweusi! **Anamkusudia Abdullahi Ibnu Sabai**. Na alikuwa akimtukana Abu Bakar na Umar.¹⁰¹"

¹⁰¹-Tazama kitabu Taarekh Dimash'qi (**The History of Damascus**) cha Imamu Ibn Asaakir juzuu ya 29 ukurasa wa 6-7.

Ufafanuzi mfupi juu ya wapokezi wa riwaya hii:

Hebu tuwatupie jicho wapokezi wa riwaya hii mmoja baada ya mwingine, je tutampata Seif Ibn Umar At-Tamimiy?

Mpokezi wa kwanza:

Muhammad Ibn Twausi, jina lake kamili ni **Hibatullahi Ibnu Ahmad Al-Bagh'dadiy, Ad-Dimash'qiy**, na huyu ni mtu Thiqa (mwaminifu, mwenye hifdhi nzuri).¹⁰²

Mpokezi wa pili:

Abu Ya'laa Hamza Ibn Hasan Ibn Al-Mufarrij, huyu ameshirikiana na mpokezi wa kwanza (Muhammad ibn Twausi) katika kupokea riwaya hii, na huyu riwaya zake zina matatizo.¹⁰³

Lakini kwa mujibu wa kanuni za uchambuzi wa habari, habari ikipokewa na mpokezi mmoja kama huyu haikubaliwi, lakini akishirikiana na mtu mwingine aliye madhubuti habari hiyo itakubalika na yeye anapata nguvu kama ilivyokuwa katika sanad hii.

Mpokezi wa tatu

Abul-Qaasim Ibnu Abil-Ala'i, jina lake kamili ni **Ali Ibnu Muhammad Al-Misiisiy**, Bwana huyu alikuwa ni mtu madhubuti.¹⁰⁴

Mpokezi wa nne:

Abu Muhammad Ibnu Abi Nasri, Abdul-Rahman Ibnu Uth'man Ibni Qaasim Ibni Ma'ruuf Ad-Dimash'qiy, aliyefariki mwaka 420 Hijiria, Bwana huyu alikuwa ni mtu madhubuti.¹⁰⁵

Mpokezi wa tano:

Khaithamah Ibnu Suleiman, jina lake kamili ni **Abul-Hasan Khaithamah Ibn Suleiman Ibn Haidarah**, amefariki mwaka 343 Hijiria.¹⁰⁶

¹⁰²-Tazama An'saabul-Ash'raaf, juzuu ya 2 ukurasa wa 143, Siyaru A'laamin-Nubalaa, juzuu ya 20 ukurasa wa 98.

¹⁰³-Tazama Taarekh Dimash'qiy, juzuu ya 5 ukurasa wa 302.

¹⁰⁴-Tazama vitabu vifuatavyo: Al-l'baru juzuu ya 3 ukurasa wa 319, na Siyaru A'laamin-Nubalaa juzuu ya 19 ukurasa wa 12.

¹⁰⁵-Tazama Al-Ibar juzuu ya 3 ukurasa wa 137. Na Shadharaat juzuu ya 3 ukurasa wa 215-216, na Siyaru A'laamin-Nubalaa juzuu ya 17 ukurasa wa 367.

¹⁰⁶-Tazama Siyaru A'laamin-Nubalaa juzuu ya 15 ukurasa wa 413, Tazama Tadh'kiratul-Hufadh juzuu ya 3 ukurasa wa 858, na Siyaru A'laamin-Nubalaa, juzuu ya 15 ukurasa wa 412, pia tazama Lisaanul-Mizan, juzuu ya 1 ukurasa wa 375.

Mpokezi wa sita:

Ahmad Ibn Zuheir Ibn Harbi, huyu ni mtu Thiqa, mkweli.¹⁰⁷

Mpokezi wa saba:

Amru Ibn Mar'zuq Al-Baahiliy; huyu ni mtu madhubuti, mwingi wa hadithi.¹⁰⁸

Mpokezi wa nane:

Shu'bah, jina lake kamili ni **Shu'bah Ibnu Hajjaaj Ibn War'di Al-Ataqiy Al-Azdiy, Abu Bistwaam**.¹⁰⁹

Mpokezi wa tisa:

Salamah Ibnu Kuheili, Ibn Huswain Al-Hadhramiy, Abu Yahya Al-Kuufiy, bwana huyu alikuwa ni katika watu madhubuti katika mji wa Kufa.¹¹⁰

Mpokezi wa kumi:

Zaid Ibnu Wah'bi, maarufu kwa jina la **Abu Suleiman Al-Juhaniy Al-Kufiy**, Bwana huyu alisafiri kutoka Kufa kuelekea Madina akimfuata Mtume swalla Ilaahu alayhi wasallam, Mtume alifariki akiwa yeye bado yuko njiani.

Amesema Imamu Ibnu Abdil-Barri na Imamu Ibnu Mandah: "Alisilimu katika uhai wa Mtume -swalla Ilaahu alayhi wasallam- na akahama kumfuata, lakini hakumdiriki. **Ni mtu mwaminifu tena mtukufu**, amefariki baada ya mwaka 80, na pia inasemekana kuwa amefariki mwaka 96 Hijiria."

Bwana huyu amepokea hadithi kutoka kwa Maswahaba hawa wafuatao:

Umar, Uth'man, Ali, Abu Dharri, Ibn Mas'oud, Hudhaifah, Abu Dar'dai, Abu Musa na wengineo. Na wamekubaliana wanachuoni wa hadithi kuwa ni mtu mwaminifu, mkweli. Imepokewa kutoka kwa Suleiman Ibn Mih'raan Al-A'mash kwamba amesema:

"إِذَا حَدَّثَكَ زَيْدُ بْنُ وَهْبٍ عَنْ أَحَدٍ فَكَأَنَّكَ سَمِعْتَهُ مِنَ الَّذِي حَدَّثَكَ عَنْهُ."

"Akikusimulia Zaid Ibn Wah'bi habari kutoka kwa mtu yeyote, basi ni kama umemsikia huyo aliyeisimulia."¹¹¹

¹⁰⁷-Tazama Lisanul-Mizaan juzuu ya 1 ukurasa wa 71, na Sualatul-Hakim juzuu ya 1 ukurasa wa 88.

¹⁰⁸ - Tazama Twabaqaatul-Kubra juzuu ya 7 ukurasa wa 305.

¹⁰⁹-Tazama vitabu vifuatavyo: Tahdhibut-Tahdhib juzuu ya 2 ukurasa wa 498-453, tarjama namba 3254. Na Taq'ribut-Tahdhib, tarjama namba 3087.

¹¹⁰-Tazama At-Tahdhib ya Ibnu Al-Asqalaaniy, juzuu ya 4 ukurasa wa 155.

¹¹¹-Tazama Al-Istia'bu juzuu ya 4 ukurasa wa 73. Na Al-Isaabah, juzuu ya 4 ukurasa wa 90 na Tah'dhibut-Tahdhib juzuu ya 3 ukurasa wa 427.

Ndugu msomaji! Ukiyatazama maelezo ya wanachuoni wa hadithi juu ya wapokezi wote kumi waliomo kwenye sanad hii, utauona ushahidi wa wazi juu ya ukweli na uaminifu wao.

Halikadhalika ukiitazama sanad hii kwa umakini na utulivu, ukamchunguza mpokezi mmoja baada ya mwingine, hutompata mpokezi mwenye jina la **Seif Ibn Umar At-Tamimiy**.

Na kwa kufanya hivyo, ndipo utakapogundua **uongo** wa Mur'tadha Al-Askariy, na wanaomuiga katika uongo huo, pale walipodai kwamba riwaya zote zinazomtaja **Myahudi Abdullahi Ibnu Sabai** zimepokewa kutoka kwa Seif Ibn Umar At-Tamimiy! Jambo ambalo ni uongo mpevu.

Riwaya hii moja peke yake inatosha katika kuubatilisha uongo na uzandiki uliozushwa na kina Murtadha Al-Askariy na kutiliwa nguvu na Jaafar Mwazoa kwa lengo la kuwadanganya wasiojua.

KAULI ZINAZOTHIBITISHA KUWEPWA KWA IBNU SABAI

Baada ya kukutajia baadhi ya Riwaya za Shia na Sunni zinazothibitisha kuwepo kwa Abdullahi Ibnu Sabai bila ya kupitia kwa Seif Ibnu Umar wala kupokewa na Twabari, ni vyema katika sehemu hii nifuatishie kauli za wanachuoni wa Shia lth'naashariyya na Ahli Sunna wal-Jamaa zinazothibitisha kuwepo kwa Myahudi huyu aliyelaaniwa, ili kuyabatilisha madai ya uongo ya baadhi ya waandishi wa Shia kwamba habari za kuwepo kwa Myahudi huyu ni ngano zilizozuliwa na Ahlus-Sunna, kwa hiyo hazina usahihi wowote.

KAULI ZA SHIA ITH'NAASHARIYYA

Kuna kauli nyingi za Maulamaa wa Shia lth'naashariyya zinazothibitisha kuwepo kwa kiumbe huyu muovu, miongoni mwa kauli hizo ni zile kauli mbili Mashia; **Hassan Bin Mussa An-Nawbakhtiy** aliyefariki mwaka 310 Hijiriyya, na **Abu Amri Muhammad Bin Umar Al-Kashiy** aliyefariki mwa 340 Hijiriyya, tulizozitaja huko nyuma chini ya kichwa cha habari kisemacho Kudhihiri kwa Ibnu Sabai.

KAULI YA TATU

Amesema Mshia Abu Ja'far As-Saduuq Muhammad Ibn Baabawayhi Al-Qummiy aliyefariki mwaka 381 Hijiriyya:

"وقَالَ أَمِيرُ الْمُؤْمِنِينَ (ع) إِذَا فَرَعَ أَحَدُكُمْ مِنَ الصَّلَاةِ فَلْيَرْفَعْ يَدَيْهِ إِلَى السَّمَاءِ وَلْيَنْصَبْ فِي الدُّعَاءِ فَقَالَ ابْنُ سَبَّأٍ: يَا أَمِيرَ الْمُؤْمِنِينَ أَلَيْسَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ فِي كُلِّ مَكَانٍ..."

"Amesema Amiiirul-Muuminina (a.s.): Atakapomaliza mmoja wenu kuswali, basi na anyanyue mikono yake juu, kisha anyenyekee katika maombi. Akasema **Ibnu Sabai**: Ewe Amirul-Muuminina! Kwani Allah si yuko kila mahali...¹¹² .?"

KAULI YA NNE

Amesema Mshia Ni'matullahi-Jazairiy aliyefariki mwaka 1112 Hijiria:

"قَالَ عَبْدُ اللَّهِ بْنُ سَبَّأٍ لِعَلِيِّ بْنِ أَبِي طَالِبٍ عَلَيْهِ السَّلَامُ أَنْتَ إِلَاهُ حَمَّاءَ فَتَفَاهَ عَلِيٌّ عَلَيْهِ السَّلَامُ إِلَى أَمْدَائِنِ، وَقِيلَ إِنَّهُ كَانَ يَهُودِيًّا فَأَسْلَمَ وَكَانَ فِي الْيَهُودِيَّةِ يَقُولُ فِي يُوشَعَ بْنِ نُونٍ وَفِي مُوسَى مِثْلَ مَا قَالَ فِي عَلِيٍّ."

"Amesema **Abdullahi Ibnu Sabai** kumwambia Ali Ibn Abi Twalib (a.s.) wewe ni ndiye Mungu wa kweli, Ali akamfukuza akampeleka Madaain, na inasemekana kwamba alikuwa ni Myahudi kisha akasilimu, katika Uyahudi wake alikuwa akisema kuhusu Joshua mwana wa Nuni na Musa mfano wa aliyoyasema kuhusu Ali.¹¹³"

KAULI YA TANO

Amesema Mshia Sayyid Husein Al-Musawiy:

نستفيد من النصوص المتقدمة ما يأتي:

١- إثبات وجود شخصية ابن سبأ ووجود فرقة تناصره وتنادي بقوله، وهذه الفرقة تعرف بالسبئية.

٢- إن ابن سبأ هذا كان يهودياً فأظهر الإسلام، وهو وإن أظهر الإسلام إلا أن الحقيقة أنه بقي على يهوديته، وأخذ يبث سمومه من خلال ذلك.

٣- إنه هو الذي أظهر الطعن في أبي بكر وعمر وعثمان والصحابة، وكان أول من قال بذلك، وهو أول من قال بإمامة أمير المؤمنين عليه السلام، وهو الذي قال بأنه عليه السلام وصي النبي صلى الله عليه وآله، وأنه نقل هذا القول عن اليهودية، وأنه ما قال هذا إلا محبة لأهل البيت ودعوة لولايتهم، والتبرؤ من أعدائهم - وهم الصحابة ومن ولاهم بزعمه-.

إذن شخصية عبد الله بن سبأ حقيقة لا يمكن تجاهلها أو إنكارها، ولهذا ورد التنصيص عليها وعلى وجودها في كتبنا ومصادرنا المعتبرة، وللاستزادة في معرفة هذه الشخصية، انظر المصادر الآتية: الغارات للثقفى، رجال الطوسى، الرجال للحلى، قاموس الرجال للتستري، دائرة المعارف المسماة بمقتبس الأثر للأعلمى الحائري، الكنى والألقاب لعباس القمي، حل الإشكال لأحمد بن طاووس المتوفى سنة (٦٧٣)، الرجال لابن داود، التحرير للطاووسى، مجمع الرجال للقهبائى، نقد الرجال للتفرشى، جامع الرواة للمقدسى

¹¹² - Tazama kitabu 'Man'laa Yahdhuruhul-Faqihi', juzuu ya 1 ukurasa wa 78, hadithi namba 955, chapa ya kwanza kimepigwa chapa na Ansariyan Publications, Qum- Iran.

¹¹³ - Tazama katika kitabu chake **Al-An'waarun-Nu'maniyyah**, juzuu ya 2 ukurasa wa 234.

الأردبيلي مناقب آل أبي طالب لابن شهر آشوب، مرآة الأنوار لمحمد بن طاهر العاملي، فهذه على سبيل المثال لا الحصر أكثر من عشرين مصدراً من مصادرنا تنص كلها على وجود ابن سبأ، فالعجب كل العجب من فقهاءنا أمثال المرتضى العسكري والسيد محمد جواد مغنية وغيرهما في نفي وجود هذه الشخصية، ولا شك أن قولهم ليس فيه شيء من الصحة.

"Kutokana na maandiko yaliyotangulia tunapata faida zifuatazo:

1-Kuthibitisha kuwepo kwa **Ibnu Sabai**, na kuwepo kwa kikundi kilichokuwa kikitetea na kuutangaza ujumbe wake, na kikundi hiki kilijulikana kwa jina la Sabaiyyah.

2- Hakika huyu **Ibnu Sabai** alikuwa ni Myahudi, kisha akadhihirisha Uislamu, na hata kama yeye alidhihirisha Uislamu, lakini ukweli ni kwamba bado alibakia kwenye Uyahudi wake, na katika kipindi hicho akawa anaeneza sumu zake.

3-Hakika yeye ndiye aliyedhihirisha matusi dhidi ya Abu Bakar, Umar, Uth'mani na Maswahaba kwa ujumla, na yeye ndiye wa kwanza kufanya hivyo, na yeye pia ndiye mtu wa kwanza kusema kuhusu Ukhalifa wa Amiril-Muuminina (a.s.), na yeye ndiye aliyesema kwamba (Ali a.s.) ni Wasii wa Mtume swalla llaahu alayhi waalihi wasallam, -na kauli hii ameichukua kutoka kwenye Uyahudi- na akadai kwamba hakusema haya yote isipokuwa kwa kuwapenda Ahlul-Baiti, na kuwaita watu kwenye kuwapenda wao na kujiweka mbali na maadui zao -ambao ni Maswahaba na wanaowapenda Maswahaba, kwa madai yake-.

Kwa hivyo basi, **Abdullahi Ibn Sabai kuwepo kwake ni jambo la hakika na wala haifai kulipuuzia au kulipinga, ndiyo maana kumekuja kutajwa kwake na kuwepo kwake ndani ya vitabu vyetu na Masadiri zetu zenye kutegemewa."**

Kisha akaendelea kusema **Mshia Al-Musawiy:**

Na kwa faida zaidi ya kumjua Ibn Sabai, tazama vitabu vifuatavyo: Al-Gharaatu cha Athaqafiy, Rijaalut-Tuusiy, Rijaalul-Hilliy, Qaamusir-Rijaali cha Tustariy, Daairatul-Ma'rifi kinachoitwa Muq'tabasul-Athari cha A'lamiy Al-Hairiy, Al-Kunaa wal-Alqaabu cha Abbas Al-Qummiy, Hallul-Ishkaali cha Ahmad Ibn Twausiy aliyefariki mwaka 673, Ar-Rijaal cha Ibn Daud, At-Tahriir cha At-Twaausiy, Maj'mau Ar-Rijaali cha Al-Qahbani, Naqdur-Rijaali cha Tafrashiy, Jamiur-Ruwaat cha Al-Maqdisiy Al-Ar'dabiliy, Manaqibu Aali Abi Twalib cha Ibn Shahri Ashuup na Mir'atul-An'waari cha Muhammad Ibn Twahir Al-Aamiliy.

Kisha akamalizia Mshia huyu kwa kusema:-

"(Vitabu) hivi tulivyovitaja ni kwa njia ya kutolea mfano tu, na si kwa kuvidhibiti (vitabu vyote), bali kuna zaidi ya vitabu ishirini katika vitabu vyetu vikubwa vinavyoelezea wazi wazi juu ya kuwepo kwa **Ibnu Sabai**.

Sasa ajabu ya maajabu yote iko kwa wanachuoni wetu kama vile **Mur'taza Al-Askariy, Sayyid Muhammad Jawad Mugh'niyyah na wengineo wanapopinga kuwepo kwa mtu huyu! Hapana shaka kuwa kauli yao hii haina usahihi wowote**¹¹⁴ Mwisho wa kunukuu.

Muhtasari wa kauli hizi:

Kauli hizi tano tulizozinukuu ni miongoni mwa kauli chache za Maulamaa wa Shia lth'naashariyya zinazothibitisha uhakika wa kuwepo kwa kiumbe hiki kiovu (**Myahudi Abdullahi Ibnu Sabai**), wanachuoni hao wa Shia wanakiri kwamba Myahudi huyu alikuwepo na si mtu wa kubuni. Na miongoni mwa ushahidi wenye kuthibitisha kuwepo kwa mtu huyo ni:-

- i- Riwaya sahihi zilizomo kwenye vitabu vikubwa vya Shia.
- ii- Kuwepo kwa kikundi cha watu wenye kumtetea na kuzitangaza fikra zake, kikundi hicho kilijulikana kwa jina la Sabaiyyah.
- iii- Kutajwa kwake katika vitabu vikubwa, vikongwe, tena vyenye kutegemewa kwa Shia lthnaashariyya.

Ndugu msomaji! Hebu izingatie kauli hii ya tano ya Mshia Al-Musawiy na zile hoja zetu tulizozitoa, kisha uzilinganishe na hoja za kina Murtadha Al-Askariy na Jaafar Mwazoa, bila shaka kwa kufanya hivyo utabainikiwa na ukweli wa kuwepo kwa **Myahudi Abdullahi Ibnu Sabai**.

KAULI ZA AHLI SUNNA WAL-JAMAA

Wanachuoni wote wa Ahlu Sunna wanathibitisha juu ya kuwepo kwa mtu huyu na wafuasi wake Sabaiyya ambao ni Maghulaati, lakini kwa kuogopea kurefuka kwa kitabu chetu nitakutajia baadhi ya vitabu na nambari za juzuu na kurasa;

- 1- Maqaalaatul-Islaamiyyina juzuu ya 1 ukurasa wa 85 cha Imamu Abul-Hasan Al-Ash'ariy
- 2- Kitabul-Majruuhina juzuu ya 2 ukurasa wa 262, cha Imamu Ibnu Hibbaan Al-Bustiy.
- 3- Al-Bad'u wat-Taarekh juzuu ya 5 ukurasa wa 129 cha Imamu Al-Maqdisiy.
- 4- Taarekh Dimash'iqy (**The History of Damascus**) juzuu ya 3 ukurasa wa 29, cha Imamu Ibn Asaakir.

¹¹⁴-Tazama kitabu chake "Kash'ful-As'raari wa Tab'riatu Aimmatil-At'haari" ukurasa wa 12-13.

- 5- Ad-Dhuafaa juzuu ya 1 ukurasa wa 339, Al-Mizan juzuu ya 2 ukurasa wa 426 na Taarekhul-Islami juzuu ya 2 ukurasa wa 122-123, vyote vya Imamu Ad-Dhahbiy.
- 6- Al-Waafi wal-Wafayaat, juzuu ya 17 ukurasa wa 20 cha Imamu As-Swafadiy. Na vinginevyo miongoni mwa vitabu vya historia na Firaq (makundi) n.k.

Ndugu msomaji! Kwa kauli hizo za wanachuoni wa Shia na Ahli Sunna imetuthibitikia kuwa kadhia ya kuwepo **Abdullahi Ibnu Sabai** ni kadhia kongwe tangu karne za mwanzo za Uislamu, na wanachuoni wote wa Kiislamu waliomzungumzia Myahudi huyu wamethibitisha kuwepo kwake kwa kutegemea vyanzo madhubuti vinavyotegemewa.

Ama fikra ya kupinga kuwepo mtu huyu ni fikra iliyozushwa na Wazandiki na Makafiri wa Kizungu, kisha ikabebwa na Mshia Murtadha Al-Askariy na wengineo katika wanafunzi wa Wazandiki hao kama vile Twaha Husein na mfano wake.

FAIDA:-

Wakati nikiwa katika hatua za mwisho wa utafiti wangu juu ya suala la kuwepo kwa **Myahudi Abdullahi Ibnu Sabai** kiliangukia mikononi mwangu kitabu cha Kishia kiitwacho **Lillaahi walil-Haqiiqah**, cha Mshia **Ali Aali Muhsin**, kupitia **Shabakat Shia't Al-Aalamiyyat**, kitabu ambacho mtunzi wake amekusudia kumjibu Mshia mwenzake **Sayyid Husein Al-Musawiy** juu ya uandishi wa kitabu chake **Lillaahi Thumma lit-Taarekh**.

Mshia Sayyid Husein Al-Musawiy alipokuwa akimzungumzia Ibnu Sabai, na kuonesha masikitiko yake dhidi ya baadhi ya waandishi wa Shia katika zama hizi namna wasivyokuwa waaminifu kwa kupinga kwao kuwepo kwa **Myahudi Abdullahi Bin Sabai** bila hoja za kielimu, na hali ya kuwa vitabu vyao vya Hadithi, Itikadi, Historia n.k. vinathibitisha kuwepo kwa mtu huyu, Mshia huyu Sayyid Husein akajibiwa na Mshia mwenzake Bwana Ali Aali Muhsin kwa maneno haya yafuatayo:

وَأَقُولُ: إِنَّ الْعَجَبَ مِمَّنْ يَدَّعِي الْفُقَاهَةَ وَالْإِجْتِهَادَ كَيْفَ تَخْفَى عَلَيْهِ مَسْأَلَةُ بَسِيطَةٍ مِنْ أَبْسَطِ الْمَسَائِلِ الرَّجَالِيَّةِ، وَهِيَ أَنْ الْمَشْهُورَ الَّذِي كَادَ أَنْ يَكُونَ إِجْمَاعاً بَيْنَ عُلَمَاءِ وَفُقَهَاءِ الْإِمَامِيَّةِ قَدِيمًا وَحَدِيثًا أَنْ عَبْدَ اللَّهِ بْنِ سَبَأٍ شَخْصِيَّةً كَانَ لَهَا وَجُودٌ، وَقَدْ نَصَّ الْعُلَمَاءُ عَلَى ذَلِكَ فِي كَتْمِهِمُ الرَّجَالِيَّةَ الْمَعْرُوفَةَ.

فقد قال الشيخ الطوسي في رجاله: "عبد الله بن سبأ الذي رجع إلى الكفر وأظهر الغلو." رجال الشيخ الطوسي ص ٨٠. وقال العلامة الحلي في كتابه خلاصة الأقوال: "عبد الله بن سبأ غال ملعون، حرّقه أمير المؤمنين عليه السلام بالنار، كان يزعم أن علياً عليه السلام إله، وأنه نبي." رجال العلامة الحلي ص ٢٣٧ " اهـ.

"Na ninasema; ajabu ni kwa mtu anayejidai kuwa ana utambuzi na Jitihada (katika mambo ya dini), inawezekana vipi kufichikana kwake masuala mepesi mno (kama haya) katika masuala ya wapokezi! Jambo lililotangaa ambalo linakurubia kuwa ni Ijmai (maafikiano) baina ya wanachuoni na watambuzi wa fiq'hi katika (madhehebu ya) Imaamiyya tangu kale hadi sasa ni kwamba; **Abdullahi Ibnu Sabai ni mtu aliyekuwepo**. Na wamelielezea jambo hilo wanachuoni katika vitabu vyao vya Rijaali (wapokezi) vilivyo maarufu. Amesema Sheikh At-Tusiy katika kitabu chake Ar-Rijaal; Abdullahi Bin Sabai ambaye alirejea kwenye ukafiri na akadhihirisha Ghuluwu (kuvuka mipaka kwa kuwapa viumbe sifa za Allah), tazama Rijaal Sheikh At-Tusiy ukurasa wa 80. Na amesema Allaamah Al-Hilliy katika Khulaasat Al-Aq'waali; **Abdullahi Ibnu Sabai ni mtu aliyevuka mipaka**, aliyelaaniwa, Amirul-Muuminina (a.s.) alimchoma moto.

Alikuwa anadai kwamba Ali a.s. ni Mungu mwenye kuabudiwa kwa haki na kwamba yeye ni Nabii. Tazama kitabu Ar-Rijaal cha Al-Allaamah Al-Hilliy ukurasa wa 237.¹¹⁵ Mwisho wa kunukuu. Pia amesema tena Mshia huyo akimjibu mwenzake;

وأقول: إن مشهور علماء الشيعة ومن جملتهم كاشف الغطاء قد ذهبوا إلى وجود عبد الله بن سبأ، وأنه ادعى الألوهية لأمير المؤمنين عليه السلام، فأحرقه بالنار في جملة رجال ادعوا ذلك معه، وهذا يعرفه كل من بحث في كتب الرجال وتفحص الأقوال.

"Na ninasema; kwa hakika walio mashuhuri katika wanachuoni wa Shia, akiwemo katika jumla yao Kaashiful-Ghitai wameelekea kwenye kuwepo kwa Abdullahi Bin Sabai na kwamba alidai Uungu kwa Amiril-Muuminina alayhi salaam, na yeye akamchoma moto pamoja na jumla ya watu waliodai hilo, na hili analijua kila aliyefanya utafiti kwenye vitabu vya Rijaali na akazipima kauli.¹¹⁶"

Na pale Mshia Sayyid Husein Al-Musawiy alipoonesha tena malalamiko yake kwa kusema; "Pamoja na kuwa tunapovisoma vitabu vyetu vyenye kuzingatiwa tunakuta kwamba Ibnu Sabai ni mtu wa hakika"

Mshia Ali Aali Muhsin alimjibu kwa kumwambia;

لقد قلنا فيما مر: إن المشهور بين علماء الشيعة إن لم يكن إجماعاً أن عبد الله بن سبأ شخصية حقيقية، ولم ينكر وجودها معروف من الأساطين، وكتبتهم خير شاهد على ما نقول.

¹¹⁵-Tazama **Lillaahi walil-Haqiqah** ukurasa wa 34.

¹¹⁶-Tazama kitabu hicho hicho ukurasa wa 36.

"Tulishasema katika sehemu iliyopita kwamba; lililomashuhuri kwa Maulamaa wa Shia kama si Ijmai (maafikiano ya wote) Abdullahi Bin Sabai ni mtu wa hakika, na hakuna aliyepinga kuwepo kwake mwanachuoni yeyote mwenye kujulikana miongoni mwa wanachuoni wenye kutegemewa, na vitabu vyao ni ushahidi uliobora kwa tunayoyasema"¹¹⁷

Na pale Mshia Sayyid Husein Al-Musawiy alipoyatilia nguvu madai yake ya kuwepo Ibnu Sabai kwa kuitaja riwaya isemayo; **[Allah amlaani Abdallahi Ibn Sabai, kwa sababu amedai kwamba, Amiril-Muuminina (Ali) ni Mungu.....]**¹¹⁸ Mshia Ali Aali Muhsin akamjibu kwa kusema;

وأقول: هذه الرواية صحيحة السند، وهي إحدى ثلاث روايات أثبتت أن عبد الله بن سبياً شخصية حقيقية، وأنه ادعى الألوهية لأمير المؤمنين عليه السلام، فأحرقه أمير المؤمنين عليه السلام بالنار.

"Ninasema: Riwaya hii ni yenye sanadi iliyosahihi, **nayo ni moja miongoni mwa riwaya tatu zinazothibitisha kwamba Abdullahi Bin Sabai ni mtu wa hakika**, na kwa hakika alidai kuwa Amiril-Muuminina (Ali Bin Abi Taliba) alayhi salaam ndiye Mungu (Muumba anayestahiki kuabudiwa), na Amiril-Muuminina alimchoma moto"¹¹⁹ Na pale aliposema Mshia Al-Musawiy; "Kutokana na maandiko yaliyotangulia tunapata faida zifuatazo:

I-Kuthibitisha kuwepo kwa **Ibn Sabai**, na kuwepo kwa kikundi kilichokuwa kikimtetea na kuutangaza ujumbe wake, na kikundi hicho kilijulikana kwa jina la Sabaiyyah...." Akasema **Mshia Ali Aali Muhsin**;

وأقول: أما أنه كان له وجود فنعم، وأما وجود فرقة تناصره تُعرف بالسبئية فهو غير صحيح، وإن جاء ذكرها في بعض الأقوال، لأن ورود ذلك في بعض الكتب ناشئ من النقل من غير تحقيق للمسألة. وبدل على ما قلناه أنك لا تجد لهذه الفرقة أتباعاً معروفين، ولا علماء مشهورين، ولا أقوالاً مدونة، ولا كتباً منتشرة، وهذا هو المقوم لوجود أية فرقة من الفرق، أو اعتبار أية طائفة من الطوائف.

"Ninasema; Ama kuwepo kwake, ndio alikuwepo. Ama (suala la) kuwepo kikundi kilichomtetea, kijulikanacho kwa (jina la) Sabaiyyah hilo si sahihi. Hata kama kutajwa kwake kumekuja kupitia baadhi ya kauli, kwa sababu ujio wake katika baadhi ya vitabu umetokana na kunukuliwa pasi na kuyahakiki mas'ala. Na ushahidi wa haya tunayoyasema ni kwamba hutapata wafuasi wa kundi hili wanaojulikana,

¹¹⁷-Tazama kitabu hicho hicho ukurasa wa 39.

¹¹⁸-Tazama hadithi hii katika vitabu vya Shia vifuatavyo; **Ikh'tiyaaru Ma'rifatir-Rijaali** cha Al-Kashiy, ukurasa wa 324. Na **Bihaarul-An'waari** cha Muhammad Baaqir Al-Maj'lisiy, juzuu ya 25 ukurasa wa 478.

¹¹⁹ Tazama '**Lillaahi walil-Haqiqah'** ukurasa wa 40.

wala Maulamaa walio mashuhuri, wala kauli zilizoandikwa katika vitabu vilivyotangaa, na hiki ndicho kipimo cha kuwepo kundi katika makundi, na kuzingatwa kuwepo kwa kundi lolote miongoni mwa makundi"¹²⁰

Kisha akasema katika ukurasa wa 56;

وأما ما ذهب إليه السيد مرتضى العسكري والشيخ محمد جواد مغنية من نفي وجود ابن سبأ فهو رأي من الآراء التي وافقهما عليه بعض الباحثين من أهل السنة ، وإن كنا لا نوافقهم فيه .

"Ama yale aliyoyaelekea Sayyid Murtadha Al-Askariy na Sheikh Muhammad Jawad Mughniyya katika kupinga kuwepo kwa Ibnu Sabai, hizo ni rai miongoni mwa rai zilizoafikiwa na baadhi ya watafiti wa Ahli Sunna, hata kama sisi hatuafikiani katika hilo."

Kisha Mshia huyo akamalizia maudhui hii kwa kutoa kauli iliyojaa ujasiri wa hali ya juu kwa kusema;

ومنه يتضح أن ما زعمه الكاتب من أن فقهاء الإمامية ينفون شخصية ابن سبأ بعيد عن الصواب .

Na kutokana na hilo, inabainika kwamba yale anayoyadai mwandishi (Sayyid Husein Al-Musawiy) kwamba wanachuoni wa Shia Imaamiyya wanapinga kuwepo kwa Ibnu Sabai ni jambo lililombali kabisa na usahihi (sio kweli kwamba wanachuoni wa Shia wanapinga kuwepo kwa Myahudi Abdullahi Bin Sabai, bali wao wanakubali kuwepo kwake)!!!

Muhtasari wa mjadala huu;-

Ndugu msomaji! Katika sehemu iliyopita tulithibitisha kwa hoja za kielimu juu ya kuwepo kwa Ibnu Sabai, pamoja na kuubainisha uongo wa kina Al-Murtadha Al-Askariy wenye kudai kuwa riwaya zinazomtaja Ibnu Sabai ni riwaya za kutunga zilizobuniwa na Seif Bin Umar.

Na katika sehemu hii hoja yetu imepata nguvu kupitia mjadala wa Mashia hawa wawili; Sayyid Husein Al-Musawiy na Ali Aali Muhsin.

¹²⁰ Tazama kitabu hicho hicho ukurasa wa 46-47.

Mshia Sayyid Husein Al-Musawiy katika kitabu chake **Lillaahi thumma Lit-Taarekh** anasikitishwa na ubabaishaji unaofanywa na baadhi ya Mashia wa kupinga kuwepo kwa Myahudi Ibnu Sabai na hali ya kuwa riwaya na kauli za wanachuoni wa Imaamiyyah wazamani zinathibitisha kuwepo kwake.

Naye Mshia Ali Aali Muhsin anamjibu Mshia mwenzake kwa kumwambia kuwa huna haja ya kusikitika, suala la kuwepo kwa Myahudi Ibnu Sabai ni jambo lililotangaa ambalo linakurubia kuwa ni Ijmai (maafikiano) baina ya wanachuoni na watambuzi wa fiq'hi katika (madhehebu ya) Imaamiyya tangu kale hadi sasa, kwa hiyo wanachuoni wetu wa Shia hawastahiki kulaumiwa. Ama upinzani na ukaidi wa Murtadha Al-Askariy na Muhammad Jawaad Mughniyya wa kupinga kuwepo kwa Myahudi huyo, hizo ni rai zao binafsi na sisi Shia hatukubaliani na wao katika hilo.

UONGO WA MSHIA JAAFAR MWAZOA KUHUSU IBNU SABAI

Ndugu msomaji! Kabla ya kukuletea majibu sahihi ya maswali tuliyohoji hapo nyuma, ni vyema tukaubatilisha uongo wa Mshia Jaafar Mwazoa aliouleta katika kitabu chake Shimo Refu kwenye maudhui hii. Baada ya Mshia Mwazoa kushindwa kujibu hoja kielimu juu ya madai yake ya kutokuwepo Myahudi Abdullahi Ibnu Sabai, ndipo alipoanza kutumia mbinu ya uongo na hoja za kiubabaishaji. Katika sehemu hii nitakuorodheshea baadhi ya uongo wake, kisha nitafuatishia majibu yetu kwa ufupi, na sitampatiliza kwa kila uongo aliousema kwa kuhofia kitabu kitarefuka na kutoka nje ya maudhui yetu.

Uongo wa kwanza, kuhusu wafuasi wa Ibnu Sabai:-

Mshia Mwazoa amedai katika ukurasa wa 72 wa kitabu chake kwamba mimi nimesema kuna baadhi ya Maswahaba walikuwa ni wafuasi wa Myahudi Ibnu Sabai, amenituhumu kwa tuhuma hiyo baada ya kuyanukuu maneno yangu niliyoyasema katika ukurasa wa 61 wa kitabu changu **Uyahudi nyuma ya pazia la Ahlil-Baiti** mimi nilisema hivi:-

"Katika kutimiza azma yake ya kuuvunja Uislamu aliwaendea watu vile walivyo ili apate urahisi wa kupenyeza sumu yake, alianza kwenye kumsifu Ali Ibnu Abi Twalib (r), sambamba na kumkashifu Uthmani (r). Pia aliwakashifu Maswahaba wote ila wachache¹²¹"

Ndugu msomaji! Bila shaka umeyasoma maneno yangu hayo vizuri na umeyaelewa. Kama hivyo ndivyo, kwa kuitumia neema ya akili uliyopewa na Allah, je umeelewa kwamba mimi nimesema;

1- Wafuasi wa Myahudi Ibnu Sabai walikuwa ni Maswahaba?

¹²¹-Maneno yote hayo ni yangu, na yako sawa sawa, isipokua katika herufi zilizopo kwenye mabano, hizo ni zake yeye, mimi nimekiandika; "radhia llaahu an'hu" kwa ukamilifu, na si kwa ishara ya herufi (r) kwa kuhofia upotoshaji wa wasiojua makusudio ya kifupi hicho.

- 2- Je, kwa maneno yangu hayo umefahamu kwamba waliomuunga mkono Myahudi Ibnu Sabai walikuwa ni Maswahaba?
- 3- Je, kwa mujibu wa maneno yangu hayo umefahamu kwamba Maswahaba walikuwa na nia mbaya dhidi ya Uislamu na lilikuwa lengo lao ni kuubomoa Uislamu? Bila shaka, jawabu litakuwa hapana, kama jawabu ni hilo, je Mshia Mwazoa umeutoa wapi ufahamu huo batili juu ya maneno yangu?

Hebu soma maneno yake kwenye ukurasa wa 72 wa kitabu chake 'Shimo Refu' uone namna anavyonizulia uongo:-

"Katika sura hii Ibnu Mafuta alikosa hoja kiasi cha kuwatuhumu Masahaba watukufu mambo mazito ambayo lao yangethubutu kweli kuwepo kwa Masahaba basi Uislamu hasa wa Madhehebu ya Ahlu Sunnat wal-Jamaa utakuwa mashakani, bali Usunni utakuwa ni **Ukafiri wa wazi** kabla tuhuma hiyo haijatupiwa Mashia....."

Soma tena maneno yake katika ukurasa huo huo baada ya kuyanukuu maneno yangu hayo, kisha uone namna Mshia huyu anavyonizulia uongo:-

"Hapa Wahabi huyu **mwenye uchungu wa kinafiki** juu ya Masahaba anatueleza kuwa Yahudi bin Sabai alifanikiwa kupenyeza sumu kwa urahisi **kwa sababu ya hali ya Masahaba namna walivyokuwa.**"

Kisha Mshia huyu akaendelea kunizulia uongo katika ukurasa wa 73 kwa kusema;

"Abdallah bin Sabai huyu akaweza kutimiza azma yake ya kuuvunja Uislamu kwa msaada mkubwa wa **hali za watu ambao kwa zama hizo walikuwa ni Masahaba!!!** Nao Masahaba walipoendewa na Ibnu Sabai wakasifiwa **Ali (r) wakaoneshwa kuwa yeye ndiye Khalifa....**Bali wakakashifiwa na wao wenyewe tena wengi wao, nao wakamuacha Abdallah bin Sabai mpaka akatimiza azma yake hiyo ya kuuvunja Uislamu bali baadhi yao wakamuunga mkono na kuanzisha pote lao."

Ndugu msomaji! Sina shaka umejionea mwenyewe namna kijana huyu alivyokuwa jasiri wa kuzua uongo?

Kauli hii ya kwamba: **...watu ambao kwa zama hizo walikuwa ni Masahaba!!!** Ameitoa wapi? Au Mshia Mwazoa anataka kutwambia kwamba katika zama za Khalifa wa tatu Uthmani radhia Ilaahu an'hu hakukuwa na watu wengine zaidi ya Maswahaba tu? Historia hiyo ya uongo ameisoma katika Hawzat gani ya Kishia? Kisha baada ya kuzua uongo huo, akaanza kutoa machozi ya Kinafiki, eti anawalilia Maswahaba! Akasema Mshia huyo katika ukurasa huo wa 73 huku akitokwa matusi ovyo kama kawaida yake;

"Hivi haya ni matusi madogo kwa Masahaba!!? Je, huu si ufedhuli wa wazi juu ya Uislamu na Masahaba!!? Je, huu si uhamnazo wa kiwahabi katika kuyatazama mambo kimantiki na akili salama!!? Vipi kwa mtu mwenye akili timamu na maarifa yaliyo kamilika, huku akiongozwa na mapenzi juu ya Masahaba, kisha awakejeli Masahaba kwa kiwango hiki?

MAJIBU YETU

Al-hamdu lillaahi, sisi Ahlu Sunna wal-Jamaa nyoyo zetu, ndimi zetu na kalamu zetu zimesalimika juu ya Maswahaba, hatuwachukii wala hatuwataji ila kwa wema, na tunawaomba Maghfira na Radhi kwa Allah kutokana na kazi kubwa ya kuibeba dini hii adhimu ya Allah, na tunayafanya hayo kwa kufuata mwongozo wa Qur-ani na mafunzo sahihi ya Bwana Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam. Na wakati huo huo tunaitakidi kwamba mtu yeyote anayewatukana Maswahaba hao kuwa ni Mzandiki, tena Mnafiki.

Na hili ni moja katika ya mambo mengi yanayotutofautisha baina yetu na Mashia Raafidhwa, Mashia ambao muhimili wa dini yao ni kuwachukia Maswahaba, kuwatukana, kuwalaani na kuwakufurisha. Na ndiyo maana hutapata kwenye maneno yangu hayo na mengineyo kauli yoyote yenye viashiria vya kuwadharau, au kuwatukana au kuwakashifu Maswahaba, kinyume na anavyodai Mshia Mwazoa. Na ukisoma vitabu vya Maulamaa wa Shia ambao Mwazoa anawakubali utasadikisha kwamba kauli yangu ya kwamba machozi ya Mshia huyu ni machozi ya kinafiki, na

lengo lake ni kuwacheza shere wasomaji wa kitabu chake, kwa sababu Mashia huwasomesha watoto wao tangu wakiwa wadogo fadhila za kuwatukana Maswahaba na dua ya kuwalaani Masanamu wawili wa Ki-Qureishi (Abu Bakar na Umar)?

Hivyo basi, ukweli ambao nimeusimamia juu yake ni kwamba hakuna Swahaba hata mmoja aliyetekwa kiitikadi na Myahudi Ibnu Sabai, kwa sababu Maswahaba radhia Ilaahu an'hum walikuwa ni watu wenye maarifa mazuri mno na elimu ya kutosha kuhusu dini yao. Kadhalika Ibnu Sabai hakufanikiwa kupata wafuasi katika miji ya Makka wala Madina, kwa sababu sehemu hizo waliishi Maswahaba wengi, na wafuasi wengi wa Ibnu Sabai walikuwa ni watu wageni katika Uislamu, na wale walioishi sehemu ambazo idadi ya Maswahaba ni ndogo au hakuna kabisa, kama vile miji ya Basra, Kufa, na Misri¹²². Lakini kwa lengo la kuupotosha ukweli mwandishi huyu wa Shia katika kitabu chake '**Shimo Refu**' amenizulia uongo kwa kusema kwamba eti mimi nimesema walikuwa wafuasi wa Ibnu Sabai ni Maswahaba! Kisha katika ukurasa wa 76 wa kitabu chake hicho kilichojaa uongo mwingi anauliza maswali ya ubabaishai kwa kuhoji:

Je, Bwana Kassim Mafuta anamkusudia Ammar Yasir? Miqdaad? AbuuDharri? Bilal? Abdallah bin Abbas? Zubeir bin Awwaam? Khabbaab? Fatimah Zahraa (as) Na wengineo miongoni mwa Maswahaba? Je, hao si Maswahaba wa Bwana Mtume (s.a.w.w.) !!? Je, ni hao waliokuwa na nia mbaya dhidi ya Uislamu!!? Je? ndiyo hao Masahaba waliomkubali Abdallah bin Sabai na kusadikisha madai yake ya upotoshwaji wa Qur'ani na udhalimu wa Makhalfi waliopora ukhalifa wa Ali (as) na kizazi chake (as)!!!? Je, ndio hao waliomlinda Abdallah bin Sabai Myahudi mpaka akatimiza azma yake!!!

Maswali yote haya atajijibu mwenyewe, kwa sababu na mimi nitamuuliza; ni wapi katika kitabu changu niliposema; Maswahaba walimkubali, au kumuunga mkono Ibnu Sabai?

¹²² -Tazama kitabu Al-Bidaaya wan-Nihaaya cha Imamu Ibnu Kathiir, juzuu ya 7 ukurasa wa 183.

Nina uhakika wa asilimia zote kuwa hataweza kuthibitisha hilo. Na haya ndiyo madhara ya mtu kuandika masuala ya dini huku akiwa na chuki binafsi, nia mbaya, elimu duni na ufahamu finyu.

Mwisho Mshia huyu akamalizia kwa kunipa challenge ya kumtaja watu kumi tu waliomkubali Ibnu Sabai ambao si Maswahaba, akasema katika ukurasa wa 76;

"Na kama hawa siwo basi hebu Wahabi yeyote duniani atutajie japo watu kumi tu waliomkubali huyo Ibnu Sabai na wakawa dhidi ya Khalifa Uthman kutokana na athari hiyo ya Yahudi huyo!"

Eti huyu ndiye mwandishi anayetegemewa na Mashia wenzake, anayejidai kuwa anajua sana historia, matokeo yake anatoa Chalenji za kitoto kama hizi, hivi kweli nikimtaja hao watu kumi ndio atatoka kwenye Ushia, au bado atang'ang'ania kwa sababu amezaliwa huko? Allah ndiye anayejua zaidi sababu iliyompelekea kijana huyu kutoa challenge hii ya kitoto, huwenda amefanya hivyo kwa kudhania kuwa nitashindwa, au huwenda akili yake imefikia ukomo, ikamwambia kuwa maadam yeye hajui basi hakuna mwingine anayewajua watu hao, kwa hiyo, ametoa challenge hiyo akidhani kuwa nitashindwa, na hatimaye nitafedheheka! Sasa mimi kwa lengo la kuikata kiu yake nitamtajia watu zaidi ya hao kumi katika hao wanafunzi wa Myahudi Ibnu Sabai ambao si Maswahaba:-

1. **Kinaana Ibn Bishri At-Tujiibiy**
2. **Umair Ibn Dhaabiy Al-Burjumiy**
3. **Rushaid Al-Hijriy**
4. **Al-Mughira Ibn Said Al-Bajaliy**
5. **Jaabir Ibn Al-Haarith Al-Juufiy**
6. **Abu Nadhri Muhammad Ibn Saaib Al-Kalbi**
7. **Al-Ghaafiqiy Ibn Harbi**
8. **Abdur-Rahman Ibn Udais Al-Balawiy**
9. **Suudan Ibn Humraan Al-Muraadiy**
10. **Abdullahi Ibn Zaid Ibn Warqaa**
11. **Amru Ibn Hamiqi Al-Khuzaiy**

12. Hurquus Ibn Zuhair
13. Hukaim Ibn Jabalah
14. Qutayra As-Sukuuniy
15. Ziyaad Ibn An-nadhri Al-Haarithiy

Hawa ni wachache miongoni mwa wafuasi wa Ibnu Sabai, na wote hao hakuna Swahaba hata mmoja, Mshia Mwazoa alitaka kujua watu kumi tu ambao si Maswahaba na ni wafuasi wa Ibnu Sabai, mimi nimemtajia watu kumi na tano kama zawadi kwake na kwa Mashia wenzake, je wako tayari kutoka kwenye upotovu wa Ushia?

Uongo wa pili, kuhusu Joshua Ibn Nuun:-

Katika kitabu changu '**Uyahudi nyuma ya pazia la Ahlul-Baiti**', ukurasa wa 15, chapa ya kwanza, na ukurasa wa 3, chapa ya pili, baada ya kuzinukuu kauli za Wanachuoni wa Shia zinazothibitisha kuwepo kwa Myahudi Ibnu Sabai nilitaja nukta takribani sita, katika nukta ya pili nilisema hivi:

Kabla ya kusilimu, Myahudi huyu alikuwa akiitakadi kwamba Yoshua ni wasii wa Musa alayhi-salaam.

Maneno hayo yako wazi, lakini Mshia Jaafar Mwazoa kwa kuwa tabia yake ni kusema uongo na kuupotosha ukweli, akanizulia uongo kwa makusudi bila ya kuona aibu, akasema katika ukurasa wa 16 wa kitabu chake **Shimo Refu**:

"Katika nukta ya pili Mafuta anadai kuwa aliyeleta itikadi ya kuwa Ali (a.s.) ni wasii wa Mtume (s.a.w.w.) ni Abdallah Bin Sabai, kama ambavyo hapo mwanzo **alianzisha itikadi** ya kuwa Yoshua ndiye wasii wa Musa (a.s.) ..."

Kisha akamalizia kwa kusema:

"Hivyo Yoshua kuwa wasii wa Musa (a.s.) si kwa dai la Abdallah Bin Sabai, bali ndio hakika ya mambo."

MAJIBU YETU

Ndugu msomaji! Kama ulivyojionea mwenyewe kwenye maneno yangu, sikusema kwamba Abdullahi Ibnu Sabai ndiye **aliyeanzisha itikadi ya kuwa Yoshua ndiye Wasii wa Musa**, bali huo ni uongo aliouzua Mshia Jaafar Mwazoa kwa matashi ya nafsi yake, bali nilisema; **Kabla ya kusilimu, Myahudi huyu alikuwa akiitakadi kwamba Yoshua ni wasii wa Musa alayhi-salaam**, bila shaka maneno haya yako wazi na kila mwenye akili timamu atafahamu kuwa sikuzungumzia kabisa **suala la**

kuanzisha itikadi, bali nilizungumzia suala la kuwa Ibnu Sabai kabla ya kusilimu kwake **aliitakidi kuwa Joshua ni Wasii wa Musa alayhi salaam**.

Uongo wa tatu, kuhusu kauli ya An-Nawbakhtiy;

Miongoni mwa udanganyifu wa makusudi alioufanya Mshia Jaafar Mwazoa ni kufanya tarjama ya uongo kwenye maneno ya mwanachuoni wao wa Kishia aitwaye **Hassan Ibn Musa An-Nawbakhtiy**. Katika kitabu changu '**Uyahudi nyuma ya pazia la Ahlul-Baiti**', niliyanukuu maneno ya mwanachuoni huyo aliyefariki mwaka 310 Hijiriyya, alipokuwa akimuelezea Ibnu Sabai alisema:

"وَحَكَى جَمَاعَةٌ مِنْ أَهْلِ الْعِلْمِ مِنْ أَصْحَابِ عَلِيِّ عَلَيْهِ السَّلَامُ أَنَّ عَبْدَ اللَّهِ بْنَ سَبْيَأَ كَانَ يَهُودِيًّا فَأَسْلَمَ، وَوَالَى عَلِيًّا عَلَيْهِ السَّلَامُ، وَكَانَ يَقُولُ وَهُوَ عَلَى يَهُودِيَّتِهِ فِي يُوشَعَ ابْنِ نُونٍ بَعْدَ مُوسَى عَلَيْهِ السَّلَامُ بِهَذِهِ الْمَقَالَةِ، فَقَالَ فِي إِسْلَامِهِ بَعْدَ وَقَاةِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ فِي عَلِيِّ عَلَيْهِ السَّلَامُ بِمِثْلِ ذَلِكَ. وَهُوَ أَوْلُ مَنْ شَهَرَ الْقَوْلَ بِفَرْضِ إِمَامَةِ عَلِيِّ عَلَيْهِ السَّلَامُ وَأَظْهَرَ الْبِرَاءَةَ مِنْ أَعْدَائِهِ، وَكَاشَفَ مُخَالَفِيهِ. فَمِنْ هُنَا قَالَ مَنْ خَالَفَ الشَّيْعَةَ: إِنَّ أَصْلَ الرَّفْضِ مَاخُودٌ مِنَ الْيَهُودِيَّةِ.."

"Limesimulia kundi kubwa miongoni mwa watu wenye elimu katika wafuasi wa Ali (as) kwamba; Abdullahi Ibnu Sabai alikuwa ni Myahudi akasilimu na akampenda Ali (a.s), na alikuwa akisema na hali yakuwa yuko ndani ya Uyahudi wake: Joshua bin Nun (ndiye mrithi wa Musa) baada ya Musa maneno haya. Na akasema baada ya kusilimu, baada ya kufariki Mtume swalla Ilaahu alayhi wa Aalihi wasallam kuhusu Ali mfano wa hayo (ya Joshua, kwamba Ali naye ni mrithi wa Mtume swalla Ilaahu alayhi wa Aalihi wasallam). Na yeye ndiye mtu wa kwanza kuitangaza kauli ya ulazima wa Uimamu wa Ali (as) na akadhihirisha uadui kwa maadui wa Ali, na akawakashifu (akawatukana) wapinzani wake. Na kuanzia hapo wakasema wapinzani wa Shia: **Asili ya Ushia umechukuliwa kutoka kwenye Uyahudi**¹²³."

Ndugu msomaji! Mshia Jaafar Mwazoa anadai kwamba nilipofanya tarjama ya maneno; وحكى جماعة من أهل العلم; kwa kusema; **"Limesimulia kundi kubwa miongoni mwa watu wenye elimu..."** ni tarjama ya makosa! Na usahihi ningesema; **"limenukuu kundi..."** Baada ya kuleta upinzani huo, akazitaja sababu ambazo zimempelekea yeye kuipinga tarjama yangu na kuiona kuwa ni ya makosa, kisha

¹²³-Tazama katika kitabu chake; "Firaqus-Shia" ukurasa wa 19-20, kimechapishwa na Maktabatu Haidariya iliyoko Najaf chapa ya mwaka 1959 AD.

akaipa nguvu tarjama yake, akasema katika ukurasa wa 20 katika kitabu chake Shimo Refu;

"Tukiangalia msuko wa ibara katika nukuu hii tunaona maana ya 'kusimulia' inawezakana kutumika na kukusudiwa hapa iwapo tu, itatumika kwa kufungamanishwa na neno "kunukuu", yaani iwe maana ya neno "حكي" iliyokusudiwa hapa ni "kusimulia kwa kunukuu maelezo ya mwengine". Maana ambayo itakuwa na ukaribu mkubwa na maana yetu ya pili yaani "kunukuu".

Kisha akasema;

"Hiyo ni kwa sababu ya (Qarina) zifuatazo:-1.Hakuna hao As-haabul ilmi katika wafuasi wa Ali (a.s) waliodai kuwa Abdallah Bin Saba ndiye aliyemtawalisha Ali (a.s). 2. Dai la kuwa "Ushia" umeanzishwa na Myahudi si la Mashia bali ni la wasiokuwa Mashia (Mawahabi). Hivyo wao ndio wanaonasibiana moja kwa moja na ibara hizo. 3. Ibara ya mwisho inayosema; "...ومن هنا قال من خالف الشيعة...." "Na kutokana na maelezo hayo, ndipo walipodai kwa kusema wale walio kinyume na Mashia...."

MAJIBU YETU

Kwanza, ukiyasoma maneno ya An-Nawbakhtiy kuanzia mwanzo hadi mwisho utafahamu kuwa Ibnu Sabai alikuwepo na alikuwa na wafuasi, jambo ambalo Mshia huyu amelipinga bila hoja wala ushahidi wowote.

Pili, maneno haya ya Mshia Mwazoa hayana ukweli hata kidogo, bali yemezungukwa na uongo katika kila upande, na hilo utalifahamu kwa sababu hizi zifuatazo;

Sababu ya kwanza, ni msuko wa maneno ya Mshia An-Nawbakhtiy, kama utayasoma maneno yake kuanzia mwanzo utafahamu kwamba Mshia huyo na yeye ni miongoni mwa wanaosema kuwa Ibnu Sabai ndiye mtu wa kwanza kuutangaza Ukhalifa wa Ali, na hakusema hivyo akimnukuu mtu yeyote, na ushahidi wa hilo ni pale aliposema Mshia huyo;

"السَّبَيْئَةُ قَالُوا بِإِمَامَةِ عَلِيٍّ وَأَتَمَّهَا فَزَضُ مِنْ اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ، وَهُمْ أَصْحَابُ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ سَبْيٍ، وَكَانَ مِمَّنْ أَظْهَرَ الطَّعْنَ عَلَى أَبِي بَكْرٍ وَعُمَرَ وَعُثْمَانَ وَالصَّحَابَةَ وَتَبَرَّأَ مِنْهُمْ، وَقَالَ: "إِنَّ عَلِيًّا أَمْرُهُ بِذَلِكَ" فَأَخَذَهُ عَلِيٌّ فَسَأَلَهُ عَنْ قَوْلِهِ هَذَا، فَأَقْرَبَ بِهِ فَأَمَرَ بِقَتْلِهِ فَصَاحَ النَّاسُ إِلَيْهِ: يَا أَمِيرَ الْمُؤْمِنِينَ أَتَقْتُلُ رَجُلًا يَدْعُو إِلَى حُبِّكُمْ أَهْلَ الْبَيْتِ وَإِلَى وِلَايَتِكَ، وَالْبِرَاءَةَ مِنْ أَعْدَانِكَ؟ فَصَيَّرَهُ إِلَى الْمَدَائِنِ".

"Sabaiyyah, wanaitakidi Uimamu wa Ali, na kwamba huo Uimamu ni faradhi kutoka kwa Allah Azza wa Jalla, wao ni wafuasi wa Abdillahi Ibnu Sabai, alikuwa ni katika waliodhihirisha matusi dhidi ya Abu Bakar, Umar, Uth'mani na Maswahaba wengine na akajitenga nao, na akasema kwamba "Ali amemuamrisha kufanya hivyo" Ali akamkamata kisha akamuuliza kuhusu kauli yake hii, naye akakiri. Ali akaamrisha auwawe, watu wakapiga makelele; Ewe Amirul-Muuminina! Unataka kumuua mtu ambaye analingania watu kwenye kuwapenda nyinyi Ahlul-Baiti! Na anawaita watu kwenye kukupenda wewe na kuwachukia maadui zako, Ali akamfukuza, akampeleka Madaaini"

Ukiyatazama kwa umakini maneno haya utaona kwamba An-Nawbakhtiy anakubali kuwepo kwa Ibnu Sabai na harakati zake, pia anatuthibitishia kuwa miongoni mwa aliyoyalingania ni Ukhalifa wa Ali, halikadhalika kuwatukana Maswahaba wakubwa kama Abu Bakar, Umar na Uthman, kwa madai ya kwamba Ali radhia Ilaahu an'hu amemuamrisha kufanya hivyo.

Sababu ya pili, ni kuwa sababu iliyompelekea Mshia Jaafar Mwazoa kuikataa tarjama tuliyoitoa ni ufahamu wake dhaifu pale aliposema: *"Hakuna hao As-haabul ilmi katika wafuasi wa Ali (a.s) waliodai kuwa Abdallah Bin Saba ndiye aliyemtawalisha Ali (a.s)."*

Sisi tunamwambia Mshia huyu; Hata sisi hatukusema kwamba Ibnu Sabai ndiye aliyemtawalisha Ali, kilichosemwa hapo na Mshia An-Nawbakhtiy ni kuwa Ibnu Sabai **ndiye mtu wa mwanzo aliyedhihirisha kauli ya ulazima wa Uimamu wa Ali,** na kwa sababu hiyo ikasemwa kuwa asili ya Ushia imetokana na yeye.

Sababu ya tatu; ni pale An-Nawbakhtiy alipoyafunga maneno yake kwa kusema: *"Na kutokana na maelezo hayo, ndipo walipodai kwa kusema wale walio kinyume na Mashia...."* Maneno haya yanatoa ushahidi wa wazi juu ya kwamba msimamo uliotangulia kabla ya kauli hiyo ni msimamo wa Maulamaa wa Shia na Sunni. Maulamaa wa Ahli Sunna wao wanaona kuwa mwanzilishi wa Ushia ni Myahudi Abdullahi Ibn Sabai.

Ama Maulamaa wa Shia, pamoja na kuwa wengi wao wanakubaliana na suala la kuwa Myahudi Abdullah Ibnu Sabai ndiye mtu wa kwanza kuitangaza kauli ya ulazima wa Uimamu wa Ali radhia Ilaahu an'hu na ndiye mtu wa kwanza kudhihirisha uadui dhidi ya Maswahaba kwa madai ya kuwa ni maadui wa Ali, na akawatukana aliowaita kuwa ni wapinzani wa Ali, pamoja na yote hayo, lakini Mashia hao hawaoni kuwa yeye ndiye mwanzilishi wa madhehebu yao.

Kwa hiyo, ninasema; maana ya neno "حی" (Hakaa) iliyokusudiwa hapa ni **"Kusimulia"** na si **"Kunukuu"** kama anavyodai Mshia Jaafar Mwazoa. Na hayo pia utayafahamu kwa kuyasoma maneno ya Mshia Al-Kashiy. Ama kauli yake aliposema katika ukurasa wa 22;

"Halafu nataka nikuulize Ibnu Mafuta, hivi kwa akili yako yawezekana kwa hao maulamaa wa wa kishia wajue na wakubali kuwa Ushia ulianzishwa na myahudi na wao wakabakia kwenye Ushia? Una nini kiumbe wewe? Ni mzima kweli?"

MAJIBU YETU

Kwanza, hii si hoja ya kielimu, kwa sababu hizi zifuatazo;

1. Hakuna aliyesema kuwa Maulamaa wa Shia wanaamini kuwa Ibnu Sabai ndiye mwanzilishi wa madhehebu ya Shia, pamoja na kwamba wanakubali kuwa mtu huyu alikuwepo, na alifanya vituko vingi na kuacha athari mbaya ndani ya Ushia.
2. Hakuna sababu ya kushangaa, kwa sababu kuna mambo mengi ndani ya Ushia ambayo Maulamaa wenu wamekiri kuwa yanatoka kwa Maghulaati (wanafunzi wa Ibnu Sabai) lakini bado nyinyi mmeyang'ang'ania na mnayaitakidi kuwa ni mambo muhimu katika madhehebu yenu? Na mfano wa mambo hayo ni;- Ghuluwu (kuvuka kwenu mipaka) kwa Maimamu wenu na Shahada ya tatu kwenye adhana zenu.
Maulamaa wenu wanakiri kuwa Shahada ya tatu haikufundishwa na yeyote katika Imamu wenu wa Ahlul-Baiti ambao mnadai kuwa mnawafuata.

Na wanakiri kuwa watu mwanzo walioizusha Shahada hiyo ya uongo ni Maghulaati (wanafunzi wa Ibnu Sabai) lakini bado kwenu nyinyi ni dini, mnaitumia katika Adhana na Iqaamah! Sasa kinachokushangaza ni kitu gani **ewe Makhluuq wa ajabu usiyeelewa!**

ATHARI ZA IBNU SABAI KATIKA USHIA

Miongoni mwa athari mbaya alizoziacha Myahudi Ibnu Sabai ni kuzalisha kikundi cha wanafunzi waovu waliojulikana kama **Sabaiyya (wafuasi wa Ibnu Sabai)** Kikundi hiki kilibadilika kimuelekeo na kimalengo kila baada ya muda fulani.

Mwanzo wa kudhihiri kwake kilianza kama kikundi cha kisiasa chenye muelekeo wa kuleta mabadiliko ya kiutawala kwa kuwapinga baadhi ya watawala wanaowaitakidi kuwa ni madhalimu, harakati hizo zilianza chinichini katika baadhi ya miji aliyoizungukia **Myahudi Abdullahi Ibnu Sabai**, kama vile; **Kufa, Basra**, na harakati hizo zilishamiri zaidi nchini **Misri** na kupata nguvu kwa kupata wafuasi wengi. Hatimaye kikundi hiki kiovu kilifika **Madina** na kumuwa Khalifa wa tatu Uthman Ibnu Affaan radhia llaahu an'hu.

Baada ya kuuwawa Uthman na kutawalishwa Ali Ibn Abi Twalib radhia llaahu anhu, **Sabaiyya** walidhihiri kwa sura nyingine yenye muelekeo wa kiitikadi zenye **Ghuluwu (kuvuka mipaka)**, walifikia kumwita Ali kuwa ni Mungu! Na kuanzia hapo **Sabaiyya** walijulikana kwa jina la **Ghulaati** (watu wenye kuvuka mipaka kwa kuwapa wanadamu sifa za Allah Jalla Jalaaluh).

Walipofikia kiwango hicho cha kuitakidi kuwa Ali Ibn Abi Twalib kuwa yeye ndiye Mungu wa kweli!!! Ali radhia llaahu an'hu hakuuvumilia ukafiri wao huo, bali aliwakamata baadhi ya Maghulaat na kuwaadhibu kwa kuwatupa kwenye mashimo ya moto. Na hili linathibitishwa na mwanchuoni mkubwa wa Shia lthnaashariyya **Sultanu Waizin Muhammad Al-Musawiy As-Shiraz** katika kitabu chake **Mikesha ya Peshawar** ukurasa wa 28 aliposema;

"Mara kwa mara Ali aliwakataza kushikilia itikadi hii, lakini hakuna athari iliyotokea (hawakuacha). Hatimaye, kama ilivyoandikwa katika vitabu vingi vya Tarekh, Ali aliamrisha wauwawe ndani ya visima vya moshi. Maelezo ya habari hii yameandikwa katika Biharul-An'war, juz 7¹²⁴, na mwanachuoni mkubwa, Agha Muhammad Baqir Majlis."

Kwa hiyo, ifahamike kwamba tunapozungumzia Maghulaati wa Shia tunazungumzia wanafunzi na wafuasi wa Abdullahi Ibnu Sabai. Bila shaka, itakuwa ni kuchanganyikiwa kifikra na kuukwepa ukweli, mtu kukubali kuwepo kwa Maghulaati ambao ni wanafunzi na wafuasi, kisha ukamkana mwalimu wao na kiongozi wao mkuu **Myahudi Abdullahi Ibnu Sabai!**

Katika kitabu chetu **Uyahudi nyuma ya pazia la Ahlul-Baiti** tulitaja kwa ufupi kuwa Myahudi huyu ndiye muhusika mkuu katika uanzilishi wa pote la Shia na yeye ndiye chemchem ya Uzandiki wote uliomo kwenye vitabu vya Shia lth'naashariyya. Na kupitia wanafunzi wake waovu waliojipenyeza katika mikusanyiko na vikao vya Maimamu wa Shia waliweza kupachika hadithi nyingi za uongo na kupandikiza itikadi nyingi potofu, kama vile; Ghululu kwa Maimamu kwa kuwapa sifa za Allah, kwa kudai kuwa Maimamu wao wanajua Ghaibu, pia wamedai kuwa Maimamu wao ni Ma'sumuun (hawakosei wala hawasahau), na itikadi nyinginezo miongoni mwa itikadi chafu za Kikafiri.

Hawakutosheka na hayo, bali pia walielekeza upotoshaji wao dhidi ya kitabu kitukufu cha Allah, kwa kutunga riwaya zinazoelezea kwamba Qur-ani tuliyonayo imepotoshwa na Maswahaba, kwa kuziondosha Aya zote zilizokuja kumsifia Ali Ibn Abi Twalib na kizazi chake, pia wameweka riwaya zenye kuzitafsiri Aya kinyume na makusudio yake.

¹²⁴ -Kwa mujibu wa chapa niliyonayo iliyochapishwa na Dar Ihyaai Al-Kutubi Al-Islamiyya, ya Qum- Iran, manane haya yamo katika juzuu ya 25 ukurasa wa 415.

Sambamba na hilo, pia walifanikiwa kuwapandikiza chuki wafuasi wao dhidi ya Maswahaba wa Mtume swalla llaahu alayhi waalihi wasallam, ambao ni watu bora katika umma huu, kwa madai ya kuwa Maswahaba wamewadhulumu Ahlul-Baiti haki yao ya Ukhalifa, na kupitia madai hayo ya uongo wamewakufurisha Maswahaba na kuwatukana dhahiri shahiri kwa tuhuma nyingi za kubuni.

Uzandiki wa aina hiyo umejaa kwenye vitabu vya Shia lth'naashariyya bila ya kificho, bali hata kwenye kauli zao na vikao vyao hayo yamedhihiri, na wala mtu hapati taabu akitaka kulithibitisha hilo.

Mifano iko mingi sana na huko mbele Insha-Allah tutakutajia mifano michache kati ya mingi yenye kuthibitisha hilo. Na Mashia wenyewe pia wanakiri kwamba sehemu kubwa ya madhehebu yao ni zao la Maghulaati na Wazandiki ambao ni wanafunzi wa Myahudi Ibnu Sabai (Sabaiyya). Jambo la kusikitisha si suala la kuwepo kwa kundi la Wazandiki na Maghulaati katika safu za Shia na kufanya harakati zao kwa wasaa, bali jambo la kusikitisha zaidi ni kushindwa kwa wanachuoni wa Shia lth'naashariyya kuizuia hujuma hii iliyoelekezwa na Maghulaati dhidi riwaya zao na vitabu vyao vyenye kutegemewa. Na hilo linatokana na kushindwa kwa Maulamaa wa Shia kuweka kanuni za uchunguzi wa habari zao na wapokezi wao wa riwaya mapema, jambo lililopelekea kupatikana fursa kwa Wazandiki na Maghulaati kuzichezea riwaya zao na vitabu vyao kwa muda mrefu, hadi kufikia riwaya hizo za Kizandiki kuota mizizi, na kupata soko kubwa, Mashia wakazipokea kwa heshima na taadhima, wakidhania kwamba hayo ni mafunzo yatokanayo na Maimamu wao watwahaarifu! Na wenyewe wakajifaharisha kwa hilo!!! Na Insha-Allah katika sura ifuatayo tutatoa ushahidi wenye kuthibitisha hilo.

MBEGU WALIYOIPANDA MAGHULAATI KWENYE USHIA

Kama tulivyotangulia kusema hapo awali kwamba Mashia wenyewe wanakiri kuwa sehemu kubwa ya madhehebu yao ni mbegu iliyopandwa na Maghulaati na Wazandiki, na ushahidi juu ya hilo ni mwingi mno na hizi zifuatazo ni miongoni mwa kauli za wanachuoni wa Shia zenye kuthibitisha hilo. Anatuelezea Mshia **Haashim Ma'ruuf Al-Hasaniy** katika kitabu chake '**Al-Maudhuaatu fil-Aathaari wal-Akhbaari**', ukurasa wa 148-149 kwa kusema:-

"وَكَانَ مِنْ أخطرِ الدُّخْلَاءِ عَلَى التَّشْيِيعِ جَمَاعَةٌ تَطَاهَرُوا بِالأَوْلِيَاءِ لِأَهْلِ البَيْتِ، وَانْدَسُّوا بَيْنَ الرُّوَاةِ وَأَصْحَابِ الأَيْمَةِ مُدَّةً طَوِيلَةً مِنَ الزَّمَنِ اسْتَطَاعُوا خِلَالَهَا أَنْ يَتَقَرَّبُوا مِنَ الإِمَامِينَ؛ البَاقِرِ وَالصَّادِقِ وَاطْمَأَنَّ إِلَيْهِمْ جَمِيعُ الرُّوَاةِ، فَوَضَعُوا مَجْمُوعَةً كَبِيرَةً مِنَ الأَحَادِيثِ وَدَسُّوْهَا بَيْنَ أَحَادِيثِ الأَيْمَةِ، وَفِي أُصُولِ كُتُبِ الحَدِيثِ، كَمَا تُشِيرُ إِلَى ذَلِكَ بَعْضُ الرُّوَايَاتِ."

"Na ikawa miongoni mwa hatari kubwa za watu waliojipenyeza kwenye Ushia, ni kundi la watu waliojidhihirisha kuwapenda Ahlul-Baiti, walijipenyeza kati ya wapokezi na wanafunzi wa Maimamu kwa muda mrefu. Na kwa kipindi hicho waliweza kujikurubisha na Maimamu wawili; Al-Baaqir na As-Saadiq, waliaminika na wapokezi wote, wakatunga sehemu kubwa ya hadithi na wakazipenyeza kwenye hadithi za Maimamu, na kwenye vitabu vya hadithi, kama zinavyoashiria hilo baadhi ya riwaya." Kisha akasema tena Mshia huyo katika kitabu chake hicho ukurasa wa 253;

"وَبَعْدَ التَّتَبُّعِ فِي الأَحَادِيثِ المُنْتَشِرَةِ فِي مَجَامِيعِ الحَدِيثِ كَالكَافِي وَالوَافِي وَغَيْرِهِمَا نَجِدُ أَنَّ الغُلَاةَ وَالْحَاقِدِينَ عَلَى الأَيْمَةِ الهُدَاةَ لَمْ يَتْرُكُوا بَاباً مِنَ الأبْوَابِ إِلاَّ وَدَخَلُوا مِنْهُ لِإِفْسَادِ أَحَادِيثِ الأَيْمَةِ وَالإِسَاءَةِ إِلَى سُمْعَتِهِمْ، وَبِالتَّالِي رَجَعُوا إِلَى القُرْآنِ الكَرِيمِ لِيَنْفُثُوا عَنْ طَرِيقِهِ سُمُومَهُمْ وَدَسَّاسَهُمْ لِأَنَّهُ الكَلَامُ الوَحِيدُ الَّذِي يَحْتَمِلُ مَا لَا يَحْتَمِلُهُ غَيْرُهُ، فَفَسَّرُوا مَنَاتِ الأَيَاتِ بِمَا يُرِيدُونَ وَأَلصَقُوا بِالأَيْمَةِ الهُدَاةَ زُوراً وَتَضَلِيلًا."

"Na baada ya kuzifuatilia hadithi zilizosambaa kwenye vitabu vya hadithi kama Al-Kaafiy, Al-Waafiy na vinginevyo, tunakuta kwamba Maghulaati na wenye chuki dhidi ya Maimamu waongofu, hawakuacha mlango wowote katika milango (ya dini) isipokuwa wameuingia ili kuziharibu hadithi za Maimamu na kuchafua utajo wao. Kisha wakairudia Qur-ani tukufu ili wapulizie sumu zao kupitia njia hiyo, kwa sababu ndiyo maneno pekee ambayo yanaweza kubeba kile ambacho hakiwezi

kubebwa na maneno mengine, wakatafsiri mamia ya Aya (za Qur-ani) vile watakavyo, **kisha wakazibambikiza kwa Maimamu waongofu kwa kuzua na kutaka kupoteza (watu).**" Mwisho wa kunukuu.

Naye **Mshia Al-Ghuraifiy** anasema;-

"إِنَّ كَثِيرًا مِنَ الْأَحَادِيثِ لَمْ تَصُدُّ عَنِ الْأَيْمَةِ، وَإِنَّمَا وَضَعَهَا رِجَالٌ كَذَّابُونَ وَنَسَبُوهَا إِلَيْهِمْ: إِذَا بِالِدِّسِّ فِي كُتُبِ أَصْحَابِهِمْ، أَوْ بِغَيْرِهِ. وَبِالطَّبَعِ لَا بُدَّ وَأَنْ يَكُونُوا قَدْ وَضَعُوا لَهَا أَوْ لِكَثَرِهَا إِسْنَادًا صَحِيحًا كَيْ تُقْبَلَ حَسَبًا فَرَضْتُهُ عَلَيْهِ الدِّسِّ وَالتَّدْلِيْسِ."

"Kwa hakika Hadithi nyingi (za Shia) hazikutoka kwa Maimamu, wameziweka watu waongo na wakazinasibisha kwa (Maimamu), ima kwa kuzipenyeza katika vitabu vya wanafunzi wao au kwa njia nyingine, na bila shaka watakuwa wamezitungia sanad sahihi (hadithi zote hizo) au nyingi zake ili zikubalike kwa namna ile ambayo imepelekea kazi hiyo ya kupenyeza na kughushi."¹²⁵

Naye **Mshia Muhammad Hussein Fadhlul-Ilaahi** anasema;-

"إِنَّ هُنَاكَ قَوْضَى أَحَاطَتْ بِالْأَحَادِيثِ الْوَارِدَةِ عَنِ الْأَيْمَةِ مِنْ وَضَاعِ الْحَدِيثِ الَّذِينَ كَانُوا لَا يَكْتُمُونَ بِتَقْلِيدِ الْأَحَادِيثِ الْمُؤْضُوعَةِ بِشَكْلِ مُبَاشِرٍ، بَلْ كَانُوا يَدُسُّونَهَا فِي كُتُبِ أَصْحَابِ الْأَيْمَةِ الْمُؤْتَوِقِينَ كَرُزْرَةَ وَمُحَمَّدِ بْنِ مُسْلِمٍ وَأَمْثَالِهِمْ لِيَدْخُلَ الْحَدِيثُ الْمَوْضُوعُ إِلَى الدَّهْنِيَّةِ الْإِسْلَامِيَّةِ الْعَامَّةِ مِنْ خِلَالِ هَؤُلَاءِ الثَّقَاتِ الَّذِينَ لَا يَدْخُلُ الرَّبُّ إِلَى مَا يَنْقُلُونَهُ عَنِ الْأَيْمَةِ انْطِلَاقًا مِنْ وَثَاقِهِمْ."

"Kwa hakika kuna fujo kubwa iliyozitunguka Hadithi zilizopokewa kutoka kwa Maimamu, kutokana na watunzi wa hadithi ambao walikuwa hawatosheki kunukuu hadithi za kutunga moja kwa moja, bali walikuwa wanazipachika katika vitabu vya wanafunzi wa Maimamu wanaotegemewa, kama vile Zuraarat, na Muhammad Bin Muslim na mfano wao, ili hadithi za kutunga ziingie ndani ya Uislamu (Ushia) wote, kupitia hawa wapokezi wenye kuaminika ambao haingii shaka kwa kile walichokinukuu kutoka kwa Maimamu kutokana na uaminifu wao."¹²⁶ Naye Mshia **Muhammad Baaqir Al-Majlisiy** katika kitabu chake '**Bihaarul-An'waari**' ameitaja kauli inayomtaja **Al-Mughira Ibn Said Al-Bajaliy**¹²⁷ kutoka kwenye kitabu '**Rijaali**

¹²⁵ Angalia kitabu 'Qawaaidu At-Tahdiithi, cha Al-Ghariifiy, ukurasa wa 135.

¹²⁶ Angalia Majallaatul-Fikri Al-Jadiid, makala ya Muhammad Husein Fadhlul-Ilaahi, ukurasa wa 8.

¹²⁷ - Mzandiki huyu ni mmoja kati ya wale Maghulaati 15, kati ya wanafunzi wa Ibn Sabai tutakaowataja huko mbele, Insha-Allah.

Al-Kashiy', kwa sanad kutoka kwa Yuunus kutoka kwa Hishaam Ibnul-Hakami kwamba amemsikia Abu Abdillahi (a.s.) anasema;

"كَانَ الْمُغِيرَةُ بْنُ سَعِيدٍ يَتَعَمَّدُ الْكَذِيبَ عَلَى أَبِي وَيَأْخُذُ كُتُبَ أَصْحَابِهِ، وَكَانَ أَصْحَابُهُ الْمُنْتَسِرُونَ بِأَصْحَابِ أَبِي، يَأْخُذُونَ كُتُبَ أَصْحَابِ أَبِي فَيَدْفَعُونَهَا إِلَى الْمُغِيرَةَ، فَيَدُسُّ فِيهَا الْكُفْرَ وَالرَّذَىةَ وَيُسْنِدُهَا إِلَى أَبِي ثُمَّ يَدْفَعُهَا إِلَى أَصْحَابِهِ فَيَأْمُرُهُمْ أَنْ يَبْتُوهَا بَيْنَ الشَّيْعَةِ، فَكُلُّ مَا كَانَ فِي كُتُبِ أَصْحَابِ أَبِي مِنَ الْعُلُوِّ فَذَلِكَ مِمَّا دَسَّهُ الْمُغِيرَةُ بْنُ سَعِيدٍ فِي كُتُبِهِمْ."

"Alikuwa **Al-Mughira Ibn Said** anakusudia kumzulia uongo baba yangu, anachukua vitabu vya wanafunzi wake, na wanafunzi wake (**Al-Mughira**) walikuwa wanajificha kwa wanafunzi wa baba yangu, wanachukua vitabu vya wanafunzi wa baba yangu, kisha wanampa **Al-Mughira**, na yeye anafanya kazi ya kupenyeza Ukafiri na Uzandiki, kisha anauegemeza (ukafiri huo) kwa baba yangu, kisha anawapatia wanafunzi wake na anawaamrisha waueneze kwa Mashia. Kwa hiyo, kila kilichomo kwenye vitabu vya wanafunzi wa baba yangu katika **Ghuluwu** (kuvuka mipaka) hilo ni katika yale aliyoyapenyeza Al-Mughira Ibn Said kwenye vitabu vyao.¹²⁸ !!!

Tafakuri juu ya maneno haya:-

Ndugu msomaji! Bila shaka huu ni uthibitisho mzuri sana kutoka kwenye vinywa vya Mashia wenyewe juu ya kutokea kwa uharibifu mkubwa kwenye madhehebu yao. Mshia **Haashim Ma'ruuf Al-Hasaniy** anatuthibitishia kwamba **Maghulaati** (wafuasi wa Myahudi Ibnu Sabai) wamefanya mchezo mchafu wa kutunga riwaya kwa kiwango cha kutisha, maana hawakuacha mlango wowote miongoni mwa milango ya dini yao isipokuwa wamepenyeza ndani yake hadithi za uongo, hasa kwenye vitabu vikubwa kama **Al-Kaafiy cha Al-Kulayniy na Al-Waafiy cha Al-Faidhu Al-Kaashaaniy**, kisha wakaziegemeza kwa Maimamu wa Ahli Baiti, kama vile **Muhammad Al-Baaqir na Ja'far As-Sadiqi**.

Swali la msingi:

Kutokana na taarifa hii ya Mshia Maarufu Al-Hasaniy, je Mashia wamefanikiwa kuusafisha uongo na uzandiki uliowekwa na Maghulaati wanafunzi wa Ibnu Sabai kwenye vitabu vyao?

Kama jibu ndio, ni kwa kutumia misingi gani? Na kama hapana, je Mashia wanafuata mafunzo ya Maimamu kumbi na mbili wa Ahlil-Baiti au wanafuata mafunzo ya Maghulaati? Majibu sahihi ya maswali haya yanapatikana kwenye sura ya sita ya kitabu hiki, tafadhali isome kwa umakini.

¹²⁸ - Tazama Bihaarul-An'waari juzuu ya 2 ukurasa wa 292.

Majibu:-

Baada kumuweka sawa Mshia Mwazoa kwa kuubatilisha uongo wake, turudi kwenye majibu ya maswali yetu ya msingi; Je, Mashia wamefanikiwa kuusafisha uongo na uzandiki uliowekwa na Maghulaati wanafunzi wa Ibnu Sabai kwenye vitabu vyao? Mashia hawakuweza na hawataweza kuuondoa uzandiki wa **Maghulaati/Sabaiyya** (wafuasi wa Myahudi Ibn Sabai) kwenye madhehebu yao. Na kwa ushahidi wa hilo katika sehemu hii tutakutajia mambo matatu tu.

Jambo la kwanza:- Ghuluwa (Kuvuka mipaka katika kuwatukuza Maimamu wao)

- i- **Miongoni mwa Ghuluwu zao kwa Maimamu wao ni itikadi yao ya kwamba Maimamu wao hawakuumbwa kutokana na manii bali wameumbwa kutokana na nuru!**

Shia Imaamiyya wanaitakidi kuwa Maimamu wao wameumbwa kutokana na nuru, na kutokana na nuru yao Allah akaumba viumbe vingine vilivyobakia. Anasema **Mshia Ahmad Mustafa Ya'quub** katika kitabu chake **Qabasun min Nuuri Aali Muhammad**, ukurasa wa 12:

"اعْلَمُ أَيَّدَكَ اللهُ أَنْ أَوَّلَ مَا خَلَقَ اللهُ نُورَ النَّبِيِّ ﷺ وَمِنْهُ فَتَقَى نُورَ عَلِيِّ عَلَيْهِ السَّلَامُ، وَمِنْ نُورِ عَلِيِّ عَلَيْهِ السَّلَامُ كَانَ بَقِيَّةُ الْخَلْقِ، وَاعْلَمُ أَنَّ الْخَلْقَ خُلِقُوا مِنْ أَجْلِ مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ صَلَوَاتُ اللهِ وَسَلَامُهُ عَلَيْهِمْ، فَهُمْ أَصْلُ الْوُجُودِ."

"Fahamu -Allah akupe nguvu- kitu cha mwanzo alichokiumba Allah ni nuru ya Mtume swalla llaahu alayhi waalihi wasallam na kutokana na nuru hiyo akaibandua nuru ya Ali alayhi salaam na kutokana na nuru ya Ali alayhi salaam akaumba viumbe vilivyobakia. Fahamu kwamba viumbe wameumbwa kwa ajili ya Muhammad na familia ya Muhammad a.s na wao ndio chimbuko la ulimwengu."

Kisha akaendelea kusema Mshia huyu katika kututhibitishia kuwa Maimamu wao hawakuumbwa kwa manii kama wanadamu wengine:-

"وَيَجِبُ أَنْ يَعْلَمَ الْقَارِئُ أَنَّ أَهْلَ الْبَيْتِ صَلَوَاتُ اللهِ وَسَلَامُهُ عَلَيْهِمُ الَّذِينَ أَذْهَبَ اللهُ عَنْهُمْ الرِّجْسَ وَطَهَّرَهُمْ تَطْهِيراً لَمْ يُخْلَقُوا مِنْ مَاءٍ مَهِينٍ كَالْبَشَرِ بَلْ هُمْ أَنْوَارٌ انْتَقَلَتْ مِنَ الْأَصْلَابِ الشَّامِخَةِ إِلَى الْأَرْحَامِ الْمُطَهَّرَةِ."

"Ni wajibu kwa msomaji kufahamu kuwa Ahlul-Baiti (a.s.) ambao Allah amewaondolea uchafu na kuwatwahaisha **hawakuumbwa kutokana na maji dhalili (manii) kama watu wengine!** Wao ni nuru iliyohama kutoka migongo mitukufu kwenda katika mafuko ya uzazi yaliyotwahaishwa."

ii- Itikadi ya kwamba Maimamu wao wanajua Ghaibu;-

Itikadi sahihi ya Kiislamu ni kuamini kwamba hakuna mtu yeyote anayejua mambo ya Ghaibu (yaliyojificha, kama vile; siku ya kufa, yatakayotokea kesho, siku ya kusimama Qiyama n.k.) isipokuwa Allah peke yake, na mtu yeyote atakayeamini kwamba yuko katika viumbe mwenye ujuzi wa Ghaibu basi huyo ni kafiri, kwa sababu itikadi hiyo inapingana na mafundisho sahihi ya uislamu. Lakini pamoja na maelezo haya, Shia wanaamini kuwa Maimamu wao wana ujuzi wa mambo ya Ghaibu. Anasema **Mshia Sultanul-Wai'dhin As-Shirazi** alipokuwa akimuelezea Ali Ibnu Abi Twalib radhia llaahu an'hu:-

"Ukweli huu umekubaliwa na wote, wafuasi wa Ali na maadui zake. Huyu Imam Mtukufu alikuwa ni Imamul-Muttaqin (Kiongozi wa wacha Mungu). Alikuwa na elimu kamili ya Qur'ani Tukufu. **Zaidi ya hayo, alikuwa na elimu ya Ghaib¹²⁹.**" Mwisho wa kunukuu.

Mshia Sultanul-Waadhina As-Shirazi anasema kwamba Ali alikuwa na ujuzi wa Qur'ani yote na zaidi ya ujuzi huo, pia alikuwa na elimu ya Ghaib.

Na amesema **Mshia Muhammad Ya'qub Al-Kulayni** akiwanasibishia Maimamu wao elimu ya kujua siku za vifo vyao:

بَابُ أَنَّ الْأَيْمَةَ (ع) يَعْلَمُونَ مَتَى يَمُوتُونَ وَأَنَّهُمْ لَا يَمُوتُونَ إِلَّا بِاخْتِيَارٍ مِنْهُمْ.

"Huu ni mlango (unaozungumzia) kwamba Maimamu (a.s.) wanajua watakufa lini na wao hawafi isipokuwa kwa hiyari zao¹³⁰"

Halikadhalika Mashia pia wanaitakidi kuwa Maimamu wao wana elimu ya kila jambo hadi yale yaliyomo vifuani mwa wafuasi wao!

Anasema **Muhammad Baaqir Al-Majlisiy:**

"بَابُ أَنَّهُ لَا يُحْجَبُ عَنْهُمْ شَيْءٌ مِنْ أَحْوَالِ شَيْعَتِهِمْ وَمَا تَحْتَاجُ إِلَيْهِ الْأُمَّةُ مِنْ جَمِيعِ الْعُلُومِ وَأَنَّهُمْ يَعْلَمُونَ مَا يُصِيبُهُمْ مِنَ الْبَلَايَا وَيَصِيرُونَ عَلَيْهَا، وَلَوْ دَعَا اللَّهُ فِي دَفْعِهَا لِأَجْبِيئُوا، وَأَنَّهُمْ يَعْلَمُونَ مَا فِي الضَّمَائِرِ وَعِلْمَ الْمُنَايَا وَالْبَلَايَا وَقِصْلَ الْخَطَابِ وَالْمَوَالِيدِ."

"Huu ni mlango (unaozungumzia) kwamba Maimamu hawazuliwi kujua kitu chochote katika hali za Shia wao, na yote wanayohitajia umma katika elimu zote, na waanayajua matatizo yanayowasibu na wanayavumilia, na lau kama watamuomba

¹²⁹ -Tazama kitabu Mikesha ya Peshawar, ukurasa wa 446, chini ya anuani isemayo: "Ali alikuwa na elimu ya ulimwengu wa Ghaib", kimetarjumiwa na Dr. M. S. Kanju, na kuchapishwa na Al-Itra Foundation, Dar es Salaam.

¹³⁰ -Tazama Usuulul-Kaafi, Kitabul-Hujja, juzuu ya I ukurasa wa 135, na Bihaarul-An'waari, juzuu ya 27 ukurasa wa 803.

Allah awaondoshee (mitihani hiyo) wangekubaliwa. **Wao wanajua yaliyomo kwenye nyoyo (za watu) na elimu ya mauti (watakufa lini), elimu ya matatizo, na kauli ya upambanuzi (katika hukumu) na elimu ya vizazi (wataziliwa lini).**¹³¹

iii- Itikadi yao ya kwamba Maimamu wao ni bora zaidi kuliko Mitume na Malaika

Miongoni mwa ghuluwu za Shia Ith'naasharia ni kuwatukuza Maimamu wao zaidi ya Mitume wa Allah na zaidi ya Malaika watukufu.

Amesema **Mshia Muhammad Husein Al-Hurru Al-Aamilyi;**

"باب أن النبي والأئمة الاثني عشر - عليهم السلام - أفضل من سائر المخلوقات من الأنبياء والأوصياء السابقين والملائكة وغيرهم"

"Huu ni mlango (unaoelezea kwamba) Mtume na Maimamu kumi na mbili (a.s.) ni bora kuliko viumbe vyote, kuliko Manabii, Mawasii waliotangulia na kuliko Malaika na wengineo"¹³² Na amesema **Khomein:**

«وإن من ضروريات مذهبنا أن لأئمتنا مقامًا لا يبلغه ملك مقرب، ولا نبي مرسل».

"Miongoni mwa mambo ya lazima katika madhehebu yetu ni kuamini kwamba Maimamu wetu wana daraja ambayo haifikii Malaika mwenye kukurubishwa (kwa Allah) wala Nabii aliyetumwa"¹³³

Itikadi hii potofu pia inaungwa mkono na mwanachuoni wao wa ki-Shia mzaliwa wa Shiraz (Iran) aitwaye **Sayyid Abdul-Fani Muhammad al-Musawi (Sultanul-Wa'idhin)**¹³⁴, aliposema: "**Cheo cha Uimamu ni cha juu zaidi kuliko cheo cha Utume wa kawaida**, lakini kiko chini kuliko cha Utume Maalumu. Mtume wa mwisho ndiye kiwango cha hali ya juu cha Utume maalum." Mwisho wa kunukuu.

¹³¹ - Tazama Bihaarul-An'waari, juzuu ya 26 ukurasa wa 583.

¹³² -Tazama Al-Fusuulul-Muhimma fiy Usuulil-Aimmah, ukurasa wa 151.

¹³³ -Tazama katika kitabu chake Al-Hukuumatul-Islaamiyyah ukurasa wa 52.

¹³⁴ Tazama katika kitabu chake "ليالي بشاور" "Mikesha ya Peshawar" kilicho tarjumiwa na Dr. M. S. Kanju na kupigwa chapa na Alitrah Foundation Dar es Salaam, katika ukurasa wa 80 wa toleo la kwanza Augasti 2008.

Maneno haya yako wazi kwamba Shia wanaitakidi kuwa Maimamu wao wana daraja za juu zaidi kuliko Mitume wote wa Allah Alayhimus Swalaatu was Salaam ukimtoa Mtume wa mwisho swalla llaahu alayhi wasallam! Jambo ambalo ni ukafiri wa wazi.

iv- Itikadi yao ya kwamba Maimamu wao hawakosei wala hawasahau Miongoni mwa **Ghuluwu zilizoingizwa katika medhehebu ya Shia ni itikadi ya kwamba Maimamu wao kumi na mbili hawakosei wala hawasahau**, tangu kuzaliwa kwao hadi kufa! Sifa ambayo hakuna kiumbe yeyote anayesifika nayo zaidi ya Allah peke yake, amesema mwanachuoni mkubwa wa Shia **Muhammad Ibn Nu'maani Al-Mufid**, aliyefariki mwaka 413 Hijiria:

"أقول إنّ الأئمة القائمين مقام الأنبياء عليهم السلام في تنفيذ الأحكام وإقامة الحدود وحفظ الشرائع وتأديب الأنام معصومون كعصمة الأنبياء ، وإنه لا يجوز منهم السهو في شيء في الدين ، ولا ينسون شيئاً من الأحكام ، وعلى هذا مذهب سائر الإمامية إلا من شدّ منهم وتعلق بروايات لها تأويلات على خلاف ظنّه الفاسد من هذا الباب..."

"Ninasema; hakika Maimamu waliosimama kwenye nafasi za Manabii (a.s.) katika kupitisha hukumu, na kusimamisha **Haddi** (visasi na adhabu za kisheria), na kulinda sheria na kuwafundisha watu adabu. **Wao wamekingwa kufanya makosa kama walivyokingwa Manabii, na haijuzu (haifai) kwao Kusahau kitu chochote katika dini, na hawasahau kitu chochote katika hukumu, na huu ndio mwenendo wa Shia Imaamiyyah wote**, ila wachache waliojitenga miongoni mwao wakashikilia riwaya ambazo zina maelezo yaliyo kinyume na dhana yake mbaya katika mlango huu..."¹³⁵

Ni wapi ilipochimbuka itikadi hii chafu?

Majibu ya swali hili, yanatolewa na mwanachuoni wao mkubwa wa Shia **Abu Ja'far As-Saduuq Muhammad Ibn Baabaweyhi Al-Qummi**, aliyefariki mwaka 381 Hijiria:-

"إنّ الغلاة والمفوّضة - لعنهم الله - ينكرون سهو النّبويّ -ﷺ- يقولون: لو جاز أن يسهو في الصّلاة لجاز أن يسهو في التّبليغ؛ لأنّ الصّلاة فريضة كما أنّ التّبليغ فريضة.. وكان شيخنا محمد بن الحسن بن أحمد بن الوليد يقول: أوّل درجة في الغلو نفي السّهو عن

¹³⁵ - Tazama Awaailul-Maqalaat ukurasa wa 35.

النَّبِيِّ ﷺ - وأنا أحتسب الأجر في تصنيف كتاب مفرد في إثبات سهو النَّبِيِّ والرَّد على مُنكره."

"Hakika Maghulaat na Mufawwidhah –Allah awalaani- wao wanapinga kusahau kwa Mtume swalla Ilaahu alayhi wasallam (wanasema kwamba Mtume swalla Ilaahu alayhi wasallam hasahau). Na wanasema; lau kama ingefaa kusahau ndani ya swala basi pia ingefaa kusahau katika ufikishaji, kwa sababu swala ni faradhi kama ilivyokuwa kufikisha ni faradhi... Na alikuwa Sheikh wetu Muhammad Ibn Hasan Ibn Ahmad Ibn Al-Walid akisema: **Daraja ya mwanzo ya Ghuluwu (kuvuka mipaka) ni kukataa kusahau kwa Mtume swalla Ilaahu alayhi wasallam, na mimi ninatarajia kupata ujira (kutoka kwa Allah) kwa kutunga kitabu maalumu cha kuthibitisha kusahau kwa Mtume na kuwajibu wenye kulipinga hilo.**¹³⁶"

Angalia ndugu msomaji! Maghulaati na Mufawwidha ndio wanaosema kuwa Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam na Maimamu hawasahau, kisha kwa Shia hio ndio inakuwa itikadi ya lazima kwao!!! Amesema Sheikh wao Al-Maamaqani:

".....أن نفي السهو عن الأئمة أصبح من ضرورات المذهب الشيعي"

".....Kupinga (kwamba) Maimamu hawasahau ni jambo ambalo sasa limekuwa ndiyo itikadi ya lazima katika Madhehebu ya Shia.¹³⁷" Naye Muhammad Baaqir Al-Majlisiy katika hili hakurudi nyuma, anasema:

"إن أصحابنا الإمامية أجمعوا على عصمة الأئمة - صلوات الله عليهم - من الذنوب الصغيرة والكبيرة عمدًا وخطأً ونسيانًا من وقت ولادتهم إلى أن يلقوا الله عزَّ وجلَّ"

"Hakika wenzetu katika Shia Imaamiyyah wameafikiana juu ya kuwa Maimamu (a.s.) wamekingwa na makosa madogo na makubwa, kukosea kwa kukusudia, na kukosea kwa (bahati mbaya) **na (wamekingwa na) kusahau tangu kuzaliwa kwao hadi watakapokutana na Allah Azza wa Jalla.**" Tazama Bihaarul-An'waari juzuu ya 25 ukurasa wa 350-351.

Ubatili wa itikadi hizi;

Mwisho tunaufunga mjadala huu kwa kukutajia ushahidi kutoka kwenye Qur-ani unaobatilisha itikadi hii potofu ya **Maghulaati** iliyopenyezwa kwenye Ushia, na ushahidi wa hilo ni kauli yake Allah aliposema kuhusu Nabii Adam *alayhi salaam*.

(وَلَقَدْ عَهِدْنَا إِلَىٰ آدَمَ مِنْ قَبْلُ فَنَبِيٍّ وَلَمْ نَجِدْ لَهُ عَزْمًا) سورة طه ١١٥

¹³⁶ - Tazama kitabu Man'laa yahdhuruhul-Faqihi juzuu ya 1 ukurasa wa 234.

¹³⁷ - Tazama kitabu Tan'qihul-Maqaali, juzuu ya 3 ukurasa wa 240.

“Hakika tulimuahidi Adam hapo kabla, kisha **akasihau** na hatukuona kwake azma yoyote” Surat Twaha Aya ya 115.

Na amesema Allah kuhusu Nabii Musa alayhi salaam alipomwambia Al-Khidh’ri:

((قَالَ لَا تُؤَاخِذْنِي بِمَا نَسِيتُ وَلَا تُرْهِقْنِي مِنْ أَمْرِي عُسْرًا)) سورة الكهف (٧٣)

“(Musa) akasema usinichukulie **kwa niliyoyasahau**, wala usinipe uzito kwa jambo langu.” Suratul-Kahfi Aya ya 73.

Naye Mshia **Sayyid Murtadha** alipokuwa akiitafsiri Aya hii akasema:

”إِنَّ النَّبِيَّ إِنَّمَا لَا يَجُوزُ عَلَيْهِ النَّسِيَانُ فِيمَا يُؤَدِّيهِ عَنِ اللَّهِ تَعَالَى أَوْ فِي شَرَعِهِ أَوْ فِي أَمْرٍ يَقْتَضِي التَّنْفِيرَ عَنْهُ ، فَأَمَّا فِيمَا هُوَ خَارِجٌ عَمَّا ذَكَرْنَاهُ ، فَلَا مَانِعَ مِنَ النَّسِيَانِ.”

“Hakika Mtume haijuzu kwake kusahau kwa yale anayoyafikisha kutoka kwa Allah, au katika Sheria yake, au jambo ambalo litapelekea kuchukiwa, ama yaliyo nje ya hayo tuliyoyataja hakuna kizuizi (kwake) kusahau.¹³⁸”

Ndugu msomaji! Hii tuliyoitaja ni baadhi ya mifano iliyomo kwenye Qur’ani inayotudhihirishia kwamba hata Manabii wanasahau.

Ama katika Sunna, kuna hadithi nyingi mno za Mtume swalla Ilaahu alayhi wasallam zenye kuthibitisha hilo.

Imamu Bukhari ameelezea kisa katika sahihi yake kutoka kwa Abdillahi Ibn Masoud kwamba siku moja Bwana Mtume swalla Ilaau alayhi wasallam aliwaswalisha watu swala ya rakaa nne kisha akasihau akatoa salamu katika rakaa ya pili, Mtume swalla Ilaahu alayhi wasallam alipokumbushwa kuhusu hilo akasujudu sijda mbili za kusahau kisha akasema:

«إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِثْلُكُمْ ، أَنْسَى كَمَا تَنْسُونَ ، فَإِذَا نَسِيتُ فَذَكِّرُونِي.»

“Mimi ni mtu mfano wenu, **ninasahau kama mnavyosahau**, basi nikisahau nikumbusheni.¹³⁹”

¹³⁸ - Tazama kitabu ‘Tanzihul-An’biyaa, ukurasa wa 87.

¹³⁹ - Tazama Sahihi Bukhari, hadithi namba 401. Na Sahihi Muslimu, hadithi namba 1311 na 1312.

Ndugu msomaji! Nataka ufahamu kwamba hadithi hii haikupokewa na Ahlu Sunna peke yao kama wanavyodai baadhi ya wajinga wa Kishia¹⁴⁰, na kwa sababu ya ujinga wao wakawatukana baadhi ya Maswahaba walioipokea hadithi hii, bali hadithi kama hii imetajwa ndani ya vitabu vikubwa vya kutegemewa katika madhehebu ya Shia lth'naashariyya kama tulivyozielezea hapo nyuma. Je, baada ya ushahidi wote huu kunahitajika ushahidi mwingine mkubwa zaidi yake?

Jambo la pili; Shahada ya tatu katika adhana;

Kuendelea kuwepo Shahada ya tatu katika Adhana za Mashia, ni moja kati ya mifano hai na uthibitisho wa wazi juu ya athari zilizoachwa na Maghulaati ndani ya madhehebu ya Shia lth'naashariyya, pia huo ni ushahidi wa kutosha juu ya kufeli kwa harakati za Usuliyyiina za kutaka kuisafisha madhehebu yao na uchafu wa Maghulaati na Wazandiki kama tutakavyoelezea hapo mbele.

Shahada katika Uislamu ni mbili tu, na Shahada ndiyo ufunguo wa Uislamu, kama hakuna Shahada mbili hakuna Uislamu. Kwa hiyo, kama Maghulaati na Wazandiki wamefanikiwa kupenyeza **Shahada ya tatu** ndani ya Ushia, basi hakuna kilichosalimika ndani ya madhehebu hiyo inayojinasibisha na Ahlul-Baiti. Tena jambo baya zaidi ni kuwa Shahada hiyo ya tatu wameiongeza kwenye moja kati ya nembo kuu za Uislamu, nembo ya dhahiri, isiyo na usiri ambayo ni Adhana, ushupavu ulioje huu!

¹⁴⁰-Miongoni mwao ni Mshia Muhammad Tijani As-Samawi, aliposema katika kitabu chake 'Waulizeni wanaofahamu' uk wa 359-360: "**Haiwezekani kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kusahau ndani ya sala yake akakosa kufahamu ni rakaa ngapi amesali.....Riwaya kama hizi ni za uongo dhidi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) zinawafanya maamiri na masultani wa Kibanu Umayyah na bani Abbas na wengineo waipuuze sala na wapuuz kutawadha na wapuuz kila kitu kiasi kwamba mfano huo umeenea kwetu sisi.**" Mwisho wa kunukuu. Haya ni maneno ya kijinga yaliyojaa chuki na uadui.

Pia tazama kitabu Abu Hureirah cha Mshia Sharafud-Din Al-Musawiy, ukurasa wa 86, utaona namna anvyomtukana Swahaba Mtukufu Abu Hureirah kwa sababu ya kuipokea hadithi hii! Ambayo imo kwenye vitabu vya Shia, na wala humo haikupokewa na Abu Hureirah!

Baadhi ya wanachuoni wakubwa wa Shia lth'naashiriyya wametubainishia mahali na asili ya jambo hili, na ni kina nani walioanzisha, lakini pamoja na hayo Mashia hawawezi kuiacha kutokana na kustawi kwa athari za Maghulaati ndani madhehebu yao, mpaka baadhi yao wakadhani nembo ya Ushia ni kuleta **Shahada tatu kwenye Adhana!** Anasema **Mshia Muhammad Mahdi Al-Khalisiy** akibainisha walioanzisha Shahada hiyo ya tatu:

"...أن علماء الشيعة الإمامية مجمعون من زمان أئمتهم المعصومين في أخبارهم المتواترة إلى هذا الزمان على تجريد الأذان من كلمة "أشهد أن علياً ولي الله" ولم يخالف فيه أحد... وإن الذين زادوا هذه الكلمة هم الغلاة والمفوضة لعنهم الله..."

"Maulamaa wa Shia Imaamiyyah wote wamefikiana tangu zama za Maimamu wao Ma'sumin kupitia habari zao Mutawatiri hadi zama za leo juu ya kutokuwepo katika Adhana neno; "أشهد أن علياً ولي الله" **"Ash'hadu anna Aliyyan waliyyu Ilaahi"** na hakuna yeyote aliyekwenda kinyume na msimamo huo... Na hakika waliozidisha neno hili (Ash'hadu anna Aliyyan waliyyu Ilaahi) ni **Ghulaati na Mufawidha, Allah awalaani...**¹⁴¹

Naye **Mshia Dr. Husein Al-Madrasiy At-Twabawabai** anasema:

"تغلغلت بعض أفكار وبدع المفوضة واتخذت لها مكانا في نظام المذهب الشيعي ، وكمثال على ذلك : إضافة الشهادة الثالثة إلى الأذان ، وهي التي يصرح الشيخ الصدوق بأنها من بدعهم وشعاراتهم ، والتي أصبحت شعاراً وتقليداً للشيعة بالرغم من اعتراض أو عدم موافقة الكثير من فقهاء الشيعة."

"Zimezama baadhi ya fikra na bid'a za **Mufawwidha**¹⁴² na zikapata nafasi katika mfumo wa madhehebu ya Kishia, kwa mfano; kuongeza Shahada ya tatu kwenye Adhana, jambo ambalo Sheikh As-Saduuq ameelezea wazi wazi kwamba jambo hilo ni uzushi na ni alama za Mufawwidhah, lakini leo imekuwa ndiyo nembo ya Shia

¹⁴¹ - Tazama kitabu "Al-l'tisaam bi hablillaahi" ukurasa wa 17.

¹⁴² -Mufawwidhah ni sehemu kati ya makundi ya Maghulaati!!!

pamoja na kuwepo kwa pingamizi au kutokubaliwa na wengi miongoni mwa wanachuoni wa Kishia¹⁴³.”

Mwanachuoni mwingine wa Shia lth'naashariyya aitwaye Jaafar Aali Kashiful-Ghita anapigilia msumari mwingine kwa kusema:

”وَلَيْسَ مِنَ الْأَذَانِ قَوْلُ أَشْهَدُ أَنَّ عَلِيًّا وَلِيُّ اللَّهِ أَوْ أَنَّ مُحَمَّدًا وَآلَهُ خَيْرُ الْبَرِيَّةِ مَرَّتَيْنِ مَرَّتَيْنِ وَأَنَّ عَلِيًّا أَمِيرَ الْمُؤْمِنِينَ حَقًّا لِأَنَّهُ مِنْ وَضْعِ الْمُفَوَّضَةِ لِعَنَمِ اللَّهِ...وَلِأَنَّهُ لَوْ كَانَ مِنْ فُصُولِ الْأَذَانِ لَنُقِلَ بِالتَّوَاتُرِ فِي هَذَا الزَّمَانِ وَلَمْ يَخَفْ عَلَى أَحَدٍ مِنْ آحَادِ نَوْعِ الْإِنْسَانِ وَإِنَّمَا هُوَ مِنْ وَضْعِ الْمُفَوَّضَةِ الْكُفَّارِ الْمُسْتَوْجِبِينَ الْخُلُودَ فِي النَّارِ.”

“Si katika adhana Kusema; **“Ash’hadu anna Aliyyan waliyyu llaahu”** au (kusema); **Anna Muhammadan wa Aalahu khairul-bariyya** mara mbili, au (kusema); **Anna Aliyyan Amirul-muuminina haqqan**, kwa sababu hilo ni katika mambo waliyoyaweka Mufawwidhah, Allah awalaani... Na lau kama ingekuwa ni sehemu ya adhana ingenukuliwa kwa wingi katika zama hizi na wala jambo hilo lisingejificha kwa yeyote kati ya wanadamu, jambo hilo ni katika mambo waliyoyaweka **Mufawwidhah ambao ni makafiri wanaostahiki kukaa motoni milele.**¹⁴⁴”

Hoja yetu:-

Ndugu msomaji! Bila shaka umefahamu mahali ilipotoka Shahada hii ya uzushi (**Shahaadatuz-Zuuri**)! Tulipotaja kwenye kitabu chetu Uyahudi nyuma ya pazia la Ahlul-Baiti riwaya zinazoelezea kwamba Shia wanasema; Qur-ani tuliyonayo imepotoshwa kwa kupunguzwa. Mshia Jaafar Mwazoa na Mashia wenzake walilipinga hilo kwa nguvu kubwa na kwa kupitia elimu ya uchambuzi wa riwaya wakajitetea kwa kudai kuwa riwaya hizo ni uzushi uliotungwa na Maghulaati, na Maghulaati kwao ni makafiri! Lakini hapa tumeona kwamba Shahada ya tatu inayorindima kwenye Adhana za Shia lth'naashariyya ni uzushi uliowekwa na hao Maghulaati, na wala haikufundishwa na yeyote kati ya hao Maimamu wao kumi na

¹⁴³ -Tazama kitabu Tatwawurul-Mabaani Al-Fikriyyah cha Husein Al-Madrasiy At-Twababwaiy ukurasa wa 73.

¹⁴⁴ - Tazama Kash’ful-Ghita ukurasa wa 27 na Al-l’tiswamu bi hablillaahi ukurasa wa 50-52.

mbili wanaojinasibu nao. Na kwa sababu hiyo ndiyo tukawaambia kwamba Ushia huu mlionao ni; **UYAHUDI NYUMA YA PAZIA LA AHLUL-BAITI!!!**

Ndugu msomaji! Mshia Jaafar Mwazoa alitwambia katika kitabu chake Shimo Refu, ukurasa wa 115 na halikadhalika katika ukurasa wa 151, kwamba Maghulaati ni makafiri, na kwa sababu hiyo habari zao hazifai kuchukuliwa!

Na katika sehemu hii tumeona kwamba walioongeza Shahada ya tatu kwenye Adhana za Shia ni hao Maghulaati na wao Mashia wameikubali Shahada hiyo kwa kuitumia katika Adhana zao.

Swali; Je, mtu akisema kwamba Ushia ni mbegu chafu iliyopandwa na Maghulaati, atastahiki lawama?

Na je, tutaamini vipi kwamba hizo itikadi zenu nyingine zilizojaa Ghuluwu na Mazingaombwe hazikuwekwa na hao Maghulaati?

Na je, kwa kuitumia Shahada hii feki iliyotungwa na Maghulaati hao, mtakuwa mmeipanda Safina ya Ahlul-Baiti au Safina ya Maghulaati? Na kama si hivyo, ziko wapi hizo juhudi zenu dhidi ya uzushi huu wa Maghulaati? Au mnataka kuitumia elimu ya uchambuzi wa riwaya ili kuficha uchafu wa madhehebu yenu?

Jambo la tatu; Kudhihiri Mah'di

Ndugu msomaji! Kabla ya kukuletea visa vya kubuni vilivyowekwa na Maghulaati kuhusu Mahdi wa Shia Ithnaashariyya ni vizuri kwanza tukakufahamisha tofauti kiitikadi iliyopo kati ya Shia na Ahli Sunna wal-Jamaa kuhusu Mahdi.

1- Itikadi ya Ahli Sunna kuhusu Mahdi;-

Kwa mujibu wa itikadi yetu sisi Ahlu Sunnat wal-Jamaa, kupitia hadithi sahihi za Bwana Mtume swalla llaahu alayhi waalihi wasallam tunaamini juu ya kudhihiri kiongozi wa Kiislamu aitwaye Mahdi, kiongozi huyo atadhihiri katika zama za mwisho na ataijaza dunia haki na uadilifu baada ya kuwa dunia imejaa dhulma na uonevu.

Na kwa itikadi yetu sisi Ahlu Sunna wal-Jamaa ni kuwa kiongozi huyu bado hajazaliwa, na atatokana na kizazi cha mjukuu wa Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam, **Hasan Ibn Ali Ibn Abi Twalib** Radhia Ilaahu an'huma. Na jina la kiongozi huyo limefanana na jina la Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam, na jina la baba yake limefanana na jina la baba yake Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam, anaitwa **Muhammad Ibn Abdillahi (Al-Mahdi)**. Na Hadithi za Ahlu Sunna zilizokuja katika kuithibitisha itikadi hii ni Mutawaatiri na hazina shaka ndani yake.¹⁴⁵

ii- Itikadi ya Shia Ithnaashariyya kuhusu Mahdi;-

Ama kwa upande wa Shia Ithnaashariyya, wao wanaamini na kuitakidi kuwa Mahdi wao ameshazaliwa, na yuko mafichoni, naye anatokana na kizazi cha Mjukuu wa Mtume swalla Ilaahu alayhi wasallam **Husein Ibn Ali Ibn Abi Twalib** Radhia Ilaahu an'huma, na jina lake ni **Muhammad Ibn Hasan Al-Askariy**. Na huyo ndiye Imamu wao wa kumi na mbili. Atadhihiri Mahdi wao na moja kati ya malengo yake ni kuwalipizia kisasi wale wote waliodhulumu Ukhalifa wa Ali na kizazi chake kwa mujibu wa madai ya Shia.

Tofauti ya itikadi hizi;-

Bila shaka kwa maelezo haya mafupi utakuwa umefahamu kwamba kuna tofauti kubwa baina ya Mahdi wa Ahli Sunna na Mahdi wa Shia kwenye nukta zifuatazo;-

1- Kuhusu jina lake;

-Mahdi wa Ahli Sunna wal-Jamaa anaitwa **Muhammad Bin Abdillahi**

-Mahdi wa Shia anaitwa **Muhammad Bin Hasan Al-Askariy**

2- Nasabu yake;

-Mahdi wa Ahli Sunna wal-Jamaa anatokana na kizazi **cha Hassan Bin Abi Twalib** radhia Ilaahu an'huma

¹⁴⁵-Tazama kitabu Musnad cha Imam Ahmad, juzuu ya 6, ukurasa wa 44-45, hadithi nambari 3573, kilichochapishwa na Muassasatu Ar-Risaalah, Beirut-Lebanon, Sunan ya Imamu Abi Daud As-Sijistaaniy, hadithi nambari 4282, Al-Jaamiu/Sunan Tirmidhiy cha Imamu Abu Issa At-Tirmidhiy hadithi nambari 2230, na Twabaraani katika Mu'jamul-Kabiir, hadithi nambari 10223.

-Mahdi wa Shia anatokana na kizazi cha **Hussein Bin Ali Bin Abi Twalib** radhia llaahu an'huma

3- Kuzaliwa kwake;

-Mahdi wa Ahli Sunna wal-Jamaa **bado hajazaliwa**

-Mahdi wa Shia **ameshazaliwa** na yuko mafichoni

4- Malengo ya kudhihiri kwake;

-Mahdi wa Ahli Sunna **atakuja kwa lengo la kuleta haki na uadilifu duniani**

-Mahdi wa Shia **atakuja kwa lengo la** kuwalipizia kisasi waliompora Ali na kizazi chake Ukhalifa wao.

VISA VYA KUBUNI KUHUSU MAHDI

Kama tulivyoelezea hapo awali kwamba Maghulaati (wafuasi wa Myahudi Ibnu Sabai) kuwa wamefanikiwa kwa kiasi kikubwa sana kuasisi uzandiki kwenye madhehebu ya Shia lthnaashariyya, na miongoni mwa mbinu walizozitumia ni kutunga visa vingi vya uongo, na miongoni mwa mambo yaliyotungiwa visa hivyo vya uongo tena vya kubuni ni suala hili la kuwepo kwa Mahdi, na hivi vifuatavyo ni baadhi ya visa hivyo vilivyotungwa na Maghulaati hao;-

KISA CHA KWANZA

Kuposwa kwa mama yake Mahdi;-

Anasema Mshia **Mulla Muhammadjaffer Sherif Dewji**, kwenye kitabu chake alichokiita IMAM ZAMAN HADHRAT MAHDI¹⁴⁶ (A.S.), katika ukurasa wa 40-41; "Usiku huo huo nilimwona Nabii Issa katika ndoto. Yeye alikuwa pamoja na masahaba wake waliokuwa wamehudhuria sherehe ya ndoa yangu. Kiti cha enzi kiliwekwa pahali palipowekwa kiti cha mwana wa mfalme (aliyetaka kunioa) na kilikaliwa na mtu mkubwa mwenye uso uliojaa nuru. Baada ya muda mfupi tu niliwaona watu wenye nyuso za nuru na hapo Nabii Issa alisimama kuwakaribisha na kuwapa nafasi karibu yake. Nilimwuliza mtu mmoja anijulishe hao waliokuja walikuwa nani?"

¹⁴⁶-Kimetolewa na kuchapishwa na **Bilal Muslim Mission of Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania**, toleo la kwanza 1991, kimetarjumiwa na **Alhaj Zakirhussein M. S. Lakha**.

Nikaarifiwa kwamba hao ni Mtume wa Islam pamoja na mrithi wake na Maimamu kumi na moja wanaotokana na dhuria yake.

Mtume Mtukufu hapo akamwomba Nabii Issa kumchumbia Malika binti wa Shmunusaafa mjukuu wake Imam Hassan Askari ambaye uso wake uking'aa kwa nuru (ombi hilo lilifanywa kwa Nabii Issa kwa sababu Malika alitokana na kizazi cha Hadhrat Shamoona mrithi wa Nabii Issa). Nabii Issa akamwomba Hadhrat Shamoona atoe kibali chake na papo hapo Hadhrat Shamoona akakubali kwa kuona hiyo heshima kuu. Kwa hiyo ndoa yangu ikafungwa na Imam Hassan Askari (A.S.).

KISA CHA PILI

Kusilimu kwa mama yake Mahdi (Narijiskhatun):-

Amesema **Mulla Muhammadjaffer Sherif Dewji**, katika ukurasa wa 41; "Safari moja nilimwona binti wa Mtume (S.A.W.W.) mwana-Fatima (A.S.) na katika ndoto mimi nilisimama kwa taadhima na nikamweleza hali yangu na kutomwona Imam Hassan Askari (A.S.). aliniamrisha nisome "SHAHADA" nikawa Mwislamu na baadaye kila usiku nilimwona Imam Hassan Askari katika ndoto akinituliza."

Mambo hayo! Mama wa Mahdi wa Shia amesilimu kwenye ndoto, na uislamu wake ni sahihi!!!

KISA CHA TATU

Mahdi aswalisha Swala ya Jeneza akiwa na miaka mitano!:-

Miongoni mwa vituko vya Shia lth'naasharia wanavyowasingizia Maimamu wao, wanadai kwamba Mah'di wao wa kubuni aliwaswalisha watu swala ya jeneza alipofariki baba yake Hasan Al-Askariy mwaka 260 Hijiria akiwa ni mtoto wa miaka mitano! Amesema Mshia **Maulana Sayyid Ali Naqi Saheb**: "Imamu Hasan Askari (a.s.) alipofariki na ulipowadia wakati wa kumswalia sala ya maiti, Mwenyezi Mungu akaliondoa pazia la Ughaibu kwa muda mfupi.

Watu wote wanaohusiana na jamii ya wafuasi wa ukoo wa Mtume (s.a.w.) walikuwa wamesimama katika safu kwa ajili ya sala ya maiti na Bwana Jaafar, nduguye Imamu Hasan Askari (a.s.) alikuwa kisha simama mbele kuiongoza sala hiyo, alipotokea kwa ghafla kijana mdogo tokea nyuma ya pazia la chumba cha wanawake, na akaenda pale aliposimama Jaafar kupitia katikati ya safu. Akalivuta

joho la Bwana Jaafar na kumwambia, "Rejea nyuma, Ami: Mimi nina haki zaidi ya kuongoza swala ya maiti ya baba yangu". Bwana Jaafar alirudi nyuma, na Imamu Kijana akaiongoza sala. Baada ya sala Imamu akatoweka tena nyuma ya lile pazia¹⁴⁷."

Faida:

- ➔ Jaafar Bin Ali na Hasan Bin Ali (Al-Askariy) ni ndugu, lakini walikosana katika uhai wao mpaka wakawa hawasemani, kwa sababu Jaafar na yeye alidai kuwa ni Imamu.
- ➔ Jaafar na wafuasi wake, walikuwa na uhakika kwamba kaka yake Hassan Al-Askariy alikuwa mgumba, hana mtoto.
- ➔ Inasemekana kwamba Hasan Al-Askari alimficha mwanaye huyo aliyeswalisha ili asidhuriwe na maadui, na miongoni mwa maadui wa mtoto huyo ni Ami yake Jaafar (ndugu yake Hassan Al-Askariy).
- ➔ Shia wanadai kwamba Khalifa wa Bani Abbas wa wakati huo pia naye alikuwa akimwinda mtoto huyo.
- ➔ Baada ya kifo cha Hasan Al-Askariy (Imamu wao wa kumi na moja) Shia waligawanyika katika makundi kumi na mbili, na sababu kuu ya kugawanyika kwao ni ile fikra ya kuwa Uimamu unaendelea na Hasan hakuacha mtoto!

¹⁴⁷-Tazama kitabu cha Kishia kiitwacho "ANAYENGOJEWA" cha **Ali Naqi Saheb**, ukurasa wa 8, kimetafsiriwa kwa Kiswahili na **Sayyid Muhammad R. M. Mahdi El-Moosawy**, Kimetolewa na Kuchapishwa na **Bilal Muslim Mission of Tanzania, Dar es Salaam**. Na kitabu **IMAM ZAMAN HADH'RAT MAHDI (A.S.)** cha **Mulla Muhammadjaffer Sherif Dewji** katika ukurasa wa 47-48.

MGAWANYIKO WA SHIA BAADA YA KUFARIKI IMAMU WAO WA KUMI NA MOJA

Miongoni mwa mambo yenye kuthibitisha kwamba uzandiki umeathiri katika madhehebu ya Shia lthnaashariyya kupitia **Maghulaati** na wamefanikiwa kutunga chungu ya hadithi walizozinasibisha na Maimamu wao, ni mizozo iliyojitokeza baina ya Shia wenyewe kwa wenyewe, mara tu baada ya kufariki Imamu wao wa kumi na moja **Hasan Al-Askariy**. Mashia waligawanyika kwenye makundi kumi na mbili yenye kukufurishana:¹⁴⁸

Kundi la kwanza lilidai kwamba, Hasan Ibn Ali (Al-Askariy Imamu wa kumi na moja) yuko hai, hajakufa, amejificha tu. Na yeye ndiye **Mah'di anayengojewa** na atajitokeza tena zama za mwisho.

Kundi la pili lilidai kwamba Hasan Ibn Ali (Al-Askariy) amekufa, lakini aliishi kwa kujificha baada ya kifo chake, na yeye ndiye **Mah'di**. Wamesema; Hasan Ibn Ali amekufa na hatuna shaka juu kifo chake, na wala hakuacha mtoto na hakuna Wasii mwengine, kwa hiyo Hasan atadhihiri tena na ataijaza ardhi uadilifu kama ilivyojazwa dhulma.

Kundi la tatu limesema; **Hasan Ibn Ali** (Al-Askariy) amekufa na hakuacha mtoto, na Imamu baada yake ni ndugu yake **Ja'far Ibn Ali**, huyo ndiye aliyekusiwa na Hassan kuwa Imamu baada yake.

Walipoambiwa kwamba nyinyi mnajua kuwa Hasan na Ja'far walikuwa ni maadui wanaogombana na walikuwa hawasemeshani maisha yao yote! Wakajibu kwa kusema; kwa dhahiri walionekana kuwa wanagombana, lakini ukweli ni kwamba ndani ya nafsi zao walikuwa wakipendana.

Kundi hili lilikuwa likiongozwa na mtu mmoja kutoka sehemu za Kufah Iraq, alikuwa akiitwa **At-Twahi Al-Khazaar**.

Kundi la nne limesema; Imamu baada ya **Hasan Ibn Ali** ni **Ja'far Ibn Ali**. Na Uimamu aliupata kutoka kwa baba yake **Ali Ibn Muhammad (Al-Haadi)** na hakuupata kutoka kwa ndugu yake Hassan Bin Ali wala Muhammad Bin Ali.

Kwa sababu Muhammad alifariki katika Uhai wa baba yake na Hasan amefariki akiwa hana mtoto, na Hassan aliudai Uimamu kwa batili, kwa sababu Imamu hawezi kufa isipokuwa ausie na awe na mtoto wa kumrithi. Na Hasan amefariki bila wasia wala mtoto, hivyo hakustahiki kudai kwamba yeye ni Imamu!

Kundi la tano; kundi hili lilirudi likadai Uimamu wa **Muhammad Ibn Ali Ibn Muhammad**, ndugu yake Hasan Ibn Ali ambaye alifariki katika kipindi cha uhai wa

¹⁴⁸ -Rejea maelezo haya kwenye kitabu **Al-Maqalaatu wal-Firaqu** cha **Sa'd Al-Qummiy** kuanzia ukurasa wa 106.

baba yake (Imamu wao wa tisa, Ali Ibn Muhammad Al-Haadi) wakadai kwamba Hasan na Ja'far walidai Uimamu na kujitwika jambo ambalo si haki yao, kwa sababu baba yao hakuwausia wawe Maimamu.

Kwa sababu pia Hasan alikufa na hakuacha mtoto na haiwezekani Imamu asiwe na mtoto wa kumrithi. Ama Ja'far yeye alikuwa mtu mwovu, mwenye ufuska mwingi, alikuwa akifanya maasia dhahiri shahiri na mtu kama huyu hastahiki kutoa ushahidi japo wa dirhamu moja vipi ataweza kuwa Imamu!?

Kwa hiyo Imamu ni **Muhammad Ibn Ali Ibn Muhammad**, na yeye ndiye **Mah'di anayengojewa**.

Kundi la sita, limedai kwamba, Hassan Ibn Ali alikuwa na mtoto aliyeitwa Muhammad, na alimuusia. Na si kama wanavyodai watu kwamba alikufa hali yakuwa hana mtoto. Itakuwaje! Huyu ni Imamu ambaye umethibiti Uimamu wake kisha asiwe na mtoto. Ukweli ni kwamba aliacha mtoto kabla ya kifo chake kwa miaka miwili.

Baba yake alipokuwa hai aliamrisha afichwe kwa sababu ya kuogopea maadui zake kama vile; Ami yake Ja'far na wengineo. Na mtoto huyo ndiye huyo **Mah'di anayengojewa**.

Kundi la saba, lilidai kwamba Hasan alipata mtoto, lakini alizaliwa baada ya kufariki kwake kwa miezi nane, kwa maana ya kwamba, alifariki wakati mke wake ana mimba ya mwezi mmoja takriban, na wale wanaodai kwamba alipata mtoto katika uhai wake, hao ni waongo, na lau kama angekuwa na mtoto asingemficha kwa sababu ya kuwaogopa watu kama walivyofanya waliomtangulia, wala haifai kubishana juu hilo.

Ukweli ni kwamba aliondoka duniani na hali ya kuwa hana mtoto, na mirathi yake ikazuiliwa mpaka alipozaliwa baada ya miezi nane, na mwenyewe aliusia kwamba akizaliwa aitwe Muhammad.

Na wafuasi wa kundi hili, wakatoa hoja kwa kauli ya Abul-Hasan Ali Ar-Ridha Ibn Musa Al-Kadhim, aliposema:

ستبتلون بالجنين في بطن أمه والرضيع ...

"Mtajaribiwa kwa mtoto aliyetumboni na anayenyonya"

Kundi la nane, likasema; Hasan Al-Askariy hakuwa na mtoto kabisa, kwa sababu sisi tulijaribu kumtafuta kwa njia zote, kwa siri na kwa dhahiri, na tuliulizia habari zake katika kipindi cha uhai wa Hasan lakini hatukupata habari yoyote.

Na lau kama tutakubaliana na madai haya ya kwamba Hasan alikuwa na mtoto kisha akajificha, tutalazimika kukubaliana na madai ya mtu mwingine atakayekufa bila ya kuacha mtoto....habari zinazoelezea kuwa Hasan amefariki bila ya kuacha

mtoto ziko wazi sana kama zile habari za kuwa Bwana Mtume swalla Ilaahu alayhi wasallam alifariki bila ya kuacha mtoto wa kiume.

Kundi la tisa, limeshai kwamba zimethibiti habari nyingi za uhakika juu ya kifo cha Hasan Ibn Ali kama walivyokufa wazee wake na jambo hili halina shaka, pia zimethibiti habari kama hizi zinazoelezea kwamba Hasan hakuacha mtoto baada yake.

Kutokana na usahihi wa habari hizi, sisi tunasema kwamba hakuna Imamu mwingine baada ya Hasan, na Uimamu umekatikia kwake, na hilo ni jambo linalowezekana kiakili na kwa mujibu wa vipimo sahihi. Na kundi hili linaamini kuwa hakuna ulazima wa kuja Mah'di.

Kundi la kumi, ni kundi linaloitwa **Nafiisiyyah**, wao wanaamini kwamba Uimamu ulikuwa ni wa Muhammad Ibn Ali ambaye alifariki katika uhai wa baba yake. Baba yake alimuusia kuwa atakuwa Imamu, lakini alipojiwa na mauti na hali ya kuwa baba yake bado yuko hai, hakuweza kumuusia mtu mwingine awe Imamu baada yake, kwa sababu baba yake ndiye Imamu wa wakati huo, yeye akaamua amkabidhi mtumwa wake aitwaye **"Nafiis"** vitabu na Wasia, kama yeye atatangulia kufa, basi angojee mpaka atakapofariki baba yake kisha amkabidhi vitabu hivyo na Wasia huo ndugu yake Ja'far kama alivyofanya Husein Ibn Ali Ibn Talib (a.s.) alipotoka kwenda Kufah, yeye alimwachia Ummu Salamah ambaye ni mke wa Mtume swalla Ilaahu alayhi wasallam silaha na vitu vinginevyo ili amkabidhi Ali Ibn Husein (Zainul-Abidin) atakaporudi Madina, na kweli Ali Ibn Husein (Zainul-Abidiina) aliporudi Madina, Ummu Salamah alimkabidhi amana aliyokabidhiwa na baba wa mtoto huyu. Kwa hiyo, hivi alivyofanya Muhammad Ibn Ali, kumkabidhi Nafiis Usia wa ndugu yake, ni sawa sawa na alivyofanya Husein. Na kweli Ja'far alidai kuwa yeye ni Imamu kwa njia hii! Kundi hili linaitwa **Nafiisiyyah**, na hayo ndiyo madai yao.

Kundi la kumi na moja, hawa walipoulizwa kuhusu Uimamu ni wa nani, ni wa Ja'far au ni wa mtu mwingine? Wao wakasema sisi hatujui, mambo yametuchanganya, hatujui huo Uimamu ni wa mtoto wa Hasan au ni wa ndugu zake, kwa sababu pia hatujui kwamba Hasan aliacha mtoto au laa! Isipokuwa sisi tunasema kwamba Hasan Ibn Ali alikuwa Imamu, na Uimamu wake umethibiti, na kifo chake pia kimethibiti, hatuna shaka kuwa amekufa, na ukweli ni kwamba ardhi haiwezi kuwa na uhai bila ya kuwepo Imamu, lakini hatumjui Imamu huyo ni nani, na tutaendelea kusubiri mpaka hapo mambo yatakapotubainikia.

Kundi la kumi na mbili; wao wanasema si kweli wanayoyasema hawa waliotangulia. Allah ameiweka hoja yake katika ardhi, nayo ni **Mahdi** mtoto wa **Hasan Ibn Ali Ibn Muhammad Ibn Ali Ar-Ridha**, na mtoto huyo ndiye Wasii wa baba yake na yeye ndiye **Mah'di aliyeahidiwa**, atakayedhihiri zama za mwisho, na lau kama itabakia japo siku moja tu, basi Allah ataichelewesha ili adhihiri **Mahdi**.

Na kundi hili ndio hawa Shia Ithnaashariyya au Shia Imaamiyya tunaojadiliana nao, lakini pamoja na itikadi yao hiyo juu ya Mahdi na kuzaliwa kwake, Shia Ithnaashariyya hawana riwaya hata moja iliyosahihi inayokubalika kwa mujibu wa misingi ya utafiti wa habari, na kwa ushahidi wa haya soma maelezo yafuatayo.

UCHUNGUZI JUU YA RIWAYA ZA SHIA KUHUSU KUZALIWA MAHDI

Mwanachuoni mkongwe wa hadithi katika madhehebu ya Shia, Bwana **Muhammad Ibn Ya'qub Al-Kulainiy**, katika kitabu chake Usuulul-Kaafi amezitaja riwaya 31 (**TheIathini na moja**) chini ya mlango aliouita "**Baabu Maulidi Swaahibiz-Zamaani (a.s.)**", lengo lake ni kuthibitisha kuzaliwa kwa Imamu wao wa 12 (Mahdi), lakini kwa masikitiko makubwa ni kwamba Mwanachuoni mkubwa wa hadithi wa Shia **Muhammad Baaqir Al-Majlisy** katika kitabu chake "**Mir'aatul-Uquuli fiy Sharhi Akh'baari Aalir-Rasuuli**" juzuu ya 6 kuanzia ukurasa wa 171-202, amezihukumu hadithi 22 (Ishrini na mbili) kati ya hizo 31 (**TheIathini na moja**) kuwa ni **dhaifu** kwa kuwa wapokezi wake ni **MAGHULAATI na MAJAAHIIL** (watu wasiofahamika uadulifu wao), kisha akazisahihisha hadithi tisa zilizobakia bila kutumia vigezo vya elimu ya uchambuzi wa habari kama tutakavyoona katika uchambuzi wetu.

Ama Mshia **Muhammad Baaqir Al-Bahbuudiy** mwenye kitabu **Sahihul-Kaafi** yeye amezidhoofisha hadithi zote, isipokuwa moja tu, nayo ni hadithi nambari 24, na hadithi hiyo haina ushahidi wowote juu ya kuzaliwa kwa Mahdi, kwa sababu haikuzungumzia suala hilo.

Uchambuzi wetu kuhusu hadithi za kuzaliwa Mahdi alizozisahihisha Al-Majlisiy;

Ama kuhusu zile hadithi tisa alizozisahihisha **Muhammad Baaqir Al-Majlisiy** ambazo amezisahihisha kwa kufuata matamano ya nafsi yake, na si kwa kuchunga kanuni za uchambuzi wa riwaya, uchambuzi wetu ni huu ufuatavyo:-

Hadithi ya kwanza ni hadithi nambari; 4, hadithi hii amezisahihisha na hali ya kuwa sanad yake ni **dhaifu!** Na kadhalika matni yake haina ushahidi wowote wa kuzaliwa huyo Mahdi, zaidi ya kuwa Abu Sadaam alimsikia mtu nyuma ya ukuta akimwelezea jambo, na yeye akatafsiri kuwa mtu huyo ni Mahdi, na pia aliletewa barua kuwa asiwe na shaka, kisha akapewa Sanda na mikate miwili!!!!

Hadithi ya pili, ni hadithi nambari; 8, hadithi hii katika sanad yake kuna mtu **Majhuul** (hajulikani dhati yake wala hali yake), amemtaja kuwa ni mtu katika Ahlu Sawaad, lakini hajulikani ni nani.

Hadithi ya tatu, ni hadithi nambari; 15, hadithi hii katika sanad yake yuko **Ali Ibn Muhammad**, naye pia ni **Majhuul** na yupo **Muhammad Ibn Swaleh** wanachuoni wao wa hadithi wametofautiana kuhusu yeye.

Hadithi ya nne, ni hadithi nambari; 20, hadithi hii katika sanad yake pia kuna mtu **Majhuul**, imesemwa kuwa ni mtu katika watu wa Aabah, lakini hajulikani ni nani?

Hadithi ya tano, ni hadithi nambari; 24, na hadithi hii haizungumzii suala la kuzaliwa Mahdi.

Hadithi sita, ni hadithi nambari; 25, hadithi hii pia haina ushahidi wowote wa kuzaliwa Mahdi.

Hadithi ya saba, ni hadithi nambari; 26, pia haina ushahidi wowote wa kuzaliwa kwa Mahdi.

Hadithi ya nane, ni hadithi nambari; 29, pia hadithi hii haina ushahidi wowote wa kuzaliwa Mahdi, zaidi ya kuelezea habari za kuuzwa kwa Mjakazi, na hakuna cha ziada.

Hadithi ya tisa, ni hadithi nambari; 31, hadithi hiyo ndiyo haina ushahidi kabisa wa kuzaliwa Mahdi, bali hadithi inazungumzia kuwa Waziri amekataza watu kuzuru makaburi! Hizi ndizo hadithi tisa ambazo Mshia **Muhammad Baaqir Al-Majlisiy** amezisahihisha ili kuthibitisha kuwa Mahdi ameshazaliwa!

UBABAISHAJI WA JAAFAR MWAZOA KUHUSU MAHDI

Kabla ya kufungua mjadala huu kuhusu suala la athari mbaya iliyowekwa na Maghulaati kwenye madhehebu ya Shia Ithnaashariyya, nitapenda kuujiibu ubabaishaji uliofanywa na Mshia Jaafar Mwazoa kuhusu suala la Mah'di, katika ukurasa wa 196 wa kitabu chake Shimo Refu amesema:

"Kwa hakika tunasikitishwa mno na ta'asubi yako iliyokusababisha uamini na kuitakidi uwepo wa kiumbe cha kubuni kilichokuwa na jina la Abdallah bin Sabai, kisha uwe na mtazamo wa kuwa Imam Mahdi (as) ni mtu wa kubuni!! Hali ya kuwa ulimwengu wa elimu na dini umemthibitisha kwa dalili ya Aya za Qur'ani na hadithi sahihi za Bwana Mtume (saw) na Maimamu (as) huku Maulamaa wa Kiislamu wakimkanusha Abdallah bin Sabai ambaye amebuniwa na Saif bin Umar."

MAJIBU YETU

Kwanza, napenda kumnasihia Mshia Mwazoa asiwe na masikitiko juu yangu anatakiwa ajisikitikie mwenyewe kwa kuwa yuko ndani ya madhehebu batili iliyojengwa juu ya fikra za Myahudi Ibnu Sabai na wanafunzi wake Maghulaati.

Pili, kuhusu suala la kuwepo kwa Myahudi Ibnu Sabai hilo tumeshalithibitisha kwa hoja za kielimu zenye nguvu ambazo hazipingi ila mtu mjinga, mkaidi, mwenye ta'asubi na chuki binafsi.

Tatu, ni kuhusu suala Mahdi, jambo hili nalo tumelifafanua kiasi cha uwezo wetu, hivyo tunamshauri Jaafar Mwazoa arudie maelezo yetu hapo nyuma kama atapenda kuujua ukweli.

Kisha Mshia huyu akaendelea kusema katika ukurasa huo huo maneno haya yafuatayo:

Mbali na masikitiko yetu hayo, pia tungependa kukuhoji kuwa: ni nani aliyekujua kuwa Imam Mahdi yuko pangoni? Au ni nani aliyekujua kuwa Qur'ani iko pangoni na Mahdi? Je, tatizo lako juu ya Mahdi ni juu ya muda alioghibu au ni juu ya ukweli wa kuwepo kwake?

MAJIBU YETU

Maswali haya ya kitoto aliyoyaleta Mshia Mwazoa huwenda yametokana na uzembe wake wa kutosoma vitabu vikubwa vya madhehebu yao, hivi kweli Mshia huyu hajui kwamba kuna vitabu vingi vya Shia lth'naashariyya tena vya kutegemewa vinavyohibitisha kuwa Mahdi yuko pangoni? Kwa mfano; lau kama angekuwa amesoma vitabu vinavyozungumzia adabu za ziara kama vile; kitabu **Bihaarul-An'waari**, juzuu ya 102, ukurasa wa 391, kitabu **Kalimatul-Mahdi** cha **Mshia Ash-Shiirazi** ukurasa wa 471-472, **Al-Mazaar Al-Kabiiru** cha **Mshia Muhammad Al-Mash'hadiy** ukurasa wa 206, kitabu **Mis'baahu Az-Zaairi** cha **Mshia Ali Twaausi** ukurasa wa 229, asingefikia kuhoji maswali ya aina hii.

Katika adabu na mwongozo wa kumfanyia ziara Imamu wao wa kumi na mbili (Mahdi), kuna maelezo haya yafuatayo yaliyotolewa na wanachuoni hao tuliowataja hapo nyuma kwenye vitabu, juzuu na kurasa tulizozitaja;

"ثم ائت سرداب الغيبة وقف بين البابين، ماسكاً جانب الباب بيدك، ثم تنحج كالمستأذن، وسم وانزل، وعليك السكينة والوقار، وصلي ركعتين في عَرْضَةِ السرداب وقل: اللهم طال الإنتظار، وشممت بنا الفجار، وصَعِبَ علينا الإنتظار، اللهم أرنا وجه وليك الميمون، في حياتنا وبعد المنون.....يا مولاي يا ابن الحسن بن علي جئتكَ زائراً لك."

"Kisha liendee **PANGO LA GHAIBU** (ALIMOJIFICHA IMAMU) na usimame kati ya milango miwili, hali ya kuwa umeshika upande wa mlango kwa mkono wako, kisha jikohoze kama unayepiga hodi, kisha soma **Bismillahi** na ushuke, na lazimiana na utulivu na upole, kisha swali raka mbili ndani ya uwanja wa **PANGO**, na useme; Ewe Allah! Umerefuka muda wa kusubiri, na watu waovu wanatucheka, na kusubiri kumekuwa kuzito, Ewe Allah tuoneshe uso wa Walii wako wenye Baraka, katika uhai wetu na baada ya mauti....Ewe Bwana wangu! **Ewe mwana wa Hassan Ibn Ali!** Nimekujia hali ya kukufanyia ziara."

Bila shaka, maneno haya peke yake ni majibu ya kutosheleza juu ya maswali dhaifu nay a kitoto aliyoyauliza mwandishi huyu chipukizi wa Shia.

Ndugu msomaji! Pamoja na jibu langu hilo kwa Mshia Mwazoa kuwa Mahdi wao yuko pangoni ni vizuri ujue vile vile kuwa Mashia wana riwaya nyingi zinazogongana juu ya wapi alipojificha Mahdi wao. Na sababu ya mgongano wa riwaya hizo ni kutokana na mchezo mchafu uliofanywa na **Maghulaati** kwenye madhehebu yao, hasa katika mlango huu, kila aliyejisikia kuzua uongo, au kutunga riwaya, anatumka riwaya kisha anawabambikia Maimamu wao, kiasi ambacho umetokea mkorogo mkubwa katika suala hili. Kwa sababu miongoni mwa Shia wapo wanaosema;

MAHDI HAJULIKANI ALIPOJIFICHA

Kuna riwaya zinazoonisha kuwa Mahdi amejificha na hapajulikani mahali alipojificha, amefanya hivyo kwa kuhofia kuwa akijulikana wambea watamchomea kwa viongozi madhalimu! Kama alivyoelezea wakala wa Mahdi, Tazama Usuulul-Kaafi juzuu ya 1 ukurasa wa 333. Kuna riwaya zinazofundisha namna ya kuomba dua wakati wa ziara zao, kama alivyotaja Al-Majlisiy katika Bihaarul-An'waari juzuu ya 102, ukurasa wa 108, Al-Kulainiy katika Usuulul-Kaafi juzuu ya 1 ukurasa wa 337-338, na An-Nuumaniy katika kitabu chake Al-Ghaiba ukurasa wa 116. Na miongoni mwao wapo wanaosema kwamba;

MAHDI AMEJIFICHA MADINA

"لابد لصاحب هذا الأمر من غيبة، ولا بد له في غيبته من عزلة، ونعم المنزل طيبة"

"Hapana budi kwa mwenye jambo hili kughibu (kujificha), na hapana budi katika kughibu kwake kujitenga, na sehemu bora ya kujitenga ni Twaibah (Madina)¹⁴⁹. Pia aliulizwa Hasan Al-Askariy (Imamu wa 11);

"إِنْ حَدَّثَ بِكَ حَدَّثٌ فَأَيْنَ أَسْأَلُ عَنْهُ؟ قَالَ: بِالْمَدِينَةِ [أصول الكافي: ٣٢٨/١. وقال المازندراني في شرح الكافي: يحتمل أن يراد بالمدينة سر من رأى (شرح جامع: ٢٠٨/٦)]"

"Je, likizuka kwako jambo (ukifariki) nimuulizie wapi (Imamu wa 12)? Akasema; Madina."

¹⁴⁹-Usuulul-Kaafi juzuu ya 1 ukurasa wa 176, hadithi nambari 899, Al-Ghaibah cha An-Nuumaniy ukurasa wa 125, na Bihaarul-An'waari juzuu ya 52 ukurasa wa 153.

Usoolul-Kaafi juzuu 1 ukurasa wa 328. Lakini amesema Mshia Al-Mazindaraaniy alipokuwa akiisherehesha hadithi hii kwenye kitabu chake Sharhul-Kaafi; inawezekana ikawa Madina iliyokusudiwa ni mji wa Samarra. Tazama Sharhu Jaami'l juzuu ya 6 ukurasa wa 208. Na wapo wanaosema kuwa;

MAHDI AMEJIFICHA JABAL RADH'WA

Naye Sheikhu Twaafah (At-Tuusiy) katika kitabu chake Al-Ghaiba, anaelezea kuwa Imam wa 12 anaishi kwenye Mlima unaoitwa; Jabal Radh'wa, amepokea riwaya kutoka kwa Abdul-A'laa Maulaa wa Aali Saam, amesema;

Nilitoka mimi na Abu Abdullahi (as) na tulipofika Rauhaa (ni kitongoji kilichopo umbali wa maili 41 kutoka Madina) alitazama kwenye mlima unaoulekea kitongoji hicho, kisha akasema; unauona mlima ule? Huu ni mlima unaitwa Jabal Radh'wa, ni katika **milima ya Uajemi (Iran!!!)** Lakini Allah ametupenda sana **akauhamishia huku**, kwa hakika kila mti uliomo humo una matunda, na sehemu bora kwa usalama wa mwenye hofu, ametamka hayo mara mbili. Mwenye jambo hili (Imamu Mahdi) amejificha humo mara mbili, kwa muda mfupi na kwa muda mrefu. Tazama Kitabul-Ghaiba cha At-Tuusiy ukurasa wa 103. Pia wapo wanaosema;

MAHDI AMEJIFICHA MAKKA

Zimekuja baadhi ya riwaya na kauli kutoka kwa Maimamu wao kuwa Mahdi amejificha Makka, sehemu za Zi Tuwan. Tazama Tafsiri ya Mshia Al-Ayyaashi juzuu ya 2 ukurasa wa 56, Al-Burhaani juzuu ya 2 ukurasa wa 81-82, na Bihaarul-An'waari, juzuu ya 52 ukurasa wa 341. Pia wapo wanaosema;-

MAHDI YUKO ULAYA!!!

Anasema **Mulla Muhammadjaffer Sherif Dewji** katika ukurasa wa 105; "Hadhrat Mehdi (A.S.) yupo hai duniani na huwaokoa wafuasi wake wanapohitaji msaada wake. Mahali pengi pameainishwa kuwa ni makazi yake. Miongoni mwao ni Rabwa huko Yemen, Zi tuwa n.k. kama ilivyoelezwa katika dua mbalimbali. Zaidi ya hayo, **JAZIRATUL KHADHRAA (Kisiwa cha Kijani)** ni nchi kubwa mno katika ufalme wa Imam (A.S.) na kuna majiji mengi makubwa yenye umati mkubwa wa Kishia. Hayo hutawaliwa na wana wa Imam (A.S.) kundi la visiwa linalojulikana kwa jina hilo lipo katikati ya Bahari Nyeupe (**White Sea**) **MAGHARIBI YA UINGEREZA**. Kwa amri ya Mwenyezi Mungu wengi wamekwishawahi kuzuru visiwa hivyo. Hata hivyo, kutokana

na vitabu vya historia, mizunguko mikali ya maji huzingira visiwa hivyo na huwa ngumu na hatari kwa vyombo kufika huko"!!!

Kisha akasema tena Bwana Dewji katika ukurasa wa 112; "Katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani Imam pengine huhudhuria msikiti wa Kufa, au wa Najaf na vile vile Karbala. Katika kila msimu wa Hija yeye huenda kuhiji. Baadhi ya makazi yake yametajwa katika vitabu vingi, k.m. majiji makubwa chini ya utawala wake katika makundi ya visiwa vinavyojulikana kama **JAZEERATUL KHADHRAA** huko Bahari Nyeupe ambako mtu huweza kufika baada ya safari ya siku kumi na tano hadi ishirini kwa meli kutoka mwambao wa Kaskazini Magharibi (**Northwest**) ya Afrika. Majina ya majiji hayo ni haya yafuatayo:

1. **MUBARAKA**: Gavana wa kisiwa hicho ni Hadhrat Tahir, mwana wa Imam (A.S.) na makao makuu ya kisiwa hiki ni jiji linaloitwa Zahera.
2. **RAEQUA**: Gavana wa huko ni mwana wa pili wa Imam (A.S.) aitwaye Hadhrat Qassim.
3. **SAFIYA**: Lililo chini ya utawala wa Hadhrat Ibrahim ambaye vile vile ni mwana wa Imam (A.S.).
4. **ZALOOM**: Huko Gavana ni Hadhrat Abdulrahman ambaye vile vile ni mwana wa Imam (A.S.).
5. **PANATIS**: mtawala wa huko ni mwana wa Imam (A.S.).

Mbali na visiwa hivi vitano, Imamu anayo maskani mengine ya upekee huko Yemen na Iraq ambapo waumini wachache wameweza kuzuru na maelezo yake yametolewa kwingine katika kitabu hiki." Mwisho wa kunukuu.

Ndugu msomaji! Hivyo ndivyo vituko vya Mashia walivyowekewa na Maghulaati na Wazandiki, na sijui Mashia wanasubiri nini humu mitaani wasiokwenda kwao huko **JAZIRATUL KHADHRAA** kwenye Bahari Nyeupe (**White Sea**) **MAGHARIBI YA UINGEREZA!**

SURA YA SITA

HARAKATI ZA SHIA KATIKA KUYASAFISHA MADHEHEBU YAO

Kwanza, nataka ufahamu ndugu msomaji kwamba, pamoja na hujuma ya muda mrefu iliyofanywa na **Maghulaati**, ambao ni wanafunzi wa Myahudi Ibnu Sabai kwenye madhehebu ya Shia lth'naashariyya nyuma ya pazia la Ahlul-Baiti kwa kutunga riwaya nyingi za uongo kisha kuzipachika riwaya hizo kwenye vitabu vikubwa vya Shia, nitapenda nikufahamishe kwamba Maulamaa wa Shia lth'naashariyya na watafiti wao wameshindwa kuzibabadua na kuzisafisha riwaya hizo kwenye madhehebu yao, bali riwaya hizo zimekuwa ndio muhimili mkubwa wa madhehebu hiyo kongwe.

Na jambo la mwanzo lililopelekea kwenye kufeli na kushindwa kwa harakati hizo, ni kutofautiana kwa Maulamaa wao kwenye makundi mawili makuu yenye kuhasimiana na kila kundi lilifikia kulikufurisha kundi jingine, na makundi yenyewe ni haya;

-Usuuliyyuuna;-

Kundi hili, lililazimisha kwamba habari zote zilizopokewa kwenye vitabu vya hadithi, ima kutoka kwa Maimamu au kutoka kwa Mtume swalla llaahu alayhi waalihi wasallam ni lazima zichunguzwe kwa kufuata kanuni za uchambuzi wa habari kama wanavyofanya Ahlu Sunna.

-Akhbaariyyuuna;-

Kundi hili, lilisema; hapana, maadamu hadithi imetajwa kwenye vitabu vyetu vya hadithi vyenye kutegemewa, basi hadithi hiyo haihitajii uchunguzi wowote wa kisanad, bali habari hiyo ni sahihi, kwa sababu kufanya hivyo ni kuwaiga mahasimu zetu (Ahlu Sunna), na sisi tumekatazwa na Maimamu wetu kuwaiga watu hao!

Hali za mizozo baina yao;-

Makundi haya yaliingia kwenye mzozo mkubwa kiasi cha kufikia kupigana na kuuana, bali hata kukufurishana na kuwaharamishia wafuasi wa kundi moja kuswali nyuma ya kundi jingine!

Mzozo huo ulianza mwanzoni mwa karne ya kumi na moja Hijiriyah kupitia Sheikh wao **Muhammad Al-Amin Al-Itsraabaadiy** mwenye kitabu **Al-Fawaidul-Madaniyyah**, kisha mzozo huo ulizuka tena kwa kasi kubwa mwishoni mwa karne ya kumi na mbili zikiongozwa na Wanachuoni wakubwa wa Shia Ith'naashariyya walioko Karbalaa. Na kwa uadilifu tutawaacha wanachuoni wa Shia Ithnaashariyya wao wenyewe watuelezee mzozo huu, na katika Mashia walioelezea mzozo huu kwa uwazi ni Mshia **Sayyid Muhammad Hassan Aalu At-Twaaliqaaniy**, anasema kwenye kitabu **Tan'qihul-Maqaali fiy Ah'wali Ar-Rijaali**:

"...ولم تقتصر على طلبة العلوم وأهل الفضل ، بل تسربت إلى صفوف العوام مما أدى إلى الاستهانة بالعلم والاستخفاف بحملته ، وبلغ التطرف حدا حكم فيه الوحيد الجهاني بعدم صحة الصلاة خلف البحراني."

"(Mzozo) haukuishia kwa wanafunzi na watu bora (wanachuoni) bali ulienea mpaka kwenye safu za Awaamu (watu wasiojishughulisha na elimu) kiasi ambacho ilipelekea kudharauliwa elimu na kuwadharau walioibeba, msimamo mkali (baina yao) ulifikia kiwango cha (Mwanachuoni wa Shia) **Wahiid Al-Bahbahaaniy** kutoa hukumu ya kutoswihi Swala nyuma ya (Mwanachuoni mwingine wa Shia aitwaye) **Al-Bahraaniy!**¹⁵⁰ Kisha akasema tena **Mwanachuoni huyo wa Shia**:

"وأوغل الأخباريون في الازدراء بالأصوليين إلى درجة عجيبة، حتى إننا سمعنا من مشايخنا والأعلام وأهل الخبرة والاطلاع على أحوال العلماء: أن بعض فضلائهم كان لا يلمس مؤلفات الأصوليين بيده تحاشيا من نجاستها ، وإنما يقبضها من وراء ملابسه."

"**Akh'baariyyuuna** walizama ndani zaidi katika kuwadharau **Usuuliyyuuna** mpaka wakafikia daraja ya ajabu kabisa, mpaka tumewahi kuwasikia masheikh zetu na wataalamu mbalimbali na watu wenye maarifa na uzoefu kuhusu hali za wanachuoni (wakisema); baadhi ya watu bora wao walikuwa hawavigusi vitabu vya Usuuliyyiina kwa mikono yao, wakichelea unajisi wake, bali huvikamata kwa nyuma ya nguo zao.¹⁵¹"

¹⁵⁰-Tazama Tan'qihul-Maqaali fiy Ah'waalir-Rijaali juzuu ya 2 ukurasa 85, na kitabu "Ma'a Ulaamai An-Najaf ukurasa wa 74.

¹⁵¹-Tazama; Jaamiu As-Sa'daati ukurasa wa kwanza katika utangulizi, na As-Shaikhiiyah ukurasa wa 39.

Wakati wa mapambano hayo, **Akh'baariyyuuna** walikuwa wakiongozwa na **Mirza Muhammad An-Nishapuur**, na **Usuuliyyuuna** walikuwa wakiongozwa na **Jaafar Kaashiful-Ghitaa An-Najafiy (aliyefariki mwaka 1228 Hijiriyah)**¹⁵².

Mshia At-Twaaliqaaniy anaelezea kuwa baada ya mzozo huo kutoka katika sura za kielimu, ulichukua sura za kihuni, kiasi cha watu kutukanana matusi mazito na kutoleana maneno machafu na kauli za kudharauliana, na hatimaye Usuuliyyuuna walipanga mashambulizi ya kigaidi, wakamvamia kiongozi wa kundi la Akhbaariyyuuna **Mirza Muhammad An-Nishapuriy** nyumbani kwake sehemu ya **Kaadhiyya** wakamuua yeye pamoja na mtoto wake mkubwa wa kiume, kisha mwili wake wakautupa barabarani ili watu wauchezee¹⁵³!!! Na sababu ya kuuliwa kwake ni baada ya kutoa kashfa nzito dhidi ya Wanachuoni wenzake wa Shia (Usuuliyyuuna) kama **Sayyid Muhsin Al-A'raajiy, Sheikh Abul-Qaasim Al-Qummiy, Sayyid Ali Twabaatwaaiy** na wengineo kuwa wanajuzisha kufanya **Liwati (vitendo vya Qaumu Luut)!!!**¹⁵⁴. Jambo ambalo liliwaghadhibisha Usuuliyyuuna, ndipo Mshia **Jaafar Kaashiful-Ghitaa** alipojitokeza na kuandika kitabu alichokiita "**Kaashiful-Ghitwaa an Ma'aibi Al-Mirzaa Muhammad Al-Akhabariy Aduwil-Ulamai**" maana ya jina la kitabu hiki ni; "**Kulifunua pazia, kuhusu aibu alizonazo Mirza Muhammad Al-Kh'baariy adui wa Maulamaa**"!

Nao Akhbaariyyuuna wakajibu mashambulizi kwa kuandika kitabu walichokiita "**As-Swaihatu bil-Haqi Alaa man Alhada watazandaqa**" maana ya jina la kitabu hiki; "**Ukelele wa haki dhidi ya mwenye kumkana Allah na Mzandiki**"¹⁵⁵

Vile vile Mshia Sayyid At-Twaaliqaaniy anatwambia kuwa; baada ya kufariki Kaashiful-Ghitaa kwa maradhi ya Nguruwe, Mirza Muhammad An-Nishaapuuriy

¹⁵²-Tazama As-Shaikiyya ukurasa wa 39.

¹⁵³-Tazama kitabu As-Shaikiyyah ukurasa wa 40.

¹⁵⁴ Tazama As-Shaikiyya ukurasa wa 41.

¹⁵⁵-Tazama Raudhaatul-Jannaati fiy Ahwaali Al-Ulamaai was-Saadaati, juzuu ya 1 ukurasa wa 52, na Ad-Dharia ilaa Tasaanifi As-Shia, juzuu ya 7 ukurasa wa 38.

alisema; "مات الخنزير بالخنزير" **"Amekufa Nguruwe kwa maradhi ya Nguruwe¹⁵⁶!!!**
Mwisho ilifikia kila upande kutoa fat'wa juu ya uhalali wa kuwauwa watu wa upande wa pili! Ameendelea kusema Mshia Sayyid At-Twaaliqaaniy;

"حتى أدت إلى هتك البعض لحرمة البعض ، وانتقاص كل واحد الآخر . وكان كل فريق يرى وجوب قتل الفريق الآخر ، وتطورت القضايا إلى أمور شخصية بحتة تقريبا ، فكان كل من الخصمين يهدف إلى الانتقام من خصمه والتطويح به."

"Mpaka ilifikia kuvunjiana heshima wenyewe kwa wenyewe (Shia lth'naashariyya) na kila mmoja kumdharau mwengine, na kila kundi likaona wajibu wa kuwauwa watu wa kundi jingine, kadhia ziliendelea mpaka kwenye mambo binafsi, ikawa kila mmoja kati ya mahasimu hawa wa pande mbili anakusudia kumlipizia kisasi mwingine na kummaliza kabisa.¹⁵⁷"

Ndugu msomaji! Huwenda ukajiuliza ni sababu gani ya msingi iliyopelekea mizozo yote hiyo baina ya Wanachuoni wa Shia lthnaashariyya wenyewe kwa wenyewe hadi kufikia kukufurishana na kuuwana?

Jibu:

Pamoja na kuwepo kwa sababu nyingine, lakini sababu kubwa na ya msingi iliyopelekea mizozo yote hiyo ni kuwa kundi moja (**Usuuliyyuuna**) lilitaka kufanya mabadiliko, baada ya kugundua kwamba habari na riwaya zilizomo kwenye vitabu vyao si salama bali ni mkusanyiko wa uzandiki na uzushi uliotungwa na Maghulaati, kwa hiyo ni lazima riwaya zichunguzwe kabla ya kufanyiwa kazi.

Na kundi la pili (**Akhbaariyyuuna**) likasema; hapana, habari zetu zisiguswe, ziachwe kama zilivyo, kwa sababu kuchunguza habari si katika utaratibu wa Shia, bali ni katika utaratibu wa Ahlu Sunna wal-Jamaa, na Maimamu wetu wametuharamishia kuwaiga Ahlu Sunna!!!

TANBIHI MUHIMU:

Kwa maelezo haya mafupi tuliyoyatoa hapo juu kuhusu mzozo wa wanachuoni wa Shia lth'naashariyya baina ya Usuuliyyuuna na Akh'baariyyuuna utagundua tabia chafu na utovu wa adabu waliokuwa nao Maulamaa wa Shia lthnaashariyya na unafiki wa kujidai kuwa ni watu wenye maadili mema.

¹⁵⁶-Tazama As-Shaikhyya ukurasa wa 42, Lubaabul-Alqaabi fiy Al-qaabi Al-At'yaabi, ukurasa wa 87 na Qasasul-Ulamai ukurasa wa 133.

¹⁵⁷ - Tazama kitabu As-Shaikhyya u-kurasa wa 42

Katika sehemu hii tumeona namna walivyozozana wenyewe kwa wenyewe na walivyotukanana, wamekashifiana, na wametuhumiana kwa tuhuma chafu, wamekufurishana hadi kuuwana! Je, wangezozana na watu wa madhehebu nyingine ingekuwaje?

Hivyo basi, maelezo hayo nimeyatoa kama zawadi ya bure, kwa Sheikh wake Jaafar Mwazoa, Bwana AbdulRazaq Amir Juma, ambaye kwa makusudi ameamua kuwashutumumu watu wa madhehebu nyingine kwa vitendo vinavyofanywa na wajinga katika wao. Kwa hiyo, ayafungashe maelezo haya pamoja na kauli yake aliposema katika utangulizi wa kitabu Shimo Refu, ukurasa wa (vi):

"Kundi hili la kiwahabi lililoasisiwa kwa misingi ya kisiasa mwanzoni mwa karne ya kumi na nane lau kama wangeachwa waishi peke yao katika dunia hii basi wangeuwana wao kwa wao kutokana na tafauti za kimitizamo. Kama tulivyoona mizozo baina ya Mawahabi wa Tanga na pia baina ya Mawahabi wa Arusha...."

KWA NINI AKHBAARIYYUUNA WALIKATAA KUCHUNGUZA RIWAYA ZA MADHEHEBU YAO?

Huwenda mtu yeyote mwenye akili ya kawaida akashangazwa sana na msimamo huu hasi waliouchukua wanachuoni hawa wa Shia lth'naashariyya, pale waliposimama kidete kulipinga jambo hili zuri, lenye kheri kwenye madhehebu yao, lakini kiukweli ni kwamba, hawa Akhbaariyyuuna walitazama mbali zaidi kuliko hao wenzao Usuuliyyuuna, kwa nini nimesema hivyo? Sikusema hivyo, kwa kukubaliana na upumbavu wao huo, bali nimesema hivyo kutokana na namna Akhbaariyyuuna walivyoelewa kwamba kuzichunguza riwaya zao ili wazikubali zilizothibiti kutoka kwa Maimamu wao na kuzikataa zilizotungwa na Maghulaati kwamba kufanya hivyo ni kuuu Ushia na kuufanya utoweke katika ardhi hii. Na hiyo ndiyo sababu kubwa iliyowafanya Akh'baariyyuuna kuukataa utaratibu huo na wakaona kuwa salama kwao ni kuzifumbia macho riwaya hizo, na kama watajaribu kujiingiza katika kampeni hiyo ya kuvisafisha vitabu vyao dhidi ya riwaya chafu zilizopachikwa na Maghulaati, basi watalazimika kunyamaza na kujifungia kwenye nyumba zao, na Ushia nao utakuwa umekwisha!!!

Na ushahidi wa haya ni maneno ya **Mshia Yuusuf Al-Bahraaniy** (aliyefariki mwaka 1186 H), alipokuwa akiwatahadharisha Mashia wenzake juu ya hatari ya jambo hili kwenye madhehebu yao kwa kuwaambia:

"الواجب إما الأخذ بهذه الأخبار، كما هو عليه متقدمو علمائنا الأبرار، أو تحصيل دين غير هذا الدين، وشريعة أخرى غير هذه الشريعة لنقصانها وعدم تمامها؛ لعدم الدليل على جملة أحكامها، ولا أراهم يلتزمون شيئاً من الأمرين...."

"Wajibu (wetu) ni kuzipokea habari hizi kama zilivyopokelewa na waliotutangulia katika wanavyuoni wetu wema, **au tutafute dini nyingine isiyokuwa hii (ya Ushia), na sharia nyingine isiyokuwa sharia hii, kutokana na upungufu wake na kutokukamilika kwake**, kwa sababu ya kukosekana dalili juu ya sehemu kubwa ya hukumu zake, na wala sioni kama wataweza kujilazimisha kukubali moja kati ya haya mambo mawili.....¹⁵⁸"

Naye Mshia **Murtadha Al-Aamiliy** kwenye kitabu chake **Ma'saatu Az-Zahraa**, juzuu ya 1 ukurasa wa 27 anasema;

"ليس من حق أحد أن يطلب من الناس أن يقتصروا فيما يثرونه من قضايا على ما ورد عن النبي والأئمة بأسانيد صحيحة وفق المعايير الرجالية في توثيق رجال السند، لأن ذلك معناه أن يسكت الناس كلهم عن الحديث في جل القضايا والمسائل دينية كانت أو تاريخية أو غيرها."

"Hakuna haki kwa mtu yeyote kuwataka watu wanapotaja kadhia zilizopokewa kutoka kwa Mtume swallaahu alayhi waalihi wasallam na Maimamu (a.s.) wafupizike na kutaja sanad sahihi kwa mujibu wa vipimo vya (elimu ya) Rijaali katika kuwapa hukumu ya kukubalika wapokezi wa sanad hizo, kwa sababu maana ya jambo hilo ni kuwataka watu wote wazinyamazie hadithi kwenye kadhia zote na masuala yote, yawe ya dini au ya ki-historia au mingineyo.¹⁵⁹ Kisha akasema tena;

¹⁵⁸ - Tazama kitabu; Luuluatul-Bahraini ukurasa wa 47.

¹⁵⁹ -Tazama kitabu Marji'yyatul-Marhala wa

"بل إن هذا الذي يطلب ذلك من الناس لو أراد هو أن يقتصر في كلامه على خصوص القضايا التي وردت بأسانيد صحيحة عن المعصومين، فسيجد نفسه مضطراً إلى السكوت والجلوس في بيته لأنه لن يجد إلا النزر اليسير الذي سيستنفذه خلال أيام أو أقل من ذلك."

"Bali, huyo anayeyataka hayo kwa watu, lau kama yeye atataka katika maneno yake kufupizika juu ya kadhia maalumu zilizopokewa kwa sanad sahihi kutoka kwa Ma'sumiina, basi atajikuta yeye mwenyewe analazimika kunyamaza na kukaa nyumbani kwake, kwa sababu hatapata isipokuwa kiasi kidogo ambacho atakitumia ndani ya siku chache au chini ya hapo."

Ufafanuzi juu ya kauli hizi:-

Ukizitazama kauli hizi, hupati tabu kuona hofu ya Shia lth'naashariyya juu ya madhehebu yao. Na sababu kubwa iliyowapelekea kwenye hofu hiyo ni kule kufahamu kwao namna vitabu vyao vya **Tafsiri, Itikadi, Hadithi, Fiq'hi, Taarekh** na vinginevyo vilivyosheheni maelfu ya riwaya na hadithi za uongo zilizotungwa na Maghulaati, wafuasi na wanafunzi wa Myahudi Ibn Sabai! Kwa hiyo, lau kama watakurupuka, na kuanza kuziiga taratibu na kanuni za Ahlu Sunna juu ya utafiti wa habari na uchambuzi wa riwaya, basi na wao hawatakuwa na Ushia tena, bali watalazimika kufunga Hauzaat zao, na kufungua biashara za kuuza Mchele na Mboga n.k.

Kwa lugha nyingine; kuleta Manhaji hiyo ndani ya Ushia ni kuifanyia uchuro madhehebu hiyo! Na sababu ni kuwa wapokezi wengi waliopokea habari na hadithi za Mashia ni Maghulaati, watu wasiofahamika kwa uadilifu, waongo na mfano wa watu wenye sifa kama hizo.

KUFELI KWA USUULIYYUUNA KATIKA HARAKATI ZAO ZA KUUSAFISHA USHIA NA SABABU ZAKE

Swali la msingi: je, Usuuliyyuuna waliweza kulifikia lengo kuu la kuvisafisha vitabu vya madhehebu yao ya Shia lth'naashariyya dhidi ya riwaya za uongo zilizojaa Ghuluwu na Uzandiki zilizowekwa na Maghulaati?

Jibu:- Ukweli ni kwamba, harakati na juhudi za Usuuliyyuuna hazikufua dafu, kwa sababu hawakuweza kuzisafisha riwaya zilizopachikwa na wafuasi wa Myahudi Abdullahi Ibnu Sabai ndani ya madhehebu yao, na hilo linatokana na sababu hizi zifuatazo;

SABABU YA KWANZA

KUCHELEWA KWA ELIMU YA MUSTALAHUL-HADITHI KATIKA MADHEHEBU YA SHIA

Hii ni elimu ya misingi na kanuni inayohusiana na utambuzi wa hali za sanad na wapokezi wa habari, pamoja na matni za habari wanazozipokea kwa kukubaliwa au kukataliwa. Kwa mfano; inapokujia habari yoyote, unatakiwa uitazame, je walioileta habari hiyo ni watu waadilifu, wenye sifa za ukweli na hifdhi nzuri, na je habari yenyewe imesalimika na kasoro zenye kuiporomoshwa au laa?

Miongoni mwa faida ya elimu hii, ni kumfanya mtu kuwa na uwezo wa kutambua habari/hadithi zinazokubalika na zisizokubalika.

Hivyo basi, mtu yeyote anayetaka kuzungumzia masuala ya usahihi na udhaifu wa habari yoyote, ni mamaja habari yenyewe ni hadithi iliyonasibishwa kwa Mtume swalla llaahu alayhi wasallam, au Swahaba, au Imamu miongoni mwa Maimamu wa Kiislamu, au matukio ya kihistoria ni lazima awe na maarifa na utambuzi wa kutosha juu ya kanuni za elimu hii, kinyume cha hivyo hatafanikiwa. Lakini jambo la kusikitisha ni kwamba elimu hii haikuwepo kabisa kwa Mashia kwa karne nyingi mno.

MAULAMAA WA SHIA WENYEWWE WANAKIRI HILO

Shia Ithnaashariyya pamoja na kwamba wana tabia ya kujifaharisha sana lakini kwenye jambo hili wao wenyewe wanakiri kwamba elimu hii ya uchambazi wa riwaya haikuwepo kwao na imechelewa mno kwao, na mtu wa kwanza kuwawekea kanuni na istilahi za elimu hii katika madhehebu yao ni Mshia **Zainud-Diini Al-Aamiliy** wanayemwita **As-Shahiidu At-Thaaniiy**, aliyeuwawa mwaka 965 Hijiriyaa!!! Na yeye ameiiga elimu hii kutoka kwa Ahli Sunna wal-Jamaa, na hilo linathibitishwa na mwanachuoni wao **Al-Haairiy** katika kitabu chake **Muq'tabasul-Aathaari** juzuu ya 3 ukurasa wa 73 aliposema:

"وَمِنَ الْمَعْلُومَاتِ الَّتِي لَا يَشُكُّ فِيهَا أَحَدٌ أَنَّهُ لَمْ يُصَنَّفْ فِي دِرَايَةِ الْحَدِيثِ مِنْ عُلَمَائِنَا قَبْلَ الشَّهِيدِ الثَّانِي وَإِنَّمَا هُوَ مِنْ عُلُومِ الْعَامَّةِ."

"Na katika yenye kujulikana, ambayo hakuna yeyote anayetilia shaka ndani yake ni kwamba hajatunga katika elimu ya utambuzi wa hadithi yeyote kati ya wanachuoni wetu kabla ya **As-Shahiidi Thaani**, na hizo ni katika elimu za Aamah (Ahlu Sunna)." Na ukiitizama historia ya Mshia huyu **As-Shahiidu At-Thaaniiy** utaona kuwa ni mtu aliyeishi katika karne ya kumi Hijiriyaa, zama za kina **Imamu Suyuutwiy** rahimahu Ilaahu, aliyefariki mwaka 911 Hijiriyaa. Hivyo basi, madhehebu ya Shia kabla ya karne ya kumi walikuwa hawajui elimu ya Mustalahul-Hadithi, wala hawajishughulishi na utafiti wa habari, swali je kwa miaka yote hiyo walikuwa wakitumia kanuni gani za uchambuzi wa habari zao?

Majibu; hakuna, kilichokuja kiliaminiwa na kufanywa ni sehemu katika dini bila ya kuchunguzwa.

Na hilo pia linathibitishwa na mwanachuoni wao **Al-Hurru Al-Aamiliy** katika kitabu chake kitiwacho **'Waasaili As-Shia'** juzuu 20 ukurasa wa 100 aliposema;

"الاصْطِلَاحُ الْجَدِيدُ (تَفْسِيرُ الْحَدِيثِ) مُوَافِقٌ لِاعْتِقَادِ الْعَامَّةِ (أَهْلِ السُّنَّةِ) وَاصْطِلَاحِهِمْ، بَلْ هُوَ مَا خُوذُ مِنْ كُتُبِهِمْ كَمَا هُوَ ظَاهِرٌ بِالتَّتَبُّعِ وَكَمَا يُفْهَمُ مِنْ كَلَامِ الشَّيْخِ حَسَنِ وَغَيْرِهِ، وَقَدْ أَمَرْنَا الْأَيْمَةَ (ع) بِاجْتِنَابِ طَرِيقَةِ الْعَامَّةِ....."

"Istilaahi mpya (mgawanyo wa hadithi) ni wenye kuafikiana na itikadi ya Ahli Sunna na istilahi zao, bali elimu hiyo imechukuliwa kutoka kwenye vitabu vyao, kama ilivyodhahiri kwa kulifuatilia hilo, na kama inavyofahamika kupitia maneno ya

Sheikh Hasan na wengineo, na kwa hakika Maimamu wetu wametuumrisha kuepuka njia ya Ahli Sunna....."

Pia amesema mwanachuoni wa Shia **Nuur Din Al-Musawiy Al-Aamilyi**:

"وَأَمَّا الْعَامَّةُ، فَكُتِبَ لَهُمْ دَالَّةٌ عَلَى أَنَّهُمْ فِي أَوَّلِ زَمَنِ التَّابِعِينَ انْتَحَبُوا أَحَادِيثَهُمْ، وَاعْتَمَدُوا عَلَيْهَا، وَأَسْقَطُوا مِنْهَا كُلَّ شَيْءٍ اشْتَبَهَ عَلَيْهِمْ صِحَّتَهُ، حَتَّى إِنَّ مَالِكًا أَسْقَطَ مِنَ الْحَدِيثِ مَا لَا يُحْصَى، وَاتَّبَعَ مَا لَا يَخْفَى وَالصِّحَاحُ السِّتَّةُ مَشْهُورَةٌ."

"Ama Ahlu Sunna, vitabu vyao vinafahamisha kwamba wao tangu zama za Taabiina wanazichuja hadithi zao, na wamezitegemea, na wameondosha kila kilichokuwa na utata juu ya usahihi wake, mpaka imefikia Imamu Maliki ameondosha hadithi zisizodhibitika na akazithibitisha idadi ambayo haina kificho, na Sihahi sita (**Sahihi Bukhari, Muslim, Sunan za Abi Daud, Tirmidhi, Nasai na Ibn Majah**) ni vitabu mashuhuri.¹⁶⁰"

Naye Mshia **Sayyid Haashim Ma'ruuful-Hasanaiy** anasema katika kitabu chake **Al-Maudhuaatu fil-Aathaari wal-Akhbaari**:

"وَالَّذِي لَا يَجُوزُ التَّنْكَرُ لَهُ أَنَّ مَحَدَّثِي السُّنَّةِ مِنْ أَوَاسِطِ الْقَرْنِ الْخَامِسِ كَانُوا أَكْثَرَ وَعَبَاءٌ وَإِدْرَاكًا لِلْأَخْطَارِ الَّتِي أَحَاطَتْ بِالْحَدِيثِ الشَّرِيفِ مِنْ مَحَدَّثِي الشَّيْخَةِ، فَأَلْفَمُوا بِالْإِضَافَةِ إِلَى كُتُبِ الرِّوَايَةِ وَأَحْوَالِ الرِّجَالِ عَشْرَاتِ الْكُتُبِ خِلَالَ قَرْنَيْنِ مِنَ الزَّمَنِ حَوْلِ الْمَوْضُوعَاتِ وَبَعْضُهَا يَحْمِلُ هَذَا الْأَسْمَ بِالذَّاتِ، وَمِنْ بَيْنِ هَؤُلَاءِ عَبْدُ الرَّحْمَنِ بْنِ الْجَوْزِيِّ الْعَالِمُ الشَّهِيرُ الَّذِي أَلْفَ كِتَابَهُ الْمَوْضُوعَاتِ فِي ثَلَاثَةِ أَجْزَاءٍ خِلَالَ الْقَرْنِ السَّادِسِ الْهَجْرِيِّ وَتَوَالَتْ بَعْدَهُ الْمَوْلَقَاتُ فِي هَذَا الْمَوْضُوعِ فَأَلْفَ السُّيُوطِيُّ، وَالْقَتَمِيُّ وَغَيْرُهُمَا بِنَفْسِ التَّخْطِيطِ وَالْأَسْلُوبِ وَأَصْبَحَتْ كُتُبُهُمْ مِنْ أَجْلِ الْمَصَادِرِ وَأَكْثَرِهَا فَائِدَةٌ لِمَنْ يُرِيدُ أَنْ يَكْتُبَ فِي هَذِهِ الْمَوَاضِعِ. أَمَّا الشَّيْخَةُ فَقَدْ تَجَاهَلُوا هَذَا الْمَوْضُوعَ وَكَأَنَّهُ لَا يَغْنِيهِمْ مِنْ أَمْرِهِ شَيْءٌ فِي حِينِ أَنَّ الْمَوْضُوعَاتِ بَيْنَ مَرُوبَاتِهِمْ لَا تَقِلُّ فِي عَدَدِهَا وَأَخْطَارِهَا عَنِ الْمَوْضُوعَاتِ السُّنِّيَّةِ."

"Jambo ambalo halifai kulipinga, ni kwamba wanachuoni wa hadithi wa Ahlu Sunna katikati ya karne ya tano walikuwa na hifdhi na ufahamu zaidi juu ya hatari zilizo zizunguka hadithi tukufu kuliko wanachuoni wa Shia, wametunga (wanachuoni wa Sunni) makumi ya vitabu, ukiongezea vitabu vya riwaya na hali za wapokezi, wameandika katika kipindi cha karne mbili vitabu kuhusu Al-Maudhuaati (hadithi za kutunga), na vitabu vingine vimebeba jina hilo. Na miongoni mwa Maulamaa hao ni **Abdur-Rahman Ibnul-Jawziy**, mwanachuoni mashuhuri ambaye ametunga kitabu '**Al-Maudhuaati**' katika juzuu tatu katika karne ya sita ya Hijiriyaa na zikafuatia

¹⁶⁰-Tazama Haashiya ya kitabu Al-Fawaaidul-Madaniyya cha Amiin Al-Istarabaadiy, ukurasa wa 125.

baada yake tungo nyingi kwenye maudhui hii, akatunga Suyuutwi, na Al-Fataniy na wengineo kwa mpangilio na utungo huo huo, vikawa vitabu vyao ni vyanzo vitukufu, vyenye faida nyingi kwa mwenye kutaka kuandika katika maudhui hizi. **Ama Shia wao walipuuza maudhui hii kana kwamba haiwahasu**, na hali ya kuwa hadithi za kutunga miongoni mwa riwaya zao (Shia) idadi yake na hatari yake si ndogo ukilinganisha na za Sunni (hadithi za kutunga kwa Shia ni nyingi zaidi)¹⁶¹. Kisha akasema:

"وَكُلُّ مَا فِي الْأَمْرِ إِيَّاهُمْ عَالَجُوا مَشَاكِلَ الْحَدِيثِ عَنْ طَرِيقِ مُؤَلَّفَاتِهِمْ فِي عِلْمِ الرِّجَالِ وَالذِّيَابَةِ الَّذِينَ يَبْحَثَانِ عَنْ أَحْوَالِ الرَّائِي وَالرَّوَايَةِ وَيَضَعَانِ الْخُطُوطَ الْعَامَّةَ لِمَا يَصِحُّ الْأَعْتِمَادُ عَلَيْهِ وَمَا لَا يَصِحُّ ، وَلَكِنَّهُمْ لَمْ يَحَاوِلُوا خِلَالَ هَذِهِ الْقُرُونِ الطَّوَالَ أَنْ يَضَعُوا وَلَوْ كِتَاباً وَاحِداً يَشْتَمِلُ وَلَوْ عَلَى نَمُودَجٍ مِنَ الْمَوْضُوعَاتِ فِي مُخْتَلَفِ الْمَوَاضِعِ فِي حِينِ أَنْتَهُمْ لَا يَزَالُونَ يُعَانُونَ مِمَّا تَرَكْتَهُ تِلْكَ الْمَوْضُوعَاتِ مِنْ آثَارِ سَيِّئَةٍ عَلَى الْمَذْهَبِ الشَّيْعِيِّ الْبَعِيدِ عَنِ الشُّدُودِ وَالْأَسَاطِيرِ وَالْخُرَافَاتِ الَّتِي أَدْخَلَهَا الْمُتَرْتِقَةُ مِنْ أَتْبَاعِ الْحُكَّامِ وَالْقَصَّاصُونَ وَقَادَةُ الْفِرَقِ وَالْأَحْزَابِ."

"Na kwa hali yoyote, ni kwamba wao (Sunni) wametibu matatizo ya kihadithi kwa njia ya vitabu vyao kupitia elimu mbili; **elimu ya Rijaali na elimu ya Mustwalahul-hadithi**, elimu ambazo zinatafiti kuhusu hali za wapokezi na riwaya, na zinameweka mipaka ya ujumla kwa kinachofaa kutegemewa na kisichofaa.

Lakini wao (Shia) hawakuweza katika karne zote hizo kuweka hata kitabu kimoja, japo kwa kutolea mfano tu wa Maudhuaati (**hadithi za kutunga**) katika maudhui mbalimbali. Na katika wakati huo huo bado wanataabika kutokana na athari mbaya iliyoachwa na hadithi za kutunga ndani ya madhehebu ya Shia iliyotakasika na kupetuka mipaka, na ngano nyingi, mambo ya kubuni yaliyoingizwa na wenye kuganga njaa miongoni mwa wafuasi wa watawala, wasimulizi wa visa na viongozi wa makundi na vyama.

Ndugu Msomaji! Bila shaka umejionea mwenyewe namna wanachuoni wa Shia wanavyokiri kwamba kwa miaka yote hiyo bali kwa karne zote hizo Mashia hakuwa na kanuni wala misingi madhubuti kwa ajili ya kupambana na upotofu uliopenyezwa na Maghulaati na Wazandiki kwenye madhehebu yao.

¹⁶¹-Tazama kitabu chake Al-Maudhuaatu fil-Aathaari wal-Akhbaari A'rdhun wa Diraasatun, ukurasa wa 88.

SABABU YA PILI

MPAPATIKA KATIKA ELIMU YA RIJAALI (WAPOKEZI)

Jambo hili limetokana na kukosekana uadilifu katika kuwahukumu wapokezi wao wa habari, kwa sababu ya ubinafsi na taasubi, jambo ambalo limepelekea mgongano na katika kuwahukumu wapokezi, kwa hiyo wakashindwa kuzitumia kanuni zao kwa uadilifu.

Na mtu wa kwanza aliyejulikana katika Maulamaa wa Shia kuandika kitabu maalumu kwa ajili ya elimu hii ya Rijaali (kuhusu hali za wapokezi wa hadithi) katika ni **Sheikhut-Twaaifah At-Tusiy** mnamo karne ya nne Hijiriyya, na ukweli ni kwamba kitabu chake hakikukidhi mahitaji kwa kuwa amekijaza kauli nyingi zenye migongano, kiasi ambacho huwezi kutoka na kauli moja yenye mwongozo. Anasema Mshia **Ali Al-Khaqaaniy**:

"اِخْتَلَفَ عُلَمَاؤُنَا فِي تَوْثِيقِ كَثِيرٍ مِنَ الرِّجَالِ أَوْ فِي الْأَكْثَرِ ، بَلْ فِي كَثِيرٍ مِنَ الْأَعَاظِمِ ، فَتَرَى هَذَا يُوثِّقُ مُحَمَّدُ بْنُ سِنَانٍ بَلْ يَجْعَلُهُ فِي أَعْلَى دَرَجَاتِ الْوَثَاقَةِ ، وَآخَرُ يُضَعِّفُهُ بَلْ يَجْعَلُهُ غَالِيًا ، وَكَالْمُقْضَلِ بْنِ عُمَرَ إِلَى غَيْرِ ذَلِكَ . " [رجال الخاقاني / علي الخاقاني ص ٨٢].

"Wametofautiana Maulamaa wetu juu ya kuwahukumu kwa uaminifu wengi katika wapokezi, au wengi zaidi, bali (pia wametofautiana) kuhusu wakubwa wengi, utamuona huyu anampa uaminifu **Muhammad Ibn Sinani**, bali anamuweka kwenye daraja ya juu zaidi katika uaminifu, na wengineo wanamdhoofisha na kumfanya ni katika Maghulaati, na kama **Mufadhal Ibn Umar** na mengineyo.¹⁶²" Pia hilo limeshuhudiwa na Mshia **Al-Faidhul-Kaashaniy** aliposema:-

"فِي الْجَرِّحِ وَالتَّعْدِيلِ وَسَرَاطِيمِهِمَا اخْتِلَافَاتٌ وَتَنَافُضَاتٌ وَاشْتِبَاهَاتٌ لَا تَكَادُ تَرْتَفِعُ بِمَا تَطْمَئِنُّ إِلَيْهِ النُّفُوسُ كَمَا لَا يَحْفَى عَلَى الْحَبِيرِ بِهَا"

¹⁶²-Tazama Rijaalul-Khaqaaniy, ukurasa wa 82.

"Katika elimu ya **Jarhi** na **Ta'diil** na shuruti zake kuna tofauti na migongano mingi na mambo mengi ya kutatiza ambayo hayaondoki kwa kiasi cha kutulizana juu yake nafsi, na jambo hili halijifichi kwa mtu mtambuzi wa hayo.¹⁶³"

HALI ZA WAPOKEZI WA HADITHI ZA SHIA

Miongoni mwa wapokezi wao waliopokea hadithi kutoka kwa Maimamu wa Shia lth'naashariyya, wapo wanaoitakidi kuwa Allah ana mwili kama wa binadamu, na miongoni mwa wapokezi wenye itikadi hizo ni kama; **Hishaam Ibn Salim, Hishaam Ibnul-Hakam, Muumin (Sheitwan) Twaag** na **Al-Maithamiy** na hayo yameelezwa kwenye kitabu **Usuulul-Kaafi** cha **Al-Kulayniy**¹⁶⁴.

Na miongoni mwao walikuwepo **Wakristo!** Na wenyewe walikuwa wakijifaharisha na kujitangaza wazi kwa **Ukristo** wao, na wakivaa mavazi yenye kufanana na Wakristo, na wakisuhubiana nao, kama vile **Zakariyya Ibn Ibrahim An-Nasraaniy (Zacharia Mkristo)**, ambaye Abu Ja'far At-Tusiy amepokea kutoka kwake katika kitabu chake At-Tahdhiibu!

Pia wapo miongoni mwao waliopinga kifo cha Imamu wao **Ja'far As-Saadiq**, wakasema hakufa, na wakadai kuwa yeye Ja'far ndiye Mahdi anayengojewa na kwa sababu hiyo wakapinga Uimamu wa Maimamu waliobakia. Na hao wenye itikadi hiyo ndio wanaoitwa **Waaqifiyya**, nao ni wapokezi wengi sana wenye sifa hizo, na miongoni mwao ni; **Hassan Ibn Sama'ah Ibn Mihraan, Ibn Fadhaal, Amri Ibn Said** na wengineo.

Pia walikuwepo walioamua kutunga uongo kwa makusudi na kuwazulia Maimamu, na miongoni mwao ni **Abu Amri Ibn Kharqa Al-Basriy**.

Pia wapo miongoni mwao waliofukuzwa katika majlisi ya Imamu As-Saadiq, kama **Ibn Miskaani**. Wapo pia waliokiri wao wenyewe kuwa wamezua uongo, kama **Abu Basiir**.

¹⁶³-Tazama kitabu 'Al-Waafiy' cha Al-Faidhul-Kaashaniy, juzuu ya 1 ukurasa wa 11-12.

¹⁶⁴ Tazama ushahidi wa hilo katika kitabu Usuulu Al-Kaafi juzuu ya 1 ukurasa wa 56-57.

Pia walikuwepo **Maghulaati**, na hawa ndio wengi mno, kama vile; **Daraam Ibn Al-Hakami**, **Ziyad Ibn Abi Salti**, **Ibn Hilali Al-Jahmi**, **Zuraarat Ibn Saalim** na wengineo.

Baadhi yao walifikia kusutana na kukadhibishana wenyewe kwa wenyewe, kwa namna walivyokithirisha uongo, kama **Hishaamu wawili**, **Swaahib At-Twaaq** na **Al-Maithamiy**.

Bali walikuwepo wapokezi waliopokea hadithi nyingi kwa kiasi cha kutisha, na hali ya kuwa hawakuonekana katika vikao vya Maimamu wao isipokuwa mara moja tu jambo ambalo linatilia shaka juu ya ukweli wao kama **Jaabir Bin Yazid Bin Al-Harith Al-Juufiy** aliyefariki mwaka 127 Hijiriyya. Anasema Mshia **Al-Hurru Al-Aamiliy** alipokuwa akimzungumzia Jaabir Al-Juufiy;

"رَوَى سَبْعِينَ أَلْفَ حَدِيثٍ عَنِ الْبَاقِرِ - عَلَيْهِ السَّلَامُ - وَرَوَى مِائَةَ وَأَرْبَعِينَ أَلْفِ حَدِيثٍ، وَالظَّاهِرُ أَنَّهُ مَا رَوَى بِطَرِيقِ الْمُشَافَهَةِ عَنِ الْأَيْمَةِ عَلَيْهِمُ السَّلَامُ أَكْثَرَ مِمَّا رَوَى جَابِرٌ"

[Amepokea hadithi sabini elfu kutoka kwa Al-Baaqir alayhi salaam, na (kwa ujumla) amepokea (hadithi) **laki moja na elfu arobaini**, na dhahiri ni kwamba hakuna aliyewahi kupokea hadithi nyingi moja kwa moja kutoka kwa Maimamu mfano wa hadithi alizopokea Jaabir]¹⁶⁵.

Lakini pamoja na kupokea mrundo wote huo wa hadithi, hakuwahi kuonekana katika vikao vya Maimamu isipokuwa mara moja, amenukuu Mshia **Al-Kashiy** katika kitabu chake **Rijaalu Al-Kashiy**, katika ukurasa wa 191, kutoka kwa **Zuraarat Bin A'yun** amesema;

"سَأَلْتُ أَبَا عَبْدِ اللَّهِ - عَلَيْهِ السَّلَامُ - عَنْ أَحَادِيثِ جَابِرٍ؟ فَقَالَ مَا رَأَيْتُهُ عِنْدَ أَبِي قَطٍّ إِلَّا مَرَّةً وَاحِدَةً، وَمَا دَخَلَ عَلَيَّ قَطُّ"

[Nilimuuliza Abu Abdillahi (a.s.) kuhusu hadithi za Jaabir, akasema; sijawahi kumuona kwa baba yangu kabisa isipokuwa mara moja tu, na kwangu hajawahi kuingia kabisa]!

¹⁶⁵ Tazama Wasaailu As-Shia, juzuu ya 2 ukurasa wa 151.

Bila shaka atakuwa Jaabir Al-Ju'fiy ndiye mtu aliyepokea hadithi nyingi kuliko mtu yeyote, maana ameivuka hata ile idadi iliyomo kwenye vitabu vyao vinne, kwa sababu hadithi zilizomo humo hazivuki hadithi 44,244 (elfu arobaini na nne, mia mbili na arobaini na nne).

Lakini idadi hiyo si ya kustaajabisha sana kwa Shia, bali wao hustaajabishwa sana na idadi ya hadithi alizopokea Abu Hureira radhia llaahu an'hu kutoka kwa Mtume swalla llaahu alayhi wasallam ambazo hazifiki elfu sita, tena kwa kipindi cha miaka mitatu!

Ndugu Msomaji! Kwa maelezo haya utabainikiwa na kujifaharisha kwa uongo kunakofanywa na Mashia pale wanaposema kwamba eti wao wameipokea dini yao moja kwa moja kutoka kwa Ahlul-Baiti, kutoka kwa Mtume swalla llaahu alayhi waalihi wasallam, na kwa sababu hiyo wanazikataa hadithi zilizopokewa kupitia Maswahaba watukufu kutoka kwa Mtume swalla llaahu alayhi waalihi wasallam. Na ushahidi juu ya hilo ni hii kauli ya Mshia **Muhammad Husein Aalu Kashifil-Ghitaa**, aliposema katika kitabu chake **Aslu Shia' wa Usuuluha**;-

أَوْ مِمَّا إِتَّهَمُوا لَا يُعْتَبِرُونَ بِشَيْءٍ مِنَ السُّنَّةِ (أَعْمِي الْأَحَادِيثَ النَّبَوِيَّةَ) إِلَّا مَا صَحَّ لَهُمْ عَنْ طَرِيقِ أَهْلِ الْبَيْتِ عَنْ جَدِّهِمْ يَعْنِي مَا رَوَاهُ الصَّادِقُ عَنْ أَبِيهِ الْبَاقِرِ عَنْ أَبِيهِ زَيْنِ الْعَابِدِينَ عَنِ الْحُسَيْنِ السَّبِطِ عَنْ عَلِيِّ عَنِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَنِ اللَّهِ عَلَيْهِمْ جَمِيعاً، أَمَّا مَا يَزُورُهُ مِثْلُ أَبِي هُرَيْرَةَ، وَسَمُرَةَ بْنِ جُنْدُبٍ، وَمَرْوَانَ بْنِ الْحَكَمِ، وَعِمْرَانَ بْنَ حَطَّانِ الْخَارِجِيِّ، وَعَمْرٍو بْنَ الْعَاصِ وَنَظَائِرِهِمْ، فَلَيْسَ لَهُمْ عِنْدَ الْإِمَامِيَّةِ مِنَ الْاِعْتِبَارِ مَقْدَارٌ بَعُوضَةٍ {

"Miongoni mwa hayo; ni kwamba wao (Mashia Imamiyyah) hawazizingatii Sunna, (ninakusudia Hadithi za Mtume) isipokuwa zile tu ambazo zimesihi kwao kupitia njia ya Ahlil-Bait (a.s.), walizopokea kutoka kwa babu yao Mtume swalla llaahu alayhi waalihi wasallam, yaani iliyopokewa na (Imam Jaafar) **As-Saadiq** naye kutoka kwa **baba yake Al-baqir**, naye kutoka kwa **baba yake Zainul-Abidin** naye kutoka kwa **Husein mjukuu wa Mtume**, naye kutoka kwa **Ali**, naye kutoka kwa **Mjumbe wa Allah** alayhim salaam. Ama mfano wa riwaya alizopokea **Abu Hurairah**, **Samrah ibn Jundub**, **Mar'wan ibn Alhakam**, **Imran ibn Hattwaan Al-khariji** na

Amr ibn Al-A'si na mfano wao, watu hao kwa Imamiyya hawana mazingatio (yoyote) mfano wa thamani ya mbu."¹⁶⁶

Na katika kuyatilia nguvu madai hayo, wanainukuu hadithi ya uongo aliyoitaja **Al-Kulayni** katika kitabu chake **Usulu Al-Kaafiy** aliposema:-

"عَلِيُّ بْنُ مُحَمَّدٍ عَنْ سَهْلِ بْنِ زِيَادٍ عَنْ أَحْمَدَ بْنِ مُحَمَّدٍ عَنْ عُمَرَ بْنِ عَبْدِ الْعَزِيزِ عَنْ هِشَامِ بْنِ سَالِمٍ وَحَمَّادِ بْنِ عَثْمَانَ وَغَيْرِهِ قَالُوا سَمِعْنَا أَبَا عَبْدِ اللَّهِ (عَلَيْهِ السَّلَامُ) يَقُولُ حَدِيثِي حَدِيثُ أَبِي وَحَدِيثُ أَبِي حَدِيثُ جَدِّي وَحَدِيثُ جَدِّي حَدِيثُ الْحُسَيْنِ وَحَدِيثُ الْحُسَيْنِ حَدِيثُ الْحَسَنِ وَحَدِيثُ الْحَسَنِ حَدِيثُ رَسُولِ اللَّهِ (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ) وَحَدِيثُ رَسُولِ اللَّهِ قَوْلُ اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ."

[Kutoka kwa Ali Bin Muhammad, kutoka kwa **Sahli Bin Ziyaad**, kutoka kwa **Ahmad Bin Muhammad**, kutoka kwa Umar Bin Abdil-Aziz, kutoka kwa Hisham Bin Salim na Hammaad Bin Uthman na mwengine, wamesema; tumemsikia Abu Abdillahi alayhi salaam anasema; Hadithi yangu, ni hadithi ya baba yangu, hadithi ya baba yangu ni hadithi ya babu yangu, hadithi ya babu yangu ni hadithi ya Husein, hadithi ya Husein ni hadithi ya Hasan, hadithi ya Hasan ni hadithi ya Amiril-Muuminiina, hadithi ya Amiril-Muuminiina ni hadithi ya Mtume wa Allah swalla llaahu alayhi waalihi wasallam, na hadithi ya Mtume wa Allah ni kauli ya Allah Azza wa Jalla].¹⁶⁷

1- Uchambuzi wetu dhidi ya fahari yao hii ya uongo

Bila shaka hakuna hata mtunzi mmoja kati ya watunzi wakubwa wa vitabu vya Shia aliyepokea moja kwa moja kutoka kwa Imamu yeyote miongoni mwa Maimamu wa Mashia, si **Muhammad Bin Ya'qub Al-Kulayni** mwenye kitabu **Al-Kaafiy** aliyefariki mwaka 329 Hijiriyya, wala **Muhammad Ibn Ali As-Saduuq Al-Qummiy** mwenye kitabu **Manlaa Yahdhuruhul-Faqihu** aliyefariki mwaka 381 Hijiriyya, wala

¹⁶⁶ -Tazama ukurasa 164-165.

¹⁶⁷ -Tazama Usuluun minal-Kaafiy, cha Al-Kulayni, juzuu ya I ukurasa wa 28, Kitabu Fadhlil-ilmii, mlango wa Riwayatul-Kutubi wal-Hadithi, hadithi nambari 154, iliyochapishwa na Ansariyan Publications.

Muhammad Ibn Hasan Sheikut-Twaaifah At-Tusiy mwenye vitabu **Al-Istibsaaru na At-Tahdhiibu** aliyefariki mwaka 460 Hijiriyya. Kama ni hivyo, basi madai ya kwamba Mashia wanachukua dini yao moja kwa moja kutoka kwa Maimamu wa Ahlul-Baiti ni madai ya uongo wa wazi wazi.

Baada ya kufanyika uchunguzi wa kina, na utafiti wa kielimu imetubainikia kwamba sanad za hadithi baina ya watunzi wa vitabu tulivyovitaja na Maimamu wao kuna wapokezi wengi wasiojulikana, Maghulaati na waongo, na hao ndio walioziharibu hadithi za Maimamu wao kuzulia uongo.

Kwa mfano; ukiwatizama Masheikh wa Al-Kulayniy, ambao anapokea kutoka kwao hadithi za Maimamu wao kama **Ali Bin Musa Ar-Ridha, Muhammad Al-Jawaad, Ali Al-Haadi na Hasan Al-Askariy** ni watu kama **Ahmad Bin Muhammad Bin Isa, Sahli Bin Ziyaad Abu Said Ar-Raaziy, Ali Bin Ibrahim Bin Hashim, Ali Bin Asbaati na Ahmad Bin Muhammad Al-Barqiy** na mfano wa hao.

Mfano wa wazi ni hii hadithi ya uongo hapo juu ambayo Al-Kulayniy ameinukuu kutoka **kwa Abu Abdillahi Jaafar As-Sadiq** anayodai kuwa Abu Abdillahi amesema; **"Hadithi yangu, ni hadithi ya baba yangu....."** Ukiitazama sanad yake utaona wameongozana watu waongo na Maghulaati, kina **Sahli Bin Ziyaad na Ahmad Bin Muhammad Al-Barqiy!!!**

Na uzuri wenyewe Shia wao wenyewe wanajua kuwa hawana japokuwa hadithi moja yenye Sanad iliyoungana kutoka kwa watunzi wao wa vitabu waliyoipokea moja kwa moja kutoka kwa Maimamu wao.

Kwa mfano; huwezi kupata riwaya ambayo Al-Kulayniy atasema; amenisimulia **Abu Abdillaahi, au Mussa Al-Kaadhim, au Ali Ar-Ridha, au Muhammad Al-Jawaad, au Ali Al-Haadi, Hasan Al-Askariy** na mfano wa sanad kama hizo. Bali utaona anasema; wametusimulia kundi la watu.....!!! Au ametusimulia **Sahli Bin Ziyaad,** kutoka kwa...kutoka kwa.....kwamba Abu Abdillahi amesema.....au ametusimulia **Ahmad Bin Muhammad** kutoka kwa.....kutoka kwa.....kwamba amesema Abu Jaafar.....

UCHAMBUZI WETU KWENYE VITABU VYAO HADITHI

Baada ya malezo hayo hatuna budi kuvifungua vitabu vya Mashia na kuvipekua vitabu hivyo vikubwa vya hadithi kama vile; **Al-Kaafiy, At-Tahdhiibu, Al-Istibsaaru** na **Manlaa yahdhuruhul-Faqihu**, pamoja na kutaja nafasi ya vitabu hivi katika madhehebu yao, na kuzichunguza baadhi ya riwaya zilizomo humo kwa mujibu wa kanuni zao walizoziweka katika udhibiti wa wapokezi (**Ilmu Ar-Rijaali**) na elimu ya kanuni za riwaya (**Mustalahul-Hadithi**), ili kujua ni lini Mashia walianza kuzitumia elimu hizi na wamefanikiwa kwa kiwango gani? Inafahamika kwamba Shia Ithnaashariyya wana vitabu vikubwa vinne wanavyovitegemea katika misingi ya dini yao na matawi yake, na vitabu vyenyewe ni hivi vifuatavyo:-

(1) Al-Kaafi cha **Sheikh Muhammad Ibn Ya'qub Al-Kulainiy** (aliyefariki mwaka 328 H).

(2) Manlaa Yahdhuruhul-Faqihu cha **Sheikh Muhammad Ibn Ali As-Saduq** (aliyefariki mwaka 381 H).

(3) At-Tahdhiibu cha **Sheikhu Twaafah At-Tuusiy** (aliyefariki mwaka 460 H), na

(4) Al-Istibsaaru pia cha huyo huyo **Sheikh At-Tuusiy**.

Vitabu hivi vinne ndio marejeo ya Shia Ithnaashariyya katika mambo yao yote ya dini. Pamoja na Wanavyuoni wa Shia kukiri juu ya mchezo mchafu uliofanywa na Maghulaati kwenye vitabu vyao, lakini na wao kwa uzandiki wao wakavisifu vitabu hivyo kwa sifa kubwakubwa, kwa lengo la kuendeleza fikra potofu za Maghulaati zilizoasisiwa na Ibnu Sabai.

DARAJA YA VITABU HIVI KWA SHIA ITHNAASHARIYYA

Ndugu msomaji! Katika sehemu hii tutakuletea kauli kumi za Wanachuoni wakubwa wa Shia Ithnaashariyya zinazovisifu vitabu hivi na kuvitukuza.

Kauli ya kwanza: amesema Mshia **Abdul-Husein Sharafud-Din Al-Musawiy** katika kitabu chake **Al-Muraajaatu**;

"وَأَحْسَنُ مَا جُمِعَ مِنْهَا الْكُتُبُ الْأَرْبَعَةُ ، الَّتِي هِيَ مَرْجِعُ الْإِمَامِيَّةِ فِي أَصُولِهِمْ وَفُرُوعِهِمْ مِنَ الصَّادِرِ الْأَوَّلِ إِلَى هَذَا الزَّمَانِ ، وَهِيَ : الْكَافِي ، وَالْتَهَذِيبُ ، وَالْإِسْتِبْصَارُ ، وَمَنْ لَا يَحْضُرُهُ الْقَقِيَّةُ ، وَهِيَ مُتَوَاتِرَةٌ وَمَضَامِيئُهَا مَقْطُوعٌ بِصِحَّتِهَا وَالْكَافِي أَقْدَمُهَا وَأَعْظَمُهَا وَأَحْسَنُهَا وَأَتْقَنُهَا"

"Na miongoni mwa vitabu vizuri vilivyokusanya (riwaya za Maimamu) ni vitabu vinne, ambavyo ndiyo marejeo ya Shia Imaamiyya katika mambo yao ya itikadi na mambo ya matawi, tangu zama za mwanzo hadi zama hizi, navyo ni; **Al-Kaafi, At-Tah'dhibu, Al-Istib'swaru, na Man laa yah'dhuruhul-faqihu, vitabu hivyo ni Mutawaatiri, na yote yaliyomo yanahukumiwa kuwa ni sahihi.** na **Al-Kaafi** ndiyo ya zamani sana, ndiyo kubwa zaidi, nzuri zaidi, na iko katika ufanisi zaidi."¹⁶⁸

Maelezo yetu kwa ufupi:

Mshia **Abdul-Husein Sharafud-Din Al-Musawiy** anatwambia katika kitabu chake **Al-Murajaat** alichokiandika kwa mfumo wa barua, kuwa riwaya zote zilizomo kwenye vitabu hivyo ni sahihi!!! Lakini jambo la ajabu kwa Mashia waliomo hapa kwetu Afrika Mashariki, kama **Abdillahi Nassir, Omari Mayunga, Jaafar Mwazoa** na wengineo, wao wanasema hapana, si kweli kwamba yote yaliyomo kwenye vitabu vinne ni sahihi, zipo riwaya nyingi za kutunga, na wenye kusema kuwa riwaya zote zilizomo humo ni sahihi, hao ni Akhbaariyyuuna, na Akhbaariyyuuna ni Maghulaati na Maghulaati si Mashia bali ni Makafiri!!!¹⁶⁹

Swali; Je, **Abdul-Husein Sharafud-Din Al-Musawiy**, mwenye kitabu hicho **Al-Muraajaat**, ni katika hao Akhbaariyyuuna? Na ni katika Maghulaati? Na si Mshia? Na ni Kafiri?Tunaomba majibu ya kweli tena ya kielimu.

Kauli ya pili; amesema Mshia **Nour At-Twabarsiy Al-Mazindaraniy** kuhusu kitabu **Al-Kaafi;**

" الْكَافِي بَيْنَ الْكُتُبِ الْأَرْبَعَةِ كَالشَّمْسِ بَيْنَ النُّجُومِ ، وَإِذَا تَأَمَّلَ الْمُتَنَصِّفُ اسْتَعْنَى عَنْ مُمْلَحَاتِهِ حَالِ آخَادِ رِجَالِ السَّنَدِ الْمُؤَدَّعَةِ فِيهِ وَتَوَرُّثِهِ الْوَثُوقَ وَيَحْضُرُ لَهُ الْأَطْمِئِنَّانُ بِصُدُورِهَا وَتُبُوتِهَا وَصِحَّتِهَا."

"Kitabu Al-Kaafi baina ya vitabu vinne, ni kama jua katikati ya nyota, na akizingatia mwenye uadilifu atajitosheleza na kutafuta hali za mtu mmoja mmoja katika

¹⁶⁸-Tazama kitabu "Al-Muraja'atu" cha Abdul-Husein ukurasa wa 531, Barua namba 110, chapa ya Muassasatu Daaril-Kitaabil-Islaami.

¹⁶⁹ -Tazama maelezo ya Mshia Jaafar Mwazoa kuhusu Akhbaariyyuuna katika ukurasa wa 151 katika kitabu chake **Shimo Refu.**

wapokezi waliomo katika sanadi waliotajwa katika (kitabu hicho), na kutampa uaminifu, na kutapatikana kwake utulivu wa kupokewa kwake na kuthibiti kwake, **na usahihi wake.**¹⁷⁰"

Kauli ya tatu; amesema Mshia **Al-hurru Al-Aamiliy** kuhusu kitabu **Al-Kaafi:**

"الْفَائِدَةُ السَّادِسَةُ فِي صِحَّةِ الْمُعْتَمَدَةِ فِي تَأْلِيفِ هَذَا الْكِتَابِ - أَيُّ الْكَافِي - وَتَوَاتُرِهَا وَصِحَّةِ نِسْبَتِهَا وَتُبُوتِ أَحَادِيثِهَا عَنِ الْأَيْمَةِ عَلَيْهِمُ السَّلَامُ."

"Faida ya sita, inahusu usahihi wa kutegemewa katika utunzi wa kitabu hiki (Al-Kaafi) na kuwa ni Mutawaatiri, na usahihi wa kunasibishwa (na mtunzi wake) **na kuthibiti hadithi zake kutoka kwa Maimamu (a.s.).**¹⁷¹"

Kauli ya nne; amesema Mshia **Agha Buz'ruk At-Tah'raani** akikisifia kitabu **Al-Kaafi:**

"هُوَ أَجَلُ الْكُتُبِ الْأَرْبَعَةِ الْأَصُولِ الْمُعْتَمَدَةِ عَلَيْهَا ، لَمْ يُكْتَبْ مِثْلُهُ فِي الْمَنْقُولِ مِنْ آلِ الرَّسُولِ ، لِثِقَةِ الْإِسْلَامِ مُحَمَّدُ بْنُ يَعْقُوبَ بْنِ إِسْحَاقَ الْكَلْبِيِّ الرَّازِي الْمَتَوَفَّى سَنَةَ ٣٢٨ هـ ."

"Al-Kaafi ni kitabu kitukufu zaidi kati ya vitabu vinne vya misingi vyenye kutegemewa, haijawahi **kutokea kuandikwa kitabu mfano wake katika yale yenye kunukuliwa kutoka katika familia ya Mtume**, kitabu hicho ni cha Thiqatul-Islami Muhammad Ibn Ya'qub Ibn Is'haaq Al-Kulainiy Ar-Raazi, aliyefariki mwaka 328 Hijiria¹⁷² ."

Kauli ya tano; anasema Mshia **Abbas Al-Qummi** kuhusu kitabu **Al-Kaafi:**

"وَهُوَ أَجَلُ الْكُتُبِ الْإِسْلَامِيَّةِ ، وَأَعْظَمُ الْمَصَنَّفَاتِ الْإِمَامِيَّةِ ، وَالَّذِي لَمْ يُعْمَلْ لِلْإِمَامِيَّةِ مِثْلُهُ ، قَالَ مُحَمَّدُ أَمِينُ الْأَسْتِرَابَادِي فِي مُحْكِي فَوَائِدِهِ : سَمِعْنَا عَنْ مَشَائِخِنَا وَعُلَمَائِنَا أَنَّهُ لَمْ يَصْنَفْ فِي الْإِسْلَامِ كِتَابٌ يُوَازِيهِ أَوْ يَدَانِيهِ ."

"Al-Kaafi ni katika vitabu vitukufu vya Kiislamu, na ni kitabu kikubwa kwa Shia Imaamiyya, **haijawahi kutokea kuandikwa kitabu katika madhehebu ya Imaamiyya mfano wake**, amesema Muhammad Amin Is'tiraabadiy katika kuelezea faida zake; tumesikia kutoka kwa Masheikh zetu na Maulamaa wetu (wakisema);

¹⁷⁰ -Tazama kitabu Mustad'rakul-Wasaili cha Nour Tabar'si, juzuu ya 3 ukurasa wa 532.

¹⁷¹ -Tazama kitabu "Khaatimatul-Wasaili" ukurasa wa 61.

¹⁷² - Tazama "Ad-Dharia ilaa Tasaanifis-Shia" juzuu ya 17 ukurasa wa 245.

hakujawahi kutungwa kitabu katika Uislamu kinachofanana na Al-Kaafi wala kukikurubia.¹⁷³

Kauli ya sita; anasema Mshia **Sayyid Husein Bahrul-Uluumi** kuhusu vitabu vyao vinne kwa ujumla:

"إن الاجتهاد لدى الشيعة مرتكز على الكتب الأربعة: الكافي للكليني، ومن لا يحضره الفقيه للصدوق، والتهذيب، والاستبصار للطوسي، وهي من الأصول المسلمة كالصحيح الستة لدى العامة."

"Hakika ijthadi kwa Shia zimejikita kwenye vitabu hivi vinne; **Al-Kaafi** cha **Kulainiy**, **Man'laa yahdhuruhul-Faqihi**, cha **As-Saduuq**, **At-Tahdhiib** na **Al-Istibsaaru** vyote vya **At-Tusiy**, na vitabu hivyo ndiyo misingi inayotegemewa kama vitabu sita kwa Ahlu Sunna."¹⁷⁴

Kauli ya saba; amesema Mshia **Murtadha Mutwahaar** kuhusu nafasi ya vitabu hivi vinne;

"إِنَّ أَهَمَّ مَصَادِرِنَا الْمُقَدَّسَةِ بَعْدَ الْقُرْآنِ فِي الْحَدِيثِ هِيَ الْكُتُبُ الْأَرْبَعَةُ، وَهِيَ: الْكَافِي، وَمَنْ لَا يَحْضُرُهُ الْفَقِيهُ، وَالتَّهْذِيبُ، وَالْإِسْتِبْصَارُ."

"Hakika marejeo yetu muhimu yaliyotukuka katika Hadithi baada ya Qur-ani ni vitabu vinne, navyo ni; **Al-Kaafi**, **Man'laa yahdhuruhul-Faqihi**, **At-Tahdhiib** na **Al-Istibsaaru**."¹⁷⁵

Kauli ya nane; amesema Mshia **As-Shahidu At-Thani** kuhusu umuhimu wa vitabu hivi vinne;

"كتب الحديث الأربعة التي هي عماد الدين، وأساس دعائم الإسلام، وهي: الكافي، والفقيه، والتهذيب، والاستبصار."

¹⁷³ - Tazamaa Al-Kunaa wal Al-Qaabu, juzuu ya 3 ukurasa wa 98.

¹⁷⁴ - Tazama utangulizi wa kitabu Talkhisu As-Shaafiy cha Sheikhu At-Twaifah At-Tusiy, ukurasa wa 29.

¹⁷⁵ - Tazama Ma'rifatul-Qur'ani, ukurasa wa 19.

"Vitabu vinne vya Hadithi, ambavyo ndiyo muhimili wa dini, na msingi wa nguzo za Uislamu ni hivi (vifuatavyo); **Al-Kaafi, Man'laa yahdhuruhul-Faqihi, At-Tahdhiib** na **Al-Istib'saaru**"¹⁷⁶

Kauli ya tisa; amesema Mshia **Muhammad Jawaad Mughniyya** akivisifu vitabu hivi vinne:

"وَعِنْدَ الشَّيْخَةِ الْإِمَامِيَّةِ كُتِبَ أَرْبَعَةٌ لِلْمَحَّةِ دَيْنِ الثَّلَاثَةِ: مُحَمَّدُ الْكَلْبِيُّ، وَمُحَمَّدُ الصَّادِقُ، وَمُحَمَّدُ الطُّوسِيُّ، وَهِيَ: الْأَسْتَبْرَارُ، وَمَنْ لَا يَحْضُرُهُ الْفَقِيهُ، وَالْكَافِي، وَالْمَهْدِيُّ، وَهَذِهِ الْكُتُبُ عِنْدَ الشَّيْخَةِ تُشْبِهُ الصَّحَاحَ عِنْدَ السُّنَّةِ."

"Kwa Shia Imaamiyya kuna vitabu vinne vya kina Muhammad watatu, **Muhammad Al-Kulainiy, Muhammad As-Saduuq, na Muhammad At-Tusiy,** navyo ni; **Al-Istibsaaru, Man'laa yahdhuruhul-Faqihi, Al-Kaafi** na **At-Tahdhiib,** vitabu hivi kwa Shia vinafanana na Sihahi sita kwa Sunni."¹⁷⁷

Kauli ya kumi; Amesema Mshia **Jaafar Sub'haaniy** akivisifia vitabu vyao:

"وَلَوْلَا الْكَافِي وَأَضْرَابُهُ لَمَا بَقِيَ الدِّينُ، وَلَصَاعَتِ السُّنَّةُ."

"Lau kama si **Al-Kaafi** na **mfano wake,** dini isingebakia na Sunna ingepotea"¹⁷⁸
Ndugu msomaji! Hiyo ndiyo nafasi ya vitabu vyao hivi vinne kama ulivyoona kupitia kauli za wanachuoni wao wakubwa, kauli hizo zinakisifia kitabu Al-Kaafi na wenzake watatu, lakini kwa masikitiko makubwa pamoja na kusifiwa huko, ukivifungua vitabu hivyo utakutana na Uzandiki wa wazi na Kufuru zisizokuwa na kificho.

¹⁷⁶ - Tazama kitabu Al-Kulainiy wal-Kaafi cha Abdul-Rasuuli Abdul-Husein Al-Ghifaari, ukurasa wa 415-420.

¹⁷⁷ - Tazama kitabu Al-Wihdatu Al-Islaamiyya cha Muhammad Jawaad Mughniyya, ukurasa wa 261.

¹⁷⁸ - Tazama Kulliyaaat fiy Ilmir-Rijaali, ukurasa wa 371.

UCHAMBUZI WETU JUU YA VITABU HIVI VINNE

i- Kitabu Uusuulul-Kaafi cha Al-Kulainiy:-

Kitabu Al-Kaafi cha **Al-Kulayniy**, kimegawanywa katika sehemu kuu tatu; **Uusuulun minal-Kaafi**, **Furu'un minal-Kaafi**, na **Raudhatun minal-Kaafi**. Na jumla ya hadithi zilizomo humo ni 16,121 (**elfu kumi na sita, mia moja na ishirini na moja**). Mtunzi wake Mshia **Muhammad Ibnu Ya'qub Al-Kulayniy**, amekiandika kitabu hiki kwa muda wa miaka ishirini. Pamoja na mtunzi kutumia muda mrefu kukiandika, na kusifiwa kwa sifa kubwakubwa, mpaka baadhi yao wamefikia kusema lau si kitabu hicho basi Uislamu ungepotea, na hadi wengine wamefikia kusema kuwa hadithi zote zilizomo humo ni sahihi, lakini ukweli ni kwamba, kitabu Al-Kaafi kimebeba **Hadithi nyingi dhaifu na za uongo**, zilizojaa Ukafiri na Uzandiki!

Na ushahidi wa haya ni maneno ya Mshia **Ayatollah Al-Udhmaa Sayyid Abul-fadhli Ibn Ar-Ridhaa Al-Barqai'y** katika kitabu chake '**Kasru As-Sanami**', ukurasa wa 36 aliposema:-

".....كَيْفَ يَكُونُ كِتَابُ الْكَافِي كَافِيًا لَهُمْ حَيْثُ اسْتَقَى مَيَّاتِ الرَّوَايَاتِ وَالْمَوْضُوعَاتِ الْخُرَافِيَّةِ مِنْ أَعْدَاءِ الدِّينِ وَأَثْبَتَهَا.....فَفِي كِتَابِ الْكَافِي عُيُوبٌ كَثِيرَةٌ سَوَاءٌ مِنْ حَيْثُ السَّنَدُ وَرَوَاتُهُ كَانَتْ أَمْ مِنْ حَيْثُ الْمُنْتَنُ وَمَوْضُوعَاتُهُ؛ وَأَمَّا مِنْ حَيْثُ السَّنَدُ فَمُعْظَمُ رَوَاتِهِ مِنْ الضُّعَفَاءِ وَالْمَجْهُولِينَ وَمِنَ النَّاسِ الْمُهْمَلِينَ وَأَصْحَابِ الْعُقَائِدِ الرَّائِقَةِ ، وَهَذَا مَا يَقُولُ بِهِ عُلَمَاءُ الرَّجَالِ مِنَ الشَّيْخَةِ."

"Vipi kitakuwa kitabu Al-Kaafi kiwe ni chenye kuwatosheleza wao (Mashia) na hali ya kuwa (A-Kulayniy) amechota mamia ya riwaya na habari za uongo zilizotungwa na maadui wa dini, kisha yeye akauthibitisha (uongo huo) humo....Katika kitabu Al-Kaafi kuna aibu nyingi, sawasawa katika sanad na wapokezi wake, au katika upande wa matni na maudhui yake. Ama katika upande wa sanad, **sehemu kubwa ya wapokezi wake ni watu madhaifu** na **wasiojulikana**, na **wasiotajwa majina ya baba zao**, na **watu wenye itikadi potofu**, na haya ndiyo yanayosemwa na Maulamaa watambuzi wa Rijaali kwa Shia."

Ndugu Msomaji! Huo ndio ukweli, wapokezi wengi wa hadithi zilizomo kwenye kitabu Al-Kaafiy ni madhaifu na wengi wao ni Maghulaati, na ushahidi ni pale baadhi ya Wanachuoni wa Kishia walipojarajibu kuzichambua riwaya zilizomo katika kitabu hiki Al-Kaafiy zilifichuka aibu nyingi zilizosheheni kwenye kitabu hicho, na ikabainika kuwa hata zile hadithi zinazosimamisha muhimili wa itikadi na imani zao kama

hadithi za Imaamah, ni hadithi zilizotungwa na Maghulaati na watu Majhuuliina (wasiojulikana).

Kwa mfano; ukiutazama utafiti uliofanywa na Mshia **Muhammad Baaqir Al-Bahbuudiy** kwenye kitabu chake **Sahihul-Kaafiy**, utaona kuwa hadithi sahihi kwenye kitabu hiki Al-Kaafi chenye hadithi 16,121 ni hadithi 4,428 (**elfu nne mia nne na ishirini na nane tu**), yaani chini ya theluthi. Ama kwa mujibu wa uchambuzi wetu, hata hizo hadithi 4428 (**elfu nne mia nne na ishirini na nane**), nyingi katika hizo si sahihi, na hilo utalionga kwa baadhi ya mifano tutakayoitaja hapo mbele Insha-Allaah.

Juzuu ya kwanza ya kitabu Al-Kaafi imekusanya milango muhimu katika madhehebu ya Shia Ithnaashariyya, milango ambayo haimo kwenye vitabu vingine kati ya hivi vitabu vinne vyenye kutegemewa, nayo ni milango hii ifuatayo; **Kitabul-Aqli wal-Jahli, Kitabu Fadhil-Ilmi, Kitabu At-Tawhiid, Kitabul-Hujja, Ab'waabu At-Taarekh**. Katika juzuu hii, hadithi sahihi kwa mujibu wa utafiti wa Mshia **Muhammad Baaqir Al-Majlisiy** katika kitabu chake **Mir'atul-Uquuli**, hadithi sahihi ni 237!

Na kwa mujibu wa utafiti wa Mshia Sheikh **Abdul-Husein Al-Mudhaffar** katika kitabu chake **As-Shaafi Sharhu Usulil-Kaafi**, hadithi sahihi ni 231. Na kwa ushahidi zaidi, tazama kitabu As-Shaafi kilichochapishwa na Matba'atul-Aadabi ya An-Najafi mwaka 1971 AD.

Na hadithi alizozisahihisha Mshia **Muhammad Baaqir Al-Bahbuudiy** katika kitabu chake **Sahihul-Kaafi** ni 161 tu. Na kwa ujumla hadithi walizoafikiana wote watatu juu ya usahihi wake ni hadithi 87 tu, chini ya Ushri (1/10 moja ya kumi).

Ama juzuu ya pili, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Mshia Sheikh **Abdul-Husein Al-Mudhaffar** katika kitabu chake **As-Shaafi Sharhu Usulil-Kaafi**, hadithi sahihi ni 233 tu. Tazama kitabu **As-Shaafi** kilichochapishwa na Matba'atul-Aadabi ya An-Najafi mwaka 1971 AD.

Na ama hadithi zilizomo katika juzuu hii alizozisahihisha Mshia **Muhammad Baaqir Al-Majlisiy** katika kitabu chake **Mir'aatul-Uquuli** ni 467 tu.

Na alizozisahihisha **Al-Bahbuudiy** katika kitabu chake **Sahihul-Kaafi** ni hadithi 392 tu. Na kwa ujumla hadithi walizoafikiana juu ya usahihi wake katika juzuu hii ni hadithi 233 tu, chini ya Ushri (1/10 moja ya kumi).

ii- **Kitabu Manlaa Yahdhuruhul- Faqihu cha As-Saduuq:-**

Kitabu cha pili miongoni mwa vitabu vinavyotegemewa kwa Shia lth'naashariyya ni kitabu **Manlaa Yahdhuruhul-Faqihu** cha Mshia Sheikh **Muhammad Ibn Ali Ibn Baabawayhi Al-Qummi (As-Saduuq)**. Kitabu hiki kina jumla ya hadithi 5963 (elfu tano, mia tisa, na sitini na tatu), hadithi 2050 (elfu mbili na hamsini) ni Mursal (sanad zake zimekatika mwishoni), na hadithi ya aina hiyo inahesabika katika hadithi dhaifu.

Na hadithi zilizobakia ambazo ni hadithi 3,913 (**elfu tatu, mia tisa kumi na tatu**) ndio Mawsuula (sanad zake zimeungana), na katika hizo ambazo sanad zake zimeuanga pia ziko hadithi nyingi dhaifu. Na pia kuna hadithi nyingi kwenye kitabu hiki ambazo riwaya zake ni Mua'llaqah (zimekatika sanad zake mwanzoni), na kwa mujibu wa kanuni za utafiti wa habari, zinahesabika riwaya za aina hiyo kuwa ni dhaifu. Na ushahidi wa kuwa riwaya nyingi zilizomo kwenye kitabu hiki ni Mua'llaaqah (zimekatika sanad zake mwanzoni) ni kauli ya Mshia **Ja'far Sub'hani**:

"إن جل روايات الشيخ في كتابي التهذيب والاستبصار روايات معلقة ، ومثله الصدوق في الفقيه وأما التعليق في الكافي فقليل جداً."

"Hakika sehemu kubwa ya riwaya za Sheikh (At-Tusiy) katika vitabu viwili; **At-Tahdhiibu** na **Al-Istibsaaru** ni riwaya **Mua'llaqa** (zilizokatika mwanzoni mwa sanad) na mfano wake As-Saduuq katika (**Manlaa yahdhuruhu**) **Al-faqihu**....ama kukatika mwanzoni mwa sanad katika Al-Kaafi ni mara chache.¹⁷⁹" Na amesema Mshia **Ayatolla Muhammad Aasif Muhsin**:

"والقاصم للظهر وجود روايات معتبرة الأسانيد ، متضاربة المعاني ، متناقضة المتون ، من أشهر عللها جهل الرواة في التلقي ، وضعف فهمهم ، وقصور استعدادهم في كلام الإمام ، وهذا ينزل قيمة الروايات المعتمدة فضلاً عن غيرها غالباً والله الهادي والعاصم."

"Na jambo lenye kuvunja mgongo, ni kuwepo sanad zenye kuzingatiwa (kukubalika) zinazogongana kimaana na zinazopingana katika matni, na sababu kubwa ni kutojulikana wapokezi wakati wa kupokea, na udhaifu wa ufahamu wao, na maandalizi yao madogo katika kupokea maneno ya Imamu, na hili linapelekea

¹⁷⁹-Tazama Usuulul-Hadithi wa Ahkaamuhu fi ilmi Ad-Diraaya, ukurasa wa 69.

kuziteremsha riwaya zinazozingatiwa, wachilia mbali riwaya nyingine. Allah ndiye mwenye kuongoza na ndiye mlinzi.¹⁸⁰

iii- **Vitabu Al-Istibsaaru na At-Tahdhiibu vya At-Tusiy;-**

Baada ya kuona hali ya kitabu **Al-Kaafi** cha **Muhammad Ibn Ya'qub Al-Kulainiy**, na kitabu **Manlaa Yahdhuruhul-Faqihu** cha **As-Saduuq**, vitabu vinavyofuatia ni: **Al-Istibsaaru** na **At-Tahdhiibu** vyote hivyo ni vya **Sheikh At-Twaaifah At-Tusiy**. Amesema **Mshia Yusuf Al-Bahraaniy** katika kitabu chake **Al-Hadaaiqu**¹⁸¹, juzuu ya 3 ukurasa wa 287;

"إنه لا يخفى على من راجع التهذيب وتدبر أخباره ما وقع للشيخ من التحريف والتصحيح في الأخبار سنداً وامتناً، وقلما يخلو حديث من أحاديثه من علة في سند أو متن."

"Haijifichi kwamba atakayeirejea **Tahdhiibu** na kuzizingatia habari zake, na makosa aliyoyaingia Sheikh katika hadithi kwa sanad na matni, ni mara chache kusalimika hadithi miongoni mwa hadithi zake bila ya makosa ima katika sanad au matni." Na Amesema Mshia Sheikh **Ayatollah Muhammad Sindi/Sanad:**

"إن الشيخ - الطوسي - دأبه في التهذيبين على الجمع بين الأحاديث المختلفة مهما أمكن لدفع شبهة كثرة التعارض في أحاديث أهل البيت التي أدت بأحد الأشراف إلى الخروج من المذهب كما صرح بذلك في مقدمة الكتابين."

"Hakika **Sheikh Tusiy**, ilikuwa tabia yake katika Tahdhiib mbili (**Al-Istibsaar** na **Tahdhibul-Ahkami**) ni kukusanya baina ya hadithi zilizotofautina vyovyote iwezekanavyo, kwa ajili ya kuondoa utata na wingi wa mgongano uliopo katika hadithi za Ahlil-Baiti, utata ambao umempelekea mmoja kati ya Masharifu kutoka kuiacha madhehebu (ya Shia) kama alivyosema wazi hilo katika utangulizi wa vitabu vyake.¹⁸²

¹⁸⁰-Mash'raatu Bihaaril-An'waari juzuu ya 2 ukurasa 436.

¹⁸¹-Pia tazama Samaaul-Maqaali fi ilmir-Rijaali, cha Abul-Hudaa Al-Kalbasiy, juzuu ya 1 ukurasa wa 164.

¹⁸²-Tazama kitabu chake Buhuuthu fiy Mabani Ilmir-Rijaali, ukurasa wa 63.

Amesema Mshia **Nuurud-Diin Al-Musawiy Al-Aamilyi** katika Haashiya yake akimjibu **Al-Amiin Al-Istraabadiy**;

"وكان المصنف لم يكن في حال اليقظة لما نظر الى كتاب الاستبصار! وهذا الاختلاف الواقع بين الأحاديث والأكثر موافق لمذاهب العامة وليس للجمع بين أغلبها سبيل."

"Na hakuwa mtunzi katika hali ya umakini wakati alipokuwa akitazama kitabu Al-Istibsaaru! Hizi tofauti zilizomo baina ya hadithi, nyingi zinafikiana na madhehebu ya Sunni na hakuna njia ya kuzikusanya."¹⁸³

UCHAMBUZI WETU JUU YA WAANDISHI WA VITABU HIVI

Ndugu msomaji! Baada ya uchambuzi tuliufanya juu ya vitabu hivi vinne, sasa tufanye uchambuzi mfupi kuhusu waandishi wa vitabu hivi kwa mtazamo wa Wanachuoni wao wa Kishia

Mtazamo wa Mshia Al-Barqiy kuhusu As-Saduuq na Al-Kulayniy;-

Anasema Mshia **Ayatollah Al-Udhmaa Sayyid Abul-fadhli Ibn Ar-Ridhaa Al-Barqai'y** kuhusu Mshia **As-Saduuq** mwandishi wa kitabu **Manlaa Yahdhuruhul-Faqihu** na kuhusu Mshia **Al-Kulayniy** mwandishi wa kitabu **Al-Kaafi**;

"الشيخ الصدوق كان إنساناً محترفاً يبيع الأرز في قم كتب كراساً جمع فيه كل ما سمعه ممن رآه حسناً ونقله . ومحمد بن يعقوب الكليني أيضاً كان بقالاً في بغداد وقد جمع ودون طوال عشرين عاماً كل ما سمعه من أهل مذهبه واعتمد عليه لأن تلك الفترة لم يكن فيها رجال دين بالمعنى المعروف..."

"**Sheikh As-Saduuq** alikuwa ni mtu mwenye kushughulika na kuuza **MCHELE** huko Qum, kisha ndio akaandika madaftari, akakusanya ndani yake kila alichokisikia kutoka kwa kila aliyemuona na kukinukuu. Na (huyu) **Muhammad Ibn Ya'qub Al-Kulayniy** yeye alikuwa muuza **MBOGA** huko Bagh'dad! Yeye alikusanya na kuandika (kitabu Al-Kaafi) kwa muda wa miaka ishirini, kila alichokisikia kutoka kwa watu wa madhehebu yake na alikitegemea, kwa sababu kipindi hicho hakikuwa kipindi cha watu wa dini (kwa Shia) kwa maana inayofahamika....!"

¹⁸³-Tazama Haashiya ya kitabu Al-Fawaadul-Madaniyya cha Al-Amiin Al-Istraabadiy, ukurasa wa 309.

Mtazamo wa Al-Khui kuhusu At-Tusiy:

Amesema Mshia **Sayyidi Abul-Qasim Al-Khui** katika **Mu'jamu Rijaali-Hadithi** kuhusu Mshia **At-Tusiy** mwandishi wa vitabu **At-Tahdhiibu** na **Al-Istbsaaru**;

"إن الشيخ الطوسي كان يكثر عليه الخطأ فقد كان يذكر شخصاً واحداً في باب واحد مرتين ، أو يترجم شخصاً واحداً في فهرسته مرتين، وأما خطؤه في كتابيه التهذيب والاستبصار فكثير."

"Hakika Sheikh At-Tusiy alikuwa na makosa mengi, alikuwa anamtaja mtu mmoja katika mlango mmoja mara mbili, au anamfanyia tarjama mtu mmoja kwenye (kitabu chake) '**Fihriste**' mara mbili, ama makosa yake katika vitabu vyake; **At-Tahdhiibu** na **Al-Istbsaaru** ni mengi sana.¹⁸⁴" Naye Mshia **Abul-Hudaa Al-Kalbasiy** anamalizia kwa kusema;

"وبالجملة فالأغلاط فيها لا تحصى بل عن بعض السادة من متأخري المحدثين ، إنه أفرد كتاباً في توضيحها وإحصائها."

"Kwa ujumla, makosa yaliyomo humo hayahesabiki, bali wamefikia baadhi ya watukufu katika wanachuoni waliokuja nyuma katika watu wa hadithi (wa Shia) kuandika kitabu maalumu kwa ajili ya kuyahesabu na kuyabainisha (makosa hayo).¹⁸⁵"

RIWAYA ZA AHLUL-KISAA

Katika mambo yenye kustaajibisha, ni pale unapovichunguza vitabu vyao kwa umakini hutazioni riwaya kutoka kwa **Ahlul-Kisaa** ambao ni **Mtume swalla Ilaahu alayhi wasallam, Ali, Fatima, Hasan na Husein radhia Ilaahu an'hum** ila kwa uchache mno na asilimia kubwa katika hizo chache ni dhaifu, pamoja na kuwa Mashia wanajifaharisha sana kuwa wao ni wafuasi wa Ahlil-Baiti na madhehebu yao imejengwa juu ya maandiko kutoka kwa Ahlul-Baiti.

Kwa mfano; ukiitazama juzuu ya kwanza tu ya kitabu Usuulul-Kaafi yenye hadithi 1442 (**elfu moja, mia nne na arobaini na mbili**) kwa mujibu wa chapa niliyonayo, iliyochapishwa na Ansariyan Publication, na chapa ya Kiingereza iliyochapishwa na

¹⁸⁴-Tazama Mu'jamu Rijaalil-Hadithi juzuu ya 1 ukurasa 97.

¹⁸⁵ Tazama Samaaul-Maqaali fi ilmir-Rijaali, juzuu ya 1 ukurasa wa 167.

World Organization for Islamic Services (WOFIS) Tehran-Iran, utaona hadithi za Ahlul-Kisaa ni 44 tu na zote ni dhaifu! Na ufafanuzi wake ni kama ufuatavyo, hadithi zilizopokewa kutoka kwa;

1. Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam ni 4
2. Ali radhia Ilaahu an'hu.....38
3. Fatima radhia Ilaahu an'ha.....0
4. Hassan radhia Ilaahu an'hu.....0
5. Hussein radhia Ilaahu an'hu.....2

Ama kwenye juzuu ya pili, yenye hadithi 2346, (**elfu mbili, mia tatu na arobaini na sita**). Jumla ya hadithi zote zilizopokewa kutoka kwa Ahlil-Kisaa ni 49 kati ya hadithi 2346! Na mchanganuo wake ni kama ufuatavyo;-

1. Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam ni.....17
2. Ali radhia Ilaahu an'hu.....30,
3. Fatima radhia Ilaahu an'ha.....0
4. Hassan radhia Ilaahu an'hu.....1
5. Hussein radhia Ilaahu an'hu.....1

Na hadithi zote hizi zilizopokewa kutoka kwa Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam, Ali, Hasan na Husein haijaswihi hata hadithi moja, zote ni dhaifu, na hilo ni kwa mujibu wa utafiti wa Mashia wenyewe!!!

Kwa mujibu wa utafiti wa Mashia hawa wafuatao; **Al-Majlisiy, Al-Mudhaffar** na **Al-Bahabuudiy**, hadithi sahihi kati ya hizi 49 ni hadithi 4 (nne) tu, mbili ni kutoka kwa Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam na mbili ni kutoka kwa Ali Ibn Abi Twalib radhia Ilaahu an'hu.

Na riwaya hizo mbili zilizopokewa kutoka kwa Mtume swalla Ilaahu alayhi waalihi wasallam, ukiufuata utaratibu wao na kanuni zao za uchambuzi wa habari utazikuta kuwa si sahihi, kwa sababu katika sanad zake yumo mtu mmoja anayeitwa **Sahli Bin Ziyaad**, na Bwana huyu amedhoofishwa na wanachuoni wa Shia, kwa kuwa ni muongo, mwenye ghuluwu, mwenye madhehebu chafu....tazama kitabu **Aslu ilmi**

Ar-Rijaali baina An-Nadhariyyat wat-Tatbiiq cha **Ayatola Muslim Ad-Dawriy**, ukurasa wa 516.

Pia katika sanad hii yumo mpokezi aitwaye **Ahmad Bin Muhammad** naye ni **Al-Barqiy**, na Bwana huyu "alikuwa ni miongoni mwa Maghulaati, yaani makafiri ambao huwapa baadhi ya viumbe sifa za Allah Subhaabahu wa Taalaa". Rejea kitabu Shimo Refu cha Jaafar Mwazoa, ukurasa wa 115.

Na hizo riwaya mbili zilizopokewa kutoka kwa Ali, nazo pia kwa mujibu wa utafiti wa Mshia **Al-Bahbuudiy** ni dhaifu kwa sababu katika sanad zake kuna watu ambao ni wenye madhehebu chafu.

Ndugu msomaji! Hiyo ndiyo hali halisi ya elimu ya uchambuzi wa riwaya za Shia na hiyo ndiyo hali yao kuhusu elimu ya wapokezi wa riwaya zao, na hivyo ndivyo vitabu vyao vikubwa vyenye kutegemewa.

Juhudi za Usuuliyuuna waliodai kuleta mapinduzi na harakati zao za kuvisafisha vitabu vyao dhidi ya uzandiki uliowekwa na Maghulaati kwa miaka mingi zimefeli, na kwa sababu hiyo, ukaona riwaya za kutunga na visa vya uongo ndio vimekuwa muhimili mkubwa uliojengewa juu yake madhehebu ya Shia, kwa hiyo kuzikataa riwaya hizo na visa hivyo ndio kuukataa Ushia wenyewe.

KHATIMA

Mwisho kabisa hatuna budi kumshukuru tena Allah kwa kutuwezesha kukikamilisha kitabu hiki kwa wepesi tena kwa muda mfupi. Kitabu hiki kilikamilika tangu tarehe **10 Muharram 1435** Hijiriyya sawa na **14/ 11/ 2013 AD**, lakini kwa Maqaadiiri yake Allaah hakikuchapishwa kitabu hiki hadi kufikia hii **Rabiul-Akhiir 1436** Hijiriyya sawa na mwezi wa **2/ 2015 AD**. Lakini kilivyochelewa ndivyo kilivyopata ubora zaidi kwa kuongeza hili na kupunguza lile, pamoja na marekebisho mengi ambayo lau kingetoka kwa wakati ule kisingekuwa hivi kilivyo leo.

Na huu ndio mwisho wa juzuu hii ya kwanza ya kitabu chetu '**Kitanzi cha Shaba**' na bila shaka, utakuwa ndugu msomaji una shauku kubwa ya kuisubiri juzuu ya pili ya kitabu hiki, juzuu iliyobeba maudhui mama ya kitabu hiki, nayo ni Itikadi ya Shia lth'naashariyya juu ya Qur-ani Tukufu.

Je, ni kweli Shia lth'naashariyya wanasema kuwa Qur-ani tuliyonayo imepotoshwa kwa kupunguzwa baadhi ya Aya na kuongezwa nyingine au wanasingiziwa? Juzuu hiyo imebeba hoja za kielimu zenye kubatilisha ubabaishaji wote uliofanywa na Mshia Jaafar Mwazoa katika kitabu chake Shimo Refu.

Tunamuomba Allah Jalla Jalaaluh atufanyie wepesi wa kutoka kwa juzuu hiyo ya pili kama alivyotuwepesishia kutoka kwa juzuu hii ya kwanza.

كتبه مصلياً ومسلماً على نبينا محمد وعلى آله وصحبه أجمعين؛

أبو الفضل القاسم

غفر الله له ولوالديه وللمسلمين

VITABU VYA MAREJEO

Al-Qur-ani Al-Kariim

Vitabu vya Ahli Sunna:-

- 1- **Sahihi Bukhari**, cha Imamu Muhammad Bin Ismail Al-Bukhari
- 2- **Sahihi Muslimu**, cha Imamu Muslim Bin Hajjaaj Bin Muslim Al-Qushayriy
- 3- **Musnad Ahmad**, cha Imamu Ahmad Ibn Hanbali, iliyochapishwa na Muassasatu Ar-Risaalah, Beirut-Lebanon.
- 4- **Sunan Abi Daud** cha Imamu Abu Daud As-Sijistaaniy.
- 5- **Al-Jaamiu/Sunan Tirmidhiy** cha Imamu Abu Issa At-Tirmidhiy
- 6- **Mu'jamul-Kabiir** cha Imamu Twabaraaniy
- 7- **Fat'hul-Bari** ya Al-Hafidh Ibn Hajar
- 8- **Al-Minhaaj Sharhu Muslim Ibn Al-Hajjaaj**, cha Imamu Sharafud-Din An-Nawawiy
- 9- **Tafsiri ya Al-Qurtubiy**, iliyochapishwa na Dar Al-Kitabil-Arabi, Beirut-Lebanon.
- 10- **Minhaajus-Sunna** cha Sheikhu-Islaami Ibn Taymiyyah
- 11- **Lawaamiu An'waaril-Bahiyyah** cha Imamu As-Safaariniy
- 12- **Sharhu Aqidati Twahaawiyah** cha Ibn Abil-Izzi Al-Hanafiy
- 13- **Maj'muu Fatawa** ya sheikhu-Islami Ibn Taymiyyah
- 14- **Al-Khutwat wal-l'tibaar** cha Al-Maq'riziy, chapa ya Maktaba Thaqaafatid-Diniyyah, Qairo.
- 15- **Twabaqaatul-Kubra** cha Ibn Sa'd Az-Zuhriy
- 16- **Taarekh Dimash'qi (The History of Damascus)** cha Imamu Ibn Asaakir
- 17- **Al-Istia'bu Fiy Ma'rifatil-As'haabi** cha Ibn Abdil-Barri
- 18- **Al-l'baru** cha Imamu Ad-Dhahbiy
- 19- **Siyaru A'laamin-Nubalaa** cha Imamu Ad-Dhahbiy
- 20- **Shadharaat** cha Ibn l'maadi
- 21- **Tadh'kiratul-Hufadh** cha Imamu Adh-Dhahbiy
- 22- **Tahdhiibut-Tahdhib** cha Al-Hafidh Ibn Hajar Al-Asqalaniy
- 23- **Taq'ribut-Tahdhiib**, cha Ibn Hajar Al-Asqalaniy
- 24- **Al-Bidaayat wan-Nihaayat**, cha Imamu Ibn Kathiir
- 25- **Al-Isaabah fiy Tamyiiz As-Swahaba**, cha Ibn Hajar Al-Asqalaniy
- 26- **Lisaanul-Mizaani**, cha Al-Haafidh Ibn Hajar Al-Asqalaaniy, chapa ya Dar Ehia Al-Tourath Al-Arabi, chapa ya pili ya mwaka 2001, iliyochapishwa Beirut-Lebanon.
- 27- **Twabaqaatus-Shaafiyyah Al-Kubra'** cha Imamu Taajud-Din As-Subkiy
- 28- **Taarekh Najdi** cha Sayyid Mahmoud Shukriy Al-Alousiy, kilichochapishwa na Maktabatu-Thaqaafati Diiniyya - Qairo.
- 29- **Historia ya bara Arab"cha Dr, Nurud-Din Haatimi, DR. Shakir Mustafa, Dr, Jamal Zakariyya na Muhammad Abdul-Fatah.**
- 30- **Al-Badru At-Twaali'**, cha Imamu Muhammad bin Ali As-Shaukaaniy

- 31- Ajaibul-Aathaari fii Tarajumi wal-Akhbaari' cha Sheikh Abdur-Rahmani bin Hasan Al-Jabraty Al-Azhariy**
- 32- As-Swilatu baina At-Tasawufi wa At-Tashayyui'**, cha As-Shaibiy
- 33- Aalim Araai Safawi**
- 34- Iran Diraasatun Aammah** cha Dr, Muhammad Wasfiy
- 35- Shah Abbas Al-Kabiir'** cha Dr, Badii Muhammad Juma
- 36- Iran Swafawiyya** cha Dr, Amir Husein Khunjiy, chapa ya kwanza ya mwaka 2010 iliyochapishwa na Maktabatu Naafidha.
- 37- Shammul-Awaaridhi fiy dhammi Rawaafidhi** cha Mwanachuoni **Mulla Ali bin Sultan Al-Qaariy** aliyefariki mwaka 1014 Hijiriyya
- 38- Audatu As-Swafawiyyiina'** cha Abdul Aziz Al-Mahmuud
- 39- 'Kaffu Ar-Rua'I'** cha Imamu Ibn Hajar Al-Haithamiy ukurasa wa 76, iliyochapishwa na Dar Al-Kutubi Al-Ilmiyyah, Beirut-Lebanon.
- 40- Mawaahibul-Jaliil**, cha Imamu Al-Hattwabiyy
- 41- As-Sunnatu wa makaanatuha fit-Tash'ri'il-Islami** chapa ya Al-Maktabul-Islaami na chapa ya Dar Al-Warrak ya mwaka 2003
- 42- Al-Intisaaru li Ahlis-Sunnati wal-hadiith**, majibu dhidi ya Hassan Ibn farhan Al-Maalikiy, cha Sheikh Abdul-Muhsin Al-Abbad,
- 43- Al-Iqliid** cha **Sheikh Ahmad Siddiiq Al-Ghumariy**
- 44- It'haafu Saadatil-Muttaqiin** cha Az-Zabidiy
- 45- Sharafu As'haabil-Hadiithi** cha Imamu Al-Khatiibu Al-Bagh'daadiy, chapa ya Dar Al-Furqaan, 2008, Qairo.
- 46- IL-Jaamul-Awaami"**, cha Imamu Al-Ghazaali,
- 47- Al-Fikru As-Saamiy** cha **Imamu Muhammad bin Hasan Al-Hajawiy**,
- 48- Rawdhatul-Afkaari wal-Afhaami**, cha Husein bin Ghannaam,
- 49- Ad-Duraru As-Saniyya**
- 50- Al-Asinnatul-Hidaadi fiy Raddi Alaa Alawiy Al-Haddaadi** cha Sheikh Suleiman Ibn Suhman
- 51- Muallafaat Sheikh Muhammad bin Abdil-Wahabi**
- 52- Juhudul-Uthmaniyyiin Li-Inqaadhil-Andalusi**, cha Dr, Nabiil Abdil-Hayyi Ridh'wani
- 53- Ad-Daulatu Al-Uthmaaniyya Awaamilu An-Nuhuudhi wa Asbaabi As-Suqutwi**, cha Dr, Ali Muhammad As-Swallaabiy chapa ya kwanza iliyochapishwa mwaka 2005 na Muassasat Iq'ra-a
- 54- As-Swafawiyyuuna wa Daulat Uthmaaniyya** cha Abul Hasan Alawiy Al-At'rajjiy
- 55- Harakaatu Faarisiyya Mudammira'** cha Dr, Ahmad Shebliy
- 56- At-Tashayyu' Al-Alawiy wa Tashayyu' As-Swafawiy'**, cha Dr Ali Shari'ati
- 57- Uyahudi nyuma ya Pazia la Ahliil-Baiti**, Abul Fadhli Kassim Bin Mafuta

Vitabu vya Shia na Masufi:-

- 1- **Nahjul-Balaagha**
- 2- **Uusulul-Kaafi** cha Muhammad Bin Ya'qub Al-Kulainiy
- 3- **Furuul-Kaafi**, cha Muhammad Bin Ya'qub Al-Kulainiy
- 4- **Tahdhiibul-Ahkami**, cha Abu Ja'far Muhammad Ibn Hasan At-Tusiy.
- 5- **Man'laa Yahdhuruhul-Faqihi**, cha Abu Ja'far As-Saduuq Muhammad Ibn Baabawayhi Al-Qummiy, chapa ya kwanza iliyochapishwa na Ansariyan Publications, Qum- Iran
- 6- **Al-Ghaiba** An-Nuumaniy
- 7- **Firaqus-Shia** cha **Abu Amri Muhammad Ibn Umar Ibn Abdil-Aziiz Al-Kashiy** kimechapishwa na Maktabatu Haidariya iliyoko Najaf chapa ya mwaka 1959 A.D.
- 8- **Bihaarul-An'waari** cha Muhammad Baaqir Al-Maj'lisiy
- 9- **Mir'aatul-Uquuli** cha Muhammad Baaqir Al-Maj'lisiy iliyochapishwa na Daarul-Kutubi Al-Islaamiyya, Tehran-Iran.
- 10- **Al-An'waarun-Nu'maanuyyah** cha Ni'matullahi Al-Jazairiy
- 11- **Mustad'arakul-Wasaili** cha Nour Tabar'si,
- 12- **Khaatimatul-Wasaili**
- 13- **Ad-Dharia ilaa Tasaanifis-Shia** Agha Buz'ruk At-Tah'raani
- 14- **Al-Kunaa wal-Alqaabu**, Mshia Abbas Al-Qummi
- 15- **Talkhisu As-Shaafiy** cha Sheikhu At-Twaifah At-Tusiy
- 16- **Kalimatul-Mahdi** cha Ash-Shiiraziy
- 17- **Al-Mazaaru Al-Kabiiru** cha Muhammad Al-Mash'hadiy
- 18- **Mis'baahu Az-Zaairi** cha Ali Twaausi
- 19- **Tuhfatul-Az'haari'** cha Mshia Badru Din Ibn Shadqami Al-Alawiy
- 20- **Ikh'tiyaaru Ma'rifatir-Rijaali** cha Al-Kashiy
- 21- **Al-Gharaatu** cha Athaqafiy,
- 22- **Rijaalut-Tusiy**,
- 23- **Rijaalul-Hilliy**,
- 24- **Qaamusir-Rijaali** cha Tustariy.
- 25- **Daairatul-Ma'rifi** kinachoitwa **Muq'tabasul-Athari** cha A'lamiy Al-Hairiy,
- 26- **Al-Kunaa wal-Alqaabu** cha Abbas Al-Qummiy,
- 27- **Hallul-Ishkaali** cha Ahmad Ibn Twausiy aliyefariki mwaka 673,
- 28- **Ar-Rijaal** cha Ibn Daud,
- 29- **At-Tahriir** cha At-Twaausiy,
- 30- **Maj'maul-Bayan** cha Al-Qahbani,
- 31- **Mahaasinun-Nafsaniyyah**
- 32- **Naqdur-Rijaali** cha Tafrashiy,
- 33- **Jamiur-Ruwaat** cha Al-Maqdisiy Al-Ar'dabiliy,
- 34- **Manaqibu Aali Abi Twalib** cha Ibn Shahri Ashuup
- 35- **Mir'atul-An'waari** cha Muhammad Ibn Twahir Al-Aamilyiy
- 36- **Al-Maudhuaatu fil-Aathaari wal-Akhbaari** cha **Haashim Ma'ruuf Al-Hasaniy**

- 37- **Kash'ful-As'raari wa Tab'riatu Aimmatil-At'haari'** cha Sayyid Husein Al-Musawiy
- 38- **Sahifatul-Abraari** cha Muhammad Taqi At-Tibriziy Al-Maamaqaniy, chapa ya Darul Mahajjat Al-Baydhaa, chapa ya 2 iliyochapishwa Beirut-Lebanon,
- 39- **Qabasun min nuur Aali Muhammad** cha Mshia Ahmad Mustafa Ya'qub
- 40- **Uyuunu Akh'baarir-Ridha,**
- 41- **Tanzihul-An'biyaa,** cha Sayyid Murtadha
- 42- **Al-Muraja'atu** cha Abdul-Husein, chapa ya Muassasatu Daaril-Kitaabil-Islaami
- 43- **Ma'rifatul-Qur'ani,** Murtaza Mutahar
- 44- **Kashful-Irtiyaabi an Atbaai Ibn Abdil Wahabi,** cha Mshia Al-Aamilyiy
- 45- **Al-Kulainiy wal-Kaafi** cha Abdul-Rasuuli Abdul-Husein Al-Ghifaari,
- 46- **Kulliyyaat fiy Ilimir-Rijaali** Mshia Jaafar Sub'haaniy
- 47- **Al-Wihdatu Al-Islaamiyya** cha Muhammad Jawaad Mughniyya,
- 48- **Kasru As-Sanami** cha Mshia Ayatollah Al-Udhmaa Sayyid Abul-fadhli Ibn Ar-Ridhaa Al-Barqai'y
- 49- **Al-Hadaaiqu** cha Mshia Yusuf Al-Bahraaniy
- 50- **Buhuuthu fiy Mabani Ilimir-Rijaali** cha Mshia Sheikh Ayatollah Muhammad Sindi/Sanad
- 51- **Al-Fawaadul-Madaniyya** Al-Amiin Al-Istraabadiy
- 52- **Haashiya Al-Fawaadil-Madaniyya** cha Mshia Nuurud-Diin Al-Musawiy Al-Aamilyiy
- 53- **Mu'jamu Rijaalil-Hadithi** cha Sayyidi Abul-Qasim Al-Khui
- 54- **Samaaul-Maqaali fi ilmir-Rijaali** cha Abul-Hudaa Al-Kalbasiy
- 55- **Usuulul-Hadithi wa Ahkaamuhu fi ilmi Ad-Diraaya** cha Mshia Ja'far Sub'hani
- 56- **Rijaalul-Khaqaaniy** cha Mshia Ali Al-Khaqaaniy
- 57- **Muq'tabasul-Aathaari cha Al-Hairiy**
- 58- **Waasaili As-Shia'** cha Al-Hurru Al-Aamilyiy
- 59- **Tan'qihul-Maqaali fiy Ah'waali Ar-Rijaali** cha Mshia **Sayyid Muhammad Hassan Aalu At-Twaaliqaaniy,**
- 60- **As-Shaikyyah** Sayyid At-Twaaliqaaniy
- 61- **Jaamiu As-Sa'daati**
- 62- **Lubaabul-Alqaabi fiy Al-qaabi Al-At'yaabi,**
- 63- **Qasasul-Ulamai,**
- 64- **Raudhaatul-Jannaati fiy Ahwaali Al-Ulamaai was-Saadaati,**
- 65- **Luuluatul-Bahraini** cha Mshia Yuusuf Al-Bahraaniy
- 66- **Ma'saatu Az-Zahraa** Murtaza Al-Aamilyiy
- 67- **Al-I'tisaam bi hablillaahi** cha Mshia Muhammad Mahdi Al-Khalisiy
- 68- **Tatwawurul-Mabaani Al-Fikriyyah** cha Husein Al-Madrasiy At-Twabawabaiy
- 69- **Qawaaidul-Hadiithi** cha Al-Ghuraifiy
- 70- **Faslul-Khitabi** cha Ahmad Ali Al-Qibbaniy
- 71- **Misbaahul-Anaami** cha Sharifu Alawiy Al-Haddaadiy
- 72- **Ad-Duraru As-Saniyya fiy Raddi Alaal-Wahaabiyya'** Ahmad Zain Dahlaani

- 73- **Al-Fajru As-Saadiq' Jamiil Sidqiy Az-Zahaawiy**
 74- **As-Swaaqatul-Muhriqah** Sheikh Muhammad Ibn Abi Bakar
 75- **Al-Jawaahiru Al-Kalaamiyya fiy Idhaahi Al-Aqiidati Al-Islaamiyya** cha Imamu Twaahir Ibn Swaleh Al-Jazaairiy
 76- **Jalaaul-Awhaami' cha Ahmad Mukhtaar Pasha Al-Muayyad**
 77- **Upotevu wa Madhehebu ya Uwahabi' cha Khalifa Khamis Mohammed**

78-ZAMAN HADHRAT MAHDI Mulla Muhammadjaffer Sherif Dewji, Kimetolewa na kuchapishwa na Bilal Muslim Mission of Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania, toleo la kwanza 1991, kimetarjumiwa na Alhaj Zakirhussein M. S. Lakha.

79-ANAYENGOJEWANA cha Mshia Ali Naqi Saheb, kimetafsiriwa kwa Kiswahili na Sayyid Muhammad R. M. Mahdi El-Moosawy, Kimetolewa na Kuchapishwa na Bilal Muslim Mission of Tanzania, Dar es Salaam.

80-Ma'alimu l-Madrasatain cha Murtadha Al-Askariy kilichotarjumiwa na Msabaha Shabani Mapinda, kimetolewa na kuchapishwa na Al-Itrah Foundation Dsm.

81- Waulizeni wanaofahamu' cha Mshia Muhammad Tijani As-Samawi,

82-Abu Hureirah cha Mshia Sharafud-Din Al-Musawiy.

83-Abdullahi Ibn Saba' na ngano nyinginezo, kilichotarjumiwa kwa lugha ya Kiswahili na Ramadhani Kanju Shemahimbo, kimetolewa na kuchapishwa na Taasisi ya Kishia Alitra Foundation, Dar es Salaam.

84-Shimo Refu

Vitabu vinginevyo:-

Kamusi ya Kiswahili ya karne ya 21

YALIYOMO

UTANGULIZI.....3-9

SURA YA KWANZA

NENO LISILOBUDI.....10-15

MAKOSA YA JAAFAR MWAZOA.....15-21

MJADALA NA ABDUL-RAZAQ .A. JUMA.....21-29

CHOZI LA UONGO JUU YA WITO WA UMOJA.....29-39

SURA YA PILI

AHLU SUNNA WAL-JAMAA.....40-50

MJADALA NA MSHIA MWAZOA KUHUSU KAULI YA IBNU SIIRIIN.....51-57

TUHUMA ZA MWAZOA DHIDI YA MISINGI YA HADITHI YA AHLI SUNNA NA MAJIBU YETU.....57-63

SURA YA TATU

UWAHABI.....64

HISTORIA FUPI YA SHEIKH MUHAMMAD BIN ABDIL-WAHABI.....64-70

Hali ya kijamii katika miji yake.....70-73

Daawa ya Sheikh Muhammad Bin Abdil-Wahabi.....73-77

Maadui zake na uzushi wao.....77-82

Hali ya kisiasa.....82-87

Kidokezo.....88

Hali ya maadui wa Sheikh kidini.....89-91

Uongo wa Mshia Mwazoa kuhusu uhusiano wa Talibani na Mawahabi.....91-93

SURA YA NNE

DOLA YA SWAFAWIYYAH.....94

Watawala wa Dola ya Swafawiyah na vipindi vya utawala wao.....95

Wanachuoni wa Dola ya Swafawiyyah.....	96
Itikadi potofu na uzushi walioudhirisha katika kipindi cha utawala wao.....	97
Hali ya Uislamu kabla ya kusimama kwa Dola ya Swafawiyyah.....	98
Chanzo cha kudhoofika nguvu za Waislamu.....	99
Uvamizi wa Mashia katika nchi ya Iran.....	102
Uvamizi wa Mashia katika nchi ya Af'ghanistan.....	103-104
Uvamizi wa Mashia katika nchi ya Iraq.....	104
Mashia walifukua kaburi la Imamu Abu Hanifa na kuzika mahali pake mbwa!.....	105-110
Hali za Mayahudi na Wakristo wakati wa Dola ya Swafawiyyah.....	110-103

SURA YA TANO

USHIA NA MYAHUDI IBNU SABAI.....	114-118
Kudhiri kwa Ibnu Sabai.....	118-121
Udanganyifu wa Mshia Murtadha kuhusu Ibnu Sabai.....	121-124
Jaafar Mwazoa amuiga Murtadha Al-Askariy.....	124
RIWAYA ZINAZOTHIBITISHA KUWEPD KWA IBNU SABAI.....	126
Riwaya za Shia.....	127-129
Riwaya za Ahli Sunna wal-Jamaa.....	130-133
KAULI ZINAZOTHIBITISHA KUWEPD KWA IBNU SABAI.....	133-141
Uongo wa Mshia Jaafar Mwazoa kuhusu Ibnu Sabai na Majibu yetu.....	142-152
ATHARI ZA MYAHUDI IBNU SABAI KWENYE USHIA.....	152-154
MBEGU CHAFU WALIYDIPANDA MAGHULAATI KWENYE USHIA.....	155-157
Jambo la kwanza; Ghuluwu (kuvuka mipaka katika kuwasifu) Maimamu wao.....	158-164
Jambo la pili; Shahada ya tatu.....	164-167
Jambo la tatu; kuzaliwa Mah'di wao.....	167-177

Ubabaishaji wa Mwazoa kuhusu Mah'di na majibu yetu.....177-179

Mahli alipojificha Mah'di.....179-181

SURA YA SITA

HARAKATI ZA SHIA KATIKA KUYASAFISHA MADHEHEBU YAO DHIDI YA MBEGU CHAFU ZA MAGHULAATI.....182

MASHIA USUULIYYUUNA NA AKHBAARIYYUUNA NA MIZOZO YAO.....182-188

Kwa nini Akhbaariyyuuna walikataa kuchunguzwa riwaya za madhehebu yao?.....188

KUFELI KWA USUULIYYUUNA KATIKA HARAKATI ZA NA SABABU ZA KUFELI.....189

Sababu ya kwanza; Kuchelewa kwa elimu ya Mustwalahul-Hadithi katika madhehebu ya Shia.....189-193

Sababu ya pili; Mgongano usio na ufumbuzi kwenye vitabu vyao vya elimu ya Rijaali (wapokezi).....193-198

UCHAMBUZI WETU KWENYE VITABU VYAO VYA HADITHI.....199-211

KHATIMA.....212

VITABU VYA MAREJEU.....213-217